Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Thelathini - Tarehe 23 Julai, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## DUA

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):**

Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais katika mwaka uliopita pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 289

**Madaraja ya Godegode na Kijiji cha Manghangu**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya kutoka Mpwapwa - Manghangu - Kimagai - Godegode - Mugoma - Pwaga hadi Mafene ni mbaya sana, na kwa kuwa barabara hiyo ina makorongo makubwa katika Vijiji vya Manghangu - Godegode na Magoma:-

(a) Kwa kuwa makorongo hayo yakijaa maji wakati wa mvua, eneo la Godegode huwa kama kisiwa na magari kushindwa kupita, je, Serikali ina mpango gani na kulifanyia ukarabati daraja la zamani la Godegode ili magari yaweze kupita bila matatizo kuliko hali ilivyo sasa?

(b) Kwa kuwa barabara hiyo ndiyo kiungo kikubwa kati ya Makao Makuu ya Wilaya ya Mpwapwa na Kata za Godegode, Lumuma na Mbuga, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga madaraja katika makorongo ya Kijiji cha Manghangu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba makorongo yaliyopo katika barabara kati ya Mpwapwa na Mafene katika Vijiji vya Manghangu - Godegode na Magoma hufanya barabara hii kutopitika kabisa katika kipindi cha masika na hivyo kufanya Godegode kuwa Kisiwa. Serikali inatambua adha wanayopata wananchi wa Godegode kutokana na matatizo ya barabara na inafanya jitihada zaidi ili kuwaondolea wananchi wa eneo hili kero hiyo.

Kwa mwaka 2002/2003 Halmashauri ya Mpwapwa ilitenga jumla ya shilingi 7,800,000/= kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya barabara hii na mwaka huu wa 2003/2004 Halmashauri hiyo imetenga kiasi cha shilingi 19,200,000/= kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa barabara hii inapitika kwa shida baada ya daraja la Godegode kuvunjika. Inakisiwa kuwa kiasi cha shilingi milioni 62 kinahitajika katika ukarabati wa daraja hilo. Kiwango hicho cha fedha ni kikubwa sana ukilinganisha na hali ya fedha ya Halmashauri ya Mpwapwa. Kwa hiyo, Halmashauri inaendeleza jitihada za kutafuta fedha zaidi kutoka Serikali Kuu na wafadhili na punde pesa hizo zitakapopatikana daraja hilo litatengenezwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua vile vile kuwa barabara ya Mpwapwa - Lumuma ni kiungo kikubwa kati ya Makao Makuu ya Wilaya ya Mpwapwa na Kata za Godegode, Lumuma na Mbuga. Kiasi cha madaraja 10 yenye jumla ya urefu wa mita 141, kwa urefu na yanayotarajiwa kugharimu shilingi 73,700,000/= yanahitajika kujengwa katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, bado Serikali inafanya jitihada zaidi ili kuweza kuona ni namna gani inaweza ikapata kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa madaraja hayo. Kwa hiyo, kwa sasa namwomba Mheshimiwa Mbunge afanye subira. Lakini napenda nimshukuru sana kwa juhudi kubwa anazozifanya katika kufuatilia kuondoa adha ya wananchi wake kutokana na uharibifu wa barabara hiyo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa kuwa barabara hii hapo zamani ilikuwa chini ya Mkoa, ilikuwa inatengenezwa na Wizara, Serikali; na kwa kuwa hivi sasa barabara hiyo Serikali iliikabidhi kwa Halmashauri ya Wilaya ambayo haina uwezo; je, sasa Serikali ina mpango gani wa kuirudisha Mkoani ili gharama zote zitolewe na Serikali Kuu badala ya Halmashauri ambayo haina uwezo?

Mheshimiwa Spika, pili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri utakuwa tayari kutembelea sehemu hizo nilizozitaja hasa Godegode ili kuwaona wananchi wanavyopata adha ya usafiri kuja Makao Makuu ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, fedha zinazotumika kwa ajili ya utengenezaji wa barabara katika Halmashauri zetu, ni fedha zinazotoka Serikali Kuu kutoka katika Mfuko wa Barabara. Kwa hiyo, tatizo kubwa hapa ni hasa ufinyu wa Bajeti yenyewe. Lakini kutokana na swali lake tutajaribu kuzungumza na Ujenzi kuona kama hilo jambo linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, suala la kutembelea maeneo hayo halina tatizo na sisi wenyewe tumeshaanza kufanya utaratibu wa kutembelea Mkoa mzima wa Dodoma. Kwa hiyo, kama si mimi atakuja Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Na. 290

**Hospitali Teule ya Nyakahanga**

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Karagwe inatumia Hospitali Teule ya Nyakahanga kama Hospitali ya Wilaya:-

(a) Je, hospitali hiyo inaendeshwa kwa uwiano gani kati ya Serikali na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania *(KKKT)* Dayosisi ya Karagwe ambayo ndio wamiliki wa hospitali hiyo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua Zahanati ya Kayanga iliyoko Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Hospitali Teule ya Nyakahanga inamilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania *(KKKT)* Dayosisi ya Karagwe. Hospitali hiyo Teule ndiyo inatumika kama Hospitali ya Wilaya. Katika uwiano wa uendeshaji wa Hospitali hiyo Dayosisi ya Karagwe inashughulikia gharama zote za maendeleo *(Development Costs).* Aidha, Serikali inashughulikia masuala yote ya uendeshaji *(Recurrent Costs)* ikiwa ni pamoja na kulipia mishahara ya watumishi wote. Jumla ya shilingi 872,159,693/= zimekwishatolewa na Serikali kati ya mwaka 1999/2000 na gharama hizo ni wastani wa asilimia 65 ya mchango wa Serikali katika hospitali hiyo kwa kipindi chote. Aidha, wafadhili kwa kupitia *basket fund* wanatoa asilimia 35 ya fedha zinazotolewa katika mpango wa Wilaya kwa Hospitali ya Nyakahanga.

(b) Mheshimiwa Spika, Zahanati ya Kayanga imekubaliwa kupandishwa hadhi na kuwa Kituo cha Afya. Ili kuboresha huduma za afya katika kituo hicho Halmashauri ya Karagwe imefanya yafuatayo:-

Kwanza, ukarabati umefanyika na kuongeza wodi moja ya kulaza wagonjwa na kujenga vyoo, kuweka umeme na simu, imeongeza vifaa katika wodi ya wazazi kama ifuatavyo, vitanda viwili vya kuzalishia, vitanda viwili vya kuwapimia akina mama wajawazito na *kits* mbili za kuzalishia.

Mipango ya baadaye ni pamoja na kujenga sehemu ya wagonjwa wa nje *(OPD),* kujenga wodi ya wazazi, kujenga wodi mbili za wagonjwa (wanaume na wanawake), kuimarisha maabara na sehemu ya kutunzia madawa na kutafuta na kuajiri watumishi kulingana na Ikama.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pia nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na hayo ningependa kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna malalamiko mengi na tuhuma nyingi dhidi ya hospitali hii na siyo hii tu peke na nyingine Teule zote katika Mkoa kwamba hazitoi huduma nzuri kwa akinamama, wajawazito, watoto na hata wazee wanalipishwa fedha, lakini pia zipo lugha mbaya zinazotumika na hivyo wagonjwa wananyanyasika, je, Mheshimiwa Naibu Waziri au Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Afya, anaweza kuzitembelea hizi hospitali kuchunguza na kuona ukweli wa mambo na kukemea ili wananchi wasiendelee kunyanyasika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, inawezekana kwamba yapo malalamiko ya aina hiyo lakini tunachoweza kumshauri Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, mimi nadhani kazi hiyo inaweza ikafanyika vizuri sana katika ngazi ya Wilaya. Washirikiane na Mkuu wa Wilaya, washirikiane na Halmashauri na pia washirikiane na vyombo vingine pale ili kuhakikisha kwamba tabia hiyo si kukemewa tu lakini inakomeshwa kupitia Bodi za Afya ambazo zimeundwa karibu nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, kuhusu suala la kutembelea. Suala la kutembelea peke yake haliwezi kuwa ufumbuzi wa tatizo alilolisema, cha msingi hapa ni kama nilivyosema kwa sababu hata kama Mheshimiwa Waziri wa Afya atakuja, kama ninyi wenyewe mtakuwa hamjafanya kazi ya kukemea tabia hiyo sidhani kama tunaweza tukamsaidia sana. Kwa hiyo, tushirikiane katika ngazi hiyo nina hakika mambo haya yako ndani ya uwezo wetu.

**MHE. ANATORY K. CHOYA:**Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jitihada zote ambazo amezisema Mheshimiwa Naibu Waziri zimeishafanyika hususan katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Biharamulo inayomilikiwa na Kanisa Katoliki, zote hizo zimeshindikana; na kwa kuwa mnapoelezea matatizo ya wanaolalamikiwa kama wazee pamoja na watoto wanasema kwamba ni kukosekana kwa Waraka maalum kutoka Wizara ya Afya; je, Wizara ya Afya iko tayari kupeleka Waraka huo ili hayo malalamiko yakaweze kupungua?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama hoja ni Waraka tu tutazungumza na Wizara ya Afya na Waraka huo utapelekwa. Lakini naomba nisisitize kwamba, kwa kweli suala la kudhibiti nidhamu katika hospitali zetu za Wilaya pamoja na hizi Hospitali Teule maadam kuna hizi Bodi za Wilaya, kwa kweli hatuna sababu kabisa ya kudhani kwamba mambo haya hayawezekani katika ngazi ya Wilaya. Lakini hilo ombi tutalifikisha Wizara ya Afya na Waraka utapatikana.

Na. 291

**Vijiji Vilivyosahaulika Kwenye Mradi wa Umeme**

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mradi wa Umeme Mlalo ulikamilika mapema mwaka 2000 baada ya kuvisahau Vijiji vinne ambavyo tangu awali kabisa vilikuwa ndani ya mpango wa kupatiwa umeme miongoni mwa Vijiji vilivyokusudiwa; na kwa kuwa hadi sasa ni mwaka wa tatu tangu Uchaguzi Mkuu wa 2000 na Serikali bado iko kimya bila kuonyesha nia ya kuiondoa kasoro hiyo:-

(a) Je, wananchi wa Vijiji vya Mlesa, Zaizo, Ngazi na Mhelo waamini nini juu ya hali hiyo kwa Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi?

(b) Je, kama wananchi hawajapuuzwa, ni lini basi Serikali itawapelekea umeme ili kutimiza ule usemi wa kiswahili usemao ahadi ni deni?

(c) Je, kusogeza umeme hadi Mlesa, Zaizo, Ngazi na Mhelo itagharimu kiasi gani cha fedha za Kitanzania?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Mlesa, Zaizo, Ngazi na Mhelo havikuwekwa katika Mradi wa Umeme wa Mlalo kutokana na Bajeti iliyokuwepo wakati huo kutokutosheleza.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nawaomba wananchi wa Vijiji vya Mlesa, Zaizo, Ngazi na Mlalo waendelee kuwa na imani na matarajio kuwa nia ya Serikali ni kufikisha huduma ya umeme kwa wananchi wote yakiwemo maeneo ya Vijijini ili kuboresha hali ya maisha yao na pia kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, Serikali haijawapuuza wananchi hawa wa Vijiji vilivyotajwa na haijapuuza kuwapelekea umeme wananchi hao. Napenda nichukue nafasi hii kutamka kwamba wananchi hawa watapelekewa huduma hii ya umeme fedha zitakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, ili kusogeza huduma ya umeme hadi Mlesa, Zaizo, Ngazi na Mhelo tunahitaji kupata shilingi milioni 248.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo hayaridhishi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba nikimletea ushahidi wa kwamba Vijiji hivyo vilivyotajwa vinne vilikuwa kwenye mradi toka awali kwa maandishi ya Shirika la *TANESCO* na Wizara inayohusika; atakubali kusema hadharani kwenye mkutano huu kwamba Vijiji hivyo vilikuwepo toka mwanzo katika mradi huo na haya majibu aliyoyasema sasa hivi siyo sahihi?

Mheshimiwa Spika, pili, ni kwamba Vijiji hivyo husika vya Mlesa, Zaizo, Ngazi na Mhelo ni Vijiji ambavyo vilishiriki katika kuchangia gharama za kupeleka mradi huo Mlalo kwa kukubali mazao yao ya kahawa, miti ya mitunda na miti ya kawaida, migomba kuondolewa ambayo jumla ya gharama ilikuwa shilingi milioni 36 kwa wakati ule; je, kwa kigezo hicho peke yake Serikali na Wizara hii haioni kwamba wananchi wale wanastahili kutafutiwa hela, shilingi milioni 200 ni ndogo sana ili waweze kupata umeme kabla hatujafika mwaka 2005; je, Wizara hii haioni huruma hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi ambao walichangia au walishiriki katika mradi huu kwa kuchangia mazao au nguvu zao katika kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika. Kwa kweli huu ndiyo wito ambao tunautoa wakati hadi wakati kwamba katika maeneo ambayo usambazaji wa umeme unapita na kutokana na gharama kubwa ya usambazaji basi na wananchi nao wajitolee. Ndiyo maana katika kujibu swali la msingi nimesema kwamba, kwa kweli Serikali haijawapuuza na wala haitawapuuza. Ni ukweli tu kwamba kwa sasa hivi hizi pesa ambazo zinatafutwa bado hazijapatikana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakumbuka kwamba nilitembelea kwenye Jimbo la Mlalo na nilikuwa naye na tulikwenda sehemu hadi sehemu. Nadhani pia atakubaliana nami kwamba *TANESCO* imefanya kazi kubwa ya kusambaza umeme katika maeneo kadhaa. Kwa hiyo, hii jitihada ambayo imeanza kwa kweli itaendelezwa na katika mkutano wa mwisho na uongozi wa *TANESCO* kule Lushoto tulikubaliana kwamba na wao watajitahidi kwa kadri ya Bajeti yao inavyoruhusu wakati na Serikali inajitahidi kutafuta fedha nyingine ili kusambaza umeme sehemu hadi sehemu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tatizo siyo kuwekwa au kutokuwekwa katika orodha, tatizo kubwa ambalo nilisema hapa ni suala zima kwamba fedha hazikutosha. Inatokea kwamba kunakuwa na miradi ya kusambaza umeme na wakati inapofika katika utekelezaji fedha zinakuwa hazitoshi. Ndiyo maana nimesema umuhimu wa sasa hivi tuliokuwa nao ni wa kutafuta fedha. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miradi ya aina hiyo ya *TANESCO* kama ulivyo Mradi wa Mlalo imekuwa ni kawaida kwa *TANESCO* kutokukamilisha miradi yake inapoamua kupeleka mradi kwa mfano Mlalo inaacha na Vijiji vingine muhimu ambavyo viko karibu, matokeo yake ni kupata malalamiko.

Kama hivyo walivyofanya Mlalo ndivyo walivyofanya katika Mji wa Mashewa wakaacha Kijungumoto ambapo ni karibu hapo hapo; tabia hii ya *TANESCO* kufanya hivyo inaleta malalamiko makubwa sana kwa wananchi; je, Serikali inaweza kujisahihisha kuona kwamba mradi kama huo wa Mlalo

na kule Mashewa, yakamilishwe basi maeneo yote yale ili wananchi wasilete malalamiko na kutuletea matatizo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwa kweli Shirika la Ugavi wa Umeme *(TANESCO)* linafanya kazi kubwa ya kusambaza umeme.

Ningependa nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba fedha hizi za mradi mara nyingi zinakuwa ni fedha za ufadhili zikichangiwa kidogo na fedha za ndani. Ni kweli kunatokea kwamba fedha zinakuwa zimepungua kulingana na matatizo yanayotokea kutoka mradi unapobuniwa hadi mradi unapotekelezwa. Si tabia kwamba inapokuwa kila mradi unapotekelezwa basi lazima pawe na Vijiji ambavyo vinakuwemo katika mradi lakini havimaliziki kwa makusudi, hapana.

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Joel Bendera, kama ambavyo yeye na mimi tumezungumza mara nyingi kuhusu Vijiji vyake vinavyomhusu, kwamba tunajitahidi ili maeneo haya yaweze kupata umeme. Nami nakubali kwamba Waheshimiwa Wabunge hawa, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Joel Bendera na wengineo wanafanyakazi kubwa ya kuwawakilisha wananchi wao ili kuhakikisha kwamba Vijiji vyao vinapata umeme na sisi tunatambua hilo. *(Makofi)*

Na. 292

**Umeme Wilayani Bukombe**

**MHE. ROBERT K. MASHALA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Bukombe ni kati ya Wilaya ambazo hazina huduma ya umeme, na kwa kuwa wawekezaji wanasita kuwekeza kwenye Wilaya hiyo kwa sababu hiyo.

Je, Serikali itatekeleza lini ahadi yake ya kufunga umeme kwenye Wilaya ya Bukombe kama sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2002?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Robert Mashala, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa Wilaya 15 ambazo ziko katika mpango wa Serikali wa mwaka 2000 - 2005 wa kupeleka umeme ni Wilaya ya Bukombe katika Mji wake Mkuu Ushirombo. Tathmini ya awali iliyofanywa na *TANESCO* inaonyesha kuwa mradi wa kupeleka umeme Wilayani Bukombe utahusisha ujenzi wa kituo kikubwa cha kupunguza nguvu za umeme kutoka kilovoti 220 hadi 33 ambacho kitajengwa kwenye eneo la mgodi; ujenzi wa laini ya umeme wa kilovoti 33, uwekaji wa transforma ndogo ndogo za kusambaza umeme huo kwenye Miji/Vijiji na kuwaunganisha wateja.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huo kwa ujumla unategemewa kugharimu dola za Kimarekani milioni 16.6 ambazo ni sawa na pesa za Tanzania karibu shilingi bilioni 17.0. Majadiliano na wafadhili pamoja na wadau wengine wakiwemo *SIDA* ya Sweden na wenzetu wa Mgodi wa Kahama yaani *Kahama Mining Corporation Limited (KMCL)* kuchangia utekelezaji wa mradi huo vinaleta matumaini. Mradi huo unategemewa kutekelezwa katika awamu mbili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa kituo cha kupunguza umeme kwenye eneo la mgodi wa Kahama laini ya kilovoti 33 hadi Ilogi na Bugarama pamoja na kusambaza umeme katika nyumba za wafanyakazi wa mgodi. Awamu hii yote itagharamiwa na mgodi huu wa Kahama.

Baada ya ujenzi kukamilika Mgodi huu wa Kahama watakabidhi umiliki wa mradi wote kwa *TANESCO* ambayo itaendelea kusimamia kazi zote za uendeshaji, ukarabati na uuzaji wa umeme kwa wananchi. Makubaliano ya kutekeleza mradi huo kwa muundo huo tayari yamekwishafikiwa kati ya *TANESCO* na Mgodi wa Kahama.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili itahusisha upelekaji wa umeme kutoka kituo cha kupunguza umeme hapo Kahama kwenye mgodi hadi Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe yaani Ushirombo pamoja na usambazaji wa umeme katika Mji huo na sehemu nyingine katika Wilaya ya Bukombe. Kazi hii itagharimiwa na Serikali. Serikali sasa hivi inafanya majadiliano na *SIDA* ambayo imeonyesha nia ya kuchangia katika ujenzi huu.

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa ahadi hizi za kupeleka umeme katika Mji wa Ushirombo miaka mitatu sasa bila utekelezaji; je, Serikali itawathibitishia vipi wananchi wa Ushirombo kwamba ahadi yake inayoitoa sasa itakuwa ni ya kweli na itatekelezwa kabla ya mwaka 2005? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, gharama za kupeleka umeme kwenye Mji Mkuu wa Bukombe, Ushirombo kama nilivyosema katika jibu la msingi ni shilingi bilioni 17, ni fedha nyingi. Wastani tuliokuwa nao katika kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya mbalimbali ni kati ya shilingi bilioni 8 hadi shilingi bilioni 10. Ndiyo maana imetuchukua muda kutafuta uwezekano wa kupata fedha hizi zote na kama nilivyosema awali hivi sasa Mgodi wa Kahama unachukua awamu ya kwanza ambayo ni kubwa ya kujenga kituo hiki cha umeme na kusambaza kidogo umeme ili na sisi tuchukue kutoka pale.

Kwa hiyo, ningependa kuchukua nafasi hii kusema kwamba, tunatarajia kwamba fedha hizi ambazo tuna matumaini ya kuzipata katika majadiliano yanayoendelea, fedha hizi zitakapopatikana sasa hivi tunaweza tukasema kwamba wananchi wa Bukombe wataweza kupatiwa umeme wa uhakika kwenye Makao Makuu yao ya Wilaya.

**SPIKA:** Swali la msingi linahusu umeme wa Ushirombo sasa Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo mengine leteni maswali yenu kama mnataka.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kuniruhusu na mimi ili niweze kuuliza swali moja ndogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake hakutaja *time frame* ya majibu yake; je, haoni kwamba hajatoa matumaini yoyote kwa wananchi wa Bukombe? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nimetoa muda na muda wenyewe, kwanza muda wenyewe unatokana na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambao unatekelezwa na Serikali, ni kati ya mwaka 2000 hadi mwaka 2005 na kwa sasa tuko mwaka 2003 muda ambao tunatarajia kwamba majadiliano haya yatakwisha na kwamba fedha zitapatikana na ujenzi kama kuanza ni kati ya sasa hadi mwaka 2005 yaani mwaka 2003 hadi mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua nafasi hii kuthibitisha tena kwa wananchi wa Bukombe kwamba Serikali ina nia thabiti ya kuhakikisha kwamba Makao Makuu ya kila Wilaya ikiwemo Wilaya ya Bukombe yanapata umeme.

Na. 293

**Misitu ya Miyenze, Luande na Geita**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa misitu mizuri na mikubwa ya Miyenze iliyoko Jimboni Nyang'hwale na ile ya Luande na Geita iliyoko Jimboni Geita ni vivutio vikubwa vya utalii kwa nchi yetu na Hifadhi za Taifa:-

(a) Je, kwa sasa hivi ni nani anayevuna misitu hiyo bila huruma?

(b) Kwa kasi hiyo ya uvunaji ikichangiwa na ile ya wachimba Migodi wa *Geita Gold Mine* ambao wanang'oa milima mizuri inayozunguka Mji wa Geita ili kuchimba dhahabu; je, itachukua miaka mingapi kumaliza kabisa misitu hiyo na hivyo kuifanya Geita iwe na kivutio mbadala cha jangwa kwa ajili ya watalii?

(c) Je, Serikali imeweka mazingira gani ya kuhakikisha kuwa misitu hiyo inaendelea kuwepo na Halmashauri ya Wilaya ya Geita inafaidikaje na kuwepo kwa misitu hiyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Uvunaji endelevu wa mazao ya misitu umeruhusiwa kufanyika katika misitu hiyo kwa kuzingatia Sheria ya Misitu sura 389. Leseni za uvunaji na maelekezo yake hutolewa katika maeneo yaliyoruhusiwa kuvunwa tu. Aidha, maeneo hayo yanavunwa na wananchi wa kawaida. Hata hivyo kuna uvunaji haramu unaoendelea katika misitu hiyo.

Mheshimiwa Spika, hali hii inatokana na uchache wa watumishi katika Idara ya Misitu na Nyuki na wale wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita wanaotakiwa kusimamia na kulinda maeneo hayo. Aidha, kila inapobainika kuwepo kwa wahalifu ndani ya misitu hiyo watumishi wachache waliopo huwakamata wahalifu hao na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa Sheria.

Kwa mfano katika kipindi cha mwaka wa fedha cha mwaka 2002/2003 wahalifu 36 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani ambako walihukumiwa na kutozwa faini ya jumla ya shilingi 720,000/=.

(b) Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini ilitoa kibali cha miaka 25 cha uchimbaji madini ya dhahabu katika Msitu wa Hifadhi wa Geita baada ya msitu huo kufanyiwa tathmini ya athari kwa mazingira. Tathmini hiyo imebaini athari za uchimbaji madini katika msitu huo wa hifadhi na hatua za kuchukua kurekebisha maeneo yatakayoathirika. Hatua hizo ni pamoja na upandaji miti na ufukiaji mashimo katika maeneo yatakayochimbwa dhahabu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Mwanza inafuatilia kwa karibu maelekezo na masharti ya tathmini hiyo ya mazingira.

Aidha, hivi karibuni Idara ya Misitu na Nyuki imeandaa Mkataba wa kutiliana saini na *Geita Gold Mine* na kuhakikisha kwamba kampuni hiyo inazingatia masharti ya uchimbaji madini katika msitu huo kama yalivyobainishwa kwenye tathmini ya athari katika mazingira. Kwa upande wake, Wilaya ya Geita imeunda Kamati inayojulikana kama *District Mine Closure Committee* ambayo inasimamia urekebishaji wa mazingira unaofanywa na *Geita Gold Mine* wakati shughuli za uchimbaji zinaendelea na baada ya mgodi kufungwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa Serikali haina mpango wowote au kusudio lolote la kuigeuza Wilaya ya Geita iwe na kivutio mbadala cha jangwa kwa watalii. Mikakati niliyoeleza inaonyesha nia ya mpango juu ya jambo hili.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka Sera ya Misitu (mwaka 1998) ambayo imelenga na kutoa kipaumbele katika suala zima la ushirikishwaji wa wananchi katika kuhifadhi na kuendeleza misitu nchini. Ili kuhifadhi misitu ya Miyenze, Luande na Geita hatua zifuatazo zinachukuliwa:-

Kwanza, Halmashauri ya Wilaya ya Geita imetunga sheria ndogo ndogo za kudhibiti uvunaji holela kwenye misitu hiyo na Kamati za Mazingira zimeanzishwa katika baadhi ya vijiji vinavyozunguka misitu hiyo ili kusaidia kulinda na kuhifadhi misitu hiyo kwa kushirikiana na watumishi wa Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Wilaya ya Geita kufaidika na kuwepo kwa misitu hiyo, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa misitu ya Miyenze na Luande inamilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Geita ambayo bila shaka inanufaika na mapato na faida nyingine ambazo nimezitaja wakati wa kutoa maelezo kuhusu swali hili.

Msitu wa Hifadhi wa Geita unamilikiwa na Serikali Kuu na Halmashauri ya Wilaya ya Geita inatoza ushuru *(cess)* kwa mazao ya misitu yanayovunwa kutoka katika msitu huo.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba upo uvunaji haramu wa misitu hiyo kwa sababu walinzi ni wachache je, yuko tayari kunipa kibali nikawaambie Sungusungu wanaozunguka misitu hiyo na wenye uwezo wa kulinda walinde misitu hiyo kuisaidia Serikali?

(b) Kwa kuwa Wilaya ya Geita inao wakazi wengi zaidi ya 700,000 na kwa kuwa nyenzo pekee wanaotegemea ni kuni na mkaa na hivyo lazima wakate miti, Serikali inasemaje kuhusu kuisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Geita kuweka programu endelevu ya kupanda miti katika Kata kame za Kalumwa, Busolwa, Nyang'hwale, Bukwimba, Kafita, Mwingilo, Kakola ili kuepukana na tatizo la jangwa ambalo linaikabili Wilaya hii?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Sungusungu, napenda kumweleza Mheshimiwa Mbunge ni vizuri suala hili likazungumzwa katika Halmashauri husika ili maamuzi yapatikane.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la programu, jana wakati Waheshimiwa Wabunge wakichangia kulikuwa na mawazo kwamba pengine katika kila eneo la kijiji kuwe na shamba la miti kwa ajili ya kuni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani pamoja na taasisi mbalimbali. Nafikiria kwamba ni muhimu Waheshimiwa Wabunge wakawahamasisha wananchi na kutokana na Sheria ya Misitu tuliyoipitisha jambo hili linawezekana.

Na. 294

**Mahitaji ya Samaki na Soko Lake**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa tunalo soko la Kimataifa la kuuzia samaki; na kwa kuwa bado mahitaji ya walaji wa samaki hayajakidhi haja hasa kutokana na uvuvi duni wa vyombo vinavyotumika katika shughuli hiyo:-

(a) Je, kwa nini taasisi inayoshughulikia uvuvi *TAFICO* haikai pamoja na taasisi inayoshughulikia uvuvi Zanzibar *(ZAFICO)* ili kuunda mtaji wa pamoja na kuboresha uvuvi kwa kutumia vyombo vya kisasa ili kuwezesha kuvua samaki kwa wingi na kunufaisha soko la walaji?

(b) Je, Serikali inaweza kutoa takwimu ya mahitaji ya samaki kwa mwezi na yana upungufu wa kiasi gani?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kufuatia uamuzi wa Serikali wa kujitoa katika kuendesha shughuli za kibiashara, Shirika la Uvuvi la Taifa Tanzania Bara *(TAFICO)* ni moja ya mashirika ya umma ambayo yako katika orodha ya mashirika yanayobinafsishwa

kupitia Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma. Aidha, sehemu ya shirika hilo ambayo ilikuwa inaendesha shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria tayari imekwisha binafsishwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uamuzi huo wa Serikali ni vigumu kuanza tena taratibu za kuunganisha mashirika hayo mawili kwa lengo la kuunda mtaji wa pamoja. Serikali inahimiza wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza kwenye Ukanda wa Uchumi *(Exclusive Economic Zone)* kwa lengo la kuvua samaki kwa wingi ili kutosheleza mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhimiza uzalishaji samaki zaidi, Wizara yangu imeandaa mwongozo wa uwekezaji katika sekta ya uvuvi. Mwongozo huo umeainisha maeneo ambayo yanafaa kuwekeza.

(b) Mheshimiwa Spika, takwimu za uvuvi zinaonyesha kuwa kila Mtanzania anakula samaki wastani wa kilo 10.5 kwa mwaka. Takwimu hizo zinaonyesha kuwa mahitaji ya samaki kwa nchi nzima ni zaidi ya tani 357,000 kwa mwaka, sawa na tani 29,750 kwa mwezi. Samaki wanaovuliwa kwa ajili ya chakula hapa nchini ni wastani wa tani 301,913 kwa mwaka. Kiasi hicho cha samaki kinachovuliwa kina upungufu wa wastani wa tani 55,087 kwa mwaka sawa na tani 4,591 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, inakusudiwa kuwa ifikapo mwaka 2005 wastani wa ulaji wa samaki kwa kila Mtanzania utaongezeka hadi kilo 20 kwa mwaka. Hii inamaanisha kuwa ili kukidhi mahitaji ya walaji wa samaki uzalishaji wa samaki kwa mwaka unapaswa ufikie tani 660,000.

Mheshimiwa Spika, ili kuziba upungufu huo, Wizara yangu inaendelea kuwashauri na kuwahamasisha wananchi kuendeleza ufugaji samaki pamoja na wawekezaji kuwekeza katika ufugaji samaki wa kibiashara. Aidha, wananchi watafundishwa njia na mbinu bora za kuhifadhi samaki na mazao ya uvuvi ili kuondokana na upotevu wa samaki waliokwisha kuvuliwa. Hii itaongeza kiasi cha samaki kinachoweza kutumiwa na wananchi kwa chakula.

**MHE. ZUHURA KHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Serikali ina mpango wowote wa kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo ili waweze kuchangia mahitaji ya samaki katika soko hilo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa msisitizo wa Serikali uko katika wavuvi wadogo wadogo na hata jana nilipokuwa nawasilisha Bajeti yangu nilisema kwamba utaratibu maalum unawekwa kwa ajili ya kuwa na Mfuko wa kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo lakini niliongeza kusema pia kwamba Wizara ya Fedha kutakuwa na mfuko ambao utadhamini wavuvi wadogo wadogo.

**SPIKA:** Kwa niaba ya wavuvi wa Mafia, Mheshimiwa Abdulkarim Shah. *(Kicheko)*

**MHE. ABDULKARIM ESMAIL H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kutokana na utafiti uliofanywa na Kampuni moja ya Utafiti ambapo ilifanya utafiti wa mafuta katika Ukanda wa Bahari, utafiti wao ulionyesha kwamba wameonekana samaki wengi sana katika Visiwa vya Mafia kuliko Bahari ya Kanda ya Kaskazini.

Kutokana na hali hiyo, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wavuvi wa maeneo husika kuvua samaki kwa wingi kuliko ilivyo sasa ambapo wavuvi kutoka nje ya maeneo hayo wanakuja kumaliza uchumi huo na hata hivyo bado samaki wanaonekana hawatoshelezi soko, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wavuvi wa maeneo hayo ili waweze kuvua ili kuimarisha soko hilo la samaki?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, katika eneo hili la maji marefu *(Exclusive Economic Zone)* ni sehemu ambayo kuna samaki wengi lakini ni samaki wa muda yaani inawezekana kwa wakati huu kukawa na samaki Tanzania wakati mwingine wakawa katika nchi nyingine.

Kwa hiyo, ndio maana tunasisitiza ama wavuvi wakubwa kwa sababu hapa lazima uvuaji utakuwa kwa wavuvi wakubwa na uwekezaji mkubwa kwa sababu unahitaji meli kubwa. Tunasema wavuvi kutoka nje waje lakini wale wavuvi wakubwa wa ndani ya nchi waweze kushiriki katika eneo hili. Kama hawajavuliwa kwa wakati ule ambapo wako Tanzania, samaki hawa hatutaweza kuwapata

Mheshimiwa Spika, labda ningelieleza Bunge lako Tukufu kwamba sasa hivi tuna programu ile ambayo tunaiita ya *monitoring* na *surveys* kwa msaada wa *European Union* ambapo tunafanya utaratibu wa kuangalia kwa kutumia ndege wale wavuvi ambao wanavua bila leseni katika maeneo hayo.

Na. 295

**Serikali Kufuta Ada ya Sekondari**

**MHE. OSCAR T. MLOKA (k.n.y. MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Shule za Msingi sasa zimeboreshwa na kuwezesha wanafunzi wengi wanaojiunga na Shule za Sekondari kiasi kwamba wazazi wamefikia kushindwa kulipia ada ya Sekondari.

Je, Serikali haioni kuwa sasa wakati umefika wa kuleta Muswada Bungeni ili kujadili umuhimu wa kufutwa kwa ada ya Sekondari?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christopher Wegga, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali wa kufuta ada katika Shule za Msingi unatokana na ukweli kwamba Elimu ya Msingi ni haki ya kila mtoto na ni nyenzo muhimu katika azma yetu ya kufuta umaskini miongoni mwa wananchi wote na kwa sababu Elimu ya Msingi ina faida kwa jamii *(social/public benefits)* kubwa zaidi kuliko faida za kibinafsi *(private benefits).*

Katika ngazi nyingine za elimu zinazofuata baada ya Elimu ya Msingi faida za binafsi *(private benefits)* zinatoa marejesho mazuri kwa wanufaikaji kuliko faida kwa jamii. Kutokana na ukweli huo, Watanzania katika ujumla wetu tumeamua kuigharamia kwa sehemu kubwa Elimu ya Msingi kwa watoto wetu wote kupitia bajeti ya Serikali ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanaipata hata wale ambao ni yatima au wazazi wao ni maskini ili kama Taifa tuanze kuwa na rika mpya zijazo ambazo hazina maskini wa kupindukia kutokana na wote kuwa na Elimu ya Msingi iliyo bora.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo katika ngazi nyingine za elimu hapa nchini, Serikali bado inabeba sehemu kubwa ya gharama za elimu. Ada inayotozwa kwa Shule za Sekondari za Serikali inachangia sehemu ndogo tu ya gharama za elimu hiyo. Kwa Sekondari za Serikali za Kutwa ada ni shilingi 40,000/= ambayo ni sawa na asilimia 9.4 tu ya gharama ya utoaji wa elimu hiyo ambayo ni shilingi 425,392/= kwa mwanafunzi kwa mwaka.

Hata hivyo, Serikali imeanzisha utaratibu wa kuwasaidia watoto wa familia maskini na watoto yatima ambapo mwaka 2002/2003 zilitengwa shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya watoto 6,019 sawa na asilimia 10.83 ya wanafunzi walioteuliwa kuingia Kidato cha Kwanza 2003. Utaratibu huu utaendelea pia katika mwaka huu wa 2003/2004 ambapo zimetengwa shilingi bilioni 2.5 kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo niliyoyatoa wazo la Mheshimiwa Mbunge la kutoa Elimu ya Sekondari bure kwa wote yaani hata kwa wale wenye uwezo wakiwemo matajiri halikubaliki. Inabidi walio na uwezo wailipie kwa sababu inazo faida za kiuchumi za moja kwa moja kwa anayeipokea elimu na kwa kuzingatia pia kuwa uwezo wa Serikali wa kugharamia elimu katika ngazi zote ni mdogo.

Kwa hiyo, Serikali haioni itakuwa busara kutoa Elimu ya Sekondari bure hata kwa familia wenye uwezo wa kuchangia angalau kidogo katika elimu ya watoto wao.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa kati ya kati ya asilimia 7 hadi 9 ya wanafunzi wanaomaliza shule za Msingi katika nchi yetu ndio tu walio na nafasi ya kwenda Sekondari na kwa kuwa katika uwiano halisi asilimia 34 ya

wanafunzi wote wa Kenya wanasoma Sekondari, asilimia 29 ya Waganda wanasoma Sekondari na asilimia 18 ya nchi maskini kama Malawi wanaweza kusoma Sekondari, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba wakati umefika wa kuwa *Universal Secondary Education* na kwamba wale ambao ni matajiri wailipie elimu hii kwa njia ya kodi za kawaida ambazo wananchi wa Tanzania wanatozwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ni asilimia ndogo tu ya watoto wetu wanaofaulu kwenda katika Sekondari wanapata nafasi ya kwenda Sekondari. Kwa hiyo, tunalo tatizo la ufinyu au uhaba wa Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, lakini lazima tuanze kufanya jambo la kwanza huwezi kuanza kuzungumzia Elimu ya Sekondari kwa Wote *(Universal Secondary Education)* wakati bado hata hujatoa Elimu ya Msingi kwa Wote. Kwa hiyo, katika hatua ya mwanzo, mpango ule MMEM utatufikisha kwenye kutoa Elimu ya Msingi kwa watoto wetu wote.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya Bajeti nililitaarifu Bunge hili kwamba tunaandaa mpango ambao unalenga kupeleka asilimia 50 ya watoto wetu Sekondari. Unapata asilimia 100 ndani ya Elimu ya Msingi ndio tuna-*focus* sasa kwenda Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kusema kwamba katika kufanya haya yote tusiue miongoni mwa wananchi wetu ule moyo wa kupanua elimu kwa njia za kujitegemea kwa sababu ukweli ni kwamba hivi sasa tuna shule zisizo za Serikali 450 na karibu nusu ya watoto wetu wanaopata Elimu ya Sekondari wako katika shule hizo na ndio maana tunafikia hata hiyo asilimia ndogo. Kwa hiyo, pamoja na juhudi za Serikali tuendelee kuhimiza juhudi za wananchi wenyewe kupanua elimu ya Sekondari. Watoto wanaosoma katika sekondari hizo za private wanalipiwa ada kubwa kuliko hata ile ya shilingi 40,000/= ambayo inalipwa katika Sekondari za Serikali.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wanaojitokeza kuanzisha Shule za Sekondari na wanaolipia watoto wao ada katika shule hizo za Sekondari.

Na. 296

**Ufutaji wa Hatimiliki za Mashamba Arumeru**

**MHE. MATHEW TAKI OLE-TIMAN (k.n.y. MHE. ELISA D. MOLLEL)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imefuta Hati Miliki ya baadhi ya mashamba yaliyotelekezwa katika Wilaya ya Arumeru kwa nia ya kuwasaidia wananchi wasio na ardhi na kwa kuwa baadhi ya mashamba hayo yameshagawiwa kwa baadhi ya wananchi na kutakiwa kulipia fidia ya shilingi 172,030 kwa ekari moja, kiwango ambacho wananchi wengi wanashindwa kulipa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wasio na uwezo kupata ardhi hiyo kwa kiwango watakachomudu?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elisa Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu la kulipa fidia ni la msingi katika utwaaji wa ardhi. Pale ambapo ardhi inayotwaliwa ni kwa manufaa ya umma basi Serikali inawajibika kumlipa fidia yule mmiliki ambaye ardhi yake imetwaliwa.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo ardhi imetwaliwa ili wananchi waweze kumilikishwa basi mwenye wajibu wa kulipa fidia ya eneo alilopewa ni mwananchi mmoja mmoja au kijiji au Halmashauri ya Wilaya kulingana na nani atakayemilikishwa eneo hilo. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Serikali imetwaa maeneo katika Jiji la Dar es Salaam kwa manufaa ya umma ili kupima viwanja. Serikali imetumia fedha za mkopo ili kulipa fidia maeneo yote iliyoyatwaa.

Kwa kuwa madhumuni ya kutwaa maeneo hayo yalikuwa ni kupima viwanja kwa ajili ya makazi na huduma; mwananchi yeyote anayetaka kiwanja inabidi arudishe gharama ya fidia ambazo Serikali imelipa kwa niaba yake ili Serikali iweze kurejesha mkopo huo katika muda uliowekwa. Ni kwa kutumia utaratibu huo tu ndiyo Serikali imeweza kupata ardhi.

Mheshimiwa Spika, pale Wizara inapopokea mapendekezo ya kufuta miliki za mashamba kutoka Halmashauri, Wizara inachukua jukumu la kuwakumbusha jukumu la kulipa fidia kwa aliyekuwa mmiliki wa shamba hilo. Kwa mashamba yaliyotwaliwa Wilayani Arumeru, uthamini ulipofanyika ilibainika kuwa kiwango cha fidia kinachodaiwa ni shilingi 172,030/= kwa ekari moja. Halmashauri ya Wilaya, ililijua hilo tangu mwanzo.

Mheshimiwa Spika, kama kiwango hicho ni kikubwa na kimesababisha wananchi walio wengi kutoweza kukimudu, Halmashauri ya Wilaya inalo jukumu la kufikiria tatizo lao na kuhakikisha kuwa wananchi wasio kuwa na uwezo wa kulipa fidia wanasaidiwa kupata ardhi.

Na. 297

**Tatizo la Panzi Kunuka**

**MHE. ASHA A. NGEDE** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Kondoa ina tatizo sugu la panzi kunuka na Serikali inalifahamu:-

(a) Je, mikakati ya Serikali kuhusiana na tatizo hilo imefikia wapi?

(b) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge hili kuwa ni wakati gani itakuwa imelitatua tatizo hilo na kuwaondolea kabisa kero wananchi wa eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Ngede, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mikakati inayotekelezwa na Serikali kudhibiti panzi kunuka ni pamoja na kufanya uchunguzi wa kina katika maeneo ya mlipuko Wilayani Kondoa. Wataalam wa Wizara ya Kilimo na Chakula, wakishirikiana na wakulima katika vijiji vilivyoathirika, wamekuwa wakimchunguza mdudu huyu ili kujua mzunguko wa maisha yake ili kubaini wakati mzuri wa kumdhibiti kwa ufanisi.

Pia kumdhibiti panzi kunuka kwa kutumia madawa ya kemikali. Kwa mfano mwezi wa Septemba, 2002, wataalam kutoka Wizara ya Kilimo na Chakula walitembelea vijiji 11 na kuona panzi kunuka katika hatua mbalimbali za ukuaji na kuwanyunyuzia dawa aina ya *Fenitrothion.* Lita 1450 za dawa hiyo zilitumika kuangamiza wadudu hao katika eneo la hekta 5,800 za mihogo zilizoathirika.

Mheshimiwa Spika, pia kumdhibiti kwa kupalilia mashamba kwa kuwa panzi kunuka hushamiri zaidi katika mashamba yenye magugu mengi na udhibiti wa panzi kunuka kibaiolojia umeonyesha mafanikio katika nchi za Benin na Nigeria. Wizara ya Kilimo na Chakula katika miezi ya Februari na Mei, 2003 iliwasiliana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo *(FAO)* ili kumpata bingwa wa udhibiti kibaiolojia wa wadudu hao atakayeshirikiana na wataalam wetu kumdhibiti. Shirika hilo limeonyesha nia ya kutusaidia. Aidha, Wizara itapeleka wataalam wawili Afrika ya Magharibi mwezi wa Septemba, 2003 kujifunza mbinu za kumdhibiti panzi kunuka kibaiolojia.

(b) Mheshimiwa Spika, visumbufu vya mimea na mazao vinaweza kudhibitiwa lakini ni mara chache sana kuviangamiza. Kwa mfano, panzi kunuka huzaliana porini. Ili kumuangamiza kabisa mdudu huyu ni lazima kutafuta na kuharibu mazalio yake nchi nzima, jambo ambalo haliwezekani. Hata hivyo,

Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, itaendelea kutumia njia mbalimbali za udhibiti zitakazohakikisha mdudu huyu hazaliani kufikia kiwango cha mlipuko.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika Mkoa wa Dodoma ikiwa ni pamoja na Wilaya za Kondoa na Kongwa tatizo hili la panzi kunuka na viwavi jeshi ni kubwa sana na hujitokeza mwaka hadi mwaka na ufumbuzi wake unategemea dawa ambazo ni hodhi upande wa Serikali, je, Serikali itakubaliana nami kwamba ipo haja sasa dawa hizi za kudhibiti panzi kunuka, viwavi jeshi na visumbufu vingine vya mimea zikawa zinapatikana kule kule katika maeneo ya Wilaya ili kuwa rahisi zaidi kudhibiti matatizo haya?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, tungependa kufanya hivyo lakini tukumbuke kwamba dawa hizi ni sumu na sio lazima kila mwaka mdudu atokee katika maeneo hayo. Kwa hiyo, sio busara sumu hizo zikawekwa kwenye Wilaya zikazagaa zagaa na kuhatarisha usalama wa wananchi. Tutahakikisha kila mara dawa hizi ziko karibu na wataalam ambao wako Mkoani, Kitaifa na katika Kanda.

Na. 298

**Mchango wa Sekta ya Kilimo katika Kupunguza Umaskini.**

**MHE. MGANA I. MSINDAI (k.n.y. MHE. LEONARD M. SHANGO)** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati Serikali ikijibu swali Na.115 katika Mkutano wa Tisa wa Bunge kuhusu vigezo vinavyotumika kulinganisha hali halisi ya umaskini uliokithiri kati ya Mikoa na Mikoa, ilionekana kuwa katika Tanzania kati ya Mikoa yote, Mkoa wa Singida unaongoza kwa umaskini; na kwa kuwa Serikali inaelewa fika kuwa sekta ya kilimo ni sekta pekee itakayoweza kuchangia kwa kiwango kikubwa kupunguza umaskini katika Mkoa wa Singida.

(a) Je, ni hatua gani zimechukuliwa za makusudi za kuwekeza katika miradi ya kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya kilimo cha umwagiliaji ili kufanikisha mageuzi muhimu katika kilimo cha Mkoa wa Singida?

(b) Je, tangu mwaka 2000 hadi 2005 Serikali itawekeza katika miradi mingapi ya kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya kilimo cha kumwagilia na miradi hii inakadiriwa kuwa ya thamani kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Kutokana na mipango mizuri ya kusimamia kilimo katika Mkoa wa Singida chini ya utaratibu wa kutumia mbinu shirikishi jamii, Mkoa wa Singida una nafasi kubwa ya kuondokana na umaskini haraka sana kwa ikilinganishwa na Mikoa mingi nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka wa 2001/2002, Serikali kupitia mradi wa Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani *(Participatory Irrigation Development Programme - PIDP)* ilikarabati *scheme* nne Mkoani Singida zilizokuwa zimeharibiwa na mvua za *El-Nino* za msimu wa 1997/98.

Mheshimiwa Spika, *scheme* hizo ni Chikuyu (hekta 170), Lusilile (Hekta 100), Saranda (hekta 150) na Tyeme-Masagi (hekta 200). Jumla ya wakulima 888 wanafaidika kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani katika simu hizo.

(b) Katika kipindi cha 2000 na 2005, Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani *(PIDP)* itajenga *scheme* sita za umwagiliaji maji kwa njia ya majaruba na mabwawa madogo katika Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, *scheme* hizo ni Mtiwe (hekta 165), Msemembo (hekta 250) na Udimaa (hekta 410) ambazo ziko katika Wilaya ya Manyoni na Masimba (hekta 200), Mlandala (hekta 250) na Mwangeza (hekta 151) katika Wilaya ya Iramba.

Mheshimiwa Spika, aidha, mabwawa madogo manne yatajengwa katika *scheme* za Tyeme/Masagi, Kirondadaatari, Msisigiri, Masimba na Mwangeza. Ujenzi wa *scheme* hizo utafanywa kwa fedha za Serikali pamoja na mkopo kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo *(IFAD).*

Mheshimiwa Spika, gharama za ujenzi wa *scheme*na mabwawa niliyotaja unakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1.8. Serikali katika mwaka wa 2003/2004 imetenga shilingi milioni 400 kwa ajili ya kujenga mabwawa ya Tyeme/Masagi na Kirondadaatari.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa maeneo aliyoyataja ya *scheme* hayahusishi kabisa Wilaya ya Singida Vijijini na hasa Singida Kusini.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali kupitia Wizara hii ina mpango gani wa skimu kama hizo kwa eneo la Singida Vijijini na hasa Singida Kusini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, miradi niliyoitaja inahusiana zaidi na programu ya *IFAD* lakini inawezekana kabisa kwa kuwa ulileta matatizo ya maji ya umwagiiaji katika Singida Vijijini tunategemea tutalishughulikia kwa Mifuko mingine hasa katika ule mpango kamambe wa umwagiliaji. Lakini hata hivyo tutafuatilia nini umeleta, tuone nini kinaweza kufanyika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamemalizika, tunaendelea.

Waheshimiwa Wabunge wakati maswali yanaendelea aliingia mgeni wa Kimataifa katika *Gallery* napenda kumtambulisha sasa, yeye ni Mwakilishi wa hapa nchini wa Mfuko wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa Unaoshughulikia Masuala ya Idadi ya Watu *(United Nations Population Fund),* Mheshimiwa Tefery Seyum, yupo pamoja na maofisa wake. *(Makofi)*

Matangazo ya vikao vya leo Kamati mbili zimepanga kukutana Kamati ya kwanza ni Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa nne na nusu asubuhi katika chumba Namba 54, yaani baada ya kumsikiliza Waziri anayewasilisha hoja yake leo.

Kamati ya pili, ni Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Dr. Shija, anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa tano asubuhi hii kwenye chumba Namba 56.

Mwisho wa matangazo Katibu endelea na *Order Paper.*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004**
**Ofisi ya Makamu wa Rais**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge hili Tukufu baada ya kuzingatia taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Anne Makinda,

taarifa inayohusu Ofisi ya Makamu wa Rais na baada ya kuzingatia taarifa hiyo, sasa likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kuwa Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira imejadili utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha uliopita na kuchambua matumizi na makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2003/04 na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Aidha, Kamati ilitembelea baadhi ya maeneo ya miradi ya mazingira na kupunguza umaskini kwa lengo la kujifunza na kuona matatizo yaliyopo ili iweze kuishauri Ofisi ya Makamu wa Rais ipasavyo. Kamati imetoa maoni na ushauri wa masuala ya kuzingatia katika kuboresha utendaji kazi.

Nawashukuru sana wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira chini ya uongozi thabiti wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anne Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini, kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais Fungu 26 na 31.

Mheshimiwa Spika, naliomba Bunge hili sasa likubali kupitisha taarifa ya Kamati na kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mwaka 2003/04.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwa hotuba zao za mwanzoni mwa kikao hiki cha Bunge. Hotuba hizo zimefafanua sera za jumla za uchumi na Bajeti na kuweka mwelekeo na hatua ambazo Serikali inachukua kuimarisha uchumi pamoja na utoaji wa huduma muhimu za jamii.

Adiha, napenda kumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, kwa hotuba yake ambayo imetoa malengo yatakayowezesha usimamizi thabiti wa utekelezaji shughuli mbalimbali za Serikali kwa mwaka ujao wa fedha wa 2003/2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitoe shukrani za Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia shughuli za Taifa za kuwawezesha wananchi kujiondolea umaskini pamoja na mimi mwenyewe kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulikia maliasili na mazingira.

Kamati hii chini ya uongozi shupavu wa Mheshimiwa Anne Makinda, Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi la Njombe Kusini, Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib wa Jimbo la Amani na Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati hiyo. Siyo tu wametoa ushauri na maelekezo ya kuboresha utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuzingatia bajeti ya 2002/2003 na 2003/2004 na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote bali pia Kamati imetupa ushirikiano ambao kwetu sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais tunaona faraja kubwa.

Tunawashukuru wanakamati wote na tunachokiomba ni kuzidisha ushirikiano kwa lengo la kuyaelewa matatizo yaliyopo na yale yatakayojitokeza ili kwa pamoja tuyatafutie ufumbuzi katika kutekeleza kwa vitendo dhana ya viongozi watumishi wa Watanzania kwa manufaa ya nchi yetu na watu wake wote.

Aidha, Kamati kutembelea baadhi ya maeneo ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ni utekelezaji wa azma ya kuishauri na kuisimamia Serikali kwa Mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote 19 walioapishwa tarehe 10 Juni, 2003 baada ya kushinda na kuchaguliwa kuingia katika Bunge hili Tukufu kutokana na uchaguzi mdogo uliofanyika katika Majimbo 19 ya nchi yetu Mei 18, 2003.

Aidha, napenda kuvipongeza Vyama ambavyo vimefanikiwa kupata ushindi katika Majimbo mbalimbali ya uchaguzi. Napenda kumpongeza kwa namna ya pekee Mbunge wa Kigoma Kusini,

Mheshimiwa Edward Ndeka. Natekeleza msemo wa mcheza kwao hutunzwa maana anatoka Chama changu cha Mapinduzi na mkoani kwangu Kigoma.

Nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Ali Said Juma na Mheshimiwa Karim Salim Othman Mbunge wa Chambani, kwa kutaka ushirikiano katika masuala ya msingi Kitaifa kwani masuala ya msingi Kitaifa hatupaswi kuyawekea mabango kulingana na tofauti za itikadi za Vyama vyetu vya Siasa. Nawashukuru na kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichopita, nchi yetu ilipoteza jumla ya Majaji siita. Jaji Madina Muro, Jaji Eustance Katiti, Jaji Kulwa Masaba, Jaji Luhekelo Kyando, Jaji Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Francis Nyalali hapo tarehe 3 Aprili, 2003 na juzi tu, Jaji wa Mahakama ya Rufani, Kahwa Lugakingira. Wote ni mashahidi wa mchango wao mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema, peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais ina majukumu mahsusi ya Kitaifa ya kumsaidia na kumshauri Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala yote ya nchi kwa ujumla. Mheshimiwa Makamu wa Rais ndiye mwenye dhamana ya kuratibu shughuli za Muungano, kuratibu juhudi za kuondoa umaskini nchini, kusimamia sera ya mazingira, pamoja na kuratibu shughuli za mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* na Jumuiya za wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa napenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha 2002/2003 mafaniko na matatizo yaliyojitokeza katika kipindi hicho na matarajio katika kipindi cha mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu unaingia katika karne ya 21 ukiwa umeshatimiza miaka 39. Hii inatokana na juhudi na upeo mkubwa wa Waasisi wa Muungano wetu Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, ambao waliweka misingi imara ya Muungano huu. Aidha, jitihada za dhati za Serikali zetu mbili za kuhakikisha kuwa mambo ambayo bado ni kero katika utekelezaji wa masuala ya Muungano yanashughulikiwa na yanatatuliwa na juhudi zinafanywa kuyatatua. Tunawashukuru viongozi wa Kitaifa, Wabunge na wananchi wote kwa ujumla kwa juhudi wanazofanya ili kuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia malengo ya Taifa ya kuimarisha Muungano, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kutimiza jukumu lake la Kikataiba la kuratibu masuala ya Muungano kwa kufuatilia utekelezaji wa masuala haya ikiwa ni pamoja na kuratibu ushirikiano katika masuala mbalimbali ya sekta za Muungano pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi yanayohusu masuala ya Muungano yaliyotolewa na Serikali zetu kwa mwaka wa 2002/2003.

Aidha, ofisi ilitayarisha vikao vya wadau wa Muungano ambapo madhumuni makubwa ya vikao hivyo ilikuwa ni kubadilishana uzoefu, kujadili masuala mbalimbali ya ushirikiano katika sekta husika na kushauriana ili kuimarisha Muungano. Sekta mbalimbali zilishiriki katika vikao hivyo ikiwa ni pamoja na sekta za Mazingira, Biashara, Fedha, Maliasili, Afya, Mawasiliano na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, masuala ya fedha ikiwa ni pamoja na gawio la asilimia 4.5 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na faida ya Benki Kuu inayotolewa kwa Serikali ya Muungano yalijadiliwa. Aidha, Mheshimiwa Rais ameshafanya uteuzi wa wajumbe wa Tume ya pamoja ya Fedha ili kusimamia masuala haya kwa pamoja. Ni matumaini yetu kuwa masuala yote yaliyokuwa kero katika sekta ya fedha yatafanyiwa kazi na yatapatiwa ufumbuzi. Benki Kuu ya Tanzania baada ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kufungua akaunti yake katika benki hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala la utafiti na takwimu halikuachwa nyuma kwani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano wa Tanzania zimeendelea kushirikiana na kusaidiana katika kuendeleza na kukuza sayansi na teknolojia kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia ambapo wataalam kutoka pande zote mbili wamekuwa wakishirikiana kwa ajili ya kukuza na kuendeleza vipaji na ugunduzi. Aidha, pande zote za Muungano zilishiriki kikamilifu katika sensa ya watu iliyofanyika mwezi Agosti, 2002.

Mheshimiwa Spika, Serikali zote mbili zilichukua hatua ya kutekeleza muafaka ulifikiwa baina ya Vyama vya *CUF* na CCM ili kuleta amani na utulivu nchini kama ilivyopendekezwa na Vyama hivyo na kuridhiwa na Serikali zetu. Aidha, majadiliano bayana yanaendelea kuhusu maeneo mengine ili kulinda na kudumisha Muungano.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano kati ya Serikali zote mbili umezidi kukua na ni wa kuridhisha kuanzia ngazi ya viongozi wa Kitaifa hadi wananchi wa kawaida. Viongozi wamekuwa wakishirikiana katika masuala mbalimbali mfano, sherehe za Mapinduzi Zanzibar, Uhuru na Jamhuri na zile za Muungano.

Aidha, pande zote zinashiriki katika warsha, semina na makongamano kwa pamoja. Kwa mfano, hivi majuzi tu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliialika SMT katika mkutano wa wafadhili wa Mpango wa Kupunguza Umaskini Zanzibar ambapo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia kuondoa umaskini alihudhuria.

Aidha, ushirikiano umeongezeka kati ya Wizara zisizo za Muungano na SMZ na SMT. Wizara hizo ni kama Afya na Ustawi wa Jamii (SMZ) na Afya (SMT), Fedha na Uchumi (SMZ) na Fedha, Mipango na Ubinafsishaji (SMT), Mawasiliano na Uchukuzi SMT na SMZ, Maliasili na Utalii, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Ushirika na Masoko (SMT) na Kilimo Maliasili, Mazingira na Ushirika (SMZ), Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto (SMZ) na Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto (SMT), Elimu, Utamaduni na Michezo (SMZ) na Elimu na Utamaduni (SMT) na kadhalika ambapo ratiba imepangwa kukutana angalau mara mbili kwa mwaka na tayari vimefanyika vikao kumi na vitano.

Mheshimiwa Spika, katika vikao hivyo masuala mbalimbali ya ushirikiano yalijadiliwa ikiwa ni pamoja na kuainisha sera, kubadilishana utaalam na ushirika wa SMZ katika mikutano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano kati ya wananchi wa Bara na Visiwani yameboreka kwa kuongeza uhusiano wa kisiasa, kimichezo na kiutamaduni. Pamoja na Muungano wetu kuzidi kukua na kuimarika, uzoefu wetu unatuonyesha kwamba kudumishwa kwake kunahitaji juhudi za pande zote mbili, kuaminiana na kuendeleza ushirikiano wa kindugu kati ya raia wa pande zote mbili za Muungano. Subira, uvumilivu na kusikilizana havina budi kupewa kipaumbele. Wajibu wa kulinda na kudumisha Muungano wetu ni wa kila Mtanzania awe wa Tanzania Bara au Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, pia iliendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za hifadhi ya Mazingira katika kipindi cha mwaka jana. Kama Waheshimiwa Wabunge wanavyofahamu, mazingira ni suala pana na nyeti, lenye umuhimu mkubwa na linafungamana na lengo la Taifa la kuondoa umaskini. Katika kutekeleza sera ya Taifa ya Mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano na Wizara mbalimbali, taasisi za Serikali na taasisi za hiari na wadau wengine wengi iliandaa na kuendeleza utekelezaji wa mikakati, programu na miradi ya hifadhi ya mazingira katika Mikoa na Wilaya mbalimbali nchini. Ushirikiano wa Kimataifa na Kikanda kwa nchi za Afrika Mashariki, Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika na Bara la Afrika kwa ujumla, kuhusu mazingira uliimarishwa. Aidha, shughuli nyingi za uhamasishaji wa umma kuhusu hifadhi ya mazingira ziliendeshwa kote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa 2002/2003, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu utekelezaji wa programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria inayotekelezwa na nchi za Tanzania, Kenya na Uganda kwa kushirikiana. Progamu hii inalenga katika kuhifadhi mazingira ya Bonde la Ziwa Victoria.

Katika kipindi cha mwaka 2002/2003, mradi ulitekeleza shughuli mbalimbali kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka jana wakati nawasilisha hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Shughuli hizi ni kupambana na kudhibiti magugu maji kwa kutumia mbawakavu na nguvu kazi ya wananchi. Hadi sasa asilimia 95 ya magumu maji yamedhibitiwa

Mheshimiwa Spika, mradi pia ulishughulikia uvuvi endelevu katika Ziwa Victoria kwa kuboresha baadhi ya mialo inayopokea samaki. Hatua hizi zimeiwezesha Tanzania kuingia katika kundi A la nchi

zinazouza samaki katika soko la Umoja wa Ulaya. Aidha, vikundi 511 vya ulinzi wa raslimali vilivyokwishaundwa kwenye mialo vimechangia sana katika kudhibiti uvuvi haramu. Aidha, utafiti wa bailojia na bioanuwai ya samaki na viumbe wengine umefanyika katika mito, mabwawa, Ziwa Victoria na maziwa mengine madogo madogo. Utafiti huu umebaini, pamoja na mambo mengine, kuwa samaki wa asili waliohofiwa kutokuwepo katika Ziwa Victoria bado wapo katika maziwa madogo madogo na mito. Aidha, mkazo umeendelea kuwashirikisha wananchi kuhifadhi misitu ya asili na upandaji miti. Miche ipatayo milioni 1.4 imepandwa katika Wilaya za Bunda, Musoma na Tarime.

Mheshimiwa Spika, katika kuhifadhi maeneo chepechepe, programu ya Ziwa Victoria imefanya shughuli mbalimbali kama inavyoelezwa chini ya shughuli za Baraza.

Mheshimiwa Spika, utafiti kuhusu ubora wa maji ya Ziwa Victoria uliendelea kufanyika katika vituo 126 vilivyomo katika Ziwa Victoria, mito, visiwa na mashamba. Utafiti huu umebaini kuwa ukiachia mbali maeneo yaliyoko kando kando ya Ziwa Victoria maji ya Ziwa hili katika maeneo mengine hayajaathirika na bado ni bora kwa matumizi ya binadamu.

Aidha, mradi uliendelea kuelimisha wananchi waishio katika Bonde la Ziwa Victoria, wadau na wananchi wengine kwa jumla kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira na rasilimali ya bonde hili kwa kutumia redio, luninga, vipeperushi, machapisho ya vitabu katika nyanja mbalimbali na tovuti *(www.lvemp.org).* Baadhi ya wananchi katika Wilaya unakotekelezwa mradi wameshirikishwa katika kutekeleza miradi midogo midogo katika sekta ya elimu, maji, afya, usafi wa mazingira, uvuvi na barabara fupi fupi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha wa 2003/2004 mradi utaendelea kutekeleza shughuli mbalimbali zilizomo katika mpango wa kazi ambazo ni kudhibiti magugu maji kwa kuzalisha mbawakavu wapatao milioni 50 kwenye vituo 12 na kuwaeneza katika sehemu mbalimbali ambako magugu maji yanachipuka na kwenye maeneo korofi. Utafiti kuhusu ubora wa maji katika vituo 126 vilivyokwishajengwa katika Ziwa Victoria, maziwa madogo madogo, mito, visiwa na mashamba utaendelea kutekelezwa.

Aidha, mradi utaendeleza shughuli za uvuvi endelevu kwa kutoa mafunzo ya mbinu bora za uvuvi na kuhifadhi samaki wakati wa kuwauza, ulinzi dhidi ya uvuvi haramu kwa kushirikiana na vikundi 511 vya ulinzi wa rasilimali. Pia mradi utaendelea na utafiti wa bailojia na bioanuwai ya samaki na viumbe wengine katika Ziwa Victoria, maziwa madogo madogo, mito na mabwawa. Mradi unategemea kupanda miti ipatayo milioni moja.

Aidha, mradi utaendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi waendelee kuhifadhi misitu ya asili, maeneo yenye ardhi owevu na kuzuia mmomonyoko wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikisha wananchi mradi unategemea kujenga miradi midogo midogo. Aidha, mradi utafuatilia ukamilishaji wa miradi midogo midogo ipatayo 13 ambayo haijakamilka. Mwaka huu wa fedha wa 2003/2004 ni wa mwisho katika Awamu ya Kwanza ya Programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria. Kwa kuelewa kuwa uboreshaji wa mazingira ya Ziwa Victoria pamoja na vita dhidi ya umaskini haviwezi kufanikiwa katika kipindi hiki kifupi cha mradi, Serikali zetu za Afrika Mashariki zinajadiliana na Benki ya Dunia na wafadhili wengine kutayarisha na hatimaye kutekeleza Awamu ya Pili ya mradi huu kwa pamoja kwa upeo wa muda mrefu. Inategemewa kuwa Awamu ya Pili italenga katika maendeleo ya uchumi na hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka jana, maandalizi ya miradi ya kutekeleza programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika yalifanywa kwa ushirikiano na nchi jirani za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia. Miradi miwili iliandaliwa kuhusu hifadhi ya bonde la Ziwa na udhibiti wa maji machafu katika Halmashauri ya Mji wa Kigoma/Ujiji.

Aidha, Mkataba wa pamoja wa hifadhi na uendelezaji wa bonde la Ziwa Tanganyika ulikamilishwa na kuwekwa sahihi na nchi zote nne kwenye kikao cha Mawaziri wa Mazingira huko Dar es Salaam tarehe 12 Juni, 2003. Maandalizi ya miradi hii na ukamilishaji wa Mkataba vilifanywa kwa ushirikishwaji wa wadau. Warsha tatu za Kitaifa za kujadili awamu mbalimbali za maandalizi ya

miradi ya utekelezaji wa programu zilifanyika, ikiwemo warsha moja ya siku mbili iliyofanyika Mjini Kigoma.

Ningependa kuushukuru uongozi wa Mikoa ya Kigoma, Rukwa na Tabora kwa michango yao mikubwa katika kukamilisha maandalizi ya miradi hii. Mkutano wa kujadili rasimu ya Mkataba wa ushirikiano ukihusisha wawakilishi wa Mikoa husika na Wizara na Taasisi nane za Serikali ulifanyika Jumla ya dola za Marekani 701,000 zilitumika, kwa nchi zote nne, kwa kazi hii ikiwa ni msaada kutoka Mfuko wa Mazingira wa Dunia, dola 595,000 na Benki ya Maendeleo ya Afrika, dola 106,000.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha taratibu za kuridhia Mkataba wa ushirikiano wa Ziwa Tanganyika ikiwa ni pamoja na maandalizi ya rasimu za nyaraka za Baraza la Mawaziri, kufanya upembuzi yakinifu wa miradi iliyoandaliwa mwaka 2003/2004, kutoa mafunzo kwa wataalam wa Serikali za Mitaa na wa Vijiji kuendesha warasha za kukuza weledi kuhusu masuala ya mazingira, kuanza maandalizi ya mipango ya matumizi ya ardhi, kuajiri watumishi na wataalam wa miradi na kununua vifaa vya miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka 2002, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Kituo cha Uzalishaji Bora Tanzania inasimamia utekelezaji wa mradi wa usafi wa mazingira katika shughuli za viwanda vya uzalishaji mali na utoaji huduma. Mradi huu wa miaka mitano ulianza mwaka 1999 na una madhumuni ya kujenga uwezo wa viwanda na wadau wengine nchini katika teknolojia na mbinu za uzalishaji bora zenye kupunguza au kuzuia uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za viwanda.

Katika kipindi cha mwaka 2002/2003 Kituo kiliendeleza mafunzo na madhihirisho ya mbinu za uzalishaji bora kwa viwanda 11 na taasisi tatu katika Manispaa ya Tanga. Semina ya Kitaifa kuhitimisha programu ilifanyika mwezi Desemba mwaka 2002 Mjini Tanga na ilihudhuriwa na washiriki wapatao 60 kutoka viwandani na taasisi mbalimbali za Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro na Tanga. Taarifa mbalimbali za uzalishaji bora zilikusanywa na kugawiwa kwa walengwa kupitia vyombo vya habari, vipeperushi na jarida la kituo. Vile vile kituo kimekamilisha utengenezaji wa filamu ya uzalishaji bora katika baadhi ya viwanda nchini.

Aidha, kituo kwa kushirikiana na *UNEP* kiliendesha semina mbili Zanzibar na kukuza ufahamu juu ya uzalishaji Bora na Matumizi Endelevu na utumiaji wa dhana ya uzalishaji bora katika utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira. Washiriki wapatao 60 walitoka Idara za Serikali, viwandani na taasisi mbalimbali nchini kote, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Kituo cha Uzalishaji Bora Tanzania kiliratibu utekelezaji wa programu ya Kitaifa ya kudhibiti matumizi ya kemikali zinazomomonyoa ukanda wa *Ozone*. Shughuli zifuatazo zilifanyika, warsha kuhusu udhibiti wa biashara ya kemikali hizo ilifanyika Arusha mwezi Aprili, 2003 kwa maofisa wa forodha na wadau wengine kutoka nchi za Afrika Mashariki, takwimu za uagizaji na matumizi ya kemikali hizo kwa mwaka 2000 na 2001 zilikusanywa na ripoti iliandaliwa.

Baadhi ya mitambo ya viwanda vinavyotengeneza bidhaa za *sponge* vya *Panafrica Enterprises* na *Plyfoam Tanzania* ilipokelewa, kufungwa na kufanyiwa majaribio na mafunzo yalitolewa kwa wafanyakazi. Aidha, Kituo kilifuatilia ukamilishaji wa vifaa vya kufundishia mafundi mchundo kutoka Ujerumani na kufanya maandalizi ya mafunzo kwa ajili ya mafundi hao. Vifaa vilikamilika mwezi Juni, 2003. Rasimu ya kanuni za Sheria za kudhibiti kemikali zinazochangia kuharibu ukanda wa ozoni iliboreshwa. Aidha, mapendekezo ya kukipa Kituo cha Uzalishaji Bora Tanzania hadhi ya kisheria yaliandaliwa na kujadiliwa na wadau mbalimbali kwenye warsha iliyofanyika mwezi Machi, 2003. Mapendekezo hayo sasa yanafanyiwa kazi kwa lengo la kukipa kituo hicho hadhi ya kisheria mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, shughuli zitakazofanyika ni pamoja na kupokea, kukusanya, kuandaa na kugawa taarifa za usafi wa mazingira na maendeleo endelevu ya viwanda kwa walengwa kupitia vyombo vya habari na jarida la kituo, kutayarisha na kugawa majarida na

vipeperushi kwa wadau mbalimbali kwa lengo la kukuza uelewa na kutangaza shughuli za Kituo, kufanya tathmini ya uzalishaji bora na ufanisi wa matumizi ya nishati katika sekta za viwanda na huduma hususan mahoteli, kujenga uwezo wa viwanda kuhusu uandikaji wa maombi ya mikopo ya kuwekeza katika miradi inayopunguza uzalishaji taka kutoka taasisi za fedha na mifuko ya maendeleo ya mazingira iliyoanzishwa na programu ya Miji endelevu, kuratibu uanzishwaji wa mfumo wa kugharamia uwekezaji katika mbinu za kupunguza uzalishaji taka, kuandaa na kuendesha kongamano juuy a uzalishaji bora kwa walengwa kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, kufuatilia utekelezaji wa dhana ya uzalishaji bora katika viwanda na kuandaa na kuendesha semina za kukuza ufahamu juu ya dhana hii.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge hili Tukufu mwaka 2002, Serikali ilitia saini Mkataba wa Kimataifa wa Stockholm unaohusu udhibiti wa kemikali zinazodumu muda mrefu sana katika mazingira. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais ilibuni mradi na kupata fedha kiasi cha dola za Marekani 344,000 kutoka Mfuko wa Mazingira wa Dunia ili kutayarisha Mpango wa Taifa wa utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

Kukusanya taarifa na takwimu zinazohusu vyanzo vya kemikali, kiasi kinachotumika hapa nchini na usimamizi wake, tathmini ya madhara kwa binadamu na mazingira. Wataalam 16 kutoka Idara za Serikali na taasisi nyingine za Serikali na mashirika yasiyo ya Kiserikali walishiriki katika zoezi la ukusanyaji wa takwimu na kufanya tathmini ya athari za kemikali hizo nchini.

Aidha, sera na sheria mbalimbali za sekta husika zimepitiwa na kufanyiwa uchambuzi katika mnasaba wa usimamizi wa kemikali hizi. Sekta hizo ni kilimo, afya, nishati, viwanda na Serikali za Mitaa. Taarifa na takwimu zilizokusanywa zilijadiliwa katika warsha ya wadau iliyofanyika Dar es Salaam mwishoni mwa mwezi Mei, mwaka 2003. Maoni yaliyotolewa na wadau yalitumika kuboresha taarifa hizo kwa ajili ya kuandaa Mpango wa Taifa wa Utakelezaji wa Mkataba wa Stockholm. Washiriki walitoka Idara za Serikali, Jumuiya za wenye Viwanda, Taasisi za Elimu ya Juu, Mashirika yasiyo ya Serikali na vyombo vya habari.

Aidha, katika kipndi hicho vifaa vya ofisi ya mradi na vya kufanyia utafiti vilinunuliwa. Vile vile mafunzo kwa wataalam wanaoshiriki katika utekelezaji wa mradi yalitolewa. Katika kufanikisha shughuli hizi kiasi cha dola za Marekani 100,000 zilitumika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/04, shughuli zifuatazo zitatekelezwa:-

Kufanya uchambuzi wa masuala yenye kipaumbele katika utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm na kuandaa ripoti ya uchambuzi, kuandaa mikakati na mpango wa kudhibiti madhara ya kemikali hizo na kuendesha warsha mbili za wadau, mikutano ya Kamati ya ushauri ya mradi na kukamilisha taratibu za kuridhia Mkataba wa Stockholm.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mradi huu, Ofisi ya Makamu wa Rais inasimamia utekelezaji wa mradi wa kutayarisha takwimu za kemikali zisizooza aina ya *Polychlorinated Biphenyls* na vifaa vinavyotumia kemikali hizo kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika. Mradi huu ni wa mwaka mmoja na umeanza kutekelezwa mwezi Mei, mwaka 2003.

Lengo la mradi ni kuhamasisha na kukuza jitihada zinazofanywa chini ya Mikataba ya Stockholm, Basel na Rotterdam katika kujenga uwezo wa kusimamia kemikali na vifaa vinavyotumia kemikali aina ya *PCBs* ili kuweka mikakati ya pamoja ya kulinda mazingira na afya ya binadamu dhidi ya athari za kemikali hizo. Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira *(UNEP)* limetoa kiasi cha dola za Marekani 653,000 kwa nchi zote za *SADC* kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Tanzania itatumia dola za Marekani 44,000 kutekeleza shughuli za mradi.

Katika kipindi cha mwaka 2002/03, shughuli zilizofanyika ni kuandaa mpango wa utekelezaji na maeneo ya kipaumbele ya utafiti wa kemikali hizi na kutoa mafunzo kwa wataalam kuhusu ukusanyaji wa takwimu za kemikali na vifaa vinavyotuma kemikali hizo.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2003/2004, ukusanyaji takwimu utaendelea kufanyika katika maeneo teule, uchunguzi wa kikemia wa kiasi cha kemikali aina ya *PCBs* kwenye vifaa mbalimbali vya umeme utafanyika, itaandaliwa ripoti ya hali ya matumizi ya kemikali hizo hapa nchini na mikutano ya Kamati ya Ushauri itafanyika. Vile vile warsha za Kanda ya Afrika kwa nchi za *SADC* zitafanyika kujadili matokeo ya mradi na kuweka msimamo wa pamoja kuhusu utekelezaji wa majukumu ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako Tukufu linavyofahamu mwezi Aprili, mwaka 1993, Tanzania iliridhia Mkataba wa Basel. Mkataba huu unahusu udhibiti wa taka zenye sumu baina ya nchi na nchi. *(The Basel Convention on the Control of Transboundary Movements of Hazardous Wastes and Their Disposal).* Mkataba huu wa mwaka 1989 umeweka taratibu za Kimataifa za kudhibiti usafirishaji na utupaji wa taka za hatari baina ya nchi zinazotengeneza taka za aina hii na zile zinazopokea kwa madhumuni ya kurudufu au kuziteketeza.

Lengo la Mkataba huu ni kuzuia madhara kwa mazingira na afya ya binadamu yanayoweza kusababishwa na taka hizi. Marekebisho ya Mkataba ya mwaka 1995 yanazuia nchi zilizoendelea kupeleka taka za aina hii katika nchi zinazoendelea. Mwaka 2002 Bunge lako Tukufu liliridhia marekebisho haya.

Aidha, katika mkutano wa nchi wanachama wa Mkataba uliofanyika 1995 iliamuliwa kuanzishwa kwa vituo vya Kanda vya Mafunzo na uenezaji wa teknolojia. Kwa Bara la Afrika, nchi ya Senegal ilichaguliwa kuanzisha kituo kwa ajili ya nchi zinazozungumza Kifaransa, Misri kwa nchi zinazozungumza Kiarabu na Afrika Kusini kwa ajili ya nchi zinazozungumza Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, madhumuni makuu ya vituo hivi ni kutoa mafunzo na kueneza teknolojia kwa nchi wanachama wa Mkataba ili kujenga uwezo wa kitaalam wa kusimamia taka hatari kama inavyoelekezwa katika Mkataba. Kituo cha Afrika Kusini kwa nchi zinazozungumza Kiingereza kilianza kufanya kazi mnamo mmwezi Julai, 2000, ingawaje bado hakijazinduliwa rasmi. Tanzania pamoja na Uganda, Zambia, Nigeria na Afrika Kusini ni wajumbe wa muda katika Kamati ya Wataalam inayoratibu uanzishwaji wa Kituo hiki huko Pretoria. Kamati ilianza kazi yake mwezi Septemba, 1999. Katika mkutano wa Sita wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Basel ilikubalika kuwa kituo hiki kisajiliwe chini ya sheria za Kimataifa *(Inter-Governmental Organizations)* ili kiwe na hadhi ya Kimataifa. Kwa wakati huu kituo kinaendesha shughuli zake kwa ufadhili wa *DANIDA* na Serikali ya Afrika Kusini. Aidha, Dr. John Mbogoma, Mtanzania ni Afisa Mkuu wa Kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizofanywa na kituo kwa kipindi cha 2002/2003 ni pamoja na kuendesha warsha na mafunzo kuhusu usimamizi wa taka za hatari kwa maafisa wa Bandari, Forodha, Idara na Taasisi za Serikali na kutoa mafunzo kuhusu usimamizi wa taka za hospitalini na jinsi ya kuandaa miradi inayoweza kuvutia uwekezaji katika teknolojia zenye kudhibiti athari za taka za sumu.

Mheshimiwa Spika, nchi mbalimbali za Afrika zimenufaika na mafunzo hayo. Nchi hizo ni Afrika Kusini, Eritrea, Ethiopia, Gambia, Ghana, Kenya, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Nigeria, Rwanda, Sierra Leone, Seychelles, Tanzania, Uganda, Zambia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 20003/2004, kituo kinatarajiwa kuandikishwa rasmi chini ya sheria za Kimataifa. Shughuli kuu zitakazofanyika ni pamoja na kuandaa programu ya mafunzo kwa wadau mbalimbali juu ya usimamizi wa taka za sumu kwa sekta ya afya, viwanda na usafiri, kuimarisha ushirikiano na programu za Kimataifa na za Kikanda za mikataba ya mazingira *(Multilateral Environmental Agreements Programs)* na kuweka misingi endelevu ya uendeshaji wa Kituo kuhusu fedha na soko la kituo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amependekeza kuweka kodi ya kiwango cha asilimia 15 kwenye mifuko ya plastiki inayoagizwa toka nje na inayotengenezwa hapa nchini. Madhumuni ya kodi hii ni kupunguza madhara kwa afya na mazingira kutokana na kuzagaa kwa taka za mifuko hiyo katika miji mingi. Tatizo la kuzagaa kwa mifuko ya plastiki ni kero kubwa mijini na linaongezeka siku hadi siku. Baadhi ya maeneo ya Vijijini yameanza kukumbwa na tatizo hili. Kuweka kodi katika bidhaa za

mifuko ya plastiki ni hatua muhimu itakayopunguza uingizaji holela wa mifuko hii na vile vile itasaidia kuongeza kasi ya upatikanaji wa mifuko mbadala ambayo tayari imeanza kupatikana maeneo ya Mijini.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Miji itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kupanua shughuli za urudufu taka za aina mbalimbali. Tayari Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda *(UNIDO)* linakamilisha taratibu za kuanzisha kituo cha taka-rejea katika Jiji la Dar es Salaam. Kituo kinatarajiwa kuanza kazi mwezi Desemba mwaka 2003. Kituo kitafanya shughuli za kutenganisha taka za plastiki na taka nyingine, kuzisafisha, kuyeyusha na kutengeneza malighafi itakayouzwa kwa viwanda vinavyotengeneza bidhaa za plastiki nchini. Kituo kitashughulikia pia taka za karatasi. Jiji la Dar es Salaam linatoa kiasi cha tani 2300 za taka ngumu kwa siku. Inakadiriwa kuwa tani 42 kati ya kiasi hicho ni taka za plastiki. Serikali ya Norway kwa kupitia *UNIDO* imetoa kiasi cha Dola za Marekani 400,000 ili kujenga kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu mradi wa kuimarisha usimamizi na hifadhi ya mazingira ya Tarangire, Ziwa Manyara na Ugalla. Madhumuni ya mradi huu ni kukuza ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za hifadhi ya mazingira na kujenga uwezo wa vijiji na Serikali za mitaa, sekta binafsi na mashirika yasiyo ya Kiserikali katika kupanga na kutekeleza shughuli za hifadhi na uendelezaji wa mazingira katika maeneo yao.

Katika kipindi cha 2002/2003, Ofisi ya Makamu wa Rais iliandaa mafunzo ya siku mbili yenye lengo la kuhamasisha, kuelimisha na kujenga uwezo wa watendaji wa Serikali za mitaa kuhusu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira, matatizo ya mazingira na wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, warsha hii ilihusisha washiriki 100 wakiwemo Mameya, Wakurugenzi wa Manispaa na miji, Wenyeviti wa Halmashauri na Wakurugenzi Watendaji kutoka Wilaya 45 ambao zimo kwenye awamu ya pili ya utekelezaji wa programu ya uboreshaji wa shughuli za Serikali za Mitaa *(Local Government Reform Programme).* Shughuli nyingine zilizofanyika ni ujenzi wa kituo kimoja cha kupokea wageni *(visitors center)* Tarangire na uboreshaji wa miundombinu katika hifadhi za Taifa za Tarangire na Manyara na kuanza uandaaji wa mbinu za kiuchumi kwa ajili ya hifadhi ya mazingira *(Environmental Economic Instruments).*

Aidha, katika kipindi cha 2002/2003, Ofisi ya Makamu wa Rais ilikamilisha ripoti ya pili ya Mkataba wa Bioanuwai kwa kushirikiana na wataalam mbalimbali kutoka Idara za Serikali, Vyuo Vikuu Tanzania Bara na Zanzibar. Ripoti inaelezea utekelezaji wa Mkataba huu katika maeneo ya bioanuwai ya misitu na bioanuwai ya mazingira ya pwani.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, chini ya mradi wa hifadhi ya mazingira ya Tarangire, Ziwa Manyara na Ugalla, miundombinu itaimarishwa na kuendelea na tafiti mbalimbali za ekolojia katika hifadhi ya Tarangire na Manyara, kituo kimoja cha kupokea wageni kitajengwa hifadhi ya Manyara, mafunzo yataendeshwa kwa wafanyakazi wa *TANAPA* na jamii zinazozunguka hifadhi za Tarangire, Manyara na Ugalla, jamii itashirikishwa katika kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi *(land use planning)* na warsha za mafunzo kwa ajili ya viongozi wa Serikali za Mitaa zitaandaliwa katika Wilaya 38 ambazo zimo katika awamu ya tatu ya utekelezaji wa programu ya uboreshaji wa shughuli za Serikali za Mitaa. Shughuli nyingine ni kukamilisha uandaaji wa mbinu za kiuchumi kwa ajili ya hifadhi ya mazingira. Aidha, Mpango na Mkakati wa Taifa wa Hifadhi ya Bioanuwai *(National Biodiversity Strategy and Action Plan )* utakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002, Ofisi ya Makamu wa Rais ilikamilisha maandalizi ya mradi wa pamoja kuhusu hifadhi ya mazingira ya bonde la Ziwa Nyasa kwa ushirikiano wa nchi za Malawi na Msumbiji. Mradi unalenga kudhibiti uharibifu na kuendeleza hifadhi na matumizi ya maliasili ya bonde hili kwa njia ya ushirikishwaji wa wananchi. *GEF* walikubali kugharamia mradi huu kwa kiasi cha dola za Marekani 350,000 kwa shughuli za mradi kwa upande wa Tanzania na Msumbiji. Tunatarajia kwamba katika kipindi cha mwaka huu, fedha zitapatikana na mradi utatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Ziwa Jipe katika Wilaya ya Mwanga na mpakani na nchi jirani ya Kenya limekuwa na umuhimu mkubwa kwa wananchi wa pande zote mbili hususan katika kuwapatia kitoweo aina

ya samaki, maji kwa ajili ya mifugo yao na wanyamapori ambao ni raslimali ya wananchi wa nchi zote mbili. Vile vile Ziwa Jipe ni muhimu kwa kilimo kidogo cha umwagiliaji maji na humwaga maji yake katika Bwawa la Nyumba ya Mungu. Ziwa Jipe linakabiliwa na tatizo kubwa la magugu maji aina ya *Cyperus papyrus* na *Typha domingensis.* Magugu hayo yameathiri kwa kiasi kikubwa mazingira ya eneo hilo na kukwamisha shughuli za kiuchumi na kijamii za wakazi wa Vijiji vinavyozunguka Ziwa hilo. Maji ya Ziwa Jipe huingia kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu ambalo ni rasilimali muhimu kwa utoaji umeme, uvuvi na huduma za maji kwa wakazi wa maeneo hayo na mifugo yao. Mazingira ya bwabwa hilo nayo yameharibika sana kutokana na shughuli mbalimbali zisio endelevu za wananchi waliopo kwenye Bonde la Mto Ruvu na Mto Pangani. Mnamo mwezi Januari 2003 nilitembelea maeneo hayo ya Ziwa Jipe na Bwawa la Nyumba ya Mungu ili kuona hali halisi ya uharibifu wa mazingira hayo.

Aidha, tarehe 01 hadi 03 Juni, 2003 nilifuatana na Waheshimiwa wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mazingira na Maliasili, kuwaonyesha hali halisi. Kamati ilitoa maelekezo ya hatua za haraka kudhibiti uharibifu na uchafuzi wa mazingira katika maeneo hayo. Kufuatia maelekezo hayo, Ofisi ya Makamu wa Rais inaandaa mradi kuhusu hifadhi ya mazingira ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa mnamo mwezi Februari mwaka huu katika mkutano wa kumi Bunge lako Tukufu lilipitisha azimio la kuridhia Itifaki ya Cartagena kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia kwa mazingira na afya ya binadamu.

Lengo la Itifaki hii ni kuweka msimamo wa pamoja wa Kimataifa wa usimamizi wa kutosha wa usairishaji na matumizi salama ya mazao yatokanayo na bioteknolojia ya kisasa ili kuzuia madhara yanayotokana na matumizi ya mazao hayo kwa mazingira na afya ya binadamu. Kama Waheshimiwa Wabunge wanavyofahamu, Itifaki hii imetokana na Mkataba wa Bioanuwai na inaweka utaratibu wa kupeana taarifa, usafirishaji na matumizi ya viumbe na bidhaa zitokanazo na bioteknolojia ya kisasa yenye uwezekano wa kuhatarisha mazingira, hususan hifadhi ya bioanuwai.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, kufuatia Bunge hili Tukufu kutoa idhini na Tanzania kuridhia Itifaki hii, Ofisi ya Makamu wa Rais ilibuni mradi wa Kitaifa kuhusu usalama kwa mazingira na afya ya binadamu katika matumizi ya mazao ya bioteknolojia na kuuwasilisha *UNEP* kwa ufadhili. Nafurahi kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba Mfuko wa Dunia wa Mazingira *(GEF)* ulikubali kutoa msaada wa shilingi milioni 168 kugharamia mradi huu. Kamati ya Kitaifa ya uendeshaji wa mradi ilianzishwa na mpango wa utekelezaji wa mradi kwa mwezi Januari hadi Desemba 2003 ulipitishwa.

Aidha, maandalizi ya utekelezaji wa shughuli za mradi yalifanyika na shughuli mbalimbali zilitekelezwa. Uchunguzi ulifanyika kuhusu matumizi ya bioteknolojia nchini, sheria zilizopo zinazohusu matumizi ya bioteknolojia ya kisasa; mapitio ya mifumo iliyopo inayohusu tathmini, usimamizi na udhibiti wa athari za bioteknolojia kwa mazingira, athari za matumizi ya bioteknolojia ya kisasa kwa shughuli za kibiashara, uanzishwaji wa mfumo wa Kitaifa wa kubadilishana taarifa na mapitio ya mifumo ya matumizi salama ya bioteknolojia katika nchi za Kenya, Uganda, Namibia na Phillipines.

Mheshimiwa Spika, warsha ya Kitaifa ilifanyika ambapo wadau mbalimbali waliainishwa, mpango wa utekelezaji wa mradi ulifanyiwa mapitio na aina mbalimbali za matumizi ya bioteknoljia pia ziliainishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004, shughuli zifuatazo zitatekelezwa:-

Uchambuzi wa matokeo ya utafiti, kukamilisha uanzishwaji wa kituo cha utunzaji na ubadilishanaji taarifa, uchambuzi wa maeneo muhimu ya utekelezaji wa Itifaki ya Cartagena, maandalizi ya vipeperushi na njia nyingine za kukuza weledi kwa umma, kuendesha mafunzo kwa wataalamu na wadau kuhusu tathmini na udhibiti wa athari za matumizi ya bioteknolojia ya kisasa kwa mazingira, kuandaa rasimu ya mfumo wa Kitaifa wa usimamizi wa matumizi ya biotenolojia na kuandaa taarifa mbalimbali za utafiti.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi. Mapitio ya miradi

mitano iliyowasilishwa na taasisi za Serikali, vyuo vya utafiti na mafunzo, mashirika yasiyo ya Kiserikali na sekta binafsi yalifanyika na kupendekeza ufadhili kutoka *GEF* na vyanzo vingine vya fedha.

Miradi hiyo ilihusu matumizi ya nishati jadidifu *(renewable),* nishati mbadala na kuimarisha uwezo wa asasi mbalimbali kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi. *GEF* imekubali kugharimia programu ya kuhifadhi mazingira ya bonde la Mto Kagera, mradi wa kujenga uwezo wa Taifa katika kutekeleza Mikataba ya Mabadiliko ya Tabianchi, kuenea kwa hali ya jangwa na ukame na Hifadhi ya Bioanuwai na miradi ya matumizi ya nishati jadidifu na nishati itokanayo na mionzi ya jua.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwaka jana nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika Mkutano wa Saba wa nchi wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Novemba 2001 Marrakesh - Morocco, ambapo Tanzania ilishiriki, iliamuliwa kuwa nchi maskini sana duniani zisaidiwe katika kuandaa mipango ya Kitaifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Hivyo katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Ofisi ya Makamu wa Rais ilibuni mradi kuhusu Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi *(NAPA)* na kuwasilisha *GEF* kwa ufadhili.

Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tayari *GEF* kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia mazingira *(UNEP)* imeidhinisha kiasi cha dola za Marekani 200,000 na maandalizi ya utekelezaji wa mradi huu yameanza.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais imetayarisha na kukamilisha ripoti ya Taifa ya utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi na kuiwasilisha Sekretarieti ya Mkataba huu. Vile vile nakala 1,500 za miongozo ya jinsi ya kuandaa miradi ya muda mfupi, miradi ya muda wa kati na miradi ya muda mrefu kwa ajili ya ufadhili wa *GEF* imetafsiriwa katika Kiswahili. Nakala hizo zimegawiwa kwa wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Katika hatua za awali za utekelezaji wa miradi ya Itifaki ya Mkataba huu, miradi mitatu imeandaliwa na sasa inatafutiwa ufadhili.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, shughuli zifuatazo zitatekelezwa:-

Maandalizi ya Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi, kuhamasisha asasi mbalimbali na kufanya warsha za kukuza uelewa kuhusu miradi ya kupambana na ongezeko la hewa-joto, kuandaa na kukamilisha mwongozo wa utekelezaji wa miradi ya *Clean Development Mechanism,* kuendesha mafunzo kwa wataalam zaidi ya 50 kuhusu uandaaji na utekelezaji wamiradi ya *CDM* na kupendekeza miradi ya kutekeleza mpango wa Taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuchambua na kupitisha miradi ya *CDM.*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Ofisi ya Makamu wa Rais ilitarajia kupata fedha kutoka Shirika la Kimataifa la Kilimo *(IFAD),* Jumuiya ya Ulaya na Sekretariat ya *SADC* kwa ajili ya utekelezaji wa baadhi ya maeneo katika programu ya kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa.

Kutokana na matatizo ya kifedha katika vyombo hivi kwa kipindi hicho, msaada huo haukupatikana. Katika juhudi za kutafuta fedha za utekelezaji wa miradi chini ya programu hii, katika kipindi hiki, miradi miwili iliandaliwa. Mradi wa kwanza unahusu kuhuisha masuala ya uharibifu wa ardhi na kuenea kwa hali ya jangwa katika mipango na mikakati ya kuondoa umaskini. Mradi huu umepitishwa na *Global Mechanism* ambacho ni chombo kinachotafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mkataba kuhusu kuenea kwa hali ya jangwa.

Aidha, Tanzania ni moja ya nchi mbili zilizoteuliwa na *SADC* kuandaa na kupendekeza miradi ya ushirikishwaji wa vijana katika shughuli za hifadhi ya mazingira kwa ufadhili wa Serikali ya Finland. Mradi huo uliandaliwa na kuwasilishwa kwa ufadhili. Vile vile napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kufuatia uamuzi wa Baraza la Mfuko wa Mazingira duniani *(GEF Assembly)* kwenye kikao chake cha mwezi Oktoba, 2002 kilichofanyika Beijing, China, miradi ya kukabiliana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame sasa ni moja ya maeneo yanayoweza kufadhiliwa na Mfuko huu, tofauti na ilivyokuwa kabla ya hapo.

Katika kipindi cha 2003/2003, Ofisi ya Makamu wa Rais itafuatilia upatikanaji wa misaada kwa ajili ya kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa kutoka vyanzo vyote hivi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kufuatia kukamilika kwa awamu ya kwanza ya mradi wa mfumo wa kitaasisi na kisheria *(ILFEMP),* Serikali mnamo mwezi Desemba, 2002 ilipitisha muundo husishi wa kitaasisi wa usimamizi wa mazingira nchini. Serikali imethibitisha nafasi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kuendelea kushughulikia majukumu ya kisera na usimamizi wa jumla wa utekelezaji wa sheria, miongozo na masuala ya Kimataifa kuhusu mazingira, kama Sera ya Taifa ya Mazingira inavyoelekeza.

Aidha, mfumo husishi unatambua nafasi ya Wizara zinazosimamia sekta mbalimbali kuendelea kuwajibika kwa majukumu ya hifadhi ya mazingira katika maeneo yao, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kusimamia utekelezaji wa sheria ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira *(enforcement),* kufanya mapitio ya tathmini ya miradi kuhusu athari zake kwa mazingira *(EIA)* na kufuatilia *(monitoring/ auditing)* utekelezaji wake, kama inavyoelekezwa katika Sera ya Taifa ya Mazingira.

Mwisho, lakini sio kwa umuhimu, mfumo unathibitisha nafasi ya Serikali za Mitaa kuwajibika kwa majukumu ya hifadhi na usafi wa mazingira kama inavyoelekezwa chini ya sheria ya Serikali za Mitaa. Ili kuleta ufanisi kiutendaji, mfumo husishi unahitaji kuundwa kwa Kamati za Mazingira na kuteuliwa kwa waratibu wa mazingira katika ngazi ya Kijiji hadi Wilaya, mshauri wa mazingira katika ngazi ya Mkoa na waratibu wa mazingira katika Wizara mbalimbali.

Aidha, patakuwa na Kamati ya Kitaifa yenye uwakilishi wa wadau mbalimbali. Maandalizi ya sheria mama ya mazingira yameanza na warsha za wadau mbalimbali zimeanza kufanyika na zitaendelea. Endapo utekelezaji utakwenda kama ilivyokusudiwa, rasimu ya sheria itakamilika na Muswada wa sheria mama ya mazingira utawasilishwa Bungeni katika kipindi cha mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika kuhamasisha hifadhi ya mazingira katika shughuli za uchimbaji madini, Mheshimiwa Rais alianzisha tuzo kwa migodi na kwa wachimbaji wadogo. Mshindi mwaka jana ilikuwa kampuni ya *Resolute (T) Limited* Nzega, Tabora na Rais alikabidhi tuzo hiyo tarehe 12 Septemba, 2002.

Kutokana na uzoefu wa mwaka jana, Kamati ya uteuzi inayosimamia zoezi hili imefanya mapitio ya mwongozo wa mashindano haya kwa kushirikiana na Baraza la wachimbaji madini. Kwa sababu hii na kwa kuzingatia gharama na muda wa maandalizi, mashindano haya hayakuweza kuendeshwa kabla ya mwezi Juni, 2003 kama ilivyotarajiwa. Hata hivyo maandalizi ya mashindano kwa mwaka huu yameshaanza. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge hasa kutokana katika maeneo ya machimbo ya madini washirikiane na maafisa madini wa Kanda kuhamasisha wachimbaji wa madini kushiriki katika mashindano haya.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoliarifu Bunge lako Tukufu mwaka jana, katika kikao chake cha Desemba, 2000, Baraza la Umoja wa Mataifa liliazimia kufanya tathmini ya utekelezaji wa agenda 21 kwa kipindi cha miaka kumi kuonyesha mafanikio, matatizo na programu ya utekelezaji kwa miaka ijayo. Mkutano huu *World Summit for Sustainable Development* ulifanyika tarehe 26 Agosti hadi 4 Septemba, 2002 Johannesburg, Afrika Kusini. Lengo kuu la Mkutano huo lilikuwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa makubaliano ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu mazingira na maendeleo uliofanyika Rio de Janeiro, Brazil mwaka 1992. Pili, kuweka mpango wa utekelezaji wa masula mbalimbali muhimu kuhusu maendeleo endelevu. Kwa muhtasari, mkutano ulipitisha azimio la Johannesburg kuhusu maendeleo endelevu na mpango wa utekelezaji wake. Azimio linaelezea matatizo na changamoto ya maendeleo endelevu ikiwa ni pamoja na ongezeko la uharibifu wa mazingira duniani, utandawazi na ongezeko la tofauti katika nyanja ya maendeleo Kimataifa.

Aidha, azimio linaweka msimamo wa pamoja wa kushughulikia masuala haya. Mpango wa utekelezaji unahusu masuala ya kuondoa umaskini, hifadhi ya mazingira kama msingi wa maendeleo, maendeleo endelevu katika utandawazi, afya na maendeleo endelevu, maendeleo endelevu kwa nchi changa zilizo visiwani, maendeleo endelevu kwa Bara la Afrika, maendeleo endelevu kwa mabara mengine, nyenzo za utekelezaji na muundo wa kitaasisi kuhusu maendeleo endelevu Kimataifa. Katika mkutano huo, ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Rais. Ofisi ya Makamu wa Rais inaratibu maandalizi ya mpango wa Kitaifa wa utekelezaji wa matokeo haya.

Aidha, katika kikao chake cha 22, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira liliamua kuisaidia Tanzania kifedha na kitaalam katika kupambana na tatizo la mazingira katika maeneo yaliyoathiriwa na wakimbizi kama sehemu ya utekelezaji wa maamuzi ya *WSSD.* Ofisi ya Makamu wa Rais inafuatilia *UNEP* kuhusu utekelezaji wa uamuzi huo.

Mheshimiwa Spika, kama Bunge hili Tukufu linavyofahamu, kipimo cha mafanikio katika *agenda* ya mazingira lazima kijumuishe kiwango cha ushiriki wa wananchi wenyewe. Ofisi ya Makamu wa Rais inafarijika sana na ongezeko la mwamko wa mwananchi mmoja mmoja na kupitia vikundi mbalimbali vya jamii, kushiriki katika shughuli za hifadhi ya mazingira.

Katika kipindi cha mwaka jana, zaidi ya vikundi 45 vinavyojishughulisha na masuala ya mazingira vilipata huduma ya ushauri kwa ajili ya kuimarisha shughuli zake na vingine kupendekezwa usajili. Aidha, katika maadhimisho ya siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika tarehe 5 Juni, 2003, wananchi katika vikundi na taasisi mbalimbali walishiriki kikamilifu kote nchini.

Napenda kuwapongeza wote hawa, pamoja na uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam ambako maadhimisho yalifanyika Kitaifa, Wizara ya Afya kwa kuendesha mashindano ya usafi wa mazingira Mijini na Manispaa za Moshi, Ilala na Tanga kwa kushinda na kupata tuzo ya mashindano haya. Aidha, natoa shukrani za dhati kwa kampuni ya mgodi wa *Resolute Tanzania Limited,* Nzega na kampuni ya *Sunflag* ya Arusha kwa msaada wao wa *T-shirts* kwa ajili ya kufanikisha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa wito kwa vyombo vyote vinavyojihusisha na shughuli za hifadhi ya mazingira nchini kuimarisha shughuli za uenezi Mikoani, Wilayani na Vijijini ili kuzidi kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi katika suala hili muhimu.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lilianzishwa na Sheria ya Bunge Na. 19 ya Mwaka 1983. Majukumu ya Baraza yameainishwa katika sheria hiyo pamoja na sera ya Taifa ya Mazingira kuwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam, kuratibu na kukuza uhusiano kati ya taasisi mbalimbali za Kiserikali na zisizo za Kiserikali na kutoa hamasa juu ya hifadhi ya mazingira kwa kupitia uandaaji wa mipango ya mazingira, utafiti na kuongeza weledi katika masuala ya mazingira.

Aidha, sera pia imelipa Baraza majukumu zaidi ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa udhibiti wa uchafuzi wa mazingra na kusuluhisha kitaalam migongano ya shughuli za maendeleo na hifadhi ya mazingira kwa kuhimiza kufanyika tathmini ya athari kwa mazingira katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kama nilivyoeleza hapo nyuma kuhusu mfumo wa kiasasi wa kusimamia mazingira na ili kuhakikisha kwamba Baraza linabaki kuwa chombo cha kitaalam na cha kudhibiti uharibifu wa mazingira, mradi wa *ILFEM* umetoa mapendekezo ya mfumo wa kiasasi wa kusimamia shughuli za mazingira na kuainisha majukumu ya Baraza tofauti na vyombo vingine ili kuleta ufanisi.

Serikali iliridhia mapendekzo hayo na hivi sasa majukumu hayo yanafafanuliwa zaidi katika sheria mpya ya mazingira ambayo italetwa hapa Bungeni mara itakapokuwa tayari. Matarajio ya sheria mama ya mazingira ni kulipa Baraza uwezo wa kuwa na mamlaka tendaji badala ya kuwa tu chombo cha kutoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, katika jukumu la kuandaa mipango ya hifadhi ya mazingira hususan katika maeneo yenye matatizo sugu na yanayohitaji mikakati mtambuka, Baraza limeendelea kushirikiana na sekta nyingine katika kutambua maeneo mapya na kutekeleza litakiwalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/03, Baraza limeratibu mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Pwani. Malengo ya mradi huu ni pamoja na utayarishaji wa vitabu vya miongozo itakayotumiwa na wawekezaji juu ya ufugaji endelevu wa samaki, kukuza uelewa wa kisayansi ili

kufanikisha usimamizi bora wa maeneo ya pwani na kuelimisha wadau kwa njia mbalimbali ili kuweza kupata utaalam wa kuhifadhi maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha unaoisha sasa, Baraza liliandaa Taarifa ya Hali ya Mazingira ya Pwani na kuwasilisha Serikalini mkakati wa hifadhi ya mazingira ya eneo hilo. Mkakati huo umeidhinishwa na Serikali na maandalizi ya utekelezaji wake katika awamu ya pili ya mradi wa *TCMP* yamefanyika. Maandalizi haya yamo katika progamu ya ushirikiano baina ya Serikali yetu na ile ya Marekani kupitia *USAID.*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Baraza liliendelea kusimamia shughuli za mradi wa hifadhi ya bioanuwai za Wilaya za mpakani (Bukoba Vijijini, Monduli, Same) unatekelezwa na nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Malengo ya mradi yalishaelezwa kuwa ni kukuza ushirikiano na wadau wengine katika masuala ya kuhifadhi bioanuwai, kutoa ushauri juu ya mipango mbadala ya matumizi bora ya maliasili, kuelimisha watu kuhusu mbinu nyingine za kuinua kipato badala ya kutegemea maliasili ya misitu tu na kutayarisha mpango madhubuti wa kuzuia uharibifu wa bioanuwai kwa kushirikiana na wanavijiji na wahusika wengine.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoisha, msitu wa Longido uliwekwa mipaka ili kuupatia hadhi ya msitu wa hifadhi, mipango ya utekelezaji wa mfumo wa hifadhi kwa njia ya ushirikishwaji iliandaliwa na tathmini ya teknolojia ya gesi itokanayo na samadi ilifanyika.

Mheshimiwa Spika, japokuwa shughuli za mradi huu zinatarajia kwisha mwishoni mwa mwaka 2003, Baraza kwa ushirikiano na *UNDP* litaendeleza baadhi ya mafanikio muhimu ya mradi hususan katika eneo la nishati, kwa kipindi cha mwaka mmoja zaidi, wakati juhudi za muda mrefu za kuendeleza mafanikio ya mradi zikiendelea.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Baraza limeratibu utekelezaji wa mradi wa hifadhi na usimamizi wa mazingira ya bonde la Kihansi *(lower Kihansi Environmental Management Project).* Lengo la mradi huu ni kuanzisha hatua mbalimbali zitakazotekelezwa kwa muda unaofaa za kulinda kwa muda mrefu uhifadhi wa mifumoikolojia ya korongoo la Kihansi na maeneo ya misitu ya vyanzo vya maji katika lindimaji ya mto Kihansi.

Katika ngazi ya Taifa, lengo la mradi ni kusaidia katika uanzishaji wa mfumo bora wa kisheria na kitaasisi wa kusimamia na kuandaa mipango endelevu ya matumizi ya mazingira na uendelezaji wa raslimali ya maji ikiwa ni pamoja na kuimarisha mifumo ya Kitaifa ya ufuatiliaji wa tathmini ya mazingira. Mafanikio makubwa ya utekelezaji mpaka sasa ni pamoja na utunzaji wa busara ambao umewezesha vyura adimu wa Kihansi kuongezeka sana katika korongo la Kihansi na kupunguza hatari ya uwezekano wa kutoweka kwa vyura hao na jamii nyingine ya viumbe ambao wako hatarini kutoweka

Mheshimiwa Spika, aidha, tafiti za kiikolojia na tathmini za kiuchumi zimefanyika ili kuweza kupata mtiririko wa mazingira na vigezo vingine vitakavyotumika katika kutoa kibali cha matumizi ya mali yanayohitajika katika mitambo ya kufua umeme Kihansi. Katika mwaka huu wa fedha, juhudi kubwa katika utekelezaji wa mradi zitaelekezwa katika program ya kujenga uwezo wa Taasisi katika ngazi ya Taifa na kuandaa na kutekeleza mpango wa hifadhi na usimamizi wa mazingira ulioboreshwa *(Environmental Management Plan Update)* unaoshirikisha Serikali za Mitaa katika utekelezaji. Mpango huu wa hifadhi utazingatia masuala yote yanayoathiri mfumoikolojia Kihansi na utaainisha masharti yatakayoiwajibisha *TANESCO* kuendesha mtambo wa Kihansi kulingana na kibali cha matumizi ya maji *(Final Water Right).* Aidha, mpango huo utaainisha athari za mazingira na hatua madhubuti zitakazochukuliwa ili kuhakikisha kuwa mfumoikolojia wa Kihansi unahifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuhifadhi maeneo chepe chepe, Baraza liliendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya eneo hilo katika mradi mkubwa wa hifadhi ya Ziwa Victoria. Malengo yake makuu ni kuongeza uelewa wa kisayansi kuhusu uwezo wa maeneo chepe chepe, kuchuja uchafu katika mito ya Nyashishi, Mabubi, Mtakuja na Ngono, kubuni miradi midogo midogo ili kuonyesha na kuhamasisha wananchi kuboresha kilimo chao hususan mboga mboga na kusaidia wananchi kuandaa mikakati ya matumizi bora ya maeneo chepe chepe. Katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, mradi ulifanya tathmini juu ya hali ya uchafuzi wa Ziwa Victoria kutoka katika maeneo ya machimbo ya madini

na kugundua kwamba hali ya uchafuzi siyo mbaya. Maeneo chepe chepe yanayohitaji kuongolewa, pia yametambulika hususan katika Vijiji vya Nyashishi, Rubana na Lamadi.

Aidha, katika eneo la Kalemela Wilaya ya Magu na Kuruya/Kwibuse Wilaya ya Tarime baada ya wananchi kuhamasishwa wameweza kudhibiti mmomonyoko wa udongo kwa kuweka makinga maji ambayo yamewaongezea uzalishaji mali.

Vile vile, katika kipindi hicho, ramani za maeneo chepechepe tofauti yenye jumla ya hekta 422,000 zilizo katika Wilaya zote zinazolizunguka Ziwa Victoria, zimetengenezwa kwa mfano wa *Atlas* na zinaonyesha ukubwa wa eneo, matumizi makuu na aina ya uoto uliopo ramani hizi zitasaidia uongozi wa Wilaya husika kutambua na kuamua matumizi bora ya ardhi katika bonde la Ziwa Victoria. Aidha, ikishachapishwa na kutolewa, *Atlas* hii itafaa pia kwa mafunzo ya shule mbalimbali zilizo katika eneo la bonde.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa, awamu ya pili ya mradi wa kuteketeza madawa chakavu ya kilimo na mifugo nchini ulikwama baada ya Serikali ya Uholanzi kujitoa katika mradi kufuatia mabadiliko ya sera za nchi yao.

Napenda tena kuliarifu Bunge lako kwamba, kutokana na maandalizi ya mradi yaliyokwishafanyika, Tanzania imechaguliwa kuwa mshiriki kwenye awamu ya kwanza ya programu mpya inayojulikana kama *Africa Stockpiles Programme (ASP)* itakayojumuisha nchi saba katika Bara la Afrika. Programu hii ina lengo la kusafisha Bara la Afrika kutokana na mlundikano wa dawa na sumu mbalimbali chakavu za kilimo na kuhakikisha kuwa tatizo hili halijitokezi tena.

Aidha, mwaka wa fedha unaoisha, Baraza kwa ushirikiano wa Shirika la Chakula Duniani *(FAO)* liliendesha mafunzo kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kuandaa utekelezaji wa program hii ya *ASP.* Programu hii inafadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira *(GEF)* pamoja na wafadhili wengine, ikiwemo Serikali ya Japan. Masharti muhimu ili kufanikisha programu hii ni kwa Serikali yetu kuridhia Mkataba wa Stockholm uhusuo udhibiti wa kemikali za sumu zinazodumu kwenye mazingira, pamoja na kuchangia sehemu ndogo ya gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Baraza pia lilishiriki katika kuandaa mwongozo wa Kitaifa kuhusu udhibiti wa taka, pamoja na kufanya tathmini ya athari zake kwa afya ya jamii na mazingira katika jiji la Dar es Salaam na Mwanza kwa kushirikiana na Wizara ya Afya.

Vile vile, Baraza limeshiriki kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu matumizi ya mitambo midogo ya kuchoma taka za hospitalini ikishirikiana na Shirika la Afya Duniani *(WHO)* na Wizara ya Afya. Aidha, Baraza, kutokana na utafiti uliofanyika kuhusu tatizo sugu la mifuko ya plastiki, lilitoa ushauri kwa Serikali kuchukua hatua mbalimbali za kudhibiti ikiwa ni pamoja na kupendekeza kuongeza kodi ya mifuko hiyo inapoingizwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majukumu yake, Baraza liliendelea kusimamia Tathmini ya Athari kwa Mazingira *(TAM)* na kutoa suluhisho za kitaalam baina ya maendeleo na athari zake kwenye mazingira. Baraza hufanya hivyo kwa kutathmini taarifa zinazoelezea kwa undani athari zinazotokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Lengo ni kuhakikisha kwamba athari hizo zimeainishwa, kwa madhumuni ya kuzipunguza, kuzizuia zisitokee ama kutafuta njia mbadala ya kuziepusha ili kujihakikishia maendeleo endelevu, kulinda afya na maisha ya wananchi na kuleta maendeleo endelevu nchini.

Katika mwaka wa fedha 2002/2003 sekta zilizoangaliwa na kutolewa ushauri ni pamoja na Kilimo, Barabara, Nishati na Madini, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Maliasili na Utalii, Viwanda na Biashara.

Katika eneo la kilimo, uzuiaji wa ndege waharibifu kwa mazao ya nafaka, umwagiliaji wa zao la mpunga katika skimu za Mombo, Lekitatu, Ipatagwa na Luganga, katika Wilaya za Korogwe, Arumeru, Iringa na Mbeya Vijijini zilifanyiwa mapitio. Vile vile, Baraza lilifanya mapitio ya mradi wa

ushirikishwaji na maendeleo ya kilimo Vijijini *(PADEP)* unaotarajiwa kutekelezwa katika Wilaya ishirini na nane zikijumuisha Wilaya tatu za Zanzibar.

Katika eneo la uchimbaji wa madini, vibali vinavyozingatia *TAM* vimetolewa kwa miradi ya uchimbaji wa dhahabu katika Mto Zira katika Wilaya ya Chunya, mradi wa Meremeta ulioko Buhemba, Wilaya ya Musoma na mradi wa uchimbaji wa almasi wa *El Hillary Minerals* katika Wilaya ya Kishapu, Shinyanga. Kwa upande wa eneo la maji na maendeleo ya mifugo, miradi ya kupeleka maji Vijijini, Wilayani Monduli, Arusha na machinjio ya kisasa, masoko na hifadhi ya ng'ombe kabla ya kuchinjwa katika Manispaa ya Dodoma ilifanyiwa mapitio na kuruhusiwa.

Kwa upande wa maendeleo ya maliasili na utalii, shughuli za uzalishaji wa ndege aina ya mbuni Wilayani Arusha na mradi wa ufugaji kamba Mafia ilifanyiwa mapitio. Kuhusu shughuli za viwanda na biashara, kiwanda cha utengenezaji wa mabomba ya sindano cha *Medi-tech Industrial Company Limited* kilichopo Mikocheni Dar es Salaam na kile cha ufuaji wa vyuma na mabati cha *M.M.I. Steel Mills Limited* cha Dar es Salaam na kile cha saruji kilichoko Mbeya vilifanyiwa mapitio.

Aidha, katika hatua za awali, kumekuwepo na ongezeko la miradi ya usindikaji vyakula hususan samaki katika eneo la viwanda Mikocheni, Dar es Salaam. Vile vile, kwa upande wa mawasiliano, shughuli za ujenzi wa mikonga ya kurushia mawasiliano na mabango ya matangazo imeongezeka katika Manispaa zote za Dar es Salaam. Ushauri wa mambo gani ya kuzingatia kimazingira ulitolewa ili kuboresha utekelezaji wa litakiwalo. Kwa upande wa Nishati mradi wa kupeleka umeme Vijiji vya Kisiwa cha Songo ulifanyiwa tathmini na miradi mingine midogo midogo ya ufuaji umeme kutoka mabwawa madogo madogo ilifanyiwa mapitio kwa mfano mradi wa umeme katika Kata ya Wino, Songea.

Aidha, miradi ya maendeleo iliyofanyiwa ukaguzi na uperembaji ni ile ya mradi wa gesi wa Songosongo, mradi wa umeme wa *IPTL* na ule unaotarajiwa kufuga samaki aina ya kamba katika Wilaya ya Mafia, Mkoani Pwani.

Mheshimiwa Spika, katika jukumu la uhamasishaji wananchi na kuongeza weledi wao kuhusu hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu, Baraza katika kipindi cha mwaka 2002/2003 liliendelea kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa kutunza na kuhifadhi mazingira kupitia njia mbalimbali.

Katika eneo hili Baraza lilichapisha nakala 2000 za Jarida la Mazingira na kugawia watu binafsi, Halmashauri za Wilaya na Miji, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Idara za Serikali na Taasisi mbalimbali. Aidha, Baraza lilitumia Maktaba yake kutoa elimu ya mazingira kwa umma hususan kwa wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo vya elimu ya juu pamoja na watafiti zaidi ya 1,000 waliotoka ndani na nje ya nchi.

Katika kipindi hicho, Baraza lilichapisha na kugawa vitini zaidi ya 2000 vyenye kutoa maelezo na miongozo juu ya ufundishaji wa elimu ya mazingira katika shule za msingi. Vitini hivyo vilitolewa kwa ushirikiano wa Wizara ya Elimu na Utamaduni pamoja na Mfuko wa Kimataifa wa Hifadhi na Mazingira *(WWF).*

Mheshimiwa Spika, katika utaoji wa elimu ya mazingira Baraza linatilia mkazo maalum kwa shule za msingi kwa kuzingatia kwamba hapo ndipo vilipo vizazi vya kesho. Kwa hiyo, kwa kuwahamasisha juu ya utunzaji wa mazingira tunajijengea mazingira na maisha bora na endelevu kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, mbali na kutoa elimu ya mazingira kwa njia ya matoleo, Baraza liliendelea kutoa elimu hiyo kupitia vyombo vingine vya habari kama vile televisheni, redio na magazeti. Pia, Baraza kwa kushirikiana na Kampuni ya *LEOZ (T) Limited* lilishiriki kutoa mafunzo juu ya namna ya kuandaa na kuendesha mashindano ya Mrembo wa Mazingira *(Miss Mazingira).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/2003, Baraza kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* liliendesha mafunzo kwa wakufunzi 30 kutoka Vyuo vya Elimu nchini juu ya namna ya kuingiza masuala ya mazingira katika mitaala ya shule za

msingi. Utaratibu wa kuwafundisha wakufunzi una lengo la kuwafikia Walimu wengi zaidi wanapokuwa vyuoni katika mafunzo. Ili kuhakikisha kwamba elimu ya mazingira inasimamiwa kikamilifu, Baraza kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni na wadau wengine limefufua upya Kamati ya Kitaifa ya Elimu ya Mazingira *(National Environmental Education Committee)* ambayo itasimamia na kuratibu utoaji wa elimu ya mazingira katika ngazi mbalimbali za elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004, Baraza litaendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na sera, Sheria na mkakati wa mpango *Strategic Plan* wa Baraza.

Kwa upande wa mipango ya mazingira, Baraza litaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mradi wa hifadhi ya mazingira ya pwani kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Utekelezaji wa mradi wa maeneo chepe chepe kama sehemu ya program ya hifadhi ya Ziwa Victoria utaendelea kwa kipindi cha mwaka mmoja. Kuhusu mradi wa hifadhi ya mazingira Kihansi *(LKEMP)* mradi utaandaa mpango mpya wa hifadhi ya mazingira unaozingatia mahitaji ya vyura, utalenga katika hifadhi ya mimea na viumbe hai kwenye maeneo walipo vyura, tutashirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na Wizara ya Nishati na Madini kuona *TANESCO* inapewa hatimiliki ya maji inayozingatia mahitaji ya vyura. Mradi pia utasaidia kuongeza uwezo wa sekta zinazohusika na mradi kuhifadhi mazingira ikiwa ni pamoja na maji kwa ujumla.

Aidha, Baraza litaendelea na juhudi za mipango ya tafiti na hifadhi endelevu ya maeneo maalum kiikolojia. Haya ni maeneo yanayohitaji uangalizi makini ili kupunguza uharibifu na uwezekano wa kupungua au kupotea kwa bioanuwai kama ilivyoainishwa katika mkakati wa Baraza. Masuala nyeti yanayohusu jamii kama vile uchomaji moto ovyo, uchomaji mkaa unaosababisha ukataji miti kwa wingi na hatimaye kusababisha jangwa, yatashughulikiwa kwa ushirikiano na wadau.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, pamoja na ukaguzi wa maeneo mbalimbali ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira, Baraza limejiandaa kutekeleza programu ya *ASP* ambayo inategemewa kuanza mnamo Januari, 2004 na kuchukua takriban miaka minne. Aidha, Shirika la Chakula Duniani *(FAO)* linakusudia kuboresha maeneo angalau sita yaliyoathirika zaidi na dawa chakavu hapa nchini.

Aidha, Baraza linategemea kutekeleza mradi wa kudhibiti uchafuzi wa bonde la Mto Msimbazi kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kusimamia mazingira *(UNEP/GPA).* Lengo kuu la mradi huu ni kudhibiti mtiririko wa maji taka yanayoingia baharini kwa kutumia nyasi za *vetiver* zenye sifa kote duniani kuhusiana na ubora wake katika kukinga mmomonyoko wa ardhi pamoja na kuchuja maji taka hata kufikia viwango vinavyoruhusiwa kuingia baharini bila kuleta madhara yoyote kwa viumbe wa majini na mazingira kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Baraza litaendelea kufanya mawasiliano na sekta mbalimbali, hususan za kilimo, maji, nishati, barabara, utalii na wanyamapori ili kutafuta mwelekeo wa kukamilisha kazi ya kuandaa miongozo ya mazingira *(Environmental Guidelines)* ya kisekta kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira. Lengo kuu la zoezi hili ni kuhakikisha kwamba masuala ya mazingira yameainishwa barabara katika sekta mbalimbali za maendeleo ili kupunguza athari mbaya zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji. Baraza pia katika hatua za awali linatarajia kufanya stadi ya masuala ya taratibu za kufanya tathmini ya mazingira katika ngazi za sera, mipango na mikakati ili kupunguza limbikizo la matatizo ya kimazingira katika miradi ya maendeleo.

Aidha, Baraza litaendelea kukuza weledi kwa watumishi wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji ili kuwajengea uwezo wa kufanya tathmini za mazingira kwa miradi ya maendeleo iliyoko katika Halmashauri zao. Baraza litahuisha na kuainisha masuala ya *TAM* katika mipango ya programu za kisekta na katika Halmashauri kama itakavyokuwa imebainishwa na stadi zitakazokamilika.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais pia ina jukumu kubwa la kusimamia na kuratibu jitihada za Serikali za kupambana na umaskini. Jitihada hizo zimeelezwa katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini wa mwaka 2000. Mkakati huu unatekeleza malengo ya Mkakati wa Taifa wa Kusimamia Sera za

Kuondoa Umaskini na yale ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025. Dira ya Taifa inakusudia kuifanya Tanzania ya mwaka 2025 kuwa ni Taifa lenye sifa kuu tano zifuatazo:-

Jamii iliyoondokana na umaskini uliokithiri yenye maisha bora na mazuri, amani, utulivu na umoja, Utawala na uongozi bora, jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza zaidi na uchumi wenye uwezo wa ushindani kujiletea ukuaji wa kudumu kwa maslahi ya watu wote. Mengi yaliyotekelezwa na Serikali kukuza uchumi na kuboresha huduma za jamii katika kipindi kilichopita yamejitokeza katika hotuba mbalimbali zilizosomwa na Waheshimiwa Mawaziri wa sekta husika. Sera na mikakati ya Serikali inaelekezwa kujenga uchumi unaoongozwa na sekta binafsi ambayo kwa kiwango kikubwa imechangia kukuza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Pato la Taifa kwa mwaka 2002 lilikua kwa asilimia 6.2 ikilinganishwa na asilimia 5.7 mwaka 2001. Ukuaji huu umechangiwa haswa na kilimo, uuzaji wa jumla, rejareja na mahotelini pamoja na utalii, bidhaa za viwandani na sekta nyingine kama ujenzi, fedha, bima na huduma za kibiashara, madini, mawasiliano na uchukuzi na huduma nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, sasa tupo katika mwaka wa tatu wa utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini na mafanikio ya utekelezaji huo yameanza kuonekana. Ni vema tukaangalia mafanikio haya kwa upana zaidi, badala ya kuangalia kipato tu. Kiashiria cha kwanza kabisa katika kuangalia hali ya umaskini ni ukosefu wa chakula. Tafiti zilizofanyika zimeonyesha kuwa umaskini wa chakula umepungua kutoka asilimia 21.6 mwaka 1991/1992 hadi asilimia 18.7 mwaka 2000/01 na umaskini wa mahitaji muhimu kupungua kutoka asilimia 39 hadi kufikia 36.

Aidha, tukiangalia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) tunaona uandikishaji wa watoto uliongezeka kwa asilimia 23 kutoka wanafunzi 4,845,185 mwaka 2001 hadi 5,981,335 mwaka 2002 kwa shule za msingi za Serikali na binafsi. Kiwango cha wanafunzi kujiunga na shule za sekondari pia kiliongezeka hadi kufikia asilimia 21.7 mwaka 2002 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 19.5 mwaka 2001. Maendeleo makubwa pia yameonekana katika ujenzi wa barabara na ujenzi wa nyumba bora hasa Mijini. Hata hivyo kupungua kwa viwango vya umaskini kumetofautiana kati ya Mkoa na Mkoa, Mji hadi Mji na Kijiji hadi Kijiji kutokana na hatua mbalimbali za maendeleo katika maeneo hayo hasa kwa kuangalia miundombinu, hali ya hewa, raslimali na matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, utulivu wa uchumi mkuu, kupungua kwa mfumuko wa bei kunawezesha mwananchi wa kawaida kuwa na uhakika zaidi wa matumizi ya pato lake. Hayo yote ni matunda ya uwekezaji wa sera mbalimbali za Serikali, hasa mkakati wa kupunguza umaskini na ni kipimo na ushahidi wa kupungua kwa umaskini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyodhihirika upungufu pia umekuwepo. Serikali inakusudia kufanya tathmini ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini ili kuuboresha pamoja na kuandaa mipango hasa katika masuala ya kukuza uchumi, kutoa huduma bora za jamii, kuhimiza ushirikishwaji wa jamii katika kuandaa mipango ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini na kusimamia utekelezaji wake, ili kuwaletea wanachi walio wengi mafanikio.

Mheshimiwa Spika, suala la kupambana na umaskini limepewa kipaumbele na Serikali zote mbili za Muungano. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshaanza kutekeleza mpango wake wa Kupunguza Umaskini, *Zanzibar Poverty Reduction Plan (ZPRP)* na imeshaanza kuandaa mfumo wa ufuatiliaji wa jitihada hizo za kupambana na umaskini. Mwanzoni mwa mwaka 2003 wataalam wanane toka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar walitembelea Tanzania Bara kujifunza mfumo wa ufuatiliaji ili watumie uzoefu wa bara kuandaa mfumo wa ufuatiliaji kwa upande wa Zanzibar. Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kubadilishana uzoefu na utaalam ili kuimarisha utekelezaji wa mikakati ya kuondoa umaskini na kuleta maendeleo endelevu kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, watekelezaji Wakuu wa jitihada za kupambana na umaskini ni wananchi wote kwa kushirikiana na sekta za Serikali, Taasisi za kijamii, Taasisi za taaluma mbalimbali na wahisani. Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha mwaka 2002/2003 iliweka mkazo mkubwa katika kuratibu utekelezaji wa mpango wa ufuatiliaji wa jitihada za kupambana na umaskini. Mfumo huu utasaidia ukusanyaji wa takwimu mbalimbali na kuzichambua na utasaidia katika kutathmini jitihada zinazofanyika

kama zinaleta mafanikio. Utaratibu wa kukusanya taarifa na takwimu mbalimbali uliokuwepo huko nyuma haukutosheleza, kwa vile taarifa nyingi zilipitwa na wakati.

Aidha, ukusanyaji wake haukuzingatia vipaumbele na malengo ya Taifa katika jitihada za kupambana na umaskini. Tunatarajia mfumo huu wa ufuatiliaji utawezesha upatikanaji wa takwimu sahihi kwa wakati kwa ajili ya kupanga mipango bora na endelevu.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa katika ufuatiliaji wa jitihada za kuondoa umaskini ni pamoja na kuelimishana na kubadilishana uzoefu kuhusu harakati za kupambana na umaskini ili kujenga uelewa wa watu kuuchukia na kupambana nao, kunyambulisha viashiria vya umaskini na ukusanyaji wa taarifa sahihi zitakazotuwezesha kupima mwelekeo ili kubaini kama tunarudi nyuma au tunasonga mbele. Katika kuangalia hali ya umaskini uchambuzi wa takwimu zitokanazo na mfumo huu wa ufuatiliaji, maeneo makubwa mawili huchunguzwa ambayo ni umaskini usiokuwa wa kipato *(non-income poverty)* na umaskini wa kipato *(income poverty).* Hotuba yangu ya mwaka 2002/2003 ilieleza kwa kirefu kuhusu hali ilivyo, kufuatana na taarifa ya savei ya mapato na matumizi ya kaya *(Household Budget Survey)* iliyofanyika mwaka 2000/2001.

Mafanikio ya utekelezaji katika kipindi cha mwaka 2002/2003 yalikuwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini ya mwaka 2001/2002, ambayo ni ripoti ya pili iliandaliwa na kukamilika (Taarifa ambayo kama mnavyokumbuka ilizunduliwa wiki iliyopita katika ukumbi huu). Taarifa hii iliandaliwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na kukamilika mwishoni mwa mwaka 2002. Serikali iliwasilisha taarifa hii kwenye Bodi ya *IMF* na Benki ya Dunia pamoja na wafadhili wengine mwezi Machi, 2003.

Aidha, taarifa hii imekwishawekwa kwenye Tovuti ya Taifa ijulikanayo kama *http://www.tanzania.go.tz* ili kurahisisha upatikanaji kwa watumiaji. Taarifa hii imechapishwa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na kazi ya kuigawa na kuieneza inaendelea.

Ripoti hii kama ilivyokuwa ripoti ya kwanza inatoa taarifa ya utekelezaji wa sera za uchumi mkuu na uhusiano wake na jitihada za kuondoa umaskini. Ripoti imetoa maelezo ya kina ya utekelezaji katika sekta za kipaumbele zilizoainishwa ambazo ni kilimo, elimu ya msingi, barabara za Vijijini, maji safi na salama, afya na sheria. Pia imetoa maelezo ya kina ya utekelezaji wa mambo ya jumla yanayogusa sekta zote ikiwemo mkakati wa mendeleo Vijijini, mazingira, mapambano dhidi ya Ukimwi, jinsia, utawala bora, ukuzaji wa ajira, uboreshaji wa Serikali za Mitaa na maendeleo ya rasilimali watu. Ripoti inachambua mgawanyo wa bajeti ya Serikali kwa shughuli za kupambana na umaskini katika sekta za kipaumbele.

Aidha, taarifa imeelezea azma ya Tanzania kuhusu malengo ya Maendeleo ya Kimataifa *(Millennium Development Goals)* na kuwa Mkakati wa Kupunguza Umaskini utakuwa nyenzo muhimu ya kufikia malengo hayo katika ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufuatilia utekelezaji wa malengo haya kupitia mfumo wake wa kufuatilia na kutathmini umaskini *(Povery Monitering and Evaluation System)* na maendeleo ya utekelezaji yataendelea kuelezwa katika Taarifa ya utekelezaji na Ripoti ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu Tanzania. Ripoti ya Maendeleo ya Watu ya Kimataifa *(Human Development Report 2003)* iliyozinduliwa na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapa Dodoma Julai, 2003 imeainisha malengo ya maendeleo ya milenia yafuatayo kutokomeza umaskini uliokithiri na njaa, elimu ya msingi kwa wote, usawa wa kijinsia na fursa sawa kwa wanawake, kupunguza vifo vya watoto wachanga, upatikanaji wa huduma bora za uzazi, kupambana na Ukimwi, Malaria na magonjwa mengine, kulinda mazingira yetu pamoja na kujenga mshikamano wa kimaendeleo duniani, ambayo pamoja na maeneo mengine Serikali imeyatilia mkazo mkubwa katika kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na kundi la utafiti na uchambuzi *(Poverty Research & Analysis)* iliratibu uandaaji wa Ripoti ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu *(Poverty and Human Development Report (PHDR).* Ripoti hii inachambua kwa kina hali ya umaskini nchini, tofauti za kijiografia, uhusiano kati ya masuala ya Kimataifa na ya Kitaifa na hatari mbalimbali

zinazoweza kuwakabili watu na kusababisha umaskini *(vulnerability).* Ripoti hii ambayo imejumuisha taarifa mbalimbali zilizotokana na utafiti na uchambuzi wa hali ya umaskini nchini imechapishwa kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu mwaka 2002 na inakusudiwa kuandaliwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingi zilizofanyika ni pamoja na kufanya mapitio ya viashiria vya kupima umaskini na kuandaa rasimu ya marekebisho ya viashiria ili kupima vizuri zaidi mafanikio ya jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali kwa ushirikiano wa karibu na wahisani katika utekelezaji wa mkakati wa kupunguza umaskini. Viashiria hivi vitasaidia kufahamu mwelekeo, kuainisha upungufu na kuweka mipango ya uboreshaji wa jitihada hizo.

Aidha, katika jitihada za utekelezaji wa mfumo wa ufuatiliaji wa hali ya umaskini, mwongozo kwa lugha rahisi (Kiingereza na Kiswahili) uliandaliwa na kugawiwa ili kuwezesha wadau kuufahamu mfumo wa ufuatiliaji vizuri ili waweze kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake.

Mipango ya kazi za Kamati tendaji kwa kipindi cha miaka mitatu (2003/2003-2005/2006) na makisio ya gharama za kutekeleza imeandaliwa. Mipango ya kazi ya Kamati hizi imelenga kupima malengo yaliyowekwa Kitaifa ya kupunguza umaskini. Mikakati ya utekelezaji wa kazi za Kamati zote nne imeainishwa kwenye Mpango kabambe wa ufuatiliaji na tathmini ya umaskini *(Poverty Monitering Master Plan)* na shughuli kubwa inayoendelea ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mpango huo. Kamati hizo kama ilivyoelezwa mwaka jana ni Kamati ya Sensa na *Survey* chini ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Kamati ya Utafiti na Uchambuzi chini ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubianfsishaji, Kamati ya Takwimu zinazotokana na Rekodi za Mfumo wa Utawala inayosimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), na Kamati ya Uhamasishaji na Uelimishaji umma inaongozwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais inatambua kuwa ni haki ya kila Mtanzania kufahamishwa jitihada za Serikali katika kupambana na umaskini.

Aidha, ni wajibu wa Watanzania kushiriki katika mapambano haya ya kuutokomeza umaskini. Ili mipango ya kuondoa umaskini na suala zima la ufuatiliaji viweze kufanikiwa, kuna umuhimu wa kufufua ari ya wananchi kwa kuwahamasisha katika kubuni na kutekeleza mipango itakayoleta maendeleo ya wananchi yaliyotekelezwa katika kuelimisha na kuhamasisha wananchi ni pamoja na kutolewa kwa maelezo na mifano ya jitihada zilizoleta mafanikio *(success stories)* katika jitihada zifanywazo na wananchi wenyewe, kutoka sehemu mbalimbali kupitia kipindi cha redio cha TUJIKOMBOE kinachorushwa na Redio Tanzania Dar es Salaam kila Jumatano saa 10.30 jioni na kupitia Toleo la Jarida la MAPAMBANO linalotolewa mara mbili kwa mwaka na kutolewa na kufikishwa sehemu mbalimbali nchini.

Machapisho mbalimbali yalitolewa kwa wadau. Machapisho hayo ni pamoja na Ripoti ya Savei ya Mapato na Matumizi ya Kaya *(HouseHold Budget Survey (HBS)* 2000/2001 iliyozinduliwa Septemba, 2002, Ripoti ya Utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini kwa lugha rahisi na taarifa nyingine zilizochapishwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Wiki ya Sera za Kuondoa Umaskini ilifanyika mwezi Septemba, 2002 kwa lengo la kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo sekta za Kiserikali, taasisi za Kijamii, Jumuiya ya Wahisani na taasisi za taaluma mbalimbali. Wananchi walifahamishwa jitihada mbalimbali za Serikali na washiriki walitoa maoni mbalimbali yatakayosaidia kuboresha sera. Yafuatayo yalifanyika katika wiki hiyo:-

Mheshimiwa Spika, wadau na wananchi walipata nafasi ya kuchangia katika mjadala wa matokeo ya Savei ya Mapato na Matumizi ya Kaya *(Household Budget Survey (HBS)* 2000/2001 ambayo yanaonyesha hali halisi ya umaskini Tanzania. Wadau mbalimbali pia walipata nafasi ya kuchangia maoni kama utekelezaji wa mkakati wa kupunguza umaskini na uboreshaji sera mbalimbali.

Maoni yaliyotolewa yametumika kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mkakati wa kupunguza umaskini *(PRS progress report)* na maoni mengine yanafanyiwa kazi na yatasaidia sana katika kuboresha sera na mikakati ya kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka jana wakati kama huu, Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kutekeleza mradi wa *Small Enterpreneurs Loan Facility (SELF)* katika kipindi cha Julai 2002 hadi Machi, 2003 kiasi cha shilingi milioni 564 zilitolewa kwa asasi 23 na kuwafikia walengwa 3,557 ambao kati yao asilimia 61 ni wanawake. Hili ni ongezeko kubwa ikilinganishwa na kiasi cha shilingi milioni 101 kilichotolewa kwa asasi saba katika kipindi cha mwaka 2001/2002. Jitihada za kutoa mikopo zinaendelea vizuri katika maeneo ya mradi ila Wilaya nyingine hazijapata mikopo kutokana na kukosekana kwa asasi zenye sifa zilizojitokeza kuomba mikopo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge hili Tukufu kuwa asasi mbalimbali zimepatiwa mikopo kwa viwango tofauti kulingana na uwezo wa asasi, katika maeneo ya majaribio kama ifuatavyo:-

Dodoma, *Utafiti Mifugo SACCOS* (Mpwapwa), *Kibaigwa SACCOS* na *CAVI SACCOS* (Kongwa); *SIDO, PRIDE, Ukaguzi SACCOS* na *Mji Mkuu SACCOS* (Dodoma), Morogoro, *SIDO* na *AFREDA* (Kilosa); *PRIDE, Kireka SACCOS* na *Mzumbe Sekondari SACCOS* (Morogoro). Lindi, *SIDO* (Lindi), Mtwara, *COSIGA* na *SIDO* (Masasi), *SIDO* (Mtwara), *SIDO* (Tandahimba), *Newala Teachers SACCOS* (Newala), Pwani, *SIDO* (Bagamoyo), *SIDO* (Kibaha), *SELFINA, CBWTF, Kibaha Teachers SACCOS* (Kibaha), *Kisarawe District Council SACCOS (Kisarawe),* Vikindu Teachers SACCOS (Mkuranga), Singida, *SHIVU, SIDO* na *PRIDE* (Singida), *CHAMWAI SACCOS* (Iramba) na Zanzibar, *Changamoto Life Preservation Fund* na *PRIDE* (Unguja).

Kwa asasi zote zilizochukua mikopo urejeshwaji wa fedha ni asilimia 98.5. Jitihada za tathmini kama mikopo hii inawasaidia kuboresha maisha ya wananchi maskini zinaendelea kufanyika. Ili kuongeza uwezo wa asasi katika utoaji mikopo, jumla ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo 29 vilipatiwa mafunzo ili viweze kutoa huduma bora zaidi kwa wanachama wao. Katika mafunzo haya, jumla ya washiriki 95 walinufaika na mafunzo hayo wakiwemo Wenyeviti, Makatibu na Watunza Fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa jitihada za kujenga uwezo wa asasi hizi zinaendelea kwa matarajio kuwa katika kipindi cha 2003/2004, Serikali inaandaa taratibu za kufikia Mikoa zaidi ya nusu kutoka Mikoa sita ya sasa. Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mikoa yote itafikiwa. Kiasi cha shilingi bilioni 1.22 kimetengwa kufikia Mikoa hiyo. Ni matarajio ya Serikali kuwa mradi huu utakapopanuka na kuenea Mikoa hiyo mingine utachangia kupungua kero zilizopo za kukosa huduma za mikopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wahisani mbalimbali kwa azma ya kutekeleza Sera ya Taifa ya Ajira *(National Employment Policy)* ilianzisha Programu ya Taifa ya kuongeza kipato *(NIGP)* mwaka 1994. Awamu ya kwanza ilikamilika mwaka 2000. Kuanzia Januari 2001, Programu hii ipo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais na ina lengo la kuwaongezea kipato wananchi ili kuondoa umaskini katika makundi mbalimbali kama vijana wanaoingia soko la ajira kwa mara ya kwanza, wanawake wenye nia ya kuanzisha biashara ndogondogo za kujiongezea kipato, watumishi waliopunguzwa kazini katika Mashirika ya Umma na Serikalini, walemavu na mwananchi mwingine yeyote anayependa kuongeza kipato chake au kujiajiri na kujitegemea.

Hadi kufikia Juni 2003 miradi ipatayo 26 imetekelezwa kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni 25 ikiwa katika sekta za kilimo, miundombinu, biashara ndogo ndogo pamoja na sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, chini ya mpango huu, wanawake na vijana pamoja na wananchi wengine wapatao 23,892 wamepata ajira na kuongeza vipato vyao. Pia mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 297 imetolewa kwa asasi za kifedha 12 ambazo ni *SIDO* Mtwara, *Presidential Trust Fund (PTF)* - Dar es Salaam, *Women Entrepreneurship Development Trust Fund (WEDTF)* - Unguja na Pemba, *Tanzania Promotion for Self Employment (TAPSE)* - Dar es Salaam, *Tanzania Micro-Entreprenuer Association (TAMEA)* - Mwanza, *African Inland Church of Tanzania (AICT)* - Mwanza, *Mwananchi Informal Sector Development Association (MISDA)* - Kilimanjaro, *Dar es Salaam Volunteers for Women and Children Trust Fund* - Dar es Salaam, *Songea Zonal Audit Savings & Credit Co-operative Society (SACCO)* - Ruvuma. Asasi hizi kwa pamoja zimewakopesha wafanya biashara wadogo zaidi ya 2,821 kwa ajili ya kukuza biashara zao.

Katika kipindi cha mwaka 2002/2003, *NIGP* ilikusudia kuendeleza na kumalizia miradi minane kwa kutumia fedha zilizoahidiwa na Serikali ya Ubelgiji, lakini utekelezaji wake uliathiriwa na kutokupatikana kwa fedha hizo. Miradi hiyo ni Mradi wa Chumvi - Unguja na Pemba, Mradi wa soko la biashara ndogo ndogo - Mwanakwerekwe - Zanzibar, Mradi wa ukopeshaji ng'ombe wa maziwa - Unguja na Pemba, Arusha, Manyara, Mara, Mwanza, Shinyanga, Pwani, Iringa Mbeya, Morogoro, Rukwa na Ruvuma, Mradi wa kilimo cha mboga na matunda - Mwanza, Mradi wa kuendeleza wafugaji nyuki - Rufiji, Mradi wa Uboreshaji na usimamizi wa mikopo midogo midogo nchini *(Umbrella Credit Project - UCP)* na Mradi wa kudhamini mikopo midogo kupitia Benki ya Posta *(Mutual Guarantee Fund - MGF).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, *NIGP* inategemea kuikamilisha utekelezaji wa miradi iliyotajwa hapo juu kwa kutumia fedha zinazotarajiwa kutolewa na Serikali ya Ubelgiji. Aidha, ipo mipango ya muda mrefu ya kuanzisha miradi inayolenga kuongeza kipato katika Mikoa mitatu, Kigoma, Kagera na Pwani. Serikali ya Ubelgiji imeahidi kutoa kiasi cha shilingi 2.17 bilioni kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi hiyo umepangwa kufanyika katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2003 hadi 2007. Hadidu za rejea zimeshaandaliwa tayari kwa ajili ya mtaalam atakayefanya tathmini ya kuanzishwa kwa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kuwa shughuli zote kuu zilizokusudiwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2002/2003 zilitekelezwa na kufikia hatua za kuridhisha. Katika kipindi kijacho, Serikali inakusudia kufanya mapitio ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini ili kuboresha utekelezaji kwa lengo la kupata mafanikio zaidi. Mkazo utakuwa kuboresha uratibu, ufuatiliaji na kuhimiza ushirikishwaji kamili wa watu maskini na wadau wengine katika kupanga, kusimamia, kutekeleza na kutathmini jitihada za kupunguza umaskini.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais itazingatia maoni yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira tarehe 4 Julai 2003 katika kipindi cha kuelimishana na kubadilishana uzoefu kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Ufuatiliaji *(Poverty Monitoring Master Plan - PMMP),* kuhusu umuhimu wa kushiriki kwa Bunge na kuwa na Kamati ya ukaguzi katika utendaji *(Committee on Reality Checks).* Hoja hii ni ya msingi kabisa, na Ofisi ya Makamu wa Rais itajitahidi kila itakavyowezekana Kamati iundwe itakayohusisha Waheshimiwa Wabunge na Halmashauri za Wilaya. Kamati hii itatoe taarifa za tafiti na maoni yake kupitia TAMISEMI, kwa lengo la kuboresha sera na mikakati ya kupambana na umaskini, kuboresha mazingira yatakayotoa nafasi sawa kwa wanawake na wanaume kushiriki kikamilifu katika kazi ili kuinua ubora wa maisha ya Watanzania na kuleta maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la ufuatiliaji, unapoonekana ukiukwaji wa utekelezaji wa mipango, uvurugaji wa amani, wananchi kutotendewa haki na ufujaji wa raslimali ambavyo vyote vitaathiri kufikia malengo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kwa kupeana taarifa ili hatua ziweze kuchukuliwa. Wadau wote ni washiriki wa utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini na Mpango wa Ufuatiliaji wa jitihada za kuondoa hali ya umaskini.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapunguziwa makali kutokana na tatizo la umaskini, Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* imewawezesha wananchi kutekeleza miradi mbalimbali katika maeneo yao. Katika kipindi kilichopita, wananchi walianzisha na kutekeleza miradi 1,039 ya jamii na miradi 185 ya kujinusuru *(safety nets)* ilianzishwa na kutekelezwa. Kati ya hiyo miradi ya Jamii 469 na miradi 65 ya kujinusuru *(safety nets)* imekamilika na inatoa huduma kwa walengwa. Miradi iliyobaki 570 ya jamii na 120 ya kujinusuru bado inatekelezwa na itakamilika katika mwaka wa fedha 2003/2004. Miradi hiyo yote ina thamani ya dola za Kimarekani 24,736,490 na inatekelezwa katika Wilaya 42 za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, silaha mojawapo katika kupambana na umaskini ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapatiwa nyenzo za kutumia ikiwa ni pamoja na ujuzi wa kuendesha shughuli zao. Kwa kutambua hilo, Serikali kupitia Mfuko huu ilitoa mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati za Utekelezaji wa Miradi kuhusu utunzaji wa mahesabu ya fedha, taratibu za ununuzi wa vifaa, usimamizi wa utekelezaji wa

miradi, utunzaji wa vifaa vya miradi na uandaaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi. Wanakamati 10,065 katika vijiji vinavyotekeleza miradi wamepewa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa miradi ya *TASAF* katika kuwapunguzia wananchi umaskini, na kwa kuzingatia mafanikio yaliyopatikana katika maeneo ambayo Mfuko huu unafanya kazi, maandalizi kwa ajili ya awamu ya pili ya *TASAF* yataanza katika mwaka wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* inatekelezwa, Bunge hili Tukufu lilipitisha Muswada wa Sheria ya *NGOs* mwezi Novemba, 2002 na kuidhinishwa na Mheshimiwa Rais kuwa Sheria mwezi Desemba, 2002. Ofisi ya Makamu wa Rais iliandaa kanuni za kusimamia usajili na uendeshaji wa *NGOs* na kuzifikisha kwa wadau watoe maoni ili kuziboresha. Baada ya kuingiza maoni hayo, kanuni ziliwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuidhinishwa. Tarehe rasmi ya kuanza kutumika kwa sheria hii itatangazwa kwenye gazeti la Serikali baada ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuidhinisha kanuni na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sheria ya *NGOs* unahitaji kwanza mambo muhimu mawili kufanyika. Kwanza, *NGOs* wenyewe kuunda chombo chao cha Kitaifa, yaani Baraza la Taifa la *NGOs (National Council for Non Governmental Organizations)* ambacho kitakuwa chombo chao maalum cha kuwakilisha *NGOs* zote nchini kitakachokuwa huru na kujidhibiti chenyewe. Chombo hiki pia kitajiamulia muundo wake, kanuni na taratibu zake katika kuzingatia mfumo shirikishi wa *NGOs* nchini. Ili kuhakikisha kwamba chombo hiki kinaundwa kwa ridhaa ya *NGOs,* Ofisi ya Makamu wa Rais ilimwezesha kufanyika kwa mkutano wa *NGOs* kwenye Hoteli ya Morogoro kuanzia tarehe 10 hadi 11 Juni, 2003.

Kwa kuzingatia umuhimu wa kutumia mfumo shirikishi katika kuwapata washiriki kwa kutumia demokrasia, tuliwaomba Wakuu wa Wilaya kuitisha mikutano ya *NGOs* kwenye Wilaya zao. Katika mikutano hiyo walichagua mwakilishi wao mmoja kila Wilaya. Wawakilishi hawa wa *NGOs* walipokutana mjini Morogoro, waliweka utaratibu mzuri wa kuwapata wajumbe 30 watakaounda Baraza la Taifa la *NGOs*. *NGOs* zote zitachagua mwakilishi wao mmoja kila mkoa na hivyo kuwa na wajumbe 21. Nafasi 9 zinazobaki ni kwa ajili ya wawakilishi toka mitandao ya Kitaifa ya *NGOs, NGOs* za kinyanja, mitandao ya kimkoa ya *NGOs,* makundi maalum na *NGOs* za Kimataifa.

Baraza la Taifa la *NGOs* litachagua wajumbe wanne wa *NGOs* watakaoteuliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Kuondoa Umaskini) kuwa Wajumbe wa Bodi ya Uratibu wa *NGOs (The Non Governmental Organizations Coordination Board).*

Pili, Serikali itaanzisha Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* na kuteua wajumbe watakaounda na kukiendesha chombo hiki kwa mujibu wa Sheria ya *NGOs.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali inatambua na kuthamini mchango wa *NGOs* katika Maendeleo ya Taifa na wachangiaji muhimu katika Pato la Taifa. Pamoja na mchango huo mzuri wa *NGOs,* bado imekuwa vigumu kwa Serikali kubaini kiwango ambacho sekta ya *NGOs* wanachangia kutokana na kutokuwepo mfumo wa uwazi na uwajibikaji ili kurahisisha ukusanyaji taarifa katika utendaji kazi wao.

Naamini pamoja na nia nzuri ya Serikali kuweka mazingira bora ya *NGOs* kuendesha shughuli zao nchini, pia ukusanyaji wa taarifa za *NGOs,* ni wa msingi sana katika kuhuisha mipango yetu ya maendeleo. Bila shaka mtakubaliana na mimi kwamba tangu sheria hii ipitishwe na Bunge letu Tukufu, kumekuwapo hisia na maoni tofauti toka kwa wadau na hata baadhi ya vyombo vya habari kuwa inalenga kuzibana na kuzifanyia kaguzi za mahesabu ya fedha *NGOs.*

Mheshimiwa Spika, napenda kupitia Bunge lako Tukufu kuwafahamisha wananchi kwamba si nia ya Serikali kuzibana *NGOs* bali kuweka utaratibu ambao *NGOs* watakuwa wazi na kuwajibika katika utendaji kazi wao. Chini ya utaratibu huu Serikali itaweza kutambua kiwango cha mchango wa *NGOs* katika Pato la Taifa.

Aidha, wananchi wataweza kupata fursa ya kuona taarifa za kazi za *NGOs* na mahesabu kupitia Ofisi ya Msajili wa *NGO.* Uwazi wa uwajibakaji wa *NGOs,* kwa wananchi ambao ndio walengwa wakuu utasaidia kupunguza malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza sehemu mbalimbali nchini. Ikumbukwe kwamba Serikali imekuwa ikihimiza kuhusu dhana ya uwazi na uwajibikaji katika utendaji kazi wetu, sio kwa *NGOs,* tu bali taasisi zote chini ikiwemo Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba takwimu sahihi za shughuli za *NGOs* zinapatikana kwa matumizi ya wadau ikiwemo Serikali, Ofisi ya Makamu wa Rais itaanzisha Benki ya takwimu za *NGOs* ambayo kupitia utoaji taarifa pamoja na usajili wa *NGOs* tutaweza kuandaa kitabu cha orodha ya *NGOs* au *Green Book* ambacho kitakuwa kinafanyiwa marejeo kila mwaka.

Kitabu hiki kitatoa mwanga kuhusu idadi ya *NGOs* nchini, shughuli wanazozifanya kisekta, Kiwilaya na Kimkoa. Taarifa hizi pia zitatumika kikamilifu katika ngazi ya Serikali za Mitaa kwa kupanga mipango yao ambayo itahusisha pia programu au miradi ya *NGOs* katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya *NGOs* kifungu cha 25 (4) kinazuia mtu au *NGO* kufanya kazi ambazo kisheria zinatakiwa kufanywa na Baraza la Taifa la *NGOs.* Kutokana na tafsiri potofu, kipengele hiki kimeonekana kama kikwazo au zuio kwa mitandao na Mashirika miamvuli kufanya kazi zao kwa ufanisi kiasi cha kusababisha wasiwasi miongoni mwao. Napenda kuwahakikisha Waheshimiwa Wabunge, Sekta ya *NGOs* na wananchi kwa ujumla kwamba hakuna mtandao au Shirika mwamvuli watakaozuiwa kufanya kazi zao kutokana na kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la *NGOs.* Ifahamike wazi kwamba Sera ya Taifa ya *NGOs* inahimizwa kuundwa kwa vyombo hivi na pia Tanzania ni kubwa, hivyo Mashirika haya na mitandao watakuwa vyombo muhimu katika kuhakikisha kwamba Baraza la Taifa la *NGOs* linafanikisha malengo yake kwa kuwa ni chombo chao wenyewe.

Hii ina maana kwamba Mashirika miamvuli kama vile *TANGO, TACOSODE, RANGO, UNGO, ANGONET, LINGONET, MANGONET* na mengine mengi yatakayoundwa wataendelea kuwepo na kutekeleza majukumu ya kuanzishwa kwao. Tunategemea kwamba watakuwa tayari kuhakikisha kwamba chombo chao kinafanya kazi kwa ufanisi kwa kuwa ni sauti yao Kitaifa. Kwa hiyo, ile dhana ya ushindani na wasiwasi ambayo ilianza kujitokeza miongoni mwa mitandao na Mashirika miamvuli dhidi ya Baraza la Taifa la *NGOs* ifutike kabisa. Si nia ya Serikali kudhoofisha Sekta ya *NGOs* bali kuiimarisha ili iweze kutoa huduma inayostahili kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, shughuli za *NGOs* zimegawanyika Kisekta na huendeshwa katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Ili kurahisisha uratibu wa *NGOs,* kila Wizara Kisekta itatakiwa kuteua Ofisa mmoja ambaye atakuwa kiungo kikuu kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara husika. Kupitia Ofisa huyu tutaweza kupata takwimu za *NGOs* Kisekta na hivyo kurahisisha uratibu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, jumla ya wafanyakazi 16 wameajiriwa kazi na 26 wamepandishwa vyeo katika ngazi mbalimbali baada ya kukidhi masharti ya miundo ya Utumishi. Aidha, jumla ya watumishi 38 wamehudhuria mafunzo nje na ndani ya nchi ili kuboresha uwezo wa kufanya kazi na kuongeza ufanisi wa kazi na uwajibikaji. Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuchukua hatua za kuwapandisha vyeo watumishi wake pamoja na kuwapatia mafunzo wale wanaostahili kama njia mojawapo ya kuwawezesha kufanya kazi zao kwa kutilia maanani mabadiliko makubwa ya kiuchumi, teknolojia na kijamii yanayoendelea hapa nchini na duniani kote kwa kuzingatia suala zima la utandawazi.

Mheshimiwa Spika, katika kuchukua hatua mbalimbali za kuwashirikisha watumishi, Baraza la Wafanyakazi, Ofisi ya Makamu wa Rais lilizunduliwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais tarehe 20 Novemba, 2002 katika Manispaa ya Morogoro. Aidha, Baraza lilifanya kikao chake kingine tarehe 14 Machi, 2003 Mjini Zanzibar ambako masuala mbalimbali ya watumishi pamoja na mapendekezo ya bajeti hii yalijadiliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Ofisi ya Makamu wa Rais itakamilisha mipango yenye mikakati *(Strategic Plan)* ya uboreshaji wa huduma zitolewazo na Idara katika hatua yake ya kutekeleza mfumo wa utendaji kazi Serikalini wa kupima matokeo ya kazi *(Result Oriented Management).*

Katika kukabiliana na tatizo sugu la ufinyu wa nafasi katika ofisi mbalimbali, Ofisi ya Makamu ya Rais inatarajia kuanza ujenzi wa Ofisi Mjini Zanzibar baada ya ujenzi wa uzio kukamilika katika mwaka wa fedha 2002/2003 katika eneo la Mwanakwerekwe.

Aidha, Ofisi ya Dar es Salaam tunatarajia kuanza ujenzi wa kupanua jengo la sasa baada ya michoro na uchunguzi wa udongo kukamilika katika mwaka wa fedha 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, ili kupiga vita kuenea kwa maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Ukimwi, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuwaelimisha wafanyakazi wake wote, wa ngazi zote, kuhusu ugonjwa wa Ukimwi, athari zake mahali pa kazi na kwa jamii, pamoja na njia bora za kujikinga na ugonjwa huu. Katika hatua hii tumesisitiza umuhimu wa wafanyakazi kubadili tabia zao na kuacha uasherati.

Aidha, katika kupiga vita vitendo vya rushwa wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Rais walifanyiwa semina iliyoendeshwa na *PCB*. Pamoja na mambo mengine, wafanyakazi walielezwa athari za rushwa katika jamii na sehemu za kazi na kusisitizwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za kazi na kuwa wazi na wakweli katika kutekeleza majukumu yao, ikiwa ni pamoja na kuwa pia waaminifu kwa mwajiri wao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Bwana Raphael Mollel, Wakurugenzi na wafanyakazi wote kujituma na kutekeleza majukumu yao ipasavyo katika kipindi kilichopita.

Namshukuru pia Mpiga Chapa wa Serikali kwa kuchapa maelezo haya kwa unadhaifu wa hali ya juu kabisa. Napenda pia kuwashukuru Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Sekta mbalimbali, Sekta binafsi na wananchi wote kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika juhudi za kuondoa umaskini.

Natoa shukrani za pekee kwa Wahisani mbalimbali ambao wamekubali na wameendelea kusaidia Serikali ya Tanzania kugharamia miradi mbalimbali inayotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Wahisani hao ni Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Maendeleo *(UNDP),* Shirika la Misaada na Maendeleo la Sweden *(SIDA), UNICEF,* Shirika la Misaada na Maendeleo la Norway *(NORAD),* Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* Shirika la Denmark, Serikali ya Japan, Uholanzi, Finland, Ireland, Shirika la Maendeleo la Uingereza *(DFID),* Shirika la Maendeleo la Marekani, *(USAID),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuendeleza Viwanda *(UNIDO),* Shirika la Maendeleo la Uswisi *(SDC),* Shirika la Kuenea kwa Hali ya Jangwa Duniani, Mfuko wa Mazingira wa Dunia - *GEF,* Shirika la umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira *(UNEP),* Shirika la *OXFAM* na wengineo. Tunawashukuru kwa kuchangia kwa hali na mali juhudi zetu za kujiletea maendeleo endelevu.

Mwisho, ingawa si mwisho kwa umuhimu nimalizie shukrani hizi kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioshinda katika uchaguzi mdogo wa tarehe 18 Mei, 2003 na kujiunga na Bunge hili Tukufu. Pongezi za pekee ziwaendee Waheshimiwa Wabunge wapya wa CCM na hasa Mheshimiwa Edward Nziriye Ndeka, wa Jimbo la Uchaguzi la Kigoma Kusini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha makadirio ya matumizi ya fedha kwa kipindi cha mwaka 2003/2004 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004 jumla ya shilingi 1,423,363,400/= zinaombwa kugharamia Ofisi ya Makamu wa Rais *(Private Office).* Kiasi cha shilingi 124,292,549/= ni kwa ajili ya kugharamia mishahara na shilingi 1,299,070,851/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengine ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004 Ofisi ya Makamu wa Rais inaomba jumla ya shilingi 15,156,191,800/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, kiasi cha shilingi 576,864,198/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengine.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi 10,298,000,000/= kitapelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya shughuli za Muungano *(Union Government Contribution).* Kiasi cha shilingi 9,892,070,200/= kinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya hizo shilingi 671, 699,700/= ni fedha za ndani na shilingi 9,220,370,500/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIB (k.n.y. MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, kufuatana na kifungu Na. 81(1) cha Kanuni za Bunge, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha uliopita wa 2002/2003, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika**,** huu ni mwaka wa kwanza kupata nafasi ya kupitia, kujadili na kuchambua Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais chini ya Mfumo mpya wa Kamati za Kudumu za Bunge, ambao ni wa Kiwizara. Aidha, katika kupitia Ofisi hii masuala yafuatayo yalijadiliwa Dira ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Majukumu ya Ofisi.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Mwaka 2002/2003 hadi mwezi Aprili, 2003, ukiwemo utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kisekta ya Maendeleo ya Jamii katika kipindi cha mwaka 2002/2003, suala la Muungano, mazingira, kuondoa umaskini na shughuli za *NGOs.*

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa Ofisi ya Makamu wa Rais unatokana na Dira yake ambayo ni: "Kuwa na jamii huru inayojipatia mahitaji yake muhimu, inayoshikamana na yenye maendeleo endelevu na raslimali za kutosheleza jamii ya sasa na vizazi vijavyo bila kuathiri mazingira."

Mheshimiwa Spika, dira hii ina mwelekeo unaolenga kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kusimamia na kuendeleza shughuli zote za Muungano, kubuni mikakati ya kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya jitihada za kuondoa umaskini ili kufikia lengo la Taifa la mwaka 2025 *(Vision 2025),* kubuni na kusimamia Sera ya Hifadhi ya Mazingira na matumizi bora ya raslimali na kutoa Mwongozo na kuratibu Mashirika yasiyo ya Kiserikali yaani *NGOs*.

Mheshimiwa Spika, Kikatiba, Ofisi ya Makamu wa Rais imepewa kutekeleza majukumu ya kutambua na kuchambua masuala ya Muungano na kupanga utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wake, kusimamia utekelezaji wa Sera na mikakati ya kuondoa umaskini kwa lengo la kuleta maendeleo endelevu kwa Watanzania wote, kulinda na kuendeleza amani na kuhakikisha raslimali yetu inatumiwa na wananchi wote kwa maendeleo yao, kuandaa Sera, Sheria, mikakati na taratibu za kusimamia utekelezaji wake, kutathmini utekelezaji wa Sera ya Mazingira na mikakati yake na kukuza weledi juu ya uhusiano katika mazingira, umaskini na maendeleo endelevu, kwa lengo la kuongeza ushiriki wa wananchi katika utunzaji wa mazingira, kukuza ushirikiano wa Kimataifa kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Taasisi za Kimataifa kwa kuweka mikakati ya kupambana na umaskini na kuboresha mazingira na kuratibu na kutoa mwongozo kuhusu shughuli za *NGOs* na Jumuiya za Wananchi yaani *CBOs*.

Mheshimiwa Spika, Ofisi hii imeweza kuyatekeleza na kutoa maelezo ya kina kwa maagizo yote kama ilivyohitajika na ile iliyokuwa Kamati ya Kisekta ya Maendeleo ya Jamii. Maagizo hayo yaligusa karibu masuala yote yanayohusu mambo ya Muungano, Mazingira, kuondoa umaskini na *NGOs.* Kwa jumla, Kamati yangu imeridhika na utekelezaji huo. Aidha, katika hili, napenda nichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi wa Ofisi ya Makamu wa Rais na wataalam wao kwa kazi nzuri walioifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika na mafanikio ambayo Ofisi ya Makamu wa Rais imeyapata kwa kuendeleza utekelezaji wenye azma ya kuimarisha na kuboresha shughuli mbalimbali za uratibu wa masuala ya Muungano. Aidha, kwa kufanya hivyo, Ofisi imewezesha kufanyika maamuzi mbalimbali, katika nyanja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja imeundwa na Wajumbe wake kuteuliwa. Nampongeza Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, ambaye ni Mwenyekiti wa Tume hiyo, pamoja na Wajumbe wenzake kwa kuteuliwa kuongoza Tume, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeanza kutoa gawio la asilimia 4.5 kutokana na misaada inayotolewa na Wafadhili, faida ya Benki Kuu nayo itakuwa ikitolewa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, sheria ya kuratibu masuala ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* imetungwa, miradi ya maendeleo yenye sura ya Muungano huko Zanzibar, inaendelea kutekelezwa. Kwa mfano ujenzi wa Ofisi ya Bunge ya Jamhuri ya Muungano, Kituo cha Utafiti na Viumbe vya Baharini na Jengo la Benki Kuu ya Tanzania na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* unatekelezwa Tanzania Zanzibar pia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuendelea kutekeleza ipasavyo maamuzi niliyoyataja hivi punde, Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kusimamia na kuratibu shughuli za kuboresha ushirikiano baina ya Wizara na Asasi mbalimbali za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na za Serikali ya Muungano wa Tanzania katika maeneo yasiyo kuwa ya Muungano. Kamati inapongeza utaratibu huu na inashauri uimarishwe zaidi kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mafanikio iliyoyapata katika kutekeleza, kusimamia na kuratibu shughuli za mazingira, zikiwemo kuratibu utekelezaji wa Sera ya Mazingira, kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira ambayo Tanzania ni mwanachama, kuratibu utekelezaji wa Miradi na Programu za Hifadhi ya Mazingira na kuandaa mikakati ya semina, kongamano na warsha zinazohusu uhifadhi bora wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefurahishwa na jinsi Ofisi ya Makamu wa Rais inavyoendelea na kuratibu Mifuko ya kuondoa umaskini (kama vile *SELF* na *TASAF)*. Huduma hii ni muhimu na inahitajika sana kwa wananchi. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa na kusambaza Mfumo wa ufuatiliaji wa umaskini. Mfumo huo umeandikwa kwa lugha rahisi ya Kiingereza na Kiswahili ili kuwawezesha wadau kuhamasika na kuufahamu vizuri na hatimaye kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati iliona wazi kuwa Mfumo huu wa ufuatiliaji wa umaskini kwa lengo la kuondoa kabisa haukuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge na Madiwani. Kwani, makundi haya ni muhimu sana katika kufanikisha mkakati wetu wa kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa pia na kazi nzuri iliyofanywa na Ofisi katika kuratibu utekelezaji wa shughuli za Sekta ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs),* kwani imeweza Sera ya *NGOs* imechapishwa na kusambazwa; Sheria ya *NGOs* imetungwa na Kitengo cha *NGOs* kimeimarishwa.

Mheshimiwa Spika, kama utakavyoona, majukumu haya ni mazito sana. Tunaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa jitihada zake za kuweza kuyatekeleza majukumu yote hayo na mengineyo kwa ufanisi mkubwa na kwa azma ya kuwatumikia Watanzania ili waweze kuendesha maisha yao ya kila siku kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia na kuchambua kwa makini taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais, yafuatayo ni maoni, mapendekezo na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, ili kudumisha Muungano, Ofisi ya Makamu wa Rais haina budi kuorodhesha kero zote ambazo hazijashughulikiwa na kuona ni hatua gani zinachukuliwa ili kupunguza, kama si kuondosha kabisa kero hizo. Makamu wa Rais hana Ofisi Tanzania Bara wala Tanzania Zanzibar, hata Idara zake zimesambaa mahali tofauti tofauti katika Jiji la Dar es Salaam. Wakati umefika kwa ofisi muhimu kama hii kuwa na majengo yake ambayo yanajulikana yako wapi. Kwa upande wa Zanzibar, hatua zaidi zichukuliwe kufanikisha ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuunganisha nguvu za Sheria mbalimbali zinazosimamia masuala ya mazingira nchini, Kamati inapendekeza Sheria Mama ya Mazingira itungwe ili kuondoa migongano ya Sheria zinazohusu mazingira. Taarifa ambayo Kamati inayo ni kuwa zipo zaidi ya Sheria 80 za Mazingira hivi sasa. Lakini hakuna utaratibu wa uratibu na kwa kuwa Sheria hizo zilitungwa wakati tofauti tofauti, na nyingine kupitwa na wakati, huu ni wakati mzuri wa kutunga Sheria mama kwa suala la Mazingira. Kwani, mazingira si kukata miti au kuchoma moto tu, bali ni zaidi ya hapo, na ni suala linalohusu uhai.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii, Kamati inapenda kutoa pongezi nyingi sana kwa Kampuni ya mafuta ya *BP* kwa kuleta mafuta ya *petrol* ambayo hayana risasi. Tatizo la kutumia mafuta ya *petrol* yenye risasi kwa magari yetu lina madhara makubwa yakiwemo saratani, ugonjwa wa mtindio wa ubongo na kadhalika. Wananchi wengi wanapenda kulima bustani karibu na barabara. *Fumes* za magari huenda kwenye mboga hizo na hivyo kusababisha risasi yaani *mercury,* kutoka kwenye mafuta hayo ya *petrol* kuangukia kwenye mboga hizo.

Aidha, wananchi wanazila kwani chembechembe za risasi hizo hazitoki kwenye mboga hata ukiosha. Kwa hiyo, Serikali iangalie uwezekano wa kuendeleza jitihada zilizofanywa na Kampuni ya *BP* kuleta mafuta ya *petrol* yasiyo na risasi kwa matumizi ya magari. Inafahamika kuwa mafuta hayo ni aghali kidogo, lakini afya za watu ni aghali zaidi. Hivyo, Kampuni ya *BP* iungwe mkono ili Makampuni yote yaanze kuleta mafuta ya aina hiyo. Nchi nyingine Duniani zinaanza kusahau aina ya mafuta ya gari tunayotumia sasa yenye chembechembe za risasi.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea Ziwa Jipe na Bwawa la Nyumba ya Mungu, Wilayani Mwanga.

Mheshimiwa Spika, Ziwa Jipe lipo katika hatari ya kutoweka kutokana na magugu yaliyojaa ndani ya Ziwa. Hivi tunavyoongea upande wa Tanzania Ziwa hili ni kama limefutika. Wananchi walizoea kuvua samaki katika Ziwa hili. Hivi sasa kwa upande wa Tanzania hakuna shughuli za uvuvi kabisa. Kulikuwa na wavuvi wapatao 8,000, aidha, wote wamehamia Bwawa la Nyumba ya Mungu ambako uvuvi wake umepita kiwango. Yapo matumizi makubwa ya uvuvi haramu, kiasi kwamba samaki hata wadogo wameanza kutoweka. Magugu ya kutoka Ziwa Jipe nayo yananyemelea Bwawa la Nyumba ya Mungu. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kwanza ichukue hatua mahususi ya kuliokoa Ziwa Jipe ili lisitoweke. Tunafurahi kuwa zipo hatua kadha wa kadha zinazochukliwa kuokoa Ziwa hili. Lakini ufuatiliaji wake unakwenda pole pole mno. Ikiwezekana iundwe Kamati ya Wataalamu wa kutoka Asasi za ndani na za nje ya nchi kushughulikia tatizo la Ziwa Jipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, upo umuhimu wa kusimamia na kudhibiti uvuvi haramu katika Bwawa la Nyumba ya Mungu na huku wananchi wa eneo hilo wakiandaliwa utaratibu mbadala wa shughuli zao za kiuchumi. Utaratibu endelevu uwekwe ili kuzuia magugu ya Ziwa Jipe kuvamia Bwawa hili la Nyumba ya Mungu; kwani, pamoja na kupatikana samaki katika Bwawa hilo, pia ni chanzo cha umeme wa *Grid* ya Taifa.

Kamati yangu inapongeza miradi hii ya *TASAF* na *SELF.* Ni vizuri ikasambaa nchi nzima, kwani umaskini umesambaa nchi nzima. Kamati inatambua kazi nzuri inayofanywa na Mradi wa *TASAF.* Wakati Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais anayeshughulikia Utumishi akiwasilisha hotuba ya Makadirio ya Utumishi na Utawala Bora, *TASAF* ilipenyezwa katika hotuba yake. Narudia kusema kuwa ilipenyezwa humo.

Mtu yeyote aliyesoma vizuri hotuba hiyo ilionekana kama ni kipengele ambacho kilipenyezwa tu, hakikuwa mahali pake. Tunafahamu kuwa *TASAF* imetokana na juhudi zake Mheshimiwa Rais na imefanikiwa sana. Lakini Serikali nzima inasimamiwa na Mheshimiwa Rais, hata Bajeti yote hii ni ya Serikali anayoisimamia Mheshimiwa Rais. Hivyo, *TASAF* inakaa vyema katika dhana nzima ya kuondoa umaskini na siyo Utumishi wa Umma. Kwa hiyo ni vizuri suala zima la kuondoa umaskini na *TASAF* vikawa pamoja ama katika Ofisi ya Rais au Ofisi ya Makamu wa Rais, kwani ilivyo hivi sasa inachanganya kidogo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza Ofisi ya Makamu wa Rais iangalie tena mfumo wa ufuatiliaji wa umaskini ili wawakilishi wa wananchi yaani WaheshimiwaWabunge na Madiwani, washiriki katika ngazi zinazowahusu kule kwa wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kamati, kwa jumla imekubaliana na ombi la Ofisi hii kwa Bunge lako Tukufu la kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Makamu wa Rais, Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004 naliomba Bunge lako Tukufu liyapitishe.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizoombwa na Ofisi ya Makamu wa Rais chini ya mafungu yake mawili ni kama ifuatavyo, Fungu 26 - Makamu wa Rais ni shilingi 1,423,363,400/=, Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais ni shilingi 25,048,262,000/=. Jumla ni shilingi 26,471,625,400/=.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi wote wawili wanaoshughulikia masuala ya Muungano, Mazingira na Kuondoa Umaskini, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Katibu Mkuu wa Ofisi hii, Bwana Raphael Mollel, pamoja na Wataalam na Watendaji wengine kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa kwa makini mpango na bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira kwa ushirikiano walionipa hadi kuniwezesha kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, nawashukuru Katibu wa Bunge Bwana Kipenka Mussa na Katibu wa Kamati hii, Bwana Sam Manamba kwa kazi nzuri waliozozifanya za kuratibu ipasavyo shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, niwataarifu wachangiaji wanne wa kwanza watakaochangia katika hoja hii. Wa kwanza ni Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah na Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma. Hao ndiyo wachangiaji wanne wa kwanza.

**MHE. ALI SAID JUMA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake, ambayo yametuwezesha sote kukutana hapa asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuitumia fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kuondoa umaskini na mazingira, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu cha 43 (5) (b) (c) toleo la 2003. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wote wa Jimbo la Kojani - Pemba, kwa kunichagua kwa kura nyingi mno kuwa Mbunge wao. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote wapya na wa Vyama vyote kwa kuingia katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wengine wa Bunge hili, kuwapongeza sana na kuwatakia kila la kheri, Waheshimiwa Wabunge wenzetu, Mheshimiwa John Malecela na Mheshimiwa Anne Kilango, kwa kufunga pingu za maisha wiki chache zilizopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru sana Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, kwa msaada wake mkubwa wa kizalendo na wa kiungwana sana, ambao kwa kiasi kikubwa umefanikisha utayarishaji wa hotuba hii. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Mbunge, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais kuondoa umasikini kwa ushirikiano wake mzuri. Wote ninawambia hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwashukuru sana Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa Mbunge wa Gando, Mheshimiwa Karim Said Othman Mbunge wa Chambani na Mheshimiwa Masoud

Abdalla Salim  Mbunge wa Mtambile kwa kufanikisha hotuba hii. Baada kusema  hayo, sasa nakuja katika hotuba yangu halisi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la umaskini uliokithiri katika Tanzania haliwezi kuendelea kuelezwa kijuujuu kwa kusingizia ukame, vita vya Iddi Amin wa Uganda, mafuriko, na ubepari  wa Marekani kama ambavyo tumekuwa tukihubiriwa kwa uongo kadhaa sasa hivi.  Sote tunakubali kwamba sababu za kihistoria zipo, kwa mfano biashara ya utumwa, ukoloni mkongwe na hata ukoloni mamboleo.

Hata hivyo, sababu za kihistoria zisitumike kugubika sababu za kujitakia au zile za kujitengenezea wenyewe.  Ni wazi kwamba mambo kama sera mbaya, rushwa miongoni mwa viongozi wa juu na wa kati wa kisiasa na Kiserikali, matumizi makubwa ya kijeshi, kutowajibika kiuongozi na kushindwa kuwa karibu na wananchi na kujifunza pia kuyahisi matatizo yao yana mchango mkubwa katika kupalilia umaskini.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa umakini katika upangaji mipango ya Kiserikali, na hasa ile ya kiuchumi, huzaa tatizo la matumizi yasiyo makini ya raslimali muhimu za Taifa. Vipaumbele *(priorities)* visipopangwa vema vinaleta matatizo ya kujitakia, kwa mfano wananchi kutegemea mitumba katika nchi inayolima pamba kwa wingi na ambayo inavyo viwanda vingi vya nguo.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza pia kuona nchi ndogo na zenye maliasili chache kama Sychelles na Bahamas, zina maendeleo makubwa katika sekta ya utalii, kuliko nchi kubwa ya Tanzania, ambayo ina vivutio vingi sana vya utalii, ukilinganisha na nchi hizo ndogo, ambazo sana sana zinategemea fukwe zake tu, ambazo hata hivyo zina eneo dogo kuliko fukwe za Tanzania, zinazoanzia Mikindani - Mtwara hadi kule Raskazone - Tanga, ukiondoa ufukwe wa Ziwa Victoria. Tatizo ni vipaumbele, kianze kipi na kipi kisubiri.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za 2000/2001, asilimia 18.7 ya Watanzania wamekuwa wakiishi chini ya kiwango cha mstari wa umaskini wa chakula *(food poverty line)* na asilimia 33.7 wamekuwa wakiishi chini kabisa ya kiwango cha umaskini unaohusisha kukosa mahitaji muhimu ya kimaisha *(basic needs poverty line).*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba asilimia 87 ya Watanzania maskini wanapatikana vijijini, asilimia 13 ya Watanzania maskini sana wapo mijini na wanaishi kwa vipato duni au visivyoaminika na wengi wanapatikana katika sekta isiyo rasmi. Ajira katika sekta rasmi, hasa miongoni mwa vijana na hasa wasichana ni finyu  mno, hawana kabisa namna za kudunduliza mitaji, wanaishi katika maeneo ya pembezoni mwa miji mikubwa, ambayo hayajapimwa, mabondeni na kadhalika. Wanaishi bila ya matumaini na wako mbali mno na vyombo vya kutoa maamuzi na pia watoaji wa maamuzi, hasa yale ya kisiasa na kiuchumi. Wananchi maskini katika maeneo ya miji, pia hufanya kazi na shughuli zao katika mazingira ya hatari kwa afya zao na hawana hifadhi yoyote ya kijamii kama bima, pensheni, uhakika wa huduma za tiba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa huduma muhimu za kijamii kama majisafi na salama, elimu na afya, pia kukosa au kucheleweshewa haki nyingine muhimu za kiraia, ni dalili muhimu za umaskini wa kupindukia.  Mpaka kufikia mwaka 2000, ni asilimia 48.5 tu ya wananchi wa vijijini waliokuwa angalau na uwezekano wa kupata maji safi na katika miji ni asilimia 68 tu ya wananchi ambao wangeliweza kufikiwa na huduma ya maji safi.  Kwa mujibu wa takwimu za mwezi Machi 2003, Tanzania sasa inashika nafasi ya 71 kati ya nchi 106 katika uzito na kujichimbia kwa tatizo la rushwa, na hii ni kwa mujibu wa taasisi maarufu katika uwanja wa utawala bora duniani, iitwayo *Transparency International*.  Bado pia Tanzania inalo tatizo kubwa la ajira ya watoto, ambapo jumla ya watoto milioni 4.8 wapo katika ajira na tena kwenye mazingira ya hatari sana kiafya, hasa katika uchimbaji wa madini unaofanywa na wachimbaji wadogo wadogo wasiokuwa na huruma.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza yafuatayo ili kupunguza umaskini katika Tanzania kwa kujengwa kwa makusudi kwa tabaka la wazalendo watakaomiliki na kuwa injini ya uchumi, na hasa katika maeneo yenye mwelekeo wa uzalishaji *(production)* na siyo ugavi peke yake *(distribution),* hasa wa bidhaa za nje, kufanywa kwa uwekezaji mkubwa katika mambo ya utafiti na uendelezaji bidhaa mpya na huduma mpya *(research and development)* na hasa kwa kuziunga mkono kivitendo taasisi za utafiti wa kisayansi na kiteknolojia, na taasisi za elimu ya juu, kuhamasisha, siyo tu

uchumi wa kizalendo kwa lengo la kujenga uchumi wa kitaifa unaojitegemea, bali pia uzalendo wa kiuchumi, ambao ni muhimu katika suala zima la kuimarisha soko la ndani kwa kujenga utamaduni wa kutumia bidhaa zilizotengenezwa Tanzania na kuachana kabisa na tabia ya kuuza nje mali-ghafi, nyingi na kila inapowezekana kuuza nje bidhaa kamilifu na timilifu za viwandani.

Mheshimiwa Spika, pia kuzisimamia vizuri zaidi sekta za madini na utalii, ambazo zenyewe peke yake, zinao uwezo wa kulipeleka Taifa mbali sana kimaendeleo, kama kutakuwa na msukumo na ubunifu unaotakiwa, kupunguza sana gharama za elimu ya sekondari na elimu ya juu, hasa elimu ya sayansi, teknolojia na ufundi. Taifa haliwezi kupata maendeleo ya kisasa kwa kuwa na watu wenye elimu ya msingi tu. Taifa linahitaji sana raia wenye elimu ya juu na mabingwa katika fani nyeti za kiuchumi, kibiashara, kisayansi na kiteknolojia na kuwawezesha wananchi kujenga uwezo wa kuihoji, kuikemea, kuiasa na kuiwajibisha Serikali pale inapoonekana wazi kukiuka haki za msingi za wananchi au kuhatarisha maslahi muhimu ya Taifa. Pia kutumia vizuri zaidi fedha zetu na za misaada ya wahisani mbalimbali, kwa kujenga uwazi na uangavu zaidi katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Watanzania. Suala si kuhamasisha kulipa deni kubwa la Taifa tu, bali ni pamoja na kupata maelezo ya kina kuhusu matumizi ya fedha za misaada, mikopo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pia kujenga demokrasia ya kweli inayotawaliwa na ushindani wa haki, sheria halali na zinazokubaliwa na washindani wote, refarii anayeaminika na mwenye uwezo unaokubalika, na uwanja wenye vipimo sahihi kwa mchezo husika. Demokrasia ya kiini macho hailisaidii Taifa na ni kichocheo cha umaskini na demokrasia makini ina maana ya Serikali makini, na ni chanzo cha maendeleo makubwa kwa Taifa lolote lililo makini duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ulimwengu wa leo, maendeleo ya kiuchumi, kijamii, na hata kisiasa, hayaelezwi nje ya menejimenti bora ya mazingira. Ujumbe mkubwa wa ule mkutano wa Rio de Jeneiro *(Earth Summit)* mwaka 1992 na ule wa kule Johannesburg, Afrika ya Kusini *(Rio + 10)* mwaka 2002 ni suala zima la maendeleo yasiyotawaliwa na uchoyo wa kizazi cha sasa na kuyaharibu mazingira na hali hiyo kuhatarisha ustawi wa vizazi vijavyo.

Dunia nzima inataka maendeleo endelevu. Tume za Brundtland, Brandt na hata ile Tume ya Kusini iliyomhusisha sana Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, hoja yake kubwa ilikuwa ni kupambana na umaskini kwa kutumia pia mtizamo wa maendeleo endelevu. Ripoti ya Tume ya Kusini iitwayo Changamoto kwa Nchi za Kusini *(Challenge to the South)* imesheheni mikakati ya kupambana na umaskini kwa kupigania pia uboreshaji na menejimenti bora ya mazingira. Marehemu Mwalimu Nyerere, amekufa lakini mawazo yake mazuri yapo basi bora tuyatumie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania inalo tatizo kubwa sana la menejimenti duni ya mazingira na ndiyo maana misitu inafyekwa ovyo, Miji karibu yote ina uchafu wa kupindukia, uzalishaji katika sekta ya kilimo unazidi kudumaa, vyanzo vya maji vinaendelea kukauka, bidhaa taka zenye asili ya plastiki zimezagaa kila kona, uvuvi haramu wa kutumia baruti unazidi kuota mizizi na usafirishaji dhahabu kwa kutumia zebaki pia unazidi kushamiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado lipo tatizo la mbuga za wanyama na hifadhi za Taifa kuhujumiwa kwa namna moja au nyingine. Viwanda navyo vimeendelea kumwaga maji taka yenye sumu ovyo na magari mengi mabovu, yaliyojaa katika barabara za Miji mikubwa, hasa Dar es Salaam, yamekuwa yakiendelea kuhatarisha afya za watu kwa kuchafua hewa, kutokana na mifumo chakavu ya injini.

Mheshimiwa Spika, ujenzi katika maeneo yasiyopimwa na kwa namna ya kiholela pia ni aina ya menejimenti duni ya mazingira. Kelele za muziki wa dansi na kadhalika usiku wa manane jirani na makazi ya watu ni aina nyingine pia ya uchafuzi wa mazingira, kisaikolojia bila kusahau uchafuzi mkubwa wa fukwe za bahari na maziwa na takataka zinazotupwa na wasafiri wa mabasi ya Mikoani barabarani.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na utunzaji bora wa mazingira, Serikali inashauriwa kufanya yafuatayo, kwa manufaa ya Watanzania.

Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC),* lijipange vizuri zaidi kwa kuhakikisha kwamba linakuwa ni chombo huru na thabiti chenye uwezo wa kusimamia na kudhibiti mwenendo mzima

wa usimamizi wa mazingira Kitaifa. Chombo hiki ni muhimu katika kusimamia na kutoa maamuzi ambayo yanahusisha pia nguvu fulani ya kuadhibu au kupendekeza adhabu. Inashauriwa chombo hiki kiwe kikiongozwa na mtu huru, asiye na maslahi ya moja kwa moja na mambo yanayosimamiwa na *NEMC.* Ni rahisi kwa watu wengine wenye viwanda vinavyosimamiwa na Baraza hili katika eneo la mazingira, kuhofia kutotendewa haki na Bosi wa Baraza *(NEMC),* ambaye pia ni mmiliki wa viwanda, ambavyo vingine vinashindana na vya wale anaotakiwa kuwasimamia. Kuondoa wasiwasi wa kukosekana *fair play* na *level ground,* ni busara mwanaviwanda kutokuwa Bosi wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira. *(Makofi)*

Serikali ilivalie njuga tatizo kubwa la kuzagaa ovyo kwa mifuko ya plastiki (lambo) na chupa za maji za plastiki nchi nzima, mijini hadi vijijini. Kuwaongezea kodi watengenezaji wa mifuko hiyo kulikofanywa na Serikali kupitia Bajeti yake ya 2003/2004, bado si ufumbuzi wa tatizo hilo.

Utengenezaji wa mifuko hiyo upigwe marufuku na Teknolojia mbadala yenye uswahiba na mazingira *(Environmentally Friendly)* itafutwe. Kuzagaa kwa chupa za maji za plastiki pia kutafutiwe ufumbuzi wa kisayansi. Uwezekano wa uzungushwaji au *recycling* pia ufanyiwe utafiti. Ili kuwa na Taifa lisilo na kero ya kutapakaa mifuko ya lambo kila kona, lifanyike zoezi la kukusanya kisayansi mifuko hiyo ya rambo iliyokwishatupwa na zoezi hilo liendane na huo uzuiaji wa kisheria wa utengenezaji na uagizaji wa mifuko ya plastiki. Nchi za wenzetu hupendezeshwa kwa miti iliyopandwa vizuri na inayotunzwa vema, na pia maua yenye kuvutia, petu Tanzania ni mifuko ya plastiki kila rangi na kila kona na hakuna anayejali wala kushtuka. Kwa wananchi wengi mifuko hiyo ni kero kubwa ya Kitaifa. *(Makofi)*

Serikali ihakikishe miji ya yetu iko safi. Miji yetu ni michafu mno, na hasa nje ya vitovu vya miji hiyo. Miji mingi inanuka kwa uchafu uliokithiri na watendaji wote wa Serikali wapo kimya tu! Inashangaza pia kuona hata huu mji ambao Bunge linafanyia shughuli zake na pia ni Makao Makuu ya Wizara ya TAMISEMI na pia ipo Ofisi ya Waziri Mkuu na hata Ikulu ipo hapa na pia ni Makao Makuu ya Chama Tawala, ni mchafu kupindukia na watendaji wote wa Serikali Kuu, Mkoa, Manispaa, Kata, hadi Mitaa wapo kimya kama vile mambo yako shwari na hakuna tatizo! Hivi ni nini raha ya kuvaa suti za bei mbaya katikati ya marundo ya takataka yaliyojaa mjini kote? Hivi kweli Serikali inayoshindwa kuzoa takataka na kuzibua mifereji ya mji wa kawaida kama Dodoma, inawezaje Watanzania mambo makubwa, kwa mfano kuufuta umaskini ifikapo mwaka 2025 kama ilivyoelezwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo *(Vision 2025)? (Makofi)*

Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* ni lazima liwe na meno yanayong'ata na kucha zinazokwaruza, ili liweze kusimamia utekelezwaji *(enforcement)* wa maamuzi yake. Mpaka sasa Baraza hilo lina dalili nyingi za kuwa ni chui aliyetengenezwa kwa karatasi *(Paper Tiger)* au jibwa kubwa lisilo na meno *(Toothless Bulldog).* Suala si watu kuelimishwa na kushawishiwa kutunza mazingira tu, ila ni pamoja na kuadhibiwa vikali wale wanaoharibu kwa makusudi. Adhabu huwa ni mkakati muhimu katika kuhimiza mabadiliko ya tabia *(behaviour modification).*

Ni lazima sasa Serikali ianze kuwa na sera ya makusudi ya kuhakikisha Tanzania haiwi shimo la takataka la kutupa magari yaliyochoka na yasiyohitajika Marekani, Ulaya Magharibi na hasa Japan. Isije ikawa sisi tunachekelea misaada ya kujengewa barabara na Wajapan, kumbe wenzetu wanatupatia vichocheo vya kununua magari yaliyochoka toka Japan na kwa hali hiyo wao kuhamisha tatizo la uchafuzi wa hewa *(air pollution)* kutoka kwao kuja kwetu na kwa hali hiyo kuwaongezea Watanzania vifo kutokana na kansa ya mapafu pia magonjwa ya moyo na wakati huo huo wao kuvuna mapesa kwa kufanya biashara kubwa ya vipuri.

Tushukuru kwa misaada hiyo, lakini ni vizuri tukajua wazi si rahisi bepari wa kikweli kweli akafanya kazi ya kanisa au msikiti kwa maana ya *charity.* Kwenye ubepari lengo ni kupata faida kibao au *super profit* na si vinginevyo. Ubepari hauna cha bure. Hata kile kinachoonekana ni cha bure na ni hisani leo, ni lazima kina namna ya kukilipa, kama si kesho, basi ni kesho-kutwa. *(Makofi)*

Serikali ipambane na umaskini uliokithiri ili kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na kukata kuni na kutengeneza mkaa, kilimo na ufugaji wa kuhamahama, na ujenzi mabondeni na kwenye maeneo yasiyokubalika kimipango miji.

Serikali ipunguze bei ya umeme ili kuondoa vivutio vya watu kutumia mkaa na kuni kwa ajili ya kupikia. Teknolojia rahisi za kuzalisha nishati hasa vijijini kama umeme wa nguvu za mionzi ya jua *(solar energy),* nishati itokanayo na upepo *(wind energy)* na pia nishati kutokana na gesi ya samadi *(biogas)* ni lazima zipigiwe debe na zipunguziwe gharama kwa kila hali inaporuhusu kuyapenda mazingira ni gharama na Serikali itoe ruzuku kubwa kwa taasisi na Mashirika yanayojitahidi kueneza teknolojia sahihi na rahisi kama *TATEDO, Prospective College of Engineering and Technology* pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *SIDO, VETA* na kadhalika.

Kila hali inaporuhusu, kuwe na Wizara timilifu ya mazingira badala ya kulifanya jambo zito na la kidunia la mazingira ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Iwepo Wizara kamili ya mazingira, ambayo ni Wizara muhimu kwa uhai wa kibaiolojia wa Taifa. Ni jambo zito la mazingira na usimamizi wake ndiyo limeshikilia uhai wa Taifa, kwa maana ya ardhi, maji, misitu, wanyamapori, hali ya hewa, nishati ya umeme wa maji na kadhalika, utalii na mambo mengineyo mengi sana.

Mheshimiwa Spika, Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* ni sehemu muhimu ya raia wanaojua wajibu wao na wanaozijua haki zao kama raia *(Civil Society).* Mashirika hayo yametokea kuitwa sekta ya tatu kwa kujiweka katikati ya sekta ya dola (ambayo inadaiwa kuwa ni kimwaga kwa asili yake) na sekta binafsi ambayo hushutumiwa kwa kuwa na mkono wa birika na ubahili uliokithiri. Sekta hii ya *NGOs* na hata *CBOs* imekuwa ikimwagiwa sifa kwa kuwa jirani sana na wananchi wa hali ya chini, uwajibikaji mkubwa kutokea chini kuja juu, maamuzi sahihi na ya haraka, matumizi mazuri ya fedha, uwazi, ushirikishwaji mkubwa wa wadau na walengwa, ufikiaji malengo na usikivu wa hali ya juu. *NGOs* zikitumiwa vizuri ni mshirika mzuri *(partner),* katika kuwawezesha wananchi kujiletea maendeleo, kwa kushirikiana na Serikali pia sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mfumuko mkubwa wa *NGOs* tangu miaka ya katikati ya themanini, na kwa hali hiyo pia kuzuka kwa *NGOs* za kitapeli na kibabaishaji, ambazo zinaishi kwenye mifuko ya watu na katika *briefcases* za watu, bado zipo *NGOs* nyingi zilizo makini na zenye nia njema. Serikali izilee *NGOs* badala ya kuwazia tu kuzidhibiti. Serikali pia ikwepe kishawishi cha kuziteka nyara na kuziweka mfukoni *NGOs* kwa lengo zuri tu la kukuza na kuimarisha demokrasia.

*NGOs* ni taasisi muhimu za wananchi na zinasaidia sana kuishitua na kuiamsha Serikali kila inapotaka kujisahau, kwa kuongeza uelewa wa wananchi *(awareness),* kuhusu mambo mbalimbali ya kiuraia na kiserikali. Mwelekeo na msimamo uwe ni kuziunga mkono *NGOs* zote zenye nia njema na siyo kuzidhibiti tu na hata kuzipiga vita. *NGOs* si badala ya Serikali, ila ni mshirika wa Serikali, asiyemezeka na Serikali na rafiki mkubwa wa raia, ambao ndiyo hao hao wenye uwezo wa kuiweka na kuiondoa madarakani Serikali, kwa kura zao halali, kupitia uchaguzi huru na wa haki.

Mheshimiwa Spika, namna nzuri zaidi ya kiumarisha Muungano ni kuyajadili kwa kina na kidemokrasia matatizo yote yanayoukabili Muungano huo. Kero zote zinazoukabili Muungano ni lazima zishughulikiwe kwa uharaka na kwa nia njema. Muungano ni ridhaa ya watu na siyo suala la mtu mmoja kumburuza mwingine.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Muungano yasifunikwe bali yaanikwe juani na yatafutiwe ufumbuzi unaoanzia kwenye chanzo. Katiba ya Tanzania ni lazima iangaliwe upya kabisa kwa lengo la kuwa na Muungano unaoonyesha heshima kwa pande zote na unaolinda maslahi ya pande zote. Zanzibar na Tanganyika zote zimewahi kuwa na wanachama wenye haki na hadhi sawa katika Umoja wa Mataifa, kabla ya Muungano wa mwaka 1964. Kamwe Muungano usiwe na maana ya upande mmoja kuuzemeza na kuugubika kabisa upande mwingine.

Mheshimiwa Spika, adui mkubwa wa Muungano ni yule anayeficha ficha matatizo ya kimsingi ya Muungano na ni yule anayeahirisha matatizo ya Muungano badala ya kuyashughulikia kwa kina.

Mheshimiwa Spika, kuupenda Muungano ni kuunyoosha Muungano huo kwa kushughulikia kero zake, ambazo zipo nyingi tu na siyo kuusifia Muungano kwa kuuvisha kilemba cha ukoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taasisi ya Takwimu za Taifa ya Tanzania, kupitia ripoti yake ya Julai 2002 kufuatia utafiti uliofanyika mwaka 2000/2001, asilimia 43 ya Watanzania wanamiliki

nyumba za bati na asilimia 25 ya nyumba hizo zimejengwa kwa kuta za matofali ya saruji, mawe au matofali ya kuchoma. Ni asilimia 10 tu ya kaya zimeunganishwa na umeme wa gridi ya Taifa na katika vijiji, ni asilimia 2 tu ya nyumba zilizounganishwa na umeme wa gridi hiyo. Ni asilimia 9 tu ya kaya ndizo zinatumia umeme kwa ajili ya taa. Asilimia 84 ya kaya zinaendelea kutumia mafuta ya taa ikiwa ni pamoja na koroboi, ili kupata mwanga.

Mheshimiwa Spika, wa hali yoyote ile, hali ya umaskini katika Tanzania ni mbaya mno na inatisha! Kundi kubwa la Watanzania lipo katika umaskini wa kupindukia na linachemka kwa hasira kila kukicha. Siku zote njaa *(hunger)* inayo nafasi kubwa ya kuleta hasira *(anger)* na ndiyo maana Serikali inatahadharishwa kutojijengea tabaka la watazamaji wa maendeleo *(spectators of development)* na badala yake ijenge washiriki katika maendeleo *(participators in development).* Jeshi kubwa la wasio na chochote siku zote huonekana ni tishio kubwa kwa wenye chochote lakini wachache mno! Mitafaruku mingi ya kisiasa na kijamii chanzo chake ni wananchi wengi kupoteza matumaini ya maisha kutokana na umaskini uliokithiri, huku wakiwashuhudia watu wachache, hasa waliomo Serikalini na wafanya biashara wakubwa wakifaidi, huku wao wakizibiwa riziki zote inafaa tuwe waangalifu sana.

Mheshimiwa Spika, bado lipo kundi kubwa la Watanzania wanaoishi kwenye nyumba za miti na nyasi, wanaolalia ngozi na virago pia mikeka, wanaotembea pekupeku kwa kushindwa kumudu bei ya kandambili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia katika Bajeti hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais inayoshughulikia masuala ya Kuondoa Umaskini na Mazingira pamoja na yale ya Muungano.

Kwanza kabisa ningependa kuipongeza sana Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi nzuri wanazozifanya na katika mchango wangu huu nitataka kuzungumzia mikakati ya utekelezaji wa kupunguza umaskini. Nazungumzia mikakati hii kwa sababu inajielekeza katika kufikia malengo manane ya maendeleo ya milennia *(Millennium Development Goals).* Malengo haya nadhani wote tunayajua ni nane.

Mheshimiwa Spika, ya kwanza ni ya kupunguza umaskini na njaa kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2015. Lengo la pili ni kufikia Elimu kwa Wote kwa kuhakikisha kwamba watoto wote wanamaliza *Primary School* kufikia mwaka 2015. Lengo la tatu ni kupata usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake. Kuhakikisha kwamba hakuna tofauti kati ya watoto wa kiume na wa kike kumaliza Shule ya Sekondari na Msingi kufikia mwaka 2005 na kuhakikisha kwamba kuna usawa katika ngazi zote ifikapo mwaka 2015.

Lengo la nne la *Millennium Development Goals* ni kupunguza vifo vya watoto kwa asilimia 2/3 na vile vile kuboresha afya ya uzazi kwa robo tatu ifikapo 2015. Lengo lingine la sita ni lile la kupambana na Ukimwi, Malaria na magonjwa na mengine sugu na vile vile kuangalia masuala ya mazingira na kukuza ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi hii inashughulikia masuala ya kuondoa umaskini imefanya mambo mengi sana katika kutekeleza azma hii ya kuwainua wananchi wa Tanzania. Pamoja na jitihada kubwa bado kuna kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni mambo ambayo yatatakiwa kufanyiwa kazi. Kwanza kabisa ni vizuri tukakubaliana kwa pamoja kuhusu baadhi ya maneno tunayoyatumia. Kwa mfano, je, mkakati wetu ni wa kuondoa umaskini au wa kupunguza umaskini. Kwa sababu maneno haya mawili ambayo yamekuwa yakitumika *interchangeably* na maneno haya hayafanani. Utakuwa sera ya mwaka 1998 imeeleza kuondoa umaskini. Lakini katika mikakati ya *Poverty Reduction Strategy Paper* inazungumzia suala la kupunguza umaskini. Sasa ni vizuri tukakubaliana kwa pamoja nini makusudio yetu. Tunakusudia kuondoa umaskini ama tunakusudia tu kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza azma yetu hii ya kudhibiti Ukimwi, nitaanza na suala la Ukimwi na magonjwa ya malaria na mambo mengine. Katika kutimiza azma yetu hii ya kudhibiti, malaria na magonjwa ili kujitahidi kuondoa umaskini ningependa kuzingatia msemo unaosema kwamba: *"If you want to cure poverty heal the poor"* yaani kama unataka kutibu umaskini basi waponyeshe maskini.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi pamoja na jitihada kubwa Serikali imezifanya takwimu zinaonyesha kwamba idadi kubwa ya maambukizo inazidi kuongezeka na vile vile asilimia kubwa ya wale walioathirika wanaishi kwa hali ngumu sana. Jitihada hizi za kuwasaidia hizi familia zilizoathirika bado zinaachiwa jamaa na *NGOs* chache.

Mheshimiwa Spika, vile vile ugonjwa wa malaria pia unachangia sana katika vifo na hata kudhoofisha nguvu za kupambana na maradhi. Kwani ugonjwa huu ni ugonjwa ambao unamrudia mtu mara kwa mara. Hivyo nashauri Serikali za Mitaa zihakikishe kwamba mipango ya maendeleo shirikishi na pia Kamati za Afya na za Mazingira katika ngazi ya Kata kwa mijini na Kamati hizo hizo katika ngazi ya vijiji ihakikishe kwamba inafanya kazi ya ukaguzi. Kukagua mazalio ya mbu na kufanya usafi ili kuhakikisha kwamba hakuna mazalio mengi au ugonjwa huu wa malaria tunaweza kudhibiti. Naomba Kamati hizi zifanye kazi kama hizo zinazofanywa na Sungusungu. Kuhakikisha kwamba wanakuwa kweli na uwezo wa kuwashauri na kuwasimamia wananchi katika kujitahidi kuboresha mazingira haya.

Mheshimiwa Spika, vile vile nashauri kwamba jitihada zifanyike kuhakikisha kwamba vifaa vya upimaji wa malaria vinapatikana hata vijijini ili na hivi vipimo vifanyike bila na kuwa na gharama yoyote. kwa sababu ugonjwa huu kama nilivyosema unachangia sana kupunguza uwezo wa mwili na hata kufanya waathirika wa magonjwa kama ya Ukimwi kuweza kufa mapema. Ni budi basi sisi tukafanya jitihada za thabiti kabisa kuhakikisha kwamba tunadhibiti ugonjwa huu wa malaria. Jitihada ambazo tunazoweza ni kufanya pamoja na kuhakikisha kwamba chandarua zinapatikana. Tuhakikishe kwamba wale ambao hawana uwezo wanapewa chandarua bure, tuhakikishe kwamba madawa yanapatikana. Ukienda Cairo sasa hivi ukiingia tu pale *Airport* unapewa *Chlorophenicals* ili utumie kwa ajili ya kuzuia na kudhibiti malaria. Sasa sisi tuone kwamba jinsi gani tunawezesha wananchi wetu wakaweza kujitahidi kuepukana na hili tatizo la malaria.

Mheshimiwa Spika, leo hii kwenye redio tumesikia Mafia watu wanatumia mifuko ya viroba kushona kwa ajili ya kutumia kama chandarua. Sisi juzi tu tumepitisha kodi kuongeza kwa bidhaa za chandarua. Sasa tuone tunafanya nini?

**MBUNGE FULANI:** Ilifutwa.

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Ilifutwa? Tunashukuru sana kama ilifutwa. Lakini pia dawa hizi za wadudu zinazotumika kwa chandarua zitolewe bure.

Suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni jinsi gani tutawawezesha waathirika wa Ukimwi. Masuala ya umaskini kusema kweli ni masuala ambayo sisi tunaya-*complicate* sana. Tukiangalia katika sera na majarida tunayotoka, kwanza tunatoa kwa lugha ya Kiingereza, lugha ngumu na kama vile tunafanya kwa ajili ya kuridhisha matakwa ya watu wa nje na sio kwamba tunafanya kwa ajili ya kumsaidia mtu wa kawaida kabisa aweze kuelewa jinsi gani ataweze kujikwamua kwa hali ambayo yeye mwenyewe anaijua, kwa sababu umaskini ni jambo ambalo watu wote wanalijua madhara yake na matatizo yake.

Kwa hivyo ndiyo maana nazungumzia yale masuala ambayo ni basic kabisa ambayo yanaweza kuondoa umaskini na kuchangia kumfanya mtu aweze akawa katika maisha mazuri na hali nzuri zaidi. Sasa kwa wale wanaothirika na Ukimwi jinsi gani tutaweza kuwasaidia. Inavyosema Serikali inakusudia Serikali ikihusisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Makampuni Binafsi na Sekta Binafsi.

Sasa basi wale wanaothirika waangaliwe kwamba wapatiwe yale madawa Wizara Afya inafanya vizuri kwa ambao wamepima na wamejiandikisha wanapata madawa ya kuongeza muda. Lakini vile vile wapatiwe virutubisho kama *vitamins.* Kuwe na mkakati wa kuangalia jinsi gani tutawapa chakula, mgao wa chakula muhimu. Kwa sababu mimi nakumbuka mwaka 1981 mpaka 1983 wakati nikiwa nasoma Shule ya Sekondari ya Wasichana Tabora nilikuwa na matatizo kidogo ya tumbo *(Ulcers)* na sisi wakati huo tulikuwa tunapewa chakula. Wagonjwa tulikuwa na *special diet* tukawa tunapewa sukari kilo moja

kwa kila wiki. Tulikuwa tunapewa *Tanbond,* nyama ya kopo na kipindi hicho ni kipindi ambacho tulitoka kwenye vita vya Idi Amini.

Sasa mimi nilisoma 1982 mpaka 1983 nikagaiwa hivyo na Serikali. Sasa tuone jinsi gani sisi pia tutashirikisha michango ya watu mbalimbali ili tuweze kuwa na *commitment* ya kusaidia hawa watu ambao wameathirika na kusema kweli wengi wanakufa kutokana na ukosefu wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ripoti ya kutathmini utekelezaji wa haya masuala ya *MDGs,* Tanzania imejionyesha kufanya vizuri sana katika kupunguza tatizo la vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka 5 *(child mortality).*

Hata hivyo bado kuna tatizo kubwa sana katika *maternal mortality* Wanawake wengi wanakufa wakati wa kujifungua, Wanawake wengi sasa hivi karibu asilimia 50 ya Wanawake wanazalishwa na watu ambao hawana utaalamu wowote katika masuala ya kuunga.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba hizi jitihada zetu za kuondoa umaskini zielekeze katika kumsaidia mwanamke katika kupambana na magonjwa haya yanayompata mwanamke moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala kama ya kansa. Kansa ya Kizazi sasa hivi ni tatizo linalozidi kuwa kubwa, kansa ya titi ni tatizo linalozidi kuwa kubwa na Mashirika yanayotoa msaada kwa akinamama ni machache unakuta kwamba kama Maria Stopes ndiyo ambayo inashughulikia. Kwa hiyo, tuone jinsi gani tutaweza kutatua hili tatizo ili akinamama waweze kupata *smear test* ambayo ni gharama lakini tutaweza tukafanya jinsi gani tutahusisha Mashirika kama *UNICEF,* Mashirika yanayoshughulika Idadi ya Watu waweze kutoa hii *smear test* bure kwa akinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine tunalifanya vizuri Tanzania ni kuhusu uwezeshaji wa Wanawake na masuala ya kijinsia. Mimi nimeona kwamba katika ripoti inaonyesha *inshallah* tukifikia mwaka 2005 tunaweza kufikia lengo la kuwa sawa kwa sawa katika shule za Msingi na Sekondari kwa Wanawake. Lakini hata hivyo jitihada zinatakiwa ziongezeke ili kuhakikisha kwamba Wanawake wanapata haki katika ngazi zote na wanawakilishwa vizuri.

Kwa vile nazungumzia masuala haya ya jinsia naomba basi kwa niaba ya Wanawake wenzangu nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Bibi Rosebud Kurijilwa, kwa kuchaguliwa kuwa Kamishna wa kwanza katika Umoja wa Afrika .

Kushinda kwa Bibi Rosebud kwenye ushindani huu mkubwa inaipa sifa kubwa nchi yetu, kwani kati ya nchi zaidi ya 54 za Afrika ni nchi 11 tu ambazo zimeweza kupata wawakilishi. Sisi basi tunapongeza na tunapongeza jitihada za Serikali katika kum-*support* mwanamke. Nadhani jitihada hizi zitaendelea na kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2005 basi kutakuwa na uwakilishi wa asilimia 30 katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba kutoa pongezi za dhati kwa Programu ya *TASAF* katika kuchangia kupunguza umaskini. Hata hivyo ni vizuri ikaeleweka kwamba programu hii ni *safety net* au *cushion.* Programu lengo lake ni kupunguza tu makali ya umaskini.

Kwa hiyo, tusitegemee *TASAF* peke yake ikaondoa umaskini. *TASAF* inatakiwa ichangie tu pale mikakati ya kila Wizara na Idara inapo-*fall short.* Hasa ukizingatia kwamba mtaji mkubwa *TASAF* ni mkpo kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa tamko rasmi kwenyeBunge hili lako Tukufu kwamba ninayo dhamira ya kuleta hoja binafsi. Ninataka kuleta hoja binafsi itakayozitaka kila Wizara katika kuwasilisha Bajeti zao kutoa mipango ya wazi kabisa itakayoelezea mchango wao katika kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, najua Wizara zinaeleza michango yao *indirectly* lakini nataka kama vile Mheshimiwa Waziri anayeshughulika na mambo ya maji na Mifugo alivyotuletea *catalogue* inayoonyesha aina za ng'ombe na kadhalika.

Sasa mimi nataka tuletewe kiambatanisho kitakachowekwa kwenye Bajeti kueleza kila Wizara inafanya nini moja kwa moja katika kuondoa umaskini. Katika ripoti hiyo nataka nionyeshwe jinsi gani inaji-*address* katika masuala ya Ukimwi pamoja na masuala ya usawa wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa katika Wizara ya Fedha na Mipango waweze kuangalia sekta walizoziwekea kipaumbele. Sekta zilizokuwa na kipaumbele kwa sasa hivi ni sekta tano na katika hizo tano ni moja tu ambayo ni sekta ya kiuchumi na moja ni sekta ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, ningependa basi katika utaratibu wa kuweka kipaumbele ziongezwe sekta zingine tatu katika sekta za kiuchumi. Kuwe na sekta ya kilimo, viwanda na biashara na utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo nasema naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ISSA MOHAMED SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili nami nitoe mchango wangu kwa hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nawapongeza Mawaziri wawili wanaoshughulikia Ofisi ya Makamu wa Rais. Pia, nampongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira, kwa kazi nzuri anayoifanya na kwa bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo. Kwa hiyo, ninachukulia kwamba, Wizara hii ni yangu. Nitatoa mchango wangu wa kuisaidia na kuiboresha ili tufikie mahali ambapo kweli Kamati yetu itakuwa imefanya kazi ya kuisaidia Wizara na Mawaziri kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, nampongeza Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo na pongezi zangu hizi zinatokana na juhudi binafsi za Mheshimiwa Rais za kuleta *TASAF*. Mheshimiwa Maokola-Majogo anaiongoza *TASAF* kupitia kwa juhudi zilizofanywa na Mheshimiwa Rais kuipata hiyo *TASAF* na kuileta Tanzania na sasa kwa hakika *TASAF* inaonyesha kielelezo halisi kwamba, Muungano wa vitendo umeenea Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TASAF* inafanya kazi nzuri sana Tanzania Zanzibar kama vile inavyofanya kazi nzuri kama hiyo Tanzania Bara. Nafikiri si vibaya kusema kabla ya *TASAF* hakuna kielelezo cha kuona au kugusa unachoweza kusema kwamba hiki ni kielelezo halisi cha kuwepo kwa vitendo masuala yetu ya Muungano. Kwa hiyo, ninaipongeza sana *TASAF* na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nikiangalia hotuba aliyosoma Mheshimiwa Ntagazwa, kama hii ni hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais inayotolewa kila mwaka na ikawa ni hotuba ya 39, kwa sababu tangu Muungano huu ni mwaka wa 39, basi nasema haina msisimko! Nasema hivyo kwa sababu sioni mabadiliko makubwa hata kidogo ya kuonyesha kwamba, tunaelekea mahali pazuri pa Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakubali kwamba, Waasisi wa Muungano wamejitahidi sana kutufikisha hapa tulipo. Pia, Waheshimiwa Wabunge na Viongozi mbalimbali, wamejitahidi sana kutufikisha hapa tulipo. Vile vile, kila mmoja nchini Tanzania, pamoja na Wananchi wenyewe wamejitahidi sana kuulea na kuudumisha Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba, kuna mambo mawili ambayo Tanzania ni lazima tuyasisitize, tuyafanyie utafiti na yawe na mwelekeo wa wazi kabisa wa kimaendeleo. Kwa mfano, tuwe na utafiti kuhusu suala la Muungano na tujue unaendelea vipi. Hali kadhalika lile tamko tunalosema kwamba, 'Mapinduzi Daima' nalo tuwe na utafiti wake kwamba linadumishwa vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mkubwa leo katika suala la Muungano ni kuitaka Wizara hii itusaidie, tubadilishe kidogo. Muungano wetu kisiasa ni mzuri na hatuna nia ya kusema lolote, tutahakikisha kwamba utadumu, lakini kusema kweli kama hatukubadilika kidogo tukaupeleka kwenye Muungano wa kiuchumi hali haitakuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muungano wa kiuchumi ndio utakaofanya vijana wetu waamini kwamba, kweli upo Muungano wenye manufaa kwao. Suala hili ambalo limezungumzwa kwa miaka 39, ambalo limo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu Viongozi wetu walioasisi Muungano na jinsi tunavyouenzi Muungano wetu limefikia mahali liwe na kiambatisho chenye uzito ambacho ni Muungano wa kiuchumi. Ninadhani imeshazungumzwa kwamba, Sheria itatungwa ya kuwawezesha Watanzania kumiliki uchumi wao, hili ni jambo ambalo kila Mtanzania analisubiri na tunapozungumza Tanzania, Zanzibar nayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zanzibar nashauri Wizara hii iwasiliane kwenye *cabinet* yao kuwe na hoja maalum ya kuiwezesha Zanzibar kiuchumi na hii ielezwe kisheria. Kwa mfano, hivi sasa Zanzibar ina Sera yake ya Bandari Huru, ina Sera yake ya *EPZ* na ina biashara zake, lakini kuna Taasisi zetu za hapa kwa kweli zinadhoofisha Bandari Huru, haizitambui! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TRA* haitambui Bandari Huru ya Zanzibar na haitambui *EPZ* ya Zanzibar na wakati huo huo mfanyabiashara anayefanya biashara Zanzibar akija na mali yake Tanzania Bara anatakiwa aonyeshe vielelezo vingine vya biashara ile ile ambayo imekwishalipiwa *VAT* kule Zanzibar. Kwa maana hiyo, *TRA* haitambui utaratibu wa biashara wa Zanzibar na kama haitambui, inawezekana Wizara ya Fedha haitambui utaratibu wote huo kwa sababu *TRA* iko chini ya Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachosema ni kwamba, tuwe na mwelekeo wa uhakika hasa na wa dhati, tuje na mabadiliko ya Sheria na kuna baadhi ya vipengele vya Katiba itabidi pia vibadilishwe ili kuipa uzito Zanzibar iwezeshwe katika masuala ya kiuchumi. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itamke wazi kwamba, inaitambua Bandari Huru ya Zanzibar na iisaidie, tutakuwa tunakwenda sambamba kiuchumi. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itamke wazi kwamba, inaitambua *EPZ* na iisaidie kiuchumi na Waziri wa Fedha atamke wazi kwamba ni marufuku tena kuwanyanyasa wafanyabiashara kutoka Zanzibar wanaokuja Tanzania Bara katika masuala ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matamshi ya aina hiyo yatatusaidia sana kuimarisha Muungano. Hatuna wasiwasi Muungano tunao kwa mujibu wa Katiba. Tunazaliana na tunafanya mambo mengi sana kwa mujibu wa Sheria zetu, lakini kwa suala la kiuchumi bado hakuna Muungano wa aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuiwezesha namna hiyo Zanzibar, kuna jambo ambalo pia ningependa kuligusia. Jambo hilo ni la Kikatiba, lakini Katiba imetungwa na Bunge hili. Nimesikia maneno kutoka Zanzibar watu wanazungumza kwamba, hawaelewi haya mafuta ni kwa nini yakawa ya Muungano? Nasema waelewe kwa sababu yamo kwenye Katiba. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, suala la mafuta nadhani ni item ya 15 katika nyongeza za mambo ya muungano. Kwa hiyo, hilo ni suala la muungano.

Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Zanzibar pamoja na masuala ya Bandari Huru, nashauri kwamba, mafuta yasiwe ya Muungano. Hiyo itakuwa ni nafasi nzuri sana ya kuisaidia Zanzibar kujiimarisha kiuchumi. Hatuna hakika kama mafuta yenyewe yapo, pengine hayapo, lakini ukishaweka kwamba yasiwe ya Kimuungano, unawapa nafasi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutafuta wafadhili wa kufanya utafiti. Utafiti hata ukiwa ni wa Muungano kama ilivyo katika Katiba, lakini yale mafuta pale yanapopatikana ndio yawe yao. Kwa hiyo, *TRA* isiwe na madaraka ya kuchukua mapato tena ya mafuta kuyaleta Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa *TRA* inatudhoofisha sana. Kuna masuala yaliyo wazi kabisa nayo ni kwamba, madini yote yaliyopo Tanzania si ya Muungano, lakini ni mafuta tu ndiyo yanafanywa ni ya Muungano. *Gas* imeshavumbuliwa na inatambulika kwa mujibu wa Katiba, katika hiyo *item* ya 15 ya Muungano, lakini sina hakika kama Zanzibar imeshirikishwa kwenye hatua yoyote. Mpaka sasa *gas* inaletwa Dar es Salaam, Zanzibar haina habari! Hili pia ni suala la Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nizungumze kidogo suala la umeme. Mwaka 2002 nilizungumza kwa kirefu sana kuhusu suala hili na nilifarijika mnamo tarhe 17 Juni, 2003 nilipata taarifa tu kwamba, ile riba inaondolewa. Hili suala litakuwa kesho kwenye hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini,

lakini kwa sababu umeme umeingiliana na mambo ya Kimuungano na maisha ya Wananchi, inasikitisha sana kuzimwa umeme kule Zanzibar! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi nilizungumza na Madaktari, kwa bahati nzuri mtoto wangu ni *Surgeon*, nilimwuliza, je, wakati umeme unazimika kulikuwa na hatari gani? Akaniambia mimi nilikuwa Makunduchi, kila Jumatatu huwa nakwenda kufanya *operation* hospitali ya kule, ile saa saba walikuwa wameshamaliza. Lakini alipokuja kufanya mazungumzo na wenzake pale Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, walisema wakati umeme unazimwa kulikuwa na mgonjwa anafanyiwa *operation* na hawakujulishwa kwamba umeme utazimwa! Bahati nzuri wanasema huyo mgonjwa mwenyewe alikuwa anafanyiwa *operation* ya masuala ya mifupa, laiti kama ingekuwa ni matatizo mengine, basi *TANESCO* ingemuua Mzanzibari huyo! Hili ni suala la hatari sana!

Mheshimiwa Spika, kuna usemi wa Kiarabu, samahani nitauzungumza unasema, *"idhaa ghabal aslu, shufud dalilu wafinlu"*. Waliofanya kitendo hiki tunawajua, kama watu wa aina hiyo asili yake hatuijui, basi tazameni dalili zao na vitendo vyao huko nyuma. *(Makofi)*

*TANESCO* imekuwa mikononi mwa watu ambao sio Watanzania, ni watu ambao vitendo vyao na dalili zao ukizingatia nyuma zilikuwa na sura ya aina hii, kutokuwajali watu na kutokuwajali Waafrika. Kwa hiyo, vitendo hivyo sasa vinaletwa Tanzania katika hali ambayo si nzuri! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamekwenda *NBC* tumehangaika, lilipokuja suala la *NBC*, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alimpeleka Waziri Kapuya kushughulikia mambo haya, lakini suala hili la umeme kuzimwa Zanzibar hatujasikia suala lolote kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasikitika! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo ni jambo la kusikitisha sana na kabla kengele haijagongwa, nimwombe Waziri wa Nishati na Madini kesho atakapokuja na hotuba yake, kitu cha kwanza awatake radhi Wananchi wa Zanzibar na awaombe hawa watu ambao walijigamba kwenye *TV* kwamba wataendelea kukata umeme wasifanye hivyo. Leo kwetu kesho kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Si walilipa deni wakarudishiwa, tatizo ni nini? *(Kicheko)*

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ndiye anapaswa kushukuriwa kwa neema zote hizi anazotupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nikupongeze wewe binafsi kwa kuweza kunipa nafasi hii leo mapema ya kuwa mtu wa tatu katika kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nisiwe mwizi wa fadhila. Kwanza napenda nianze na kumpongeza Makamu wa Rais, kwa kuweza kuacha majukumu yake mengi na kazi zake nyingi za Kitaifa na kwa makusudi kufanya ziara kuja kutembelea Majimboni mwetu. Pia, kwa kutupa msukumo wake mkubwa, hasa kwenye Jimbo langu la Kiwani na kuendeleza miradi ya maendeleo ya Wananchi iliyoko kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpa hongera sana na pongezi nyingi kutoka kwa Wananchi wa Jimbo langu la Kiwani na tunamwomba asichoke kufanya ziara kama hizo za kutembelea kwenye Majimbo yetu. Pia, Viongozi wengine wafuatilie nyayo zake kwa kutembelea mara kwa mara kwenye Majimbo yetu na kutupa msukumo kama huo ili tuweze kufanikisha majukumu tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitakuwa mzungumzaji mkubwa sana kwa sababu sipendi maneno yawe marefu, napenda zaidi vitendo viwe virefu kuliko maneno. Napenda nianze kwa kuchangia, nina sehemu zangu tatu tu hivi ambazo napenda nizikumbushie au ziendelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niungane na Mheshimiwa aliyetangulia, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutuletea huu mradi wa *TASAF*. Kwa kweli Mradi huu wa *TASAF* nataka niupongeze sana kwa sababu umetuondolea matatizo mengi na kero nyingi zilizoko kwenye Majimbo yetu. Naomba Mungu aujaalie udumu hivi hivi na wale wahusika wenyewe pia Mwenyezi Mungu, awape nguvu ili wazidi kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba, mradi huu unafanya kazi zake vizuri na unafanya kazi zake kwa mpango na kwa kweli unatusaidia sana. Lakini napenda nishauri/nikumbushe tu kwamba, wakati wanapoelekeza kupeleka hii miradi Vijijini, basi wahakikishe kwamba, wanafanya haraka ili iweze kumalizika mapema kama ilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu Wananchi wote kwa jumla huwa wanapenda maendeleo na wanapenda kujiondolea kero walizonazo. Sasa kama miradi ikipangwa na kama itachukua muda mrefu kumalizika, basi huenda Wananchi wetu wakavunjika moyo na wakaona labda miradi ile haitamalizika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri *TASAF* kama kuna tatizo lolote linalozuia kama ni uingizaji wa fedha au vinginevyo zisichelewe kuingizwa kwa sababu mara nyingi tunapouliza tunaambiwa kwamba kuna tatizo sugu la uingizwaji wa fedha. Naiomba *TASAF* ifanyie marekebisho suala hili ili fedha hizo ziingizwe kwa wakati na tuweze kumaliza miradi iliyopo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda niipongeze sana *TASAF* na ninaishukuru sana. Kama nilivyosema, sipendi kuzungumzia sana, ninapendelea kukumbusha tu ili baadaye tufanye kazi na tupate mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda nizungumzie kuhusu Chuo cha *Science Marine* cha Zanzibar. Mwaka 2002 nafikiri niliuliza swali la msingi kuhusu Chuo hiki. Pia, napenda niseme kwamba mwaka huo wa 2002 mwezi wa nne kama sikosei tulifanya ziara ya kutembelea Chuo hiki, kwa kweli kinasikitisha kutokana na majengo yake jinsi yalivyo, yote yameshachakaa. Lakini cha kufurahisha ni kwamba, tuliambiwa kuwa kiwanja kimeshapatikana na nina hakika kimeshapatikana, lakini ndio yale niliyosema kwamba maneno bora yawe mafupi na vitendo viharakishwe kutekelezwa. Mpaka leo hii ukienda katika Chuo hicho kiwanja kipo, lakini bado hakijaanza kujengwa. Nashauri kwamba kitendo kikizungumzwa basi kifanyiwe umuhimu wa kutekelezwa. Chuo kama hiki kina umuhimu sana wa kuwepo hapa nchini kwetu kwa sababu ni Chuo chenye maendeleo. Kama siku zote kitabakia kuwa ni kiwanja tu, tutakuwa hatujafanya kitu cha maana! Nashauri sana Serikali ilitupie suala hili macho.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda niungane na Mheshimiwa Issa Mohamed Suleiman kuhusu suala zima la Muungano wetu. Tunaunga mkono watu wa Zanzibar kuhusu suala la *TANESCO*. Suala walilofanya ni la dhambi au suala la ujambazi hasa! Mgonjwa amekwishapelekwa kwenye *operation* wao wanazima umeme, huo si ni ujambazi na ukatili! Naomba watu wa *TANESCO* wasifanye tena suala hilo na kama alivyosema mwenzangu, wawaombe radhi Wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda niongelee kuhusu *BoT* kwa upande wa Zanzibar. Ndiyo yale niliyosema, bado maneno ni marefu, lakini utekelezaji ni mfupi. *BoT* Zanzibar nathubutu kusema kwamba, huu ni karibu mwaka wa nane kiwanja kipo, kama sikosei, lakini bado Serikali inaendelea kukodi majengo. Hivi hatuoni kwamba kila tunapoendelea kukodi majengo tunaendelea kupoteza fedha za umma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali iliangalie kwa kina suala hili na waendeleze ujenzi wa *BoT* ili tuepukane na kukodi majengo haya siku zote. Yaani huu ni mwaka wa nane na kama ingekuwa ni mimba, mtoto angezaliwa na sasa hivi angekuwa ameshaanza shule, lakini bado tu mipango inaendelea kupangwa na haifiki mwisho! Ninaishauri Serikali ilitazame suala hili kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda kurudia kuupongeza Muafaka. Muafaka Pemba umetusaidia sana na kila mara nikisimama nitajitahidi kuupongeza. Lakini pia naomba wenzangu wasinielewe vibaya kwa sababu kila nikisimama hapa na nikizungumzia Muafaka, wenzangu huwa

wananielewa vibaya. Naomba wasinielewe vibaya, waamini kwamba, sisi ni Viongozi na tunachaguliwa na Wananchi na Wananchi wanachohitaji ni maendeleo si kupingana. Sasa, kama hatutachukua hatua za kuwaelimisha Wananchi wetu kimaendeleo au tukawapa hali halisi ya uchumi wa nchi yetu ilivyo tukaendelea kuwadanganya, nafikiri Muafaka wetu hautafikia mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Viongozi wenzangu ni kwamba, tulione hili suala na kama tunalizungumza, tulizungumze kwa ukweli na uwazi, tuwaelimishe Wananchi hali ya uchumi wetu ilivyo na tuwashirikishe kwenye shughuli za maendeleo, lakini tusiwe na tabia za kuwadanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninavyoamini ni kwamba, uongo hauna mwisho mzuri, mwisho wake ni lazima utakufikisha pabaya tu. Naomba wenzangu tuwe na ukweli na uwazi, tuitetee Serikali yetu, tuishauri na tuisaidie ili tufike mahali tujikute kwamba yale tuliyoyakusudia tumeyakamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri nilianza mwanzo kusema kwamba sitakuwa msemaji mkubwa sana. Nilitaka kushauri na kukumbusha tu kuhusu mambo hayo yasiachwe sana mpaka yakaoza. Niseme Kiswahili cha Kipemba *'yakaoza'*. Naomba yafanyiwe kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. YUSSUF KOMBO JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami naomba niungane na Waheshimiwa wenzangu waliotangulia, kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mawazo niliyonayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, napenda moja kwa moja niende kwenye yale niliyoyakusudia, lakini kabla sijasahau, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, waliomaliza kuongea hivi punde kuhusiana na suala la umeme.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa umesema kwamba, si wamelipa, wamerejeshewa! Nadhani hiyo kwa mtu mzima ambaye tunamwamini haikuwa sahihi kusema hivyo! Hili ni tatizo tena kubwa kwa Zanzibar, umeme. Sasa tunapolichukulia tu kwamba, wamelipa ukarejeshwa, nadhani tunaenda kubaya.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuliongelea kuhusiana na hilo ni kwamba, Zanzibar ni Serikali kamili, ina mamlaka yake na tulivyoanza haya masuala ya umeme tulizungumza sana, ndio maana tukafikia pale. Sasa, nashangaa hivi Watanzania kwa umahiri wetu wa kuzungumza tumeshindwaje kuzungumzia hili hata tukaelewana mpaka ikafika hiyo hatua iliyofikia? Tahadhari ninayoitoa ni kwamba, haya mambo tusiyachukulie mzaha tutafika pabaya kwa sababu hawa wameanza, lakini watakuja wengine watamaliza! Kuhusu umeme naishia hapo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu kero za Muungano. Kwa suala la Muungano huwa tunasema, matatizo tunayashughulikia, tunaunda Kamati yanadajiliwa. Lakini huu mjadala mpaka lini kwa sababu sasa ni miaka arobaini ya Muungano? Ninapenda kuwashauri Watanzania kwamba, kama kweli tunataka Muungano wa kudumu au kama ni vinginevyo basi tuendelee kujadili, kuunda Kamati, kuunda Tume na ziwe zinaishia tu hivyo hivyo bila taarifa rasmi za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, nimesema hivyo kwa sababu mara kwa mara huwa tunasema matatizo ya Muungano yanazungumzwa, yanajadiliwa, lakini mbona kipindi kimekuwa kirefu? Hivi kweli kama mtu mzima mwenye familia yake, kuna tatizo ndani ya nyumba yake, anaweza akastahimili tu kwa miaka mitatu tatizo hilo? Lakini Watanzania tumekuwa tunaambizana maneno hayo hayo, sasa ni miaka arobaini, hivi Watanzania tutakuwa na maneno mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kuhusu suala la Muungano matatizo yapo, sote tunakubali, lakini unapozungumza unaambiwa, tayari baadhi yake yameanza kushughulikiwa na yamepatiwa ufumbuzi. Ukiuliza sana utaambiwa, 4.5 tayari, ukiendelea unaambiwa, Kamati ya Uchumi na Fedha imeshaundwa. Nataka niwaulize, hivi hayo tu ndiyo matatizo ya Muungano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani ili kuwatendea haki Watanzania wenye nia njema ya Muungano, basi zile kauli za kwamba Tume, sijui Kamati zimeundwa, kwa kweli tufanye zifikie mahali pake ziishe na tuweze kutekeleza yale mambo kwa vitendo na kama ikibidi basi turudi kwa Wananchi kuwauliza nini kinatakikana katika Muungano mpya na si ule ambao tumekuwa mara kwa mara tunaurekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo mengine ambayo tayari ilionekana yangekuwa yamepatiwa ufumbuzi, lakini bado niseme Serikali imekuwa inapiga chenga na miongoni mwa masuala hayo ni lile la ujenzi wa *BoT* Zanzibar. Pamoja na kwamba Waheshimiwa wenzangu wamelizungumza hili, lakini nami naomba nilizungumze kwa sababu ndiyo yale ninayoyasema kwamba, Watanzania zile sifa ambazo tumekuwa tukipewa na majirani zetu kuwa ukitaka kumjua Mtanzania, basi awe na kosa halafu umkamate. Atakupa Kiswahili kiasi kwamba wewe mwenyewe utaanza kumwonea huruma na hatimaye unamwachia. Sasa, kweli Watanzania tuna maneno mengi, siasa nyingi, lakini imefika mahali sisi wenyewe Watanzania tuseme kwamba, wakati wa maneno umekwisha na sasa iwe vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *BoT* Tawi la Zanzibar, hili jambo limekuwa la muda mrefu na kwa Wazanzibari imekuwa kero. Imefika mahali tumekuwa tuna mawazo kwamba haya mambo yanayohusiana na Muungano kwa Zanzibar hayatekelezeki. Kwa mfano, hili la *BoT* kiwanja kipo, nadhani miaka miwili au mwaka mmoja mimi nilipita katika maeneo haya nikakuta kuna mashine wanachukua udongo pale. Hivi huo udongo Mheshimiwa Waziri huko ulikopelekwa haujarejeshwa karibu mwaka mmoja na nusu sasa? Pia huwa tunapata wasiwasi kuona kwamba, labda kuna vitu upande mmoja wa Muungano hautaki viende katika upande wa pili wa Muungano, kwa sababu tunaamini kwamba, kama jengo lile litajengwa Zanzibar, Zanzibar tayari itakuwa ina jengo la *BoT* wakati sasa hivi hakuna, wakati Tanzania Bara yako majengo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni ujenzi wa Chuo cha *Marine Science*. Hili nalo tangu ilipovunjika Jumuiya ya Afrika Mashariki, karibu miaka zaidi ya ishirini, limekuwa linazungumzwa tu Ujenzi wa Chuo cha *Marine Science*.

Nataka kusema kwamba, hapa tusipokaa vizuri kuhusiana na hili hiki chuo hakitajengwa kama ilivyokuwa haijangwa hii *BoT*, kwa sababu kwanza kiwanja kiliwahi kupatikana Mkoa wa Kaskazini Unguja, ikaenda ikapigwa mateke huku na huku badala yake kiwanja kikabadilishwa kikawa Kusini Unguja. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nataka kujua sababu iliyofanya kile kiwanja cha Kaskazini Unguja kisijengwe na ikabadilishwa kuja Kusini ni sababu ipi? Kama ipo labda wale waliokaa kwanza wakafikiria Kaskazini hawakuwa na akili au hawakufikiria vizuri au walishauriwa vibaya na nani? Sasa hayo ni masuala mazito, lakini kwa umahiri wetu wa kuzungumza tunayaona mepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naishauri Serikali ya Muungano ione haya mambo ambayo yenyewe inadhani inayaona siyo mazito lakini ni mazito na iyachukulie hatua za kufaa za haraka kwa sababu tuna uchaguzi 2005, haya tumekuwa tunayazungumza tangu miaka ya 1960. Kwanza kama Chama Tawala, tunajiwekea mazingira magumu kurejea tena madarakani. Hili nataka niliseme tulitambue pamoja na kwamba mtaona haina uzito lakini mimi ninaona ina uzito, kwa sababu mara kwa mara tutakuwa tunawaeleza watu wetu yale yale ambayo kila siku tunarudi tunawaeleza mambo hayo hayo. Hatuna mapya tunayowaeleza kwamba lile tulilizungumza mwaka jana, lakini safari hii tayari tunakwenda na lingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naiomba Serikali haya mambo iyachukulie uzito wa hali juu ili kuona tunakwenda kule ambako tumekusudia ili CCM iweze kuendelea kutawala hasa kwa upande wa Zanzibar, kwa sababu ninapozungumza hivi hasa ni upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika mambo ambayo nimeyakusudia kuyazungumza nalo pia linahusiana na mambo ya Muungano vile vile, kuhusu magari yanayotoka Zanzibar, ambayo huwa na namba zinazoanzia na ZNZ. Sasa hapa ninachokusudia kusema ni kwamba, liliwahi kutokea hili tatizo likazungumzwa likaisha, lakini kama wiki mbili zilizopita limerudi tena na limekuwa kero. Sasa mimi huwa najiuliza hivi huu Muungano tuufanyeje? Kwa sababu mimi kwa kumbukumbu zangu, Zanzibar

yako magari TZK, TZC hayashughulikiwi, yanafanya kazi zake kama yalivyo. Cha kushangaza gari za Zanzibar zinapokuja huku tunapata taabu sana na kwa kweli hili hata kama kwa kurejea maneno yangu nitaonekana hata gari tu, siyo gari tu haya ni matatizo ya Muungano, ambayo bila ya kuchukulia hatua zinazofaa au kukaa tukayazingatia, yatatufikisha mahali pabaya kwa sababu huwa tunajiuliza magari ya Tanzania Bara yanapokuja Zanzibar siyo ya kigeni, *okay,* lakini ya Zanzibar yanapokuja Tanzania Bara yafanyiwe *harassment?* Unatakiwa ulipe kila mwezi, unaambiwa lazima ubadilishe namba, huwezi kufanya shughuli zako bila usumbufu. *(Makofi)*

Sasa huwa tunajiuliza huu Muungano hivi zaidi umeelemea upande mmoja tu na si pande zote ambazo zilikuwa zimeungana kwa *merit* sawa ambazo zilikuwa zina Serikali zilizojitawala? Sasa hili nalo mimi nimeona niliseme na kwa kutilia msisitizo vile vile isionekane tu kwamba hata magari nayo yanaleta matatizo, siyo magari tu haya mambo madogo madogo ambayo tukiyadharau basi yatatufikisha pabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa bahati nzuri nimeipitia hotuba ya Bajeti ya hawa Waheshimiwa Mawaziri wawili. Kwanza, mimi nimeshangaa tumezoea kuona Bajeti inaandikwa na Mheshimiwa Waziri mmoja hata kama hiyo Wizara ina watu wawili au zaidi. Hilo la kwanza.

Lakini lingine yale mambo ambayo niliyotegemea kuyakuta humu hayamo. Mambo yenyewe kwa mfano Wizara hii ndiyo inayoshughulikia mambo ya Muungano, kwa upeo humu hakuna. Mna yale yale tu tuliyozoea kuyasikia, 4.5, Tume inaundwa basi, yale ambayo tumeishauri Serikali kipindi kilichopita ambayo tungetegemea ingetueleza kwamba, mwaka huu tumefikia hapa na hili tumefika nusu labda humu kwenye hotuba hakuna. Sasa hii imekuwa habari nzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi naiunga hoja hii mkono kwa asilimia ninayoifahamu. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunayoifahamu ni asilimia mia moja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ABDALLAH KHAMIS FERUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili na watalaam wao, kwa kutayarisha hotuba hii nadhimu na nzuri iliyojaa kila aina ya upeo. Mimi naomba kuchangia machache yafuatayo:-

Kwanza, naipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais, angalau kwa kile kilio nilichokizungumza mwaka 2002 kuwa sasa wamechukua hatua ya awali ya kutaka kujenga Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar. Nawapongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

La pili, mwaka 2002 niliomba kitu kimoja kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ni Makamu wa Rais wa Tanzania nzima, Bara na sisi kule Zanzibar. Makamu wa Rais anahitajika kupatikana kule Zanzibar na huku Tanzania Bara. Sasa nilipendekeza mwaka 2002 kuwa tunaomba Mheshimiwa Makamu wa Rais, akiwa ni Makamu wa Jamhuri ya Muungano ikiwemo Zanzibar, apange kipindi maalum cha kuja kuonana angalau na wananchi wa Zanzibar kusikiliza kero na matatizo yao kule Zanzibar haonekani. Hilo hamkutekeleza mpaka leo halijatekelezwa wananchi wa Zanzibar wana matatizo yao. Huyu ni Makamu wao wanataka kumwona anafanya kazi kwa niaba ya Rais, wana matatizo waende wapi wale wananchi? Waje kwa Mbunge, Mbunge mwenyewe kama nilivyosema akitaka kuonana naye ilikuwa tunaanza kukwamishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri na sasa hivi naomba tena, tunakuomba wewe kama Waziri, utupelekee pendekezo letu hili kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais, apangiwe ratiba Zanzibar. Tunajua ana utaratibu wake maalum. Lakini angalau kama ni miezi minne akija mara moja Zanzibar, siku mbili au tatu, siku mbili awe Unguja, siku moja Pemba, aje kuonana na wananchi. Nalileta tena pendekezo hili naomba

Waziri lichukue, mwakani Mungu akitujalia uhai na roho, hoja hii nazuia shilingi au utupe maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizumgumzie suala la *BoT.* Benki hii kuna kiwanja kipo Kinazini Zanzibar. Kiwanja kile kulikuwa na shule ya Gulioni ilikuwa ni *Trade School.* Shule ile imevunjwa na imeondolewa haipo tena imehamishiwa eneo lingine, karibu mwaka wa 8, Benki haijajengwa. Waziri nataka utueleze kwa nini mpaka leo haijajengwa na wala katika makabrasha tukipitia hamna lolote, hakuna chochote, tupe sababu za msingi, utuhakikishie kwa nini haijajengwa na itajengwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipo Chuo cha *Marine Science* toka kipindi cha *East African Community,* pale ililetwa meli mpya kwa ajili *research.* Baada ya kuvunjika *East African Community* ile meli ikauzwa ilikuwa ya utafiti wa baharini. Basi tumekaa majengo mabovu tukaendelea hivyo hivyo, lakini baadaye kikaombwa kiwanja wakapewa sehemu moja inaitwa Buyu Zanzibar. Lakini hivi leo hakuna kinachoendelea, hakuna *estimate*, sijui utafiti wa awali, hakuna chochote, hakuna lolote.

Mheshimiwa Waziri hii ni moja ya kero za Muungano, nataka utuelezee kwa kina juu ya suala hili limefikia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuondoa umaskini, mfumo huu haukuwashirikisha Wabunge na Madiwani. Kwa hiyo, ninachokiomba suala hili Mheshimiwa Waziri lizingatiwe kwa kina ili kuboresha zaidi masuala ya kuondoa umaskini. Lakini wakati huo huo naipongeza Wizara yako kwa juhudi kubwa zinazochukuliwa katika suala zima la kuondoa umaskini nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kufika mwisho, naomba zizungumzie kwenye suala zima la umeme. Suala la kukatiwa umeme Zanzibar, kitendo kilichofanywa na *TANESCO* kwa kweli si kitendo cha kiungwana hata kidogo, bali ni kuidhalilisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nasema ni kuidhalilisha Serikali ya Zanzibar kwa sababu suala hili kwanza *politically* suala la umeme limejenga hisia kwa wananchi kuwa Serikali yao haiwathamini watu wake katika huduma mbalimbali ikiwepo umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutachangia zaidi kwa Waziri anayehusika. Lakini suala kama hili ni lazima Serikali ilizingatie, suala kama hili Serikali lazima iangalie na iingilie kati katika masuala madogo madogo kwa sababu cheche, moja, moto unaweza kuunguza uwanda mzima. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naomba suala la umeme lisubiri kesho wakati tunajadili Wizara ya Nishati na Madini.

**MHE. ABDALLAH KHAMIS FERUZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mwisho, naomba kuupongeza Mradi wa *TASAF* kwa kazi nzuri iliyofanywa. Lakini hii yote inatokana na ushirikiano mkubwa walio nao viongozi, wataalam, pamoja na ushirikiano wa wananchi katika kufanikisha miradi hii. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Pamoja na kukushukuru wewe, napenda kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada zake kubwa anazochukua katika kuwaongoza wananchi. Napenda kusema hivyo kwa sababu tunaziona jitihada zake toka alipoteuliwa. Kazi yake ni kutetea, kutembelea, kuonana na wananchi na kuona matatizo mbalimbali ya wananchi katika nchi yetu ya Tanzania na kuyatafutia ufumbuzi. Leo utasikia yuko Kondoa, kesho yuko Pemba, kesho kutwa yuko Arusha, kesho kutwa yuko Lindi. Kwa kweli tunampongeza sana kwa jitihada zake hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema hivyo kwa sababu nina ushahidi kamili. Alikuja Zanzibar hivi karibuni akatembelea Pemba mpaka Jimboni kwangu na akanipa msaada. Alitembelea Vitongoji alitoa msaada, alitembelea Kiwanja alitoa msaada, alitembelea Chake Chake akatoa msaada na Majimbo mengi *almost* Pemba nzima alitembelea Mheshimiwa Makamu wa Rais na akatoa misaada. Tunamshukuru na tunamwomba aendelee na moyo huo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumshukuru Makamu wetu wa Rais, pia napenda kuwashukuru Mawaziri wote wa Wizara hii katika Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa hotuba yao nzuri na vile vile katika uongozi wao mzuri katika kuondoa umaskini na uhifadhi wa mazingira. Vile vile kuipongeza na kuishukuru ofisi yetu iliyoko Zanzibar, ikiongozwa na viongozi ambao wapo pale kama akina Faharia. Tunashukuru sana kwa sababu wana ushirikiano mzuri na sisi kwa hiyo lazima tuwapongeze. Baada ya kushukuru napenda kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Kwanza katika kuchangia hotuba hii nitaanza kuchangia kwenye suala la kupambana na umaskini. Katika kupambana na umaskini, tuna tatizo kubwa katika nchi yetu ya Tanzania, tatizo sugu la ugonjwa wa Ukimwi. Kwa kweli inahuzunisha sana wananchi wengi wanaambukizwa virusi vya Ukimwi. Lakini tukiachia mbali hivyo, mimi nawaonea huruma sana watoto ambao wanaachwa na wazazi (yatima). Hata kama ukitazama *television* utaona vipindi maalum vinavyoelimisha juu ya kupambana na Ukimwi, unaweza ukaona watoto ndiyo wahudumu wa nyumba. Mtoto anatoka alfajiri anakwenda shule hana fedha na analea wadogo zake, hana mama, hana dada. Je, Serikali inalionaje tatizo hili na inalishughulikiaje? *(Makofi)*

Kwa kweli mpaka hivi sasa mimi naona bado sana. Wanaotia huruma ni watoto wadogo yatima. Lazima Serikali ichukue jitihada kamili ya kuwahudumia watoto hawa. Watoto wanatia huruma. Naomba sana Waheshimiwa Mawaziri, hili mlichukue kwa ajili ya kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, pili napenda kuchangia Mradi wa *NIGP* hususan mradi wa chumvi Pemba na Unguja. *NIGP* iko huku Tanzania Bara tu. Lakini Zanzibar ilikuwepo na ikaondoka na hii ni mara yangu ya tatu nasema. Kwenye maswali yangu ya Bungeni huwa nauliza, najibiwa kesho, kesho. Hawa wananchi wa Pemba walijikusanya akina mama, vijana, akina baba wakajiunga katika vikundi vya ushirika vya chumvi, waende wapi?

Hapa katika biashara ya chumvi walikuwa wanapata faida na walikuwa wanaweza kuhudumia familia zao kutokana na mradi huu wa chumvi. Leo mradi umehama moja kwa moja umekwenda wapi? Nikiuliza naambiwa sijui miradi fulani tutasaidia nchi za Belgium lakini mpaka leo hakuna na humu imo na wanasema watatusaidia tena, tuone sasa. Mimi mwakani hapa nitajua la kusema. Mradi wa chumvi urudi Pemba, Zanzibar, Chukwani, Pujini, Kangagani, Mchangamdogo, Wawi, Vitongoji. Wako akina mama, vijana, waliokuwa na miradi ya chumvi ambao walikuwa wanajipatia maslahi yao, leo hawana biashara, umaskini utaondoka vipi hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuzungumza hivyo ukosefu wa ajira uko sana kwetu Zanzibar. Kama kungekuwa na kile kiwanda ambacho kilitegemewa kufanya kazi ingeletwa ile mashine vijana wangeajiriwa pale katika Jimbo la Wawi. Katika Jimbo langu lipo hilo lengo ambalo wamesema liwe *industry.* Lakini kwa kweli mpaka sasa vijana wanahaha wanatafuta ajira hawapati, waende wapi? Naomba sana Serikali ilifuatilie hili. Safari hii hakuna kudanganywa waje tu Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchangia Mradi wa *NIGP* huwa nasikia Mradi wa *SELF*. Mimi Mradi wa *SELF* nausikia tu labda uko huku. Lakini Zanzibar hasa Pemba mimi siuoni, hakuna. Huu mradi hakuna mimi nasikia tu. Kwa hiyo, nimetumwa na wananchi wa Pemba Mradi wa *SELF* ufike Pemba na utoe mikopo midogo midogo ili iwasaidie wananchi kupambana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Mradi wa *TASAF. TASAF* Tanzania nzima, Pemba *number one*. Napenda kuisifia Wizara hii kwa kutuletea mradi huu. Kwanza napenda kumsifia Rais wetu kwa kuuleta mradi huu Tanzania kwa ajili ya kuondokana na umaskini. *(Makofi)*

Pili, napenda kuwashukuru Mawaziri kwa kuendeleza mradi huu. Pia namshukuru Bwana Kamba kwa sababu anafuatilia mradi huu pamoja na watalaam, wafanyakazi wake wa Tanzania Bara na vile vile napenda kuishukuru ofisi iliyoko Pemba inayosimamiwa na Ndugu Amran, Ndugu Mohamed, Ndugu Ali ndiyo ambao wanashirikiana na sisi, wanatushirikisha kikamilifu kama Wabunge ama Madiwani. Wanatushirikisha kikamilifu katika kupanga mikakati ya *TASAF,* miradi mbalimbali katika Kisiwa cha Pemba. Napenda kuipongeza sana na naomba iendelee. Isipokuwa kitu kimoja hizi pesa zinachelewa. Mimi

katika Jimbo langu nilikuwa sijapata. Nimepata hivi juzi mwezi wa Februari tumeipitisha tumepata mradi mmoja wa shule na mradi mmoja wa maji katika Vijiji vya Kilimahodi na Wara. Lakini kuanzia Februari, Machi, Aprili, Mei, June, sasa hivi ni Julai, hatujajua chochote kinachoendelea. Tukiuliza tunaambiwa fedha hakuna. Tunaomba fedha zisafirishwe moja kwa moja *PBZ Chake*, yaani *PBZ Pemba,* zisipitie kwingine. Zikipitia kwingine hazifiki kwa wakati. Wananchi wanataka maendeleo. *(Makofi)*

Vile vile napenda kupendekeza hii miradi ya maji kama kule Ndagoni, nimepata taarifa kwamba, kile kisima kimedidimia mchikichiki kwa hiyo inabidi wafanye kwa utalaam walete wataalam wazuri. Vile vile mimi napendekeza hizi zisiwe za kokoto au mchanga tu. Ziwe za lami kwa sababu mvua ikinyesha kubwa kokoto zinaondoka. Jitihada zote zinazofanywa na wananchi na Serikali zinapotea. Kwa hiyo, naomba sana lifuatiliwe suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya pekee napenda kuupongeza Mradi wa *Pride Tanzania*. Kwa kweli Mradi wa *Pride Tanzania* umefika Kisiwani Pemba, akina mama, vijana, akina baba, wafanyabiashara ndogo ndogo, wameneemeka. Hivi karibuni, naupongeza sana huu mradi. Naomba anayeshughulikia mradi huu, Mwenyezi Mungu, ampe uhai vile vile tuendelee kupata miradi hiyo zaidi. *(Makofi)*

Natoa salamu rasmi kutoka Pemba kuhusiana na mradi huu, wananchi sasa hivi wanaringa katika mradi huu na wanafanya biashara zao na wanapata maendeleo mazuri. Nilimwona Mheshimiwa Iddi Simba, alikuja Pemba. Kwa hiyo, Mheshimiwa Iddi Simba hongera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la uhifadhi wa mazingira. Katika Jimbo langu la Wawi kuna Kiwanda cha Makonyo, nafikiri kila mtu anajua hata wewe Mheshimiwa Spika, unakijua ulikuja siku ile pale na ukalala. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa kile kiwanda hawa waliojenga hizo enzi na enzi walikuwa ni Wafaransa. Sijui walikuwa na lengo la kutukaushia mazingira ya Pemba yawe na hali mbaya baadaye, kwa sababu kama sayansi na teknolojia ni mambo yanayokwenda na mashine za umeme, leo kiwanda kinaendeshwa kwa kuni. Kuni za Pemba ni mikarafuu, ina maana ikishakatwa mikarafuu tutaharibu mazingira. Kwa mfano kama *production* inafanyika, wafanyakazi wanakwenda misituni wanakata kuni nyingi wanaleta pale ndiyo umeme wa kuendeshea machine. Je, inakuwa huu ni uharibifu wa mazingira au uimarishaji wa mazingira? *(Makofi)*

Halafu sasa katika mradi kiwanda hiki siku kukiwa na uzalishaji moshi unaenea maeneo yale yote watu wanapata *flue* kila wakati, kwa kweli naomba Serikali ilione hili. Kwanza ile *pipe* ipelekwe juu sana, halafu vile vile kile kiwanda kitumie umeme kisitumie kuni. Sasa tukitumia kuni si miti tunayokata huko na kuharibu mazingira na uimarishaji wa mazingira uko wapi hapo? *(Makofi)*

Vile vile napenda kuchangia katika suala la umeme, wenzangu wengi wamesema lakini mimi napenda tuwe na subira.

**SPIKA:** Nimeshaelekeza kwamba, suala la umeme lisubiri kesho ndiyo mahali pake.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** *Okay*. Mheshimiwa Spika, kwa vile tumeambiwa tusubiri kesho, napenda kumalizia hapo. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi kuwa mzungamzaji wa Wizara hii ya Makamu wa Rais, ambayo inaambatanisha mazingira na kuondoa umaskini. Kabla sijaanza kupita kwenye *speed* yangu ya kawaida, naomba nikubali kikamilifu kuwa shahidi mkamilifu ninayefaa ingawa sitatosheleza kutoa ushahidi kwa Watanzania kwamba, tunakwenda vizuri katika Muungano wetu kwa sababu katika ibara ya nne ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa madaraka. Naomba ninukuu nisije nikakosea, Katiba haikosewi mara nyingi. Ibara ya nne ukurasa wa 12 toleo la mwaka 1977 kifungu kidogo cha (i) kinasema: "Shughuli za mamlaka ya nchi katika Jamhuri ya Muungano zitaendelezwa na kuthaminiwa na vyombo viwili vyenye mamlaka ya utendaji."

Vyombo viwili vya utendaji wa kisheria vinatoa haki pia kwa vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutunga sheria kwa kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Vyombo hivyo vimetajwa katika kifungu kidogo cha pili ambavyo ni Baraza la Uwakilishi na Bunge katika upande wa sheria na vile vile Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Jamhuri ya Muungano vilipewa madaraka katika utekelezaji wa sehemu ya pili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo basi, yanayozungumzwa yote na Waheshimiwa Wabunge ni kero za utekelezaji wa masuala ya kiutendaji. Kwa mfano, masuala ya kiwanja, kuwepo kutokujenga nyumba ni utendaji. Kwa hiyo, kama kweli yapo mambo ambayo yameshatekelezwa muda mrefu, upo utekelezaji mbovu katika maeneo hayo, basi ningeomba hatua zichukuliwe kwa hao Watendaji ambao wanachelewesha mambo haya ili kuuingizia dosari Muungano wa udugu wa Tanzania ambao ni mfano wa kuigwa katika Afrika. *(Makofi)*

Muungano huu hauna mlinzi, tunajilinda wenyewe tu kama nanasi, lakini ina tatizo lake. Unaweza ukapakwa matope na baadhi ya watu kutoka nje. Nanasi lina miba kuanzia shina mpaka tunda lake, lakini linaliwa. Linajilinda lenyewe. Kwa hiyo, lazima kuwa waangalifu katika matamko kuhusu masuala ya Muungano, kwa sababu Muungano wetu sio wa historia, ni wa kidugu. Katika Muungano naomba niseme kwamba, Mheshimiwa Waziri naomba uchukue haya maneno kwamba, Muungano wetu ni Muungano wa kidugu. Kwa hiyo, hakuna wa kule wala wa huku. Katika suala la watu, limo wa humo. *(Makofi)*

Narudia tena. Hakuna wa kule wala wa huku, katika Muungano, limo wa humo. Nimemaliza masuala ya Muungano, naingia upande mwingine katika utangulizi ambapo nitazungumzia masuala ya umaskini. *(Makofi)*

Robert Danford na Raphael Danford, ndugu wawili walitoa kitabu katika toleo la 1993 lilikuwa linaelezea *food shortage* katika dunia na imeorodheshwa katika nchi maskini wakasema kwamba: "Maskini anapolalamika halalamikii matajiri kwamba wamepata utajiri, analalamikia hali yake". Wameambiwa matajiri wanapojigamba wanajigambia mali zao lakini hawapondi maskini. Nchi kama hii haina ubaguzi, kwa hiyo uko mchanganyiko wa jina moja tu kwamba wote ni watu, wameumbwa, kwa hiyo hawataji kwa utajiri kuhusiana na mchanganuo wa watu hao.

Kama mchanganyiko wa kachumbari, umetaja kachumbari tu. Hawakutaja nyanya kitunguu, tofauti na vitu vingine vikichanganyika kama chai inatajwa kupuuza vyote vilivyochanganyika kwamba maji hayatajwi, maziwa wala sukari. Sasa katika umaskini inatajwa kwa jina moja tu kwamba wote ni watu, tajiri na mali yake, maskini na hali yake. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa Wizara hii ina kazi kubwa mbele yetu kwamba pamoja na programu zote, mipango ya maendeleo iliyopangwa, yapo mafanikio yaliyojitokeza kutokana na hotuba zilizotolewa na Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha. Wametaja mafanikio kadhaa ambayo tumefikia ingawa sio *hundred percent*, lakini kuna aina ya kukua kwa uchumi, lakini Muungano wa uchumi wenyewe nadhani ndio una matatizo katika kuwafikia walengwa. Hapa tutajipanga upya ili kuangalia kwamba mpira utamfikia nani. Si vizuri kama mpira unawekwa, watu kumi na moja katika timu mmoja atoke bila kuugusa, ingawa si haki yake na juhudi zake kuufuata mpira huo, lakini katika suala la umaskini, nadhani, ninachojaribu pale Mheshimiwa Maokola Majogo, ni kufanya mlinganisho katika Pato la Taifa liwe ni pato la kipato cha mtu mmoja mmoja. Hata mahesabu yanatolewa kwa pato la Mtanzania kama ni kweli ukiambiwa umepata kwa mfano shilingi laki moja na kitu, wapo Watanzania wanaopata hivyo na ziko wapi fedha zao? Wapo Watanzania wanaopata zaidi na wanazipata wapi. Ndio hapo kunakuja kitu katika jamii kinaitwa, kuna walafi na waroho. Afadhali ya walafi wanakaribisha wenzao lakini wanawapunja, ila waroho wanaficha hata kikioza, hampi mtu hata akishikwa na njaa. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa watu kama hawa walipewa mitihani na Mwenyezi Mungu, wakapewa sinia moja kubwa na familia wakaambiwa kuleni. Wake zake wote watatu wako pale na watoto saba wakateremshiwa sinia, wakapewa uwezo wa kunyoosha mikono lakini kurudisha mkononi hawakuweza. Wakaambiwa kuleni.

Saa tatu hakuna mtu aliyekula pale. Kwa hiyo, wakajitahidi kuweka midomoni mwao wakashindwa. Pale wakapewa jibu na Malaika kwamba, ninyi hamuwezi kuongozana katika familia kwa sababu nafikiria kuleta vitu vidogo. Ingekuwa mtu ana uwezo wa kumlisha mwenzake kwa sababu kuchota wanaweza kwa nini usimlishe mkeo? Kwa hiyo, huo ndio uroho ambao huwezi kufikisha kitu kwa mtu mwingine. *(Kicheko)*

Baada ya kusema hayo kuhusu mazao, tungeondoa hali hii kwa kupendekeza mapendekezo yafuatayo: Bei ya mazao ya kilimo ya biashara kama ilivyoelezwa kupunguza kodi na vitu vingine na kuwawezesha wakulima katika maeneo hayo, ukuzaji wa mazao ghafi badala ya kuleta mazao yasiyosindikwa, kama alizeti, kupata mafuta, matunda, kutengeneza *juice*, ng'ombe, kupeleka ngozi zilizosindikwa na nyama kama kawaida. Malipo halali ya watu ambao wanadai mafao yao kuna Watanzania ambao waliachishwa kazi na kupunguzwa katika Mashirika mbalimbali kama vile *Polyester, TTCL, NDC, Mzinga Corporation* na maeneo mengine, ambao wanapata umaskini wa kunyimwa haki zao. Sasa watu kama wale wakilipwa angalau wanapunguza ile kasi ya matumizi. Vile vile kuangalia baadhi ya mashamba na viwanda vilivyobinafsishwa kwa muda mrefu lakini havijafanya kazi, Serikali ivichukue bila ya gharama yoyote halafu kuwagawia watu wenye uwezo. Hawa ndio wamedumaza uchumi. Tunaita Tanzania ni nchi changa, si changa, ni kijeba. *(Makofi)*

Tumepewa ukijeba wa kiuchumi kutokana na watu kama hawa ambao wanamiliki vitu halafu hawavitumii. Nilisema siku moja katika Wizara ya Kilimo kwamba, mtoto mchanga mwenye meno, mwenye maneno, mwenye mvi halafu kitovu hakijadondoka, huyo ni mtoto wa ajabu, huwezi hata kumbeba hata yeye utamwogopa. Tanzania si nchi changa, ni miongoni mwa nchi zinazoendelea, ilifanya mambo makubwa sana katika uchumi. Imedumazwa na baadhi ya watu ambao wanamiliki maeneo ambayo yanazalisha lakini hawazalishi inavyostahili, badala yake wanatumia maeneo hayo kama ni mali zao wakati si zao. Ni tabia ya mtu ananunua miwani halafu anaita miwani ya jua wakati ya kwake. *(Kicheko/Makofi)*

Upande wa demokrasia, tunasema demokrasia ina gharama lakini tunapata vipuli. Wapo walioharibu demokrasia duniani, walileta vurugu baridi, kashfa za kina, maisha ya kutegeana. Sasa katika upande wa demokrasia ya wazi na uongozi ulio wa kweli ndani yake, Tanzania tumo katika orodha ingawa hatuvumi. Mambo yetu tunayafanya taratibu kwa uwazi na ukweli. Zipo dosari katika utendaji tu, sio katika mfumo wenyewe. Mfumo, ukisoma vijitabu ambavyo vinaongoza nchi hii, Ilani ya Uchaguzi, Sera za Chama na mambo mengine mengine na wengine wanatusaidia wataalam wetu wa uchumi wanaotunga vitabu kama hivi, tutafika. Maeneo kama vile uzawa, jina lenyewe lakini ndani *content* ya vile vitabu vyenyewe ukisoma utakuta kabisa kwamba inamzungumzia Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, *NEMC,* tunayo kazi kubwa sana ya kufanya upande wa mazingira kwa sababu wakati ule nilipoanza upande wa mazingira walidhani mazingira ni kupanda miti, kukata mti na kupanda mti na moto na vitu vingine. Kumbe mazingira yana eneo kubwa tu kwa mfano hewa, mambo ya maziwa, mambo ya maji ya kunywa na upande wa Luhumbi na vitu vingine vingine. Kwa hiyo, wakati nilipokuwa kwenye Kamati ya Mazingira, tulipendekeza kwamba, uletwe Muswada wa Sheria wenye nia pana kabisa ya kutaka Watanzania kuipa madaraka *NEMC* iwe na meno ili kuweza kuwashughulikia wote wanaoharibu mazingira. Wanakwenda kuona tu, wanalalamika pale pale wanayaacha bila kueleza utaratibu ambao wanaweza wakawachukulia hatua. Hii ni sawasawa na watu wawili ambao walikuwa wote wana makengeza halafu wakaungana, baada ya kukaa pamoja wakaambiana kwamba tutembeeje twende bega kwa bega tusigongane tena, badala ya kwenda ana kwa ana sasa wale wakaanza kulaumiana. Mmoja akamwambia kwa nini wewe bwana huangalii unakokwenda? Mwenzake naye akamwambia na wewe kwa nini huendi unakoangalia? Sasa hiyo haisaidii katika ku-*solve* tatizo, ni malalamiko tu. wangekaa pamoja wangesema tusiende ana kwa ana, twende bega kwa bega tusigongane tena. Kwa hiyo, utaratibu ule wa Kamati ya Mazingira ungepewa meno ili kusudi kuweza kufuatilia mambo haya. *(Kicheko/Makofi)*

Sifa nyingine ambayo tulikuwa tumeipata katika umahiri na wastani na utulivu wa utekelezaji wa mambo yetu unatosheleza, unavutia, uko tulivu, mahiri, wastani, unaendelea vizuri, ni kushirikiana pamoja na Watanzania ili kuunga mkono juhudi za Serikali katika utekelezaji wa mambo haya.

Upande wa umaskini, ningependa kusema umaskini wa Vijijini, kwa mfano Vijiji vya Jimbo la Kusini Mashariki kule Logo, Uponda, Mifuru, Hewe, Bagiro, Jemegadu, Mkololo, Kumba, Mino, Ludewa,

Vulugi, Lung'ala, kwamba wanazalisha mazao yao, wakati ule pamba ilikuwa inampamba mtu wa Mkulazi, Kidunda na Chanyungu. Sasa hivi ilikuwa inapambanisha kati ya viongozi na wakulima wa maeneo haya. Licha ya barabara ile mbovu ambayo ilikuwa haijachongwa muda mrefu ndio iliyopata hela mwaka jana ambayo inatengenezwa sasa hivi. Huo utakuwa ukombozi wa kutosha kwa Kata za Mkulazi, Ngerengere na Kata za Kidugaro na maeneo ya kule Tununguo na *shortcut* ya barabara ambayo inaacha Vijiji viwili baada ya kugunduliwa barabara mpya ya kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro, ikaachwa hii ya katikati pale Mikese kwenda hadi maeneo ya Ngerengere ambayo imeshakamilika tayari. Hii itapunguza umaskini.

Masuala ya maji, *TASAF* imesaidia kwa kweli malambo mawili na upande wa *World Vision* tulisaidiwa malambo kama matano. Nasikia jana tu limeisha lambo la Mlilingwa. Kama ni kweli mimi nakuja Mlilingwa Jumamosi. Hii ni katika utaratibu wa mirejesho, Mheshimiwa Spika ataniruhusu Jumapili naondoka mara moja kuja hapo Mlilingwa kuangalia kama lile lambo kweli simu niliyopigiwa leo ilikuwa ni kweli. Nitaingia huko ghafla, sipitii Wilayani. Moja kwa moja Mlilingwa huko.

Mwisho, ni kwamba, Watanzania tufanye kazi. Niwaambie kabisa, kulala sio kupumzika. Kulala ni kazi. Kwa sababu kama kweli kulala ni kupumzika mbona walioamka huwa wanachoka? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niungane na Mheshimiwa Issa aliyesema kwamba, kuwe na Muungano ambao unazingatia uchumi. Ni sawa. Kweli sasa hivi siasa ya dunia sasa hivi ni uchumi. Kwa hiyo, iko haja kwa kweli Muungano wetu uelekezwe huko. Kwa hiyo, katika mipango inayokuja, vyombo vyote vinavyohusiana na uchumi, tutaangalia na hakuna haja ya kuongelea kwenye Katiba, kwa sababu mambo ya Uchumi ni mienendo ya uchumi ya nchi. Sio lazima kuorodhesha kwa sababu hii orodha ya humu ndani si mgao wa mirathi ya nchi ambazo zinahusika katika Muungano. Huu ni mfumo wa maendeleo wa maeneo hayo ili kuweza kuyadhibiti vizuri kuendeleza nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwanza nianze kuwapongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Waziri wa Nchi, Mazingira ya Muungano na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Waziri wa Nchi, Kuondoa Umaskini na Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Napenda niwapongeze kwa kazi nzuri iliyofanywa na Wizara hii na ningependa moja kwa moja nianze kwa kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni Wizara mbili kwa moja ambazo zinawasilisha na ningependa ku-*comment* kidogo tu kuhusu Muungano halafu nije kwenye *topic* yangu ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, tutapata muda mbele ya safari ya kujadili suala la Muungano. Kama kuna wakati ambapo nchi yetu itakuwa kwenye mtihani mgumu sana, mtihani utakaoashiria kama kweli tuko pamoja, tumeshikamana na tunakwenda pamoja ni uchaguzi wa mwaka 2005. Huu ni wakati mzuri kwa Wizara na hasa Ofisi ya Makamu wa Rais, kukaa chini kutathmini na kufanya uchambuzi wa hali ya juu sana unaohusu hali ya kisiasa Zanzibar. Hali ya kisiasa Zanzibar isipokuwa tulivu na amani inaweza sana kuathiri Muungano wetu. *(Makofi)*

Mshikamano kati ya *CUF* na CCM Zanzibar usipokuwa mzuri, unaweza ukaathiri Muungano wetu. Chama Tawala Zanzibar kisipokuwa kitu kimoja na tukawa na mmomonyoko au mgawanyiko ndani ya CCM Zanzibar hilo linaweza likaathiri Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mambo ya aina hii yanayonifanya nithubutu kusema kwamba, miaka miwili na nusu iliyobaki ni michache sana. Tunatakiwa tujiweke sawa kuangalia Katiba yetu ya Jamhuri na kama kuna marekebisho ambayo tunaweza ku-*accommodate scenarios* mbalimbali zinazoweza kutokea mbele ya safari, hilo litanusuru Muungano wetu na tusilikalie kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nije sasa kwenye mada yangu ya umaskini, nikiwa mmoja wa watu wanaotoka kwenye Mikoa maskini ya nchi hii, Lindi. Sasa ninachotaka kuzungumzia kwa dakika tisa, kumi, zijazo ni ushauri wangu kwa Wafadhili, ambao wanatoa misaada au wanazo *projects* katika nchi yetu za kutusaidia sisi kuondokana na umaskini. Upo mushkeli ambao ningependa niuzungumzie leo na nadhani itaeleweka. Sina tatizo na kwanza niwapongeze watu wa *TASAF* wako Mkoa wa Lindi na wamefanya kazi nzuri sana kwenye Jimbo langu la Mtama na tunawashukuru sana kwa miradi yote waliyoifanya ya kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Sina tatizo kabisa na miradi mbalimbali ambayo ipo nchini kwetu. Lakini kinachonisumbua kila ninapolala usingizi ni kwamba, miradi inayoletwa na Wafadhili haiwafikii Watanzania wote kwa mara moja wala haiendi kwenye Mikoa yote kwa wakati muafaka. Kinachotokea ni kwamba, Wafadhili wanachagua wapi waipeleke miradi yao, kwa muda gani na kiasi gani cha fedha. Kwa mfano, *FINIDA* walikuwa Lindi na Mtwara, wanapomaliza programu yao wanaondoka na umaskini unarudi pale pale. Waingereza, wao walikuwa wanashika Iringa na Mbeya, Wajapani, Mkoa wa Kilimanjaro, Wajerumani Tanga, Wa-Irish nadhani na *DANIDA* Morogoro, Sweden, Kagera na rafiki zangu wa Canada kule nyuma ilikuwa *Hanang Wheat Project* Arusha.

Sasa wafadhili wanapojikita kwenye baadhi ya Mikoa ya nchi na fedha zile zinazoletwa bila ku-*address* nchi nzima kwa ujumla wake, mimi naona huo ni mushkeli. Ni tatizo la kwanza. Kwamba pamoja na uzuri wa misaada hii na tunawashukuru sana kwa misaada hii. Mimi nashukuru sana nchi hizi kwa misaada hii. Lakini kwa sababu hii ya *selective engagement* kwamba, wao ndio wanaamua wapeleke wapi msaada huu, kwa kiasi gani, kwa muda gani na kwamba misaada hii wanapoitoa na programu zao zikiisha wanarudi makwao, suala la upigaji vita umaskini katika nchi yetu haliwezi kuwa *sustainable*. Hatuwezi kuwa na mradi endelevu iwapo wanaotoa mradi huu au wenye miradi hii wanakuja kwa wakati wao, wanachagua mahali pa kwenda na kiasi cha fedha cha kuzitoa na halafu ukiisha muda wao wanaondoka. Huu mkakati wa kuondoa umaskini katika nchi yetu hauwezi kuwa uendelevu, yaani vita ya kuondoa umaskini haiwezi kuwa endelevu. Hili ndilo linamsumbua . Tuna matatizo ya wenzetu kuwaacha wakituamulia miradi wanayoitaka kuiendesha na sisi tunawaangalia na pale wanapoamua kutoa wanatoa, pale wanapoamua wasitoe hawatoi. *(Makofi)*

Belgium kwa mfano, kwenye hotuba imeshasema, walikuwa watoe milioni tatu Dola za Marekani. Hizo ni sawa na shilingi bilioni tatu, lakini hadi sasa nadhani wametoa shilingi laki tano tu au shilingi milioni mia tano. Matokeo yake miradi zaidi ya 12 katika nchi yetu bado haijatekelezwa na hatuna ubavu sisi wa kuwashika shingo na kuwalazimisha kwamba watufanyie hivyo katika kutekeleza Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Nawashukuru watu wa *UNDP* nadhani wameshatoa kiasi ambacho walikuwa wameahidi na watu wa *Swedish Development Cooperation (SDC)* wamekwishatoa viwango walivyoviahidi, lakini Belgium bado. Tunachotakiwa sasa ni kuwaomba tu watoe hicho.

Mheshimiwa Spika, lakini narudi tena pale pale kwamba hata wakitoa pesa hii tukawaacha hivi hivi waamue wapi pa kwenda halafu programu yao ichukue muda gani, itachukua wakati gani na ukishaisha wanaondoka, bado umaskini katika nchi yetu utaendelea kuwakumba wananchi wetu. Sasa hili ndilo linaloashiria kwamba, ni tatizo na ni vizuri tukaja na mapendekezo ya nini kifanyike na ni matumaini yangu kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais itazingatia ushauri ambao Wabunge, pamoja na mimi mwenyewe tutautoa. Ushauri wenyewe ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni vizuri tuendelee kuwaomba wafadhili watupatie misaada hiyo tunayohitaji katika kupambana na umaskini uliojikita katika nchi yetu. Lakini pili, ni vizuri nchi yetu kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na hasa hii inayoshughulika na umaskini kuhakikisha kwamba, tunakuwa na chombo cha Kitaifa kitakachokuwa kinaratibu na kupokea miradi yote hii kwa pamoja na kuangalia matatizo ya kweli ya umaskini yaliyopo katika nchi yetu ili chombo hiki kiweze kwa kushirikiana na wafadhili, kusambaza huduma, kutoa misaada, kuwasaidia wakulima, kuwasaidia wafanyakazi ili kuondokana na umaskini uliojikita katika nchi yetu. Tusipokuwa na chombo cha Kitaifa kinachoratibu, kinachoelewa matatizo ya wananchi wetu, lakini tukawaacha tu Wafadhili waamue wanavyotaka wenyewe, tutakuwa na nchi ambayo

imegawanyika katika pande mbili. Upande mmoja wa Mikoa inayosaidiwa na upande mwingine wa Mikoa ambayo hata msaada wenyewe hawaupati.

Mheshimiwa Spika, nadhani hapa umesikia kilio cha baadhi ya Wabunge wakilalamika kwamba, huku kwetu kitu hiki hakipo kabisa. Ni kutokana na hali hiyo hiyo kwamba, Wafadhili wanaamua wenyewe wapeleke wapi msaada, kwa *speed* gani, kwa muda gani na fedha kiasi gani. Hiyo nasema ni tatizo. Dawa pekee ni kuwa na chombo cha Kitaifa kitakachoweza kuratibu masuala yote haya. Sio tu kuratibu nani anafanya kazi wapi, lakini kuratibu hasa fedha kiasi gani zinaingia katika nchi katika kipindi hicho, kutoka nchi zipi na fedha zile zinatumika vipi na ikiwezekana kuwe na *management* ambayo inaweza kuwajibishwa kabisa iwapo matumizi ya fedha za kuondoa umaskini katika nchi zinatumiwa vibaya au haziendi kwa wananchi wote na badala yake zinakwenda kwa upande mmoja tu. Hilo ndilo ombi langu la pili. *(Makofi)*

Ombi la tatu, nadhani nchi iwe na uchungu. Wananchi, Wabunge na wote sisi tuwe na uchungu kwamba, kile kidogo kinachopatikana kutoka kwa wenzetu hasa Wafadhili, kiwe kinatumika vizuri basi. Hata kama hilo la pili nililolipendekeza linachelewa kutekelezeka, lakini kile kidogo kinachopatikana hakina budi kumfikia mlengwa na mlengwa hapa ni mfanyakazi, wafanyabiashara wadogo wadogo, wakulima, kwa sababu misaada yote ya kuondoa umaskini inalenga kwanza kabisa katika ku-*improve* miundombinu yetu yaani kuongeza miundombinu, inalenga katika kuleta ajira, kusaidia wafanyabiashara wadogo wadogo na Sekta nyingine na pia katika kutoa huduma kwa watu ili waweze kujitegemea. Kwa hiyo, ningeomba pesa zinapopatikana hata kama ni kidogo kiasi gani zitumike kama zinavyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda tena nimalize kwa kusisitiza mambo yangu mawili. Moja, huu ni wakati muafaka sana kuliangalia suala la Muungano kama nilivyosema. Lakini pili, suala la umaskini, wawekezaji hasa Wafadhili wasiachwe peke yao kuleta fedha wanavyotaka wao na kwenda wanakotaka. Wawe *coordinated* na hatuna budi kuwa na chombo cha Kitaifa kitakachokuwa kinaratibu fedha hizi, kuratibu wapi ziende, zitumike vipi, ili miradi hii iwe endelevu badala ya kuiacha hivi hivi. Kwa sababu tukiacha hali ilivyo, miradi hii kama ya *NIGP* inapokwisha wakiondoka na sisi tumekwisha. *SIDA, SDC* au hata *Swedish Development Cooperation* na miradi mingine yote ya *TASAF* ambayo iko *funded* na *World Bank* ikiisha tunarudi pale pale. Ili tuwe na miradi endelevu tunahitaji chombo cha Kitaifa cha kuratibu mambo yote hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na ni matumaini yangu kwamba, nimeshaeleweka na nashukuru na ninaunga tena mkono hotuba hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo tumefikia mwisho wa shughuli za asubuhi. Kwa hiyo, kabla sijasitisha shughuli za Bunge niwatangazie wale ambao watashiriki katika kutoa mawazo yao katika kipindi cha mchana.

Kwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais, ina Mawaziri wa Nchi wawili na wote watashiriki katika kujibu hoja, kwa hiyo tumepanga wachangiaji wanne tu ili waishie saa 12.00. Nao ni Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir na Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail. Wako walioomba lakini wameshachangia mara tatu na wengine mara nne, lakini kwa utaratibu wetu basi, hao naomba wachangie kwa maandishi.

Tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Leondard Derefa, mkereketwa wa uchumi wa madini, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge, wale wote wanaotoka kwenye maeneo ya migodi na ambao wangependa kukutana na Viongozi wa Migodi mikubwa ya madini, kuna migodi mikubwa ya madini, viongozi wake wako hapa, basi Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kukutana na Viongozi hao, ambao pia watakutana na Kamati ya Uwekezaji, wanaalikwa kwenye Mkutano utakaofanyika saa 9.00 mchana kwenye Chumba Na.37, Vyumba vya Kamati. Wale wanaopenda kuzungumza na Viongozi wa migodi mikubwa.

Baada ya tangazo hilo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.57 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kama mtu wa kwanza leo mchana, naanza kwa kusema ili nisije nikasahau, naiunga mkono hoja iliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nichukue nafasi fupi ya kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwanza kwa jitihada zake kutembelea nchi hii na kuifahamu zaidi. Pili, kwa kujitahidi kuhimiza yale majukumu ambayo yako chini ya Wizara yake. Kwa kweli amefanya jitihada kubwa kwa muda mfupi. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri wawili, ndugu zangu, Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kazi yao nzuri na hotuba nzuri ambayo wameileta mbele yetu. Nawapongeza pia Wataalam wote walioko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia Muungano na mambo mengine yanayofuata, lakini nitazungumzia kidogo mambo ya umaskini. Kuhusu Muungano wetu, nachukua baadhi ya maneno ya wenzangu wachache kabisa waliozungumza mapema. Muungano wa Tanganyika na Unguja kwa kweli ni Muungano wa kidugu zaidi kuliko wa Kikatiba na Sheria. *(Makofi)*

Kwa jinsi nilivyoona masuala yalivyoanza kuzungumzwa leo asubuhi hapa Bungeni, kwa jazba kubwa na hali ambayo mimi mwenyewe binafsi sikuitegemea, ninafikiri tukiendelea hivyo bila kuzungumza kwa uangalifu zaidi, inawezekana tukawa kero kubwa ya Muungano kuliko zile kero zinazowapata wananchi wetu kwa masuala ya Muungano. *(Makofi)*

Masuala ya Muungano hayataki kuzungumzwa kwa jazba kubwa. Yanataka kuzungumzwa kwa uangalifu mkubwa sana na mimi siamini kwamba, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni matatizo tupu siamini, kama ingekuwa matatizo tupu hakuna mafanikio tusingeweza kufika hapa tulipofikia, haiwezekani. Ni miaka mingi Muungano huu ni mfano katika Afrika, hakuna Muungano wowote wa namna hii kwa miaka yote hiyo. Kwa hiyo, tumefanya mengi mazuri na makubwa kiasi kwamba, tumeweza kudumu kwa kiwango cha muda wote huu na sasa yale yaliyobaki tuyatafutie ufumbuzi wa kistaarabu na kwa kweli wa kidugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kwamba, Wizara hii ya Makamu wa Rais ilikuwa na Mashirika. Ninafahamu Mashirika mengi ya Serikali nchi nzima yameshabinafsishwa, mengine yameuzwa na mengine yamepewa utawala mpya wa nje. Lakini siamini kwamba, wataalam waliokuwa wanafanya kazi kwenye mashirika hayo mapema walikuwa hawana uwezo wa kuyaendesha mashirika hayo. Ninachoamini ni kwamba, chanzo kikubwa cha mashirika yetu kuporomoka ni Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Viongozi wengi walikuwa wanapeleka vijana wao huko waajiriwe bila kuangalia ikama ya mashirika haya, yakajaa watu kwa wingi kiasi kwamba hawakuhitajika. Lakini la pili Serikali zetu zilikwepa sana kulipa madeni kiasi kwamba mashirika yalishindwa kufanya kazi. Ndiyo maana yakauzwa, ndiyo maana tukabinafsisha hata *management,* lakini kuweka kasoro ya *management* si kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kulipa deni lake haraka baada ya hili lililotokea kwa Shirika la Umeme la Tanzania. *(Makofi)*

Tunatakiwa tulipe madeni, hatutakiwi tuzungumze, kama unadaiwa lipa, kama unaona uwezo wa kulipa wakati ule huna, anzisha mazungumzo, unataka nani aanze kuzungumza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa hilo naliachia hapo lilipo. *(Makofi)*

La pili, napenda kuzungumzia maeneo ya kuondoa umaskini na hasa pale ambapo wahisani wanakuja nchini kwetu kusaidiana na vyombo mbalimbali na kuweza kusaidia miradi mbalimbali ya maendeleo. Baadhi ya wenzangu walizungumza asubuhi. Nakubaliana na wale wanaosema ni vizuri kiundwe chombo kama hakipo, kinachoweza kuratibu, fedha zinazoingia nchini na matumizi ya fedha hizo na baadaye taarifa ya ukaguzi itolewe. Hatuwezi kukubali mapesa yafurike nchini, hatujui ni fedha kiasi gani, zinatumika namna gani, halafu baadaye tunasema kuna wahisani maeneo fulani ya nchi na kule hakuna. Naomba hilo lifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msaada wa Mheshimiwa Spika, nimekuwa mzoefu wa Kamati ya Fedha kwa kuniteua, hasa Kamati za Kudumu zile za zamani za *PAC* na *LAAAC.* Ninafahamu kwamba, kuna nchi wahisani ambao wanaelekeza pesa zao moja kwa moja kwenye miradi badala ya kuzipitishia kwenye mkondo wa Serikali, Hazina. Kwa hiyo, katika wito huu wa kuanzisha chombo au Idara Maalum Hazina cha kuratibu fedha hizi na kwenda moja kwa moja na kutoa matumizi yake ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Maana tunaweza kuamini kwamba, wako wahisani wanaosaidia sehemu fulani ya nchi kumbe fedha zile hazitumiki pale, mwisho zinarudi huko huko zilikotoka. Ningependa pia niseme tusiwawekee masharti wahisani, wanapochagua Mikoa, Wilaya, mahala pa kuwekeza na kusaidia miradi fulani, tuwaachie uhuru maana ni pesa zao na ni uamuzi wao. Tuwaachie huru, wachague maeneo wanayotaka, wapeleke fedha kwenye miradi wanayotaka, wakati wanaotaka, lakini zile Wilaya nashauri na Mikoa ambayo wahisani hawapendi kwenda huko, Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano ijazie huko. Ipeleke misaada huko, ichukue nafasi ya wahisani kama hawafiki huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nirudi kwenye suala la umaskini. Suala la umaskini ni suala kwa kweli ambalo siyo suala rahisi ni suala gumu na pana na ndiyo maana baada ya Bajeti ya Serikali na taarifa ya uchumi ya Serikali, Wizara zilizofuatia kila Wizara ilikuwa na eneo linalozungumzia kuondoa umaskini. Suala hili ni pana na nadhani Mheshimiwa Rais alilipeleka kwa makusudi chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais ili kulipa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tujue kwamba, mhimili mkubwa wa suala la kupambana na umaskini na maendeleo ya Watanzania ni suala la Mheshimiwa Rais mwenyewe. Wizara zote ziko chini yake. Kuna Wizara zile ambazo ni moja kwa moja na Wizara ambazo ziko chini ya Makamu wa Rais na zile Wizara ambazo ziko chini ya Waziri Mkuu na Wizara ambazo zinajitegemea lakini masuala muhimu ya kisera uamuzi haziwezi kuamua bila Rais kukubali, maana Wizara zote ziko chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za dhati kabisa za kupambana na umaskini na kuleta maendeleo kwa Watanzania, Rais Mkapa, amekuwa mstari wa mbele kweli kweli na kusema kweli Rais amefanya kazi kubwa tangu amepata nafasi hii ya kuongoza wananchi kiasi kwamba, ningesema ni jasiri wa aina ya pekee. Tukumbuke kidogo kwamba, Rais Mkapa alipoingia Ikulu, Hazina ya Taifa hili ilikuwa haina hata thumni. Hivi sasa tunavyozungumza tunaambiwa Hazina ya Serikali inaweza ikatuendesha kwa miezi mitano au sita wakati tunapata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais amefanya kazi kubwa. Kazi ya kwanza ilikuwa ni kuwasiliana na Mataifa ya nje na marafiki pale ambapo tayari walikwisha tuona hatufai na tulinyimwa misaada na mikopo. Rais akaendelea kulipa madeni japo kwa kiwango kidogo ili kuonyesha ustaarabu na uungwana wa Watanzania baada ya madeni yale kukomaa. Rais akaendeleza hoja ya nchi tajiri kusamehe madeni nchi maskini. Rais akaendelea kuweka hoja kwamba nchi tajiri sasa zifikirie kabisa kuzisamehe nchi maskini na Tanzania ikiwa mojawapo. Baada ya hapo Tanzania ikakubalika na kupewa sifa za kukopeshwa na kupewa misaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbushane tulikotoka hilo ni eneo la mahusiano ya Kimataifa, ambapo mpaka leo Mataifa mengi yanatukopesha, mengi yanatupa misaada na hivyo Tanzania leo ipo kwenye ukurasa wa juu kabisa kama nchi inayoheshimika kwa kauli zake na vitendo vyake.

Kwa upande wa nyumbani, Rais alianza kujenga msingi wa Serikali yake wa kupambana na matatizo ya ndani. Hali hiyo ilianza kwa kukusanya mapato ya nchi kiasi kwamba tulipoanza tulikuwa na

shilingi milioni ishirini na kitu makusanyo, leo ni zaidi ya shilingi milioni mia moja. Rais Mkapa amefanya kazi ya kijasiri kweli kweli na matokeo ya kazi hiyo aliyofanya ndio hapa leo, kwamba Wanavijiji wetu kule vijijini wanasherehekea matunda ya kazi hiyo. *(Makofi)*

Baadhi ya matunda ya kazi hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, ni yale matengenezo yanayoendelea ya barabara kubwa na barabara ndogo vijijini, kuondoa karo za shule za msingi, kuondoa kodi ya maendeleo, kuondoa kodi mbalimbali zenye kero na ushuru mbalimbali, mpango wa kuboresha elimu huko vijijini, kusambaza umeme na simu vijijini. Hizo ni kazi ambazo amezifanya. Jitihada za kusambaza maji safi na salama, Mpango wa *TASAF*, kero za kuondoa vizuizi barabarani, mikopo nafuu kwa akina mama na vijana, kuanzishwa kwa mifuko mbalimbali ya kusaidia kupambana na umaskini na mengine mengi ambayo yamefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetembea kwenye Jimbo langu, nimepata hoja zaidi ya 20, lakini zote zinafanana. Zinasema hivi ni kwa nini mwaka 2005 Mkapa hawezi kuendelea? Zinasema hivyo. *(Makofi)*

Ni maneno ya wananchi wa Jimbo langu ninayozungumzia. Kwa hiyo, naomba mnisikilize. Wanasema ni kwa nini hawezi kuendelea? Jibu langu ni kwamba, jamani tuna Katiba, tumefungwa na Katiba. Lakini jambo hili ukilisema hapa, linakuwa gumu. Siku hizi hata vyombo vya habari, kumbe vina matatizo ya ajabu kabisa. Alisema ndugu yangu hapa Mheshimiwa Derefa, wakamwandama mpaka maoni ya Mhariri na kuwataka Watanzania, wampuuze na kumnyanyasa kwa kauli yake. Nimeshangaa vyombo vya habari vinasema ni kioo cha jamii. Kwa hiyo, visizuie mawazo ya watu wanaotaka kuzungumza, badala ya yake viwaachie watu uhuru wa kuzungumza. Watu watapuuzwa kwa kauli zao bila kushawishiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi Mkapa aendelee. Lakini hoja za wananchi zinasema hivyo. Ninachosema ni kwamba, hata ukisema Mkapa aendelee. Namfahamu, mtu wa heshima sana, anaheshimu kabisa Katiba. Ni mtu *up right* na mambo haya anaweza asikubali. *(Makofi)*

Ninachosema ni kwamba, Mkapa amefanya kazi kishujaa sana. Kabla ya mwaka 2005 Taifa hili lifikirie kumpa nishani ya juu kabisa ya Taifa hili kwa pongezi za uchapa kazi wake mkubwa kwa kuyafikisha maendeleo kule chini. *(Makofi)*

Nimejiuliza, kwa nini Watanzania wanasema arudie, aendelee ingawa Katiba haitaki? Jibu ninalijua. Hawana hakika Rais atakayekuja ataweza kufikisha huduma hizi kule kama Mkapa alivyofikisha. Kama tungemjua Mkapa tukamwunga mkono mapema kabisa wakati anaanza, pengine leo tungekuwa na hatua kubwa zaidi mbele kuliko sasa tunapozungumza. *(Makofi)*

Namshukuru Mzee wangu, Mheshimiwa Kingunge yuko hapa, Chama Cha Mapinduzi, naomba tubadilike kidogo. Tuendelee na utaratibu ule wa kumchagua kiongozi wa nchi yetu. Lakini tulegeze kidogo. Tuseme hivi, yeyote anayetaka kuwa Rais wetu, mpeni nafasi, itangazwe ili wanachama wafahamu. Tumjue ili wakati ukifika mkituletea yale majina machache tuwajue. Sisemi awe kijana, awe mwanamke au mzee, hapana. Ninachosema ni kwamba, wale wanaotaka kugombea wajulikane ili tuweze kuwa kwenye nafasi ya kufanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nampongeza Rais Mkapa, namwomba tu kwamba wakati anamaliza, kwa vile amefanya mambo makubwa sana, amebinafsisha mashirika mengi, amefanya kazi nzito na Tanzania imerudi kwenye ramani nzuri, naomba yale mashirika machache yaliyobaki amwachie mwenzie kwa sababu Roma haikujengwa siku moja.

Mwisho, namwomba atembelee Jimbo langu tafadhali, Kata ya Umba, Tarafa ya Mtae, wanamtaka sana, Ma-*Sister* pale Rangwi atembelee. Si lazima aanze ziara, hata wakati wa kupumzika. Najua siku hizi anapenda kupumzika Lushoto, akichoka basi anaweza kwenda kule kutembelea mpaka Mtae. Naibu Waziri wa Mawasiliano amefika, Ndugu Msabaha amefika, basi afike Rangwi wale Ma-*Sister,* vijana wetu

wazuri, wachapa kazi, wamsalimu pale, halafu basi tumshukuru na kumwombea kwa Mungu, maisha mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii leo mchana na haya niliyosema naomba Serikali iyafikirie kwamba kweli Mkapa anastahili heshima ya Taifa hili, wale wanaochukia tukisema vizuri juu ya Mkapa basi hiari yao na watafute njia ya kujinyonga, lakini ukweli ni kwamba, Mkapa amefanya kazi ya kijasiri kweli kweli. Ahsante na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Kagonji. Nadhani Mheshimiwa Derefa, hatabomoa *desk* pale na wenzake wameanza kufumba macho na masikio tushangilie lakini kwa namna nyingine.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Kwanza niungane na wenzangu kwa kuwapongeza Mawaziri wawili wa Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Kwanza nataka kusema kwamba, Ofisi hii ni muhimu sana na hasa kwa vile inagusa suala la Muungano. Muungano ni kiini na uti wa nchi hii. Hili la Muungano tukitaka tusitake ni suala ambalo litaleta utata mkubwa sana siku za baadaye. Lakini kabla sijaendelea huko na mimi niungane na wenzangu kumsifu sana Mheshimiwa Mkapa, kwa kazi kubwa sana anayoifanya kuelekeza au kuweka dira ya nchi hii na kutufikisha hapa alipotufikisha ni kazi kubwa sana amefanya na kwa kweli anastahili sifa na yale yote ambayo yameelezwa na wale walionitangulia. *(Makofi)*

Ningeomba vile vile kwa kupitia Wizara hii na kupitia kwa Mawaziri waliopo pale, nitoe pongezi zangu na kuomba watupelekee salamu na pongezi kutoka kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Matemwe Zanzibar, kwa ziara ya Mheshimiwa aliyoifanya Jimboni kwetu na msaada aliotoa kutusaidia katika ujenzi wa shule ya Mfurumatonga, mahali ambapo palikuwa hakuna shule na watoto walikuwa wakisumbuka sana kufuata shule masafa marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yote yaliyozungumzwa ya kuondoa umaskini, kusimamia mazingira, shughuli za *NGO,* nitajikita zaidi katika masuala ya Muungano. Nasema kwamba, Waheshimiwa Mawaziri katika hotuba hii ambayo tumepewa, nasema, haikuwa na kitu ambacho kingeweza tukasema kwamba kinaunganisha ama kinatupeleka kule ambako Katiba ya nchi hii ambayo ninayo mkononi inatuelekeza wapi twende. *(Makofi)*

Kama walivyozungumza wenzangu walionitangulia, ni miaka 40 au karibu miaka 40 sasa hivi lakini suala la Muungano kwa uwazi wake tunazungumzia katika hali ya kigugumizi. Matatizo tuliyonayo ya Muungano tunazungumza katika hali ya kigugumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Katiba hii ambayo ninayo mkononi leo naikamata kwa mara ya pili, kwa maana ya kwamba, kuizungumzia. Nilizungumza kwa mara ya kwanza nikakamata Katiba hii ambayo mimi mwenyewe, wewe Mwenyekiti na viongozi kati yetu sisi tumekula kiapo kuilinda Katiba hii na tukasema kwamba, tutailinda, tutaitetea na tutaitekeleza. Lakini kuna baadhi ya mambo tunakwenda katika hali ya kwamba hatuko katika dhana hiyo au katika azma hiyo na mimi nasema kwamba, ili Katiba hii itekelezeke, wale wanaochaguliwa kuwa viongozi baadhi yetu tumo kama Wabunge, Mawaziri, basi tuwe ni waumini wa Muungano. Bila kuwa muumini wa Muungano huwezi ukatekeleza haya tutababaishana tu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Katiba ukurasa wa 15 ibara ya 9, naomba kunukuu kwa ruksa yako. Inasema: "Lengo la Katiba hii ni kuwezesha ujenzi wa Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au wa chochote kati ya vyombo vyake na udugu na amani kutokana na kufuata siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, ambayo inasisitiza utekelezaji wa misingi ya kijamaa kwa kuzingatia mazingira yaliyomo katika Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, Mamlaka ya Nchi na vyombo vyake vyote vinawajibika kuekeleza sera na shughuli zake zote katika lengo kwa kuhakikisha hayo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu (d) inasema kwamba: "Maendeleo ya uchumi wa Taifa yanakuzwa na kupangwa kwa ulinganifu na kwa pamoja, siyo wa pamoja na kwa pamoja." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba hii ndiyo inavyosema. Sisi tukizungumzia Muungano, hatuzungumzii Muungano *per se*! Muungano tuuache kama ulivyo, Watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Katiba inazungumzia suala la uchumi, hilo ndilo sasa hivi tunaloliongelea na linalotutesa. Sisi Tanzania kisiasa tunanong'ona vizuri sana, lakini suala la uchumi kila mtu na lake, Katiba inazungumza kwamba, tulinganishe uchumi na tuwe na uchumi wa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo tunafika mahali kufikiria uchumi umefika nchi za Afrika Mashariki, nchi za *SADC,* lakini tunashindwa kufikiria watu laki tisa pale au milioni moja, kuunganisha tunashindwa, tatizo ni nini? Kwani ni hatuna uchumi wa pamoja tukaivua ile nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni la kweli, bila CCM hakuna Muungano. Lakini tusiliangalie hilo kwa upande mmoja. Nasema hilo tusiliangalie kwa upande mmoja, tuliangalie kwa pande zote mbili. Unguja kule tutapinduana mara ya kwanza, tutapinduana mara ya pili, tutapigana mara ya kwanza, tutapigana mara ya pili, tutakaa mahali tutasita, jamani tunapigiana kitu gani? *(Makofi)*

Lakini nasita kusema hivyo Bara itakuwa tofauti kubwa sana. Kwa hiyo, kuwepo kwa Muungano tunahakikisha kwamba, usalama wa nchi hizi zinaishi katika hali ya usalama na raia wake. Tumekuta juzi hapa katika kuzungumza, wakati wa Semina iliyofanyika tarehe 19 Julai, 2003 kulikuwa kunazungumziwa suala la Wapemba kwa maana ya Wanzibari waliokuwepo Dar es Salaam kwamba waende wakajenge kwao. Waende wakajenge kwao wapi? Tanzania ni moja, lakini hatukuzungumza suala la ndugu zangu kule Wamakonde, ndugu zangu kule Wachaga. Nampongeza sana Mheshimiwa Dr. Lamwai, aligusia suala hili akasema ni kosa kubwa sana hilo, kama tutafika mahali kuwaambia kwamba Wapemba au Waunguja waende wakajenge kwao, basi tutafika mahali ambapo Wandengereko waliopo pale watasema na ninyi hapa si kwenu tafuteni mahali mkajenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachozungumza mimi ndani ya Katiba hii inahubiri umoja, utaifa, mshikamano na hakuna ubaguzi. Sasa tunasema CCM bado iendelee kutawala. Vyama vya Upinzani vyote vinahubiri suala la mambo ya ajabu ajabu, sitaki kuyataja mnayafahamu. Tukifanya mchezo tukiacha hiyo na tatizo lililoko kule kwetu siyo suala kwamba tunaambiwa Zanzibar imekuwa kiuchumi, chakula hamna, pesa hamna, mazingira ya pesa hamna na mtu ukimnyima chakula unaweza kumtawala, ukamwambia mambo yasiyokuwepo na ukafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachohimiza na ninachokiomba ninasema kwaba, tatizo si Muungano. Tatizo tulilonalo watendaji wetu baadhi yao hawana nia hiyo. Hawana imani yaani hawakujengeka katika kuamini, siyo waumini wa Muungano, wana mambo yao lakini tujitahidi. Maana yake watu wanasema ngoma ikivuma sana, inakaribia kupasuka. Lakini *Inshallah* hii haitapasuka. Ikiwa sisi sote tuna nia moja, tuna azma moja, haitapasuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hii hotuba nachelea kusema kwamba, katunyanyasa katika hotuba hii. Ukurasa wa 6 anasema vipi? Viongozi wamekuwa wanashirikiana katika masuala mbalimbali mfano, Sherehe za Mapinduzi, Uhuru, wanazungumzia sherehe za Mapinduzi na Uhuru ndiyo kushirikiana huko? Haya tunaambizana mambo gani?

Tuna matatizo ya elimu ya sekondari na matatizo ya elimu ya msingi, hatuyazungumzi, ndiyo matatizo ya uchumi hata hatuyazungumzi. Mheshimiwa Ntagazwa, hebu uunganishe hizi mbili, wewe kama Waziri, mawazo yangu kama ni Waziri wa Serikali ya Muungano, ulitakiwa kuyafuatilia haya, Wizara ambazo siyo za Muungano. Juzi Mheshimiwa Mungai, alituambia hapa, Rais anasema kwamba, pamoja na kwamba kuna baadhi ya Wizara hatukuungana, lakini nendeni sambamba na namshukuru sana Mheshimiwa Mungai, kwa jitihada zake, namshukuru sana Mheshimiwa Magufuli, kwa jitihada zake, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, kwa jitihada zake, linapotokea tatizo tunakwenda sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla kengele ya pili haijalia, nina mengi, lakini naunga mkono hoja na nasema tatizo si Muungano. Tukizungumza hapa tuzungumze matatizo ya watendaji tulionao. Waumini wa Muungano tunakwenda nao wengine, siyo tuwatafute waumini twende sambamba huko tunakokwenda na la mwisho la kuzingatia bila ya CCM hakuna Muungano, bila ya CCM bila ya Muungano hakuna usalama, si Zanzibar si Bara. Wenzenu kule hatuna msitu, sio watu kuingia misituni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mudhihir, anakujua Jozani, lakini huku Mheshimiwa Mudhihir aliingia mpaka upande wa pili Fuoni. Tunachokiomba tukamatane na tudumishe Muungano. Muungano ndiyo uhai wa nchi hii. Muungano ndiyo uhai wetu na Muungano ndiyo nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache namwomba Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, ajitahidi ayafuatilie mengine. Tuna matatizo hayo niliyoyazungumza ya MES, *TASAF*, Ukimwi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukimwi *TACAIDS* wanazungumza kwamba, pesa zisiende Zanzibar, watu wanatoka huku wanakwenda kule, wanatoka kule wanakuja huku, wanapita kama samaki, sasa tunazuia kitu gani? Tunasema twendeni pamoja ili tuzuie hili gonjwa lakini wanasema aah bwana huku huku, eti bwana huku huku watu wanakwenda kule! Mimi katika Jimbo langu nina mazingira ya utalii, waajiriwa wote kutoka Kenya wanasema Watanzania wako pale, wanasema watu kutoka Tanzania wako pale na labda tungepiga kelele lakini Ukimwi kule umejaa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDULLATIF HUSSEIN ESMAIL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa, napenda kuanza kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais wote wawili, wanaoshughulikia masuala ya Muungano, Mazingira na Kuondoa Umaskini, Mheshimiwa Arcado D. Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar D. Maokola-Majogo, Katibu Mkuu, Bwana Raphael Mollel, pamoja na wataalam na watendaji wengine, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Napenda kuwapongeza sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kuteua Tume ya pamoja ya Fedha, nina matumaini kwamba, Tume hii itakaa pamoja vizuri, itashirikiana na kuondoa kero zote zilizokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuipongeza SMZ kwa kufahamu umuhimu wa kufungua Akaunti katika *Bank of Tanzania.* Napenda kuipongeza sana SMZ kwa hatua hiyo iliyoichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuwapongeza wananchi wote wa Tanzania, kwa kushiriki vizuri katika sensa ya mwaka 2002. Takwimu zimetusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napongeza uhusiano mzuri baina ya SMZ na SMT, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano wa Tanzania. Pia napenda kuzipongeza Wizara ambazo si za Muungano, kwa ushirikiano wao mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kudumishwa kwa Muungano ni suala la muhimu sana, kitu muhimu ni kwamba, tupendane, tuwe wakweli na waaminifu, unafiki usitutawale. Napenda kuzipongeza Serikali zote mbili za SMZ na SMT kwa amani na utulivu uliopo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuondoa umaskini, tujaribu kuwasaidia wakulima na wafanyabiashara hasa wadogo wadogo, tuwaondolee kero za kodi zinazowakabili ili wawe wafanyabiashara wakubwa na baadaye tuwatoze kodi bila ubaguzi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira, iliyosomwa leo na Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, imesema wazi kwamba, ujenzi wa Jengo la Benki Kuu, mradi

huu unaendelea kutekelezwa. Kwa hiyo, napenda kuwashauri Waheshimiwa Wabunge ya kwamba, tuwe na subira, tutazame vipi tutafikia, tusiwe na jazba, *Rome was not built in a day, it took several years to built Rome sometimes to rent is better than to build. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukakodi jengo kwa dola 2,000 kwa mwezi, ujenzi una-*cost* dola milioni 300, tutazitoa wapi kwa ghafla, tuwe na subira. Najua sote tunataka jengo zuri Zanzibar lakini tuwe na subira, tutazame wakati na hali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *TANESCO,* mimi nasema fikra zangu kwamba, hii ni ajali imetokea kwa bahati mbaya, suala hili tusilifanye la kisiasa, ni suala la kibiashara. Tusikae Waheshimiwa Wabunge humu tunabishana, tunalaumiana, hakuna wa kulaumiwa hili ni suala la kibiashara. Ikiwa SMZ imeshindwa kulipa ijirekebishe, ilipe na *Net Group* kama imefanya makosa na wao wajirekebishe. Waheshimiwa Mawaziri wote wawili wamekwishakaa, wamekwishajadiliana na wamekwishasema kwamba, jambo hili halitofanyika tena katika historia ya Tanzania. Kwa hiyo, hatuna haja ya sisi Waheshimiwa Wabunge humu ndani tukawapa faida wenzetu wa upande ule kule. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuzungumzia kidogo kuhusiana na suala hili la hotuba kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuwashukuru na kuwapongeza wote waliohusika katika kutoa hoja hii. Napenda kuanza na Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, ambao wamekuwa ni chimbuko la kumsaidia sana Mheshimiwa Makamu wetu wa Rais, kwa kazi nzuri anayoifanya hivi sasa. Nami napenda niungane na wenzangu katika kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais, kwa kazi nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni tulipoanza wote mnafahamu yeye ni mtaalam, tulisema ataiweza hii kazi? Wote tulikuwa na wasiwasi. Sasa mnaona anavyochemka, anavyofanya kazi yake vizuri huko Mikoani kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza Ilani yetu ya Uchaguzi. Mimi napenda kumpongeza na aendelee na nguvu hizo hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda niwapongeze kuanzia Katibu Mkuu na Wasaidizi wake na viongozi mbalimbali wa Taasisi mbalimbali ambazo wanapambana na umaskini na mambo ya mazingira, wote wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba nzuri zilizotolewa na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Anne S. Makinda, mimi napenda kuipongeza kwamba, wametoa taarifa nzuri. Lakini pia hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Ali Said Juma, kwa kweli nao wamejitahidi wametoa hotuba nzuri na wameiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Huu ni mwanzo mzuri wa kufanya kazi wote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kusema hayo nilikuwa na haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, baada ya sensa ya mwaka 2002, Watanzania wote tunaelewa ya kwamba, sasa tuko 34.6 milioni. Pia tunaelewa hali ya ujumla ya maisha ya Watanzania wetu kwa ujumla. Tunaelewa pia kwamba, hali ya maisha inapishana Mikoa kwa Mikoa na tunaelewa kwamba, baadhi ya Mikoa ambayo haifanyi vizuri ni pamoja na Mikoa ya Pwani, Lindi, Rukwa na Shinyanga, bado inataka kusaidiwa kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya semina iliyopita juzi, mimi naomba tutumie takwimu hizi ili kuanza kubadilisha utaratibu wetu wa kupanga mipango yetu kuanzia Vijijini, Wilayani katika Mikoa mpaka Kitaifa ili angalau kuanzia mwaka kesho tutaona Bajeti zitakazokuja zitakuwa zinajibu haya ambayo yamejitokeza. Hilo lilikuwa la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuomba kabisa kwamba, Serikali pamoja na *NGOs* zote tulizonazo, zianze kuelekeza nguvu zake kutokana na takwimu ambazo zilikuwa zimewasilishwa hata kwenye semina iliyopita. Zitawasaidia sana kuja na kitu ambacho kinaweza kuwasaidia angalau tukatokana na matatizo ambayo yamejionyesha hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda niingie kwenye Hifadhi ya Mazingira. Nataka kwanza nimpongeze kwa dhati Mwenyekiti wa *NEMC*, Ndugu Rerginal Mengi. Ndugu Mengi nampongeza kwa sababu amejitahidi sana kwa kipindi kirefu. Mimi nilimfahamu wakati bado ni Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro mwaka 1984, alipoanza kutoa fedha na zawadi kwa vikundi vinavyootesha miti. Lakini pia aliendelea kusimamia ya kwamba hata miti michache inapoota atakupa zawadi kwa kuitunza miti kidogo uliyokuwa nayo. Ametumia maelfu na mamilioni ya fedha kutoa zawadi ili angalau kuiendeleza hifadhi ya misitu. Naelewa ya kwamba hapa katikati kulikuwa na matatizo ambayo yalikuwa ni ya kutaka kuwakatisha baadhi ya watu tamaa kwa sababu kulikuwa hakuna chombo ambacho kilikuwa kinaweza kudhibiti na kusimamia hayo yanayoamuliwa na *NEMC* na tulikuwa na matatizo ya Kisheria, hata maamuzi yalikuwa wakati mwingine ni ya kisiasa zaidi badala ya kuwa ya Kisheria. Sasa tunaomba chombo hicho kwa kweli kipewe madaraka na sisi kama Waheshimiwa Wabunge, tunaweza kuwapa madaraka ili angalau waisimamie vizuri kazi yao ya kuendeleza hifadhi ya mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwana-mazingira *number one,* ambaye ninamfahamu, ni Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere. Namwita mwana-mazingira *number one* kwa sababu yeye alikuwa akifanya kazi zake kwa vitendo. Ukiangalia Kijiji chake cha Butiama, alihakikisha ya kwamba, anahifadhi mazingira na kuhakikisha ya kwamba Kijiji hicho kinakuwa ni mfano wa Vijiji vingine katika suala zima la upandaji wa miti na kuhifadhi maliasili iliyopo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia pale Chamwino, nimeona Chamwino imeendelea katika utaratibu huo huo na wote ambao mmefika Chamwino mmeona hata nyumba zilizojengwa, alihakikisha hakuondoa jiwe hata moja. Ukiangalia katika vyumba na pia katika Ofisi wewe unapishana na mawe mle ndani. Ukienda sasa Butiama ndiyo zaidi. Chumba cha Baba wa Taifa ni lazima upite kwenye jiwe ndiyo ufike kwenye chumba chake. Alihakikisha ya kwamba, kila kitu ambacho Mwenyezi Mungu, amekiacha, alikijengea utaratibu ya kwamba kinabaki kama kilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuanzia hapo mimi ombi langu ambalo nimeliona sasa baada ya Baba wa Taifa kufariki, ni jitihada gani tumeiendeleza katika kumuenzi ili kazi aliyokuwa anaifanya pale Butiama iendelezwe na sisi wenyewe? Napenda nitumie hii nafasi kuiomba Wizara kupitia *NEMC* kama inawezekana, waone namna ya kuendeleza jitihada za Baba wa Taifa katika Kijiji cha Butiama ili angalau hifadhi ya mazingira iweze kuendelea katika misingi ambayo alikuwa ameianza Baba wa Taifa. Tutakuwa tumempa heshima kubwa sana na utakuwa ni mwanzo wa kuyaenzi yale ambayo alikuwa ameyaanzisha Baba wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie kidogo suala zima la Muungano. Kwanza, napenda kuzipongeza Serikali zote mbili kwa kuendeleza na kudumisha Muungano tulionao. Napenda kuzipongeza kwa sababu suala la Muungano si jambo dogo, ni zito. Tarehe 23 Juni, 2003, kama mnakumbuka wakati nachangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilisema hivi ninanukuu: "Sikufurahishwa na matokeo ya uchaguzi wa Pemba na nikasema hali hii ni hatari kwa Muungano wetu". Wengi hata baadhi ya vyombo vya habari havikunielewa kwa nini? Walisema sikufurahishwa kwa sababu CCM haikushinda au sikufurahishwa kwa sababu kura zilizotolewa zilikuwa ndogo sana za CCM ukilinganisha na wengine? Hapana mimi nilikuwa na sababu zangu nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ilikuwa maana yangu kwanza, lazima tuelewe binadamu wakati wote kila siku hujifunza kutoka kwa mwenzake. Hilo la kwanza. Pili, ulimwengu wa sasa ambao umegeuka umekuwa kama Kijiji. Unafanya mambo mengi sana ambapo usipoangalia unaweza ukajifunza mabaya badala ya kujifunza mema. Ni nani kati yetu ambaye alijua siku moja binadamu atakuwa na tabia ya kinyama ya kumchoma mwenzake hadharani tena mbele za watoto. Ni nani aliyejua ya kwamba katika maisha yetu ipo siku moja tutakuwa tunachunana ngozi, ni nani aliyejua katika maisha yetu ya kwamba wanaume kwa wanaume watakuja kuoana na kufunga ndoa na pia ni nani aliyejua katika maisha yetu ya

kwamba mtu na umri wake na heshima yake atambaka mtoto mchanga wa mwezi mmoja? Haya wakati mwingine yanatokea kwa sababu binadamu anasema nimesikia limetokea mahali fulani, wengine wanajaribu.

Hili nalisema kwa sababu baadhi ya mambo yanayotokea katika ulimwengu wa sasa, mimi nadhani hata kama shetani yupo anashangaa, kama shetani yupo anashangaa, si mambo ya kufurahia hata kidogo. Nami ningependa niseme yafuatayo: *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichonitisha katika uchaguzi huo na kilichojitokeza wakati huo ni kwamba, kulikuwa na zile kura zilizokuwa zinaitwa kura za maruhani. Kura za maruhani tunaita ni kura hewa, ni kura za chuki. Kura za chuki ukiziangalia siyo za kupuuzia, leo kwako kesho kwa mwenzako. Hatutaki Watanzania wakaanza kuiga ya kwamba kumbe inawezekana nikafanya hivyo kwa sababu tabia ya Mtanzania au mtu yeyote kuiga kwa wengine. Hivi kwa nini yanatokea hayo? Hivi hali kweli ni mbaya kiasi hicho? Mimi kwa dhati nataka kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kazi nzuri alizozifanya kwa kipindi cha miaka miwili na nusu. Pamoja na hali ngumu ya uchumi, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, amejitahidi, binadamu kwa miaka miwili na nusu hutegemei akafanya maajabu hata kidogo, hutegemei atafanya maajabu, lazima tumsaidie ili aweze kufanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikasema suala hili la Muungano tusilichukulie kama mzaha na hatuwezi kulizungumza kwa dakika 15 hapa kwa kila mmoja, unahitajika muda wa kutosha. Twende kwa undani na kama inawezakana tufanye semina Waheshimiwa Wabunge peke yetu ikiwezekana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Hiyo itatusaidia kufanya mambo mengi. Kwanza, tutaona ya kwamba ukweli uko wapi na pia tatizo liko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara yangu ya kwanza kwenda Pemba ilikuwa ni mwaka 1972, nilikwenda kama kijana wa *volunteer,* kwa wakati huo nikitokea Makao Makuu ya Chama. Pemba niliyoiona hiyo na hivi sasa naona imebadilika ingawa mabadiliko ni kidogo sana, hivi tatizo liko wapi? Tunaanzia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka kuwaambieni kwamba, yako mambo ambayo mimi nasema sikuridhika kwa sababu katika hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Ali Said Juma katika ukurasa wake wa nne, Ibara ya 12.9 inasema yafuatayo na hiyo nazungumzia suala zima la umuhimu wa kujenga umoja miongoni mwetu anasema: "Ili kujenga demokrasia ya kweli inayotawaliwa na ushindani wa haki, Sheria halali zinazokubaliwa na washindani wote, *referee* anayeaminika na mwenye uwezo unaokubalika na uwanja wenye vipimo sahihi vya mchezo husika, demokrasi ya kiini macho haiisaidii Taifa na kichocheo cha umaskini". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nini? Katika Kitabu cha Muafaka katika ukurasa wa pili, Ibara ya kwanza, kifungu kidogo cha (i) kinasema hivi: "Vyama vya Siasa viheshimu Katiba na Sheria za nchi na kuepuka kutumia lugha zinazochochea chuki baina ya vyama vya siasa, ukabila, uhasama na kutovumiliana". Kura za chuki ni dalili ya kutovumiliana, maruhani ni dalili hiyo ya kwamba hatujengi Muafaka na hatukubaliani kwa sababu na sisi tunaanza kuvunja Muafaka. Yaliyomo ndani ya Muafaka kama tungeyazingatia, tusingekuwa na matatizo yoyote. Kuna haja ya kwenda kwa undani ili kujua tatizo liko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niombe mambo mawili. Kwanza, tufanye mpango wa kuangalia kwamba hivi tunapozungumzia tatizo la wenzetu wa Zanzibar, ni la kisiasa au la kiuchumi? Wakati mwingine tunaweza kudhani ni mambo ya kisiasa peke yake lakini kiuchumi lazima tuliangalie kwa undani zaidi. Hivi tatizo liko wapi kama tunakaa na kusema ya kwamba sasa katika Muungano wetu kiuchumi Zanzibar tunataka mfanye yafuatayo kwa makusudi mazima, mnapeana kabisa majukumu, mnafanya kwa niaba ya wenzenu, maana yake ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini katika Kamati yetu ambayo inaongozwa na Mheshimiwa William H. Shellukindo, tusije siku moja tukakaa na kuzungumzia yale ya undani, Mheshimiwa Rais, akaruhusu ya kwamba, tuzungumze mapendekezo yamekuja haya, mnasema nini Waheshimiwa Wabunge? Ingetusaidia sana kupunguza haya matatizo yaliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nisingependa tuanze katika kikao hiki kusema mafuta yakipatikana ni ya Zanzibar peke yake, tunavunja Muungano katika utaratibu huu, tukae tuyazungumze wote kwa pamoja halafu tuamue nini cha kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Warumi walipokuwa wanatawala miaka 2000 kabla ya Kristo walisema hivi, *"Melius desiderlium suirelinguere quam nausean creare"*. Tafsiri yake ya Kiswahili ni rahisi sana ya kwamba "waliochokwa katika maisha ni chanzo cha vurugu na au hutoa hongo za aina mbalimbali ili wawe mbadala wa sifa marehemu".

Mbadala wa sifa marehemu, unajua unapoitwa marehemu wanakupa sifa nyingi lakini marehemu ni marehemu hata wakikupa sifa hakuna kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hilo kwa sababu tusije tukafikia mahala fulani tukazungumza kitu ambacho hakitajibu haya matarajio yetu, tunataka tujenge umoja na mshikamano lakini pia tujione ni Taifa moja.

Kama kuna matatizo tukae tuyazungumze na hatuwezi kuzungumza tena kwa haraka haraka namna hii na ndiyo maana nilikuwa napendekeza ya kwamba, kama itawezekana tuje tuwe na kikao kikubwa tena semina ya pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kuiunga mkono hotuba ya Makamu wa Rais mia kwa mia.

Jambo langu la pili, naomba kuwapongeza Mawaziri wetu wote wawili, pamoja na Watalaamu na Watendaji wote katika Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuchangia suala la *TASAF*. Kwanza, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais Mkapa, kwa juhudi zake za kutupatia mradi huu ambao kweli ni mkombozi wa wanyonge na umaskini. Hatua nzuri imepigwa katika kuleta maendeleo ya kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jimbo langu la Bumbwini, Jimbo zima nimepata mradi mmoja tu nao ni jengo la Zahanati. Ninaomba sana nisaidiwe kuongezewa mradi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa ya kuondoa umaskini, lakini bado kuna haja kubwa ya kupambana na umaskini huo. Naomba sana tunyanyue vikundi vya washirika katika kuwasaidia kilimo cha maendeleo ya kileo kwa kuwasaidia vifaa vya kileo, kama utaalamu wa aina mbalimbali na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuvisaidie vikundi vya vijana wetu katika kuitumia Bahari na Maziwa Makuu yetu katika uvuvi wa kileo, hasa katika utaalamu, vifaa vya kileo na masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazipongeza Serikali zetu zote mbili katika juhudi za kuondoa kero hizi za Muungano. Ninaomba juhudi hizo ziendelezwe kwa juhudi kubwa ili tufanikishe kuondoa kabisa kero hizo, hasa katika wakati huu wa mvutano wa siasa ya Vyama Vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa kubwa ya kudumisha Muungano wetu ni mshikamano wetu wa kweli na kuhakikisha kwamba, Sera ya Chama na ahadi zake lazima zitekelezwe ipasavyo, tuhakikishe kwamba, kero zote za Muungano tumeziondoa kidhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia mchango wangu huu mdogo kwa kurejea kusema tena kwamba, ninaunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kazi nzuri na hotuba safi. Nawapongeza pia wasaidizi wao.

Nianze kwa kutoa pole kwa majukumu mazito iliyopewa Ofisi ya Rais, yakiwemo usimamizi wa shughuli za Muungano, hifadhi ya mazingira na vita dhidi ya umaskini. Ni kwa sababu ya unyeti na upana wa majukumu hayo kuwa Mheshimiwa Rais, ameamua kuyaweka majukumu hayo katika ngazi ya juu ya utawala na kuteua Mawaziri wawili wa nchi ili yasimamiwe kwa makini.

Napenda nichangie katika maeneo mawili tu ya mazingira na vita dhidi ya umaskini.

Nakubaliana na Kamati ya Kudumu ya Mazingira na Maliasili kuwa haitoshi kutafsiri mazingira kuwa ni kukata miti au kuchoma moto tu, wala si usafi wa maeneo. Ni suala pana sana linalohusu uhai. Kwa hiyo, tuyatazame mazingira katika nyanja mbili.

(a) Mazingira yanayoonekana *(Tangible or Physical Environment),* mifano ni pamoja na ardhi, mabonde, milima, misitu, miundombinu na kadhalika.

(b) Mazingira yasiyoonekana *(Non-physical or Intangible Environment).* Mifano ni pamoja na mila na desturi, imani, tabia, mienendo ya jamii na kadhalika.

Kwa hiyo, kwa madhumuni ya kulinda hali za watu wake na kuleta maendeleo, hapana budi tuzingatie sura au nyanja zote hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili vita dhidi ya umaskini ifanikiwe hapa kwetu, Serikali hasa Ofisi ya Makamu wa Rais, haina budi kujiweka mstari wa mbele katika kufanya yafuatayo:-

(i) Kuboresha maeneo kwa kujenga miundombinu ikiwemo upatikanaji wa barabara zinazopitika wakati wote hasa Vijijini, maji safi na salama wakati wote, umeme wa kuaminika wenye gharama nafuu kwa watumiaji, mawasiliano ya simu, barua na redio na kadhalika;

(ii) Kuweka sheria na kuzisimamia dhidi ya uharibifu wa mazingira; na

(iii) Kuwezesha wananchi kuanzisha na kuendeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kusimamia mazingira ya aina hii ni ya kila mmoja wetu katika jamii, ingawa Serikali inao wajibu wa ziada kwa maana ya kuweka na kusimamia sheria dhidi ya desturi na mienendo isiyoridhisha inapobidi kufanya hivyo. Jamii nzima inawajibika kufanya yafuatayo:-

(i) Ili tupate maendeleo hapana budi watu wote, kila mmoja kwa nafasi yake, afanye kazi ya kuzalisha bidhaa au huduma. Tuipige vita tabia ya baadhi ya watu katika jamii kukaa bure na kutegemea wengine. Ni wazee, watoto wadogo, wagonjwa na watu wenye uelemavu mkubwa tu ndio wabaki kuhudumiwa;

(ii) Ziandaliwe shughuli za kufanywa na walemavu ili na wao wachangie katika uzalishaji. Lakini Serikali ilete Bungeni sera ya sheria zinazoelekeza namna ya kuwasaidia walemavu;

(iii) Tuachane na tabia iliyojengeka nchini ya kila mmoja wetu kupendelea kufanya biashara badala ya kuweka uzito kwenye kuzalisha. Tabia hii imechangia katika ukame wa upatikanaji wa baadhi ya bidhaa na huduma. Pia imechangia katika kupandisha bei za vitu kwa kuwa katika kila ngazi ya uuzaji, wafanyabiashara wanaweka bei zinazozingatia manunuzi, huduma zao na faida; na

(iv) Tuachane na tabia ya kuchagua kazi na shughuli za kufanya. Watanzania wengi leo hawapendi kufanya shughuli za kilimo, ufugaji, uvuvi na shughuli zote zinazoandamana na uchafu. Hata wenye kisomo cha chini, wanapendelea kufanya kazi laini za maofisini. Ni bora tujenge tabia ya kugawanyika katika makundi mbalimbali ya uzalishaji.

Vita yetu dhidi ya umaskini haitaweza kufaulu iwapo hatutachukua hatua za dhati kupambana na maradhi hatari ya Ukimwi na Malaria. Wananchi tubadili tabia zetu ili kuzuia kusambaa kwa viluilui vya Ukimwi. Wanaoambukizwa kwa bahati mbaya au kwa vyovyote vile, wapatiwe huduma za kuzuia uenezaji zaidi, kurefusha maisha yao na matunzo mazuri ili wasikate tamaa na waendelee kutoa nguvukazi. Tupambane na ugonjwa wa Malaria kwanza kwa kuzuia ueneaji wake kwa kutumia vyandarua vyenye madawa, kuteketeza mazalio ya mbu wanaoeneza viluilui vya Malaria. Tuwapatie chanjo za kinga watoto wetu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo majukumu mengi lakini hapa nitataja machache.

(a) Serikali iboreshe miundombinu ya usafiri, maji, mawasiliano. Wananchi wako tayari kujikwamua, lakini walio wengi wanakwamishwa na miundombinu mibovu. Kwa mfano, katika Wilaya yangu ya Kisarawe baadhi ya barabara za Vijijini ni mbovu na hasa nyakati za mvua hazipitiki, hakuna simu isipokuwa katika Makao Makuu ya Wilaya, kuna tatizo la maji Kisarawe Mjini na Vijijini, hakuna umeme Vijijini, hivyo sehemu kubwa ya nguvukazi inapotea katika kutumia muda mwingi hasa wa akina mama katika kutafuta maji na kuni.

Kwa kuwa umeme haupatikani na katika maeneo unakopatikana haununuliki kwa sababu ya bei kuwa juu, misitu ya Wilaya ya Kisarawe sasa inakwisha kwa kutengenezwa kuni na mkaa. Wilaya inageuzwa kuwa jangwa sasa. Serikali haina budi ichukue hatua za haraka kuhakikisha kuwa maji yanapatikana kwa urahisi huko Vijijini, barabara zinapatikana, mawasiliano yanaboreshwa na nishati inapatikana.

(b) Kwa bahati nzuri nchi yetu inapata misaada mingi kutoka kwa Wahisani wa nje kupitia Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali *(Non Governmental Organizations).* Ingawa baadhi yao yanafanya kazi nzuri, yapo mengine ya Mitaani ambayo hata shughuli zao hazieleweki. Kwa mfano, katika vita dhidi ya Ukimwi, *TACAIDS* inaeleza kuwa *NGOs* zimepokea mwaka uliopita, misaada ya Shilingi bilioni 16. Lakini kwa bahati mbaya hakuna anayejua fedha hizo zimeishia wapi na manufaa yake yakoje.

Kwa hiyo, nashauri kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais, itekeleze Sheria mpya ya *NGOs* kikamilifu, tena bila ya kuchelewa ili Mashirika ambayo hayatafuata sheria yazuiliwe kufanya kazi na yatakayobakia shughuli zao ziratibiwe kikamilifu.
Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuwapongeza na naiunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeanzishwa chini ya ibara ya 47 ya Katiba ya Nchi na Muungano ikiwa ni sehemu kuu ya majukumu ya Ofisi hii. Lakini cha kushangaza jina la Kamati inayohusika na Ofisi hii, neno Muungano halikuzingatiwa. Hivyo, nashauri liingizwe neno Muungano ili jina likidhi masharti ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sijaona chochote kuhusu maendeleo ya Muungano wetu kiuchumi. Zaidi kilichoelezwa ni mahusiano ya kimichezo, kisiasa, kiutamaduni, Sherehe za Mapinduzi, Sherehe za Uhuru na Sherehe za Muungano. Sasa Ofisi hii ibadilike ionekane ushiriki wake katika mambo ya kiuchumi ikiwemo maendeleo ya elimu, mikopo na misaada ya nje, pamoja na maeneo mengine ya kiuchumi. Hapo ndipo maana halisi na umuhimu wa Muungano utaonekana na kutetewa na kila Mtanzania.

Katika hotuba hii Mheshimiwa Waziri, ameeleza mafanikio kama ujenzi wa Ofisi ya Bunge, Mradi wa *TASAF,* Kamati ya Fedha ya pamoja, mgao wa fedha za misaada ya asilimia 4.5. Hata hivyo, mafanikio haya yote hayatekelezwi wala kusimamiwa na Ofisi hii, lakini kwa vile ameyataja katika hotuba yake, ni vyema akatusaidia ufafanuzi na mwelekeo wa ujenzi wa Ofisi ya *BoT,* Chuo cha Sayansi ya Bahari, Ofisi za Wabunge na kadhalika.

Wakati Mawaziri wa Serikali ya Muungano, kwa zile Taasisi ambazo sio za Muungano wanapotoka nje ya nchi huomba misaada kwa jina la Tanzania na sio Tanzania Bara, lakini manufaa ya maombi hayo huishia Tanzania Bara tu. Aidha, Mawaziri hao hao hufanya kazi hata zile za Kimuungano kama kuiwakilisha Tanzania katika Vikao mbalimbali vya Kimataifa, kusaini Mikataba na kuridhia Mikataba kwa niaba ya Tanzania. Ili kuondoa tatizo hii ni vyema katika mazungumzo yote na *donors, partners,* Mawaziri wa Serikali zote mbili, wakawa pamoja iwe ndani au nje ya nchi. Hatua hii itaondoa utata huu ambao ni kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi hii haina uwiano wa Kimuungano. Watumishi katika ngazi za Uongozi ambao ni Wazanzibari ni wawili tu, mmoja yupo Zanzibar na wa pili yupo Dar es Salaam. Ofisi hii haionyeshi sura kamili ya Kimuungano. Hivyo, ni vyema tatizo hili likapatiwa ufumbuzi wa haraka ili nalo lisiwe kero kama yalivyo hayo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya Wizara ya Fedha kutambua magari ya watu binafsi kuwa sawa na ya wageni wasiokuwa Watanzania ni ukiukwaji wa Katiba na kuua maana halisi ya uraia wa Tanzania. Haiwezekani kuwa mwananchi kumtambua kuwa raia lakini mali yake ni ya kigeni. Tatizo hili litaibua hisia mbaya kwani magari yanayotoka Tanzania Bara yanapokwenda Zanzibar yanatumia nafasi yake ya Utanzania ndani ya Tanzania. Hivyo, kwa kuwa lipo tatizo kwa magari yanayotoka Zanzibar kuja Tanzania Bara yanapata usumbufu, nashauri Serikali ilione hili na ilipatie ufumbuzi.

Kuhusu utungaji wa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baadhi ya Mawaziri katika Bunge hili wamewahi kusema kuwa katika kushirikisha Zanzibar Wizara hizo huwasiliana na Ofisi ya Makamu wa Rais, ambapo Ofisi hiyo huwasiliana na Wizara husika na SMZ kuhusu Muswada huo. Hata hivyo, pia ipo Wizara ambayo ililieleza Bunge hili kuwa ilifanya mawasiliano ya moja kwa moja na Mheshimiwa Waziri Kiongozi. Sasa ni vyema Mheshimiwa Waziri, akatufafanulia jukumu la Ofisi hii katika Miswada ya Serikali kwa ile inayohusu Tanzania kwa jumla. Aidha, kwa nini ushirikiano huu usianzie tokea hatua za matayarisho ya *draft* ili kila upande uweze kuweka *input* zake hatimaye tuwe na sheria yenye maslahi kwa pande zote mbili?

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaelekea kupata fursa ya kuongea imekuwa kitu adimu sana. Niliomba kuongeza jana kwenye hoja ya Maliasili nikawa wa 20, sikupata nafasi. Leo tena nikawa wa 20, sikupata nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii niandike sehemu ya mawazo yangu. Wenzetu katika Ofisi ya Makamu wa Rais, wamefanya kazi nzuri sana katika Sekta zote walizo na dhamana ya kuzihudumia. Hivyo, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Waziri wa Nchi, Mazingira na Muungano, Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, pamoja na Mr. Raphael Mollel na Watalamu Wakuu wa Wizara kwa hotuba na kazi nzuri sana. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nakushukuru wewe binafsi kwa kuituma Kamati ya Mazingira, Maliasili na Kuondoa Umaskini, kulitembelea Ziwa Jipe na Bwawa la Nyumba ya Mungu, kuona matatizo yanayowakabili wananchi wa Mwanga. Shukrani zangu hazitakuwa kamili bila kumshukuru Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kutembelea Mwanga mara mbili, kwanza kwa mwaliko wa Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye na mimi, halafu akifuatana na Kamati ya Bunge. Ahsante sana. Nawashukuru Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mazingira na Maliasili na Wabunge wote wa Kamati hii ya Bunge, kwa kutembelea Ziwa Jipe na Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari hii ya Kamati imeliweka tatizo la Ziwa Jipe na Bwawa la Nyumba ya Mungu katika moja ya matatizo muhimu ya Taifa na kwa sababu hiyo hotuba ya Ofisi ya Waziri wa Nchi, imeeleza kuwa sasa tatizo hili litatatuliwa. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nimshukuru sana Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mbunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa kuongoza timu ya Wabunge wa Afrika Mashariki

kutembelea Ziwa Jipe na Bwawa la Nyumba ya Mungu na kuliweka tatizo hili kama tatizo la Afrika Mashariki yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Wana-Mwanga wote, tunaomba kazi ya kupambana na magugu ya Ziwa Jipe na Nyumba ya Mungu ianze mapema iwezekanavyo na iwashirikishe wananchi. Ahsante sana.

**MHE. SHAIBU AHMADA AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na wenzangu kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, sina budi kuwapongeza Mawaziri, Mheshimiwa Arcado D. Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar D. Maokoloa-Majogo, kwa hotuba yao nzuri waliyoiwasilisha Bungeni hii leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua nafasi hii kuwapongeza Makatibu Wakuu wa Wizara hizi. Mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati hii ya Maliasili, Mazingira na Kuondoa Umaskini, wakati tulipotembelea sehemu mbalimbali tulijionea wenyewe hali halisi vipi mazingira yalivyoharibika na hali ya umasikini ilivyo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tulipotembelea Ziwa Jipe tuliliona linakabiliwa na tatizo kubwa la magugumaji aina ya *Ciyperus, Papyrus* na *Typha Domingensis*. Magugu hayo yameathiri kiasi kikubwa mazingira ya eneo hilo na kukwamisha shughuli za kiuchumi na kijamii za Wakazi wa Vijiji vinavyozunguka Ziwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ya Ziwa Jipe pia huingia kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu, ambalo ni raslimali muhimu kwa utoaji umeme, uvuvi wa samaki na huduma za maji kwa wakazi wa maeneo hayo na mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matatizo hayo, Ziwa Jipe sasa shughuli zote za uvuvi hakuna kutokana na ongezeko la magugumaji. Pia magugu ya Ziwa Jipe huenda yakaambukiza na kuota magugumaji katika Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi sana baada ya Bajeti ya mwaka huu 2003/2004, kwa kutenga kima cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais huko Zanzibar. Kitendo cha kujenga Ofisi hiyo kitapunguza maneno ya bughudha na majungu ya watu wanaoutazama Muungano wetu kwa jicho la husuda. Sasa watasema kwa mengine, lakini sio Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kitendo cha uteuzi wa Tume itakayoshughulikia gawio la asilimia 4.5 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na faida ya Benki ya *BoT* inavyotolewa kwa Serikali ya Muungano, kitathibitisha wazi kwamba sasa SMT inashughulikia kero ya Muungano kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu unazidi kuimarika kila siku zikienda na wananchi wote wa nchi hizi zetu mbili wanaridhika kabisa. Lakini panapotokea kasoro ambayo ikiachiliwa huenda ikasababisha kero kuwa upande mwingine wa Muungano, isiachiwe. Maana kasoro hizo zikiachiwa huenda zikatia dosari wakati ambapo dosari ile ingeweza kuzuilika. Kitendo cha kukatiwa umeme Zanzibar, kingeweza kuzuilika kama vingozi wangetumia busara. Lakini sasa tumewapa mwanya wa kusema Wapinzani wetu na wasioutakia mema Muungano wetu. Nashauri wadhamini wa vyombo vyote vinavyotumika kwa matumizi ya pamoja, maamuzi yake yatoke ngazi ya juu ya Uongozi na sio Meneja au Mkurugenzi. Itolewe ilani kwa Watendaji wote wasitoe maamuzi kwa mambo ya Muungano mpaka Uongozi wa ngazi za juu wa Chama au Serikali. Kwa kufanya hivyo, Serikali zetu hazitaingia katika malalamiko kama haya ya kukatiwa umeme Zanzibar. Kwa kumaliza, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Wizara hii kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Jipe ni Ziwa ambalo wananchi walikuwa wakilitegemea sana kwa kujipatia mahitaji yao ya kila siku kwa shughuli walizokuwa wakizifanya za uvuvi. Ziwa hili limeota magugumu lote na kubakia sehemu ndogo tu. Pia Ziwa hili limepakana na Ziwa la Kenya na mvuvi wetu anapopelekwa na upepo akafika Kenya hupata adhabu na hawa huwa hawarudi tena Kijijini pale na wanakijiji wanapoteza watu wengi kwa kwenda kwenye uvuvi na hawarudi nyumbani tena na hawajulikiani walipo. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ilifuatilie suala hili kwa undani ili ilipatie ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni kupoteza Ziwa hili ni uchangiaji wa umaskini kwa wananchi wa Vijiji vinavyotegemea Ziwa hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Nyumba ya Mungu nalo limeshaanza kuota magugumaji na wavuvi wetu wanalitegemea sana, nalo linaanza kutoa magugu na Serikali inaangalia tu. Inasemekana kuna mazungumzo tu na wala hatuoni utekelezaji wake. Kweli Serikali inataka kuondoa umaskini kwa wananchi wake, kama itawaondolea magugumaji wananchi wa eneo hilo, wataweza kuondoa umasikini na mazingira mazuri.

Suala la Zanzibar kukatiwa umeme si suala zuri kwani Zanzibar ni nchi ambayo ina mambo mengi ambayo yakikosa umeme yanaharibika na wananchi wanapata hasara kubwa na uharibifu wa vifaa vinavyotumia umeme na kusababisha umaskini wa ghafla kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupambana na umaskini, tufanye juhudi za kuondoa umaskini kwa kutumia teknolojia ya kisasa ambayo itasaidia kuendeleza hifadhi ya mazingira pamoja na kuleta maendeleo *(Sustainable Development).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi tajiri sasa hivi zina tatizo la *unsustainable consumption,* hivyo, ni vyema zikabadili tabia zao ili matumizi yao yawe ni *sustainable consumption*. Hakuna haki katika biashara hivi sasa kutokana na mfumo mpya wa uchumi duniani *(globalization)*. Hivyo, ni muhimu kuzingatia matatizo ya nchi maskini kama Tanzania kwa kuwa ni vigumu kuwa nchi hizo kushindana na nchi zilizoendelea kama Marekani. *Globalization* haileti haki kwa sababu hatuwezi kupambanisha makundi ya nchi ambazo hazilingani kiuwezo na kiuchumi.

- Ili kufuta umaskini, ni muhimu sana kusomesha watoto wote, hasa wa kike angalau kiwango cha Darasa la Saba. Kwa njia hii, Tanzania itatokomeza umaskini na kuleta maendeleo.

- Nchi tajiri zinazungumzia zaidi na kukazania hifadhi ya mazingira.

- Nchi maskini zinazungumzia na kukazania kuleta maendeleo, yaani kupiga vita umaskini.

- Serikali iingilie kati na kutetea maeneo muhimu ambayo mfumo wa uchumi duniani wa soko huria unashindwa kulinda usawa *(equity)* katika jamii kati ya matajiri na masikini.

- Ili kuondoa umaskini, ni muhimu kuongeza ajira, pato na lishe bora ili kuboresha huduma za afya na kuimarisha huduma za mgao wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wachimbaji madini (Makampuni) hawaangalii suala la hifadhi ya mazingira, wanazingatia zaidi suala la uchimbaji madini licha ya kuwa na kasma ya kuhifadhi mazingira. Jambo hili linasababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Ofisi ya Makamu wa Rais, itembelee sehemu zote zenye machimbo ya madini ili kuona kama uchimbaji wa madini unakwenda sambamba na hifadhi ya mazingira.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Aidha, ninaomba kuwapongeza Mawaziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Ofisi hii kwa kazi nzuri waliyoifanya mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja hii, ninaomba Wizara izingatie yafuatayo:-

Moja, hatua za makusudi za kupambana na umaskini katika Mikoa kadhaa, hususan Mkoa wa Kigoma. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali ambazo imezichukua kupambana na umaskini hasa katika nyanja za afya, elimu na mawasiliano, bado zinatakiwa kuchukuliwa hatua za makusudi kupambana na umaskini uliokithiri katika Mikoa ya Kigoma, Rukwa, Tabora, Singida, Lindi na Mtwara. Mkoa wa Kigoma una ardhi ya rutuba na mvua za kutosha na hivyo hali ya uzalishaji kilimo siyo mbaya sana ingawa ingeweza kuongezeka mara kadhaa.

Tatizo kubwa Mkoani humo ni ukosefu wa miundombinu yaani barabara za uhakika kiasi kwamba mazao yazalishwayo Mkoani humu hayawezi kusafirishwa kwenda kwenye maeneo yenye masoko. Aidha, ukosefu wa umeme katika Mkoa huu unasababisha mazao yauzwe bila kusindikwa na hivyo kupata bei ndogo. Ni ukweli usiopingika kwamba, maendeleo hayawezi kupatikana kama miundombinu ni duni. Serikali inatakiwa leo ichukue hatua za makusudi na za upendeleo kuhakikisha Mikoa niliyoitaja na hasa Mkoa wa Kigoma, unapata miundombinu ya uhakika kama kweli tunataka kupambana na umaskini uliokithiri, vinginevyo ni ndoto ya mchana.

Pili, hatua za muda mfupi za kupambana na umaskini, Serikali iendelee kuhamasisha uanzishwaji wa mifuko mbalimbali kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wananchi na hasa wale wa Vijijini. Mashirika binafsi kama *PRIDE* na *FINCA* yanatoa mikopo kwa watu waishio Mijini tu na kuwaacha wanavijiji bila msaada. Aidha, kwa sababu Halmashauri zetu hazina uwezo, mikopo kwa vikundi vya akinamama na vijana ni michache na midogo na hivyo umaskini unaendelea. Tatu, utunzaji wa mazingira. Serikali iendeleze juhudi zake za kusambaza elimu kuhusu utunzaji wa mazingira Mijini na Vijijini na kuhimiza upandaji wa miti ili nchi yetu iepukane na janga la ukame. Elimu hii isambazwe kuanzia kwenye Shule za Msingi na iwashirikishe wananchi katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. MCHANDE SALIM MCHANDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kuchangia suala la udhibiti wa mazingira ya baharini. Kumekuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira katika sehemu zetu za Pwani. Uharibifu huo ni pamoja na uvuvi haramu wa kutumia baruti ya kuvunja mwamba, ambayo ni makalio ya samaki. Pia husababisha kuvunja matumbawe ambayo ni mazalio ya samaki. Pia kumekuwa na ukataji wa miti aina ya mkoko ovyo ovyo. Mambo yote haya husababisha uchafuzi wa mazingira ya baharini pamoja na fukwe zetu. Nashauri Serikali kupitia Wizara husika, kuimarisha ulinzi katika maeneo ya bahari zetu ili kudhibiti uharibifu huo. Aidha, Wizara iandae mikutano, semina pamoja na warsha, kwa wananchi wote ili kutoa taaluma inayohusu uhifadhi bora wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatiliaji wa lengo la kuondoa umaskini, ushirikishe Wabunge na Madiwani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utupaji wa taka za *plastic* sasa umekithiri hasa katika maeneo ya Mjini. Utupaji huo umekuwa ukihatarisha afya za binadamu. Nashauri kupitia Wizara husika, kudhibiti uagizaji holela wa mifuko ya *plastic*. Aidha, naunga mkono hotuba ya Waziri kwa kuongeza kodi katika bidhaa za mifuko ya *plastic*. Ni hatua muhimu itakayopunguza uingizaji holela wa mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naunga mkono hotuba ya Waziri kuhusu uelimishwaji wa wananchi kuhusu jitihada mbalimbali za kupambana na umaskini.

Mwisho nasema, kitendo walichokifanya *TANESCO* cha kukata umeme kwa Zanzibar ni kitendo kibaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Arcado D. Ntagazwa, Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Mazingira na Muungano na pia Waziri wa Nchi, Kuondoa Umaskini na Mashirika Yasiyo ya Serikali, Mheshimiwa Edgar D. Maokola-Majogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri Arcado Ntagazwa ni nzuri, imeainisha maeneo vizuri kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira na sheria za mazingira. Yapo matatizo ya kimsingi ambayo Wizara hii itatakiwa iyashughulikie kwa mfano uharibifu mkubwa wa idadi ya mifugo kama vile ng'ombe Wilaya ya Chunya na hasa Mkoani Mbeya kwa jumla. Suala hili limekuwa kero kwa wakulima wetu na hivyo kuleta ugomvi baina ya wakulima na wafugaji na hasa pale panapokosekana maji kwa matumizi ya wanyama na binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara hii iisaidie Wilaya ya Chunya kuipatia fedha za ziada toka Wizara hii ili zisaidie kujenga malambo na hivyo ng'ombe waende kule walikopangiwa na kuondokana na uharibifu wa mazingira katika maeneo ya mito na sehemu nyingine za makazi ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kero ya umaskini, vile vile Wizara iweke utaratibu mahususi kwa kwenda Wilayani na Vijijini ili kuelimisha wadau juu ya kuondoa umaskini na pia kutoa mikopo kwa walengwa kwa kushirikiana na Taasisi nyingine zenye kutoa mikopo kama vile *SIDO, NMB* na Benki ya Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado maeneo mengi ya Vijijini hayapati huduma za kutosha kuhusu mikopo, ndiyo maana yapo masikitiko kuwa Wizara hii haiondoi umaskini ingawa bado inafanya kazi kubwa tangu ianzishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kama nilivyoeleza mwanzo, Wizara hii ni muhimu kuwepo ili kusaidia kuondoa kero ya umaskini. Nimetoa maombi ya kupatiwa fedha za kusaidia wananchi katika uchimbaji wa malambo pamoja na kuwepo kwa Wizara ya Maji na nyingine, hii ni kwa sababu ya usumbufu wa muda mrefu wa uharibifu wa mazingira wakati wa malisho maeneo ya wakulima.

Kuhusu kuondoa umaskini, tunaomba mikopo midogo midogo ya wachimbaji wadogo wadogo wa madini ili waweze kununua mashine ndogo ndogo za *detectors*. Hili ni suala muhimu na litaondoa umaskini katika eneo zima la Jimbo la Songwe na Wilaya ya Chunya kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii.

Hata hivyo, ningependa kuchangia hoja hii katika eneo moja la umaskini mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inajulikana kwamba, ingawa umaskini katika Tanzania ni mkubwa zaidi vijijini, lakini kasi ya kukua kwa umaskini mijini ni kubwa zaidi kuliko kasi ya kukua kwa umaskini vijijini. Lakini la pili, inajulikana pia kwamba, miaka ishirini kuanzia sasa (2025), nusu ya Watanzania watakuwa wanaishi mijini.

Mheshimiwa mwenyekiti, mambo niliyotaja hapo juu yanafanya hali ya umaskini mijini kuleta changamoto kubwa sana kwa viongozi na Serikali yetu. Lakini kwa bahati mbaya sana, inaonekana kwamba, Serikali haijapata changamoto hii. Nasema hivyo kwa sababu, katika mipango ya Serikali ya kuondoa umaskini suala la kuondoa umaskini mijini halijawekewa kipaumbele na hasa hasa suala la uboreshaji wa makazi mijini.

Mheshimiwa mwenyekiti, hata mkakati wa *PSRP* haujagusia suala la kuboresha makazi mijini kama ni mkakati wa kuondoa umaskini mijini, huku tukijua kwamba, unapoboresha makazi na nyumba mijini utakuwa umewaondolea wakazi hawa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependekeza Serikali ifanye hima kurekebisha *PRSP* ili suala la kuboresha makazi na nyumba mijini liwe *mainstreamed,* waziwazi ndani ya mkakati huo na lianze kushughulikiwa kikamilifu kwenye mipango yetu kuanzia mwaka wa fedha 2004/2005. Kubwa zaidi mkakati uwekwe wa kutekeleza miradi wa *Regularization* wa makazi holela mijini ili wananchi hawa (asilimia 70 ya wakazi wote mijini) wapate hati ili ziwaondolee umaskini.

**MHE. SALIM OMAR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yake amesema ushirikiano kati ya Serikali zote mbili umezidi kukua na ni wa kuridhisha kuanzia ngazi ya Taifa hadi wananchi wa kawaida. Lengo ya mashirikiano hayo ni kuondoa umaskini nchini, warsha, semina na makongamano hufanyika kwa pamoja. Je, suala la kutafuta soko la zao la Karafuu lilizungumzwa ili kuwaboreshea wakulima wa zao hilo. Je, Shirika la *ZSTC* kujipangia bei zao hilo ambalo SMZ haipendi kulibinafsisha na Shirika hilo ndilo mnunuzi wa zao hilo, je limewahi kujadiliwa katika semina hizo na kupatiwa ufumbuzi wa aina yake?

Naomba Waziri anipatie majibu wakati wa majumuisho. Pia miezi mitano iliyopita SMZ ilizuia nazi za wakulima wa Unguja wasiuze nazi hizo nje ya Kisiwa cha Unguja na hasa kuuza nazi hizo katika Kisiwa cha Pemba, ambapo visiwa hivi vinatawaliwa na Rais mmoja. Je, hili pia nalo lilipata kujadiliwa na kupatiwa ufumbuzi? Naomba majibu.

Mheshimiwa mwenyekiti, naelewa jambo hili si la Muungano ila ni kuwa yapo mashirikiano kwa mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano, ndio nikataka majibu ya maswali hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano ni makubaliano ya nchi mbili tofauti nazo ni Serikali ya Zanzibar, ikiongozwa na Marehemu Abeid Amani Karume na Serikali ya Tanganyika, ikiongozwa na Marehemu Mwalimu Nyerere. Kwa nia njema hawa wote walichanganya mchanga wa nchi hizo mbili ili iwe Jamhuri ya Watu wa Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya Muungano yaliorodheshwa na yakawekewa sahihi ya makubaliano hayo lakini sasa mara baada ya kifo cha Marehemu Karume, mambo ya Muungano yaliongezwa bila ya ridhaa ya makubaliano ya Muungano huo. Hapo ndipo panatoa tafsiri ya kutokuaminiana katika maswali ya Muungano kwa kuhoji ni nani ambaye amepewa kibali cha kuongeza orodha ya maswali ya Muungano au kupunguza neno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza maswali ya Muungano yajadiliwe na yapate ufumbuzi wake kwa lengo la kuaminiana, tujue lipi ni la Muungano na lipi tufute au tuongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano uliopo ni tatizo kwa wananchi wa pande zote mbili, hawajui lao peke yao wala hawajui mali ya pamoja, Muungano ni tishio kama kimeta, lazima upatikane ufumbuzi. Ahsante.

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri wa Nchi, kwa hotuba nzuri. Aidha, ninawapongeza Mawaziri wote wawili wa Ofisi ya Makamu wa Rais, pamoja na wataalam wao kwa jinsi walivyotayarisha hotuba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja ya Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Ninachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mawaziri wa Nchi katika Ofisi yake na wataalam wao kwa jinsi wanavyoshughulikia mambo ya muungano. Aidha, ninaomba nichukue fursa hii, kulaani vitendo vya baadhi ya Viongozi wa Vyama vya Upinzani vyenye nia ya kuchochea uchafuzi wa hali ya kisiasa nchini, wananchi waliupokea Muafaka kati ya CCM na *CUF,* kwa furaha na matumaini makubwa. Amani na utulivu vilirudi Unguja na Pemba. Hii iliwezesha uchaguzi mdogo wa Wabunge na Wawakilishi kufanyika kwa amani na mafanikio makubwa huko Pemba.

Hata hivyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lililojitokeza wakati wa kampeni katika uchaguzi huo mdogo ni kauli na matendo ambayo yaliashiria Udini, Ubara, Upemba na Uunguja. Hali hii ikiendelea, kuna hatari ya kutokea machafuko makubwa. Kauli hizo zimekuwa na matokeo ya chuki dhidi ya Watanzania wanaotokea Pemba na wenye mali na wanaoishi Tanzania Bara.

Pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, chama cha *CUF* kimetangaza tafsiri isiyo sahihi ya Katiba ya Zanzibar na Muafaka wa CCM na *CUF* kuwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar anawajibika kuteua Wawakilishi kutoka Chama cha *CUF* na sio kutoka upande wa Upinzani kwa ujumla. Wamediriki hata kutoa tamko kuwa ikiwa hatafanya hivyo, basi atakuwa amevunja Muafaka na itakuwa zamu yake kukimbia Zanzibar! Kauli hizi za vitisho na uchochezi zinastahili kulaaniwa vikali na wananchi waelimishwe kuwa Katiba ya Zanzibar haiipi *CUF* haki ya kuhodhi siasa za Upinzani Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nitoe mawazo yangu juu ya taka za plastiki. Taka za plastiki zimekuwa kero kubwa sana hasa maeneo ya mijini. Taka hizi haziozi na bado hatujaweza kuwa na njia madhubuti ya kuziharibu. Kwa sasa ni chanzo kikubwa sana cha uharibifu wa mazingira, ninashauri ufumbuzi wa tatizo hili sio kupanua shughuli za kurudufu taka hizi, bali kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki na kusisitiza matumizi ya mifuko ya karatasi kama ilivyokuwa zamani.

Kuhusu hifadhi ya mazingira ya Pwani, ninaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC),* kwa juhudi zilizofanyika katika kuhifadhi Ukanda wa Pwani ya Dar es Salaam, hususan, maeneo ya mikoko katika Bonde la Msimbazi.

Hata hivyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mikoko inakatwa katika maeneo ya Kunduchi. Ninaomba hatua zichukuliwe kuzuia jambo hili. Pia, maeneo ya Kunduchi kuna shamba la chumvi ambalo limebadili kabisa tabia ya bahari sehemu hizo. Tuta la kuzuia maji lililojengwa limeathiri barabara iliyokuwa inapita katika mwambao wa bahari kwa kuifuta kabisa. Mikoko ambayo ilikuweko katika eneo hilo imeathirika sana na sehemu nyingine imetoweka. Iko taarifa kuwa mmiliki wa shamba hilo amepimiwa eneo hilo ili amilikishwe. Ninashauri shamba hilo liondolewe na sehemu hiyo isimilikishwe mtu yeyote.

Kwa hayo niliyoandika hapa juu, ninaunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii ili nitoe mchango wangu katika hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Makamu wa Rais na Mawaziri wote wawili bila kumsahau Katibu Mkuu, kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais, imefanya kazi nzuri sana na imejibu sehemu kubwa ya matatizo ya Watanzania. Hata kama si Wilaya zote, kwa sehemu kubwa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF),* ulikofanya kazi, jamii imepunguza kwa asilimia kubwa matatizo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Misungwi ni moja ya Wilaya tisa zilizoanzishwa 1997 hivyo ni dhahiri kuwa mapungufu mengi bado yanaikabili.

Wilaya ya Misungwi ina mapungufu mengi ikiwemo Hospitali ya Wilaya, Mahakama ya Wilaya na Makao Makuu ya Polisi. Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni baadhi tu ya matatizo yanayokwamisha maendeleo ya Wilaya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Serikali iweze kuona uwezekano wa kuitafutia Wafadhili Wilaya hii, vinginevyo itabaki nyuma, wananchi wa Wilaya hii kutokana na hamasa shirikishi waliyonayo kutokana na viongozi wilayani, wameweza kujenga shule tano za sekondari bila msaada kutoka kwa Wafadhili ukilinganisha na sehemu zingine. Wilaya hii ni vyema ikasaidiwa kwani mzigo ni mzito mno. Naiomba Serikali katika mpango wake wa awamu ya pili ya *TASAF,* Wilaya hii iwekwe na ni bora Wilaya zote zilizobaki zihusishwe, vinginevyo tutajenga tabaka la maskini zaidi na matajiri, kitu ambacho ni hatari kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maeleozo mazuri yaliyo katika hotuba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Nakushukuru.

**MHE. MWADINI ABASS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuhifadhi mazingira ni suala ambalo linagusa hisia za walimwengu walio wengi. Nchi nyingi duniani zimekuwa zinaandaa sera mbalimbali za uhifadhi wa mazingiza na matumizi bora ya raslimali, Tanzani ni miongoni mwa nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imezungukwa na bahari na takriban wananchi wengi wanaoishi kando ya bahari shughuli zao kuu za uchumi ni pamoja na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za uvuvi zinatofautiana kulingana na vifaa na zana zinazotumika, pamoja na maeneo ya bahari ambako wavuvi wanapenda kufanyia shughuli zao. Lakini kwa muda mrefu sasa kumekuwa na matatizo ya baadhi ya wavuvi kutoka sehemu moja kutoruhusiwa kuvua sehemu nyingine. Hali hii pamoja na sababu nyingine ni pamoja na wavuvi hao kutumia zana za uvuvi ambazo zinaharibu matumbawe na mazalia ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zana hizo ni pamoja na nyavu zenye macho madogo, juya, baruti, sumu na nyinginezo. Ninataka kujua Serikali imechukua hatua gani za ziada kuzidisha doria baharini ili kupunguza uvuvi haramu. Pili, nataka kujua ni kwa kiasi kipi Serikali imejitayarisha kuwapatia wavuvi zana za kisasa za uvuvi ili kuwaongezea kipato na kadhalika, kuhifadhi mazingira ya bahari na viumbe vinavyoishi baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa wavuvi wa Kikojani, ambao ni wavuvi wenye kupenda kuhamahama, wamekuwa wananyanyaswa na wananchi wenzao. Ni dhahiri kwamba, Watanzania wanayo haki ya kutembelea sehemu yoyote ya nchi iwe ni kwa kutalii au kwa shughuli za kuchumi. Kwa mantiki hiyo, wavuvi wa Kikojani nao pia wanayo haki ya kuendesha shughuli zao za kiuvuvi sehemu yoyote ya nchi ilimradi hawavunji sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima nikiri kwamba, wavuvi wa Kikojani wanatumia zana na vifaa duni vya kuvulia. Jambo ambalo linasababisha uharibifu wa mazingira ya baharini licha ya kupata kipato duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuepukana na tatizo la kuharibu mazingira ya baharini na ile azma ya kuwaongezea kipato wavuvi hao wa Kikojani, ninaiomba Serikali kutoa upendeleo maalumu kwa Wakojani kuwapatia zana za kisasa za uvuvi kwa mkopo nafuu. Kwa kufanya hivyo Serikali itakuwa inasimamia vyema utekelezaji wa sera na mikakati ya kuondoa umaskini na kufikia lile lengo la kuleta maendeleo endelevu kwa Watanzania wote.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kuwapongeza kwa hotuba nzuri, Mawaziri wawili, Mheshimiwa Arcado D. Ntagazwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano) na Mheshimiwa Edgar Maokolo-Majogo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Kuondoa Umaskini). Nawapongeza kwa kuwatia hamasa na shime ya kazi kutokana na changamoto iliyoko mbele yao ya kupambana na umaskini na mazingira duni katika nchi yetu. Nawatakia ufanisi mzuri katika mpango wa maendeleo na Bajeti yao ya kupambana na umaskini na mazingira duni nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu uko katika sehemu tatu za Umaskini, kuenea kwa hali ya jangwa/ukame na programu ya usafi wa mazingira. Kwa kuanzia na umaskini, namwomba Mheshimiwa Waziri, anayeshulikia umaskini, aweke bayana vigezo ambavyo vimetumika kupimia umaskini wa kila Wilaya nchini. Ni jambo la kusikitisha kuwa Wilaya ya Same ambayo ni moja ya Wilaya maskini sana nchini haipo katika programu ya kuondokana na umaskini. Wilaya ya Same ni kisiwa cha matatizo ya umaskini wa miundombinu duni. Kule katika Wilaya ya Same wananchi bado wanatembea kwa miguu, hakuna mawasiliano ya simu na wala umeme ukanda wa milimani ambapo ndipo 80% ya wananchi wa Same wanaishi, hivyo, maendeleo ya huduma za jamii na uchumi ni duni. Tunaliomba Shirika la *TASAF*

mtandao wake ufike Wilaya ya Same ili kuboresha huduma za jamii za maji, elimu, afya na mazingira ambazo ni duni mno.

Wananchi kwa nguvu zao wenyewe wamechimba barabara kwa mikono yao na zana duni. Barabara zote za milimani Wilayani Same, zenye urefu wa takriban km 450 zimechimbwa kwa nguvu za wananchi kwa misaragambo na matamasha ya kazi bila msaada wa Serikali. Barabara hizi zinapitika tu kwa magari madogo ya *4-wheel drive*. Tunaiomba Serikali kwa kupitia Wizara ya Ujenzi na msaada maalum wa kuondoa umaskini, itoe msaada wa kuboresha barabara hizi ili ziweze kusafirisha watu na mizigo kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili unahusu kuenea kwa jangwa na ukame nchini. Kasi ya kuenea jangwa na ukame nchini ni kubwa mno katika maeneo ya Same, Singida, Kondoa, Dodoma na Simanjiro. Katika maeneo haya ukame unakua kwa kasi kubwa sana na kukaribisha jangwa, ukame na jangwa ni mabadiliko yanayoashiria kushuka kwa uchumi kwa kukosekana mazingira mazuri ya kilimo, ufugaji na uoto wa asili. Hivyo, naishauri Wizara ianze kuchukua hatua za haraka za kukabili jangwa na ukame katika nchi yetu. Kule katika Wilaya ya Same bonde la magharibi mwa Wilaya ya Same ni kame sana na linatishia kuwepo kwa jangwa, nina imani Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, wanaona eneo hilo wanapopita hapo katika barabara kuu ya Dar es Salaam - Arusha. Eneo hili la bonde la Same Magharibi liko kinyume na pepo za mvua.

Eneo hili pamoja na bahati yake mbaya ya kuwa kinyume na pepo za mvua, bado lina raslimali kubwa ya milima ya kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya kukuza mazingira ya mimea/misitu na kilimo. Pembeni na raslimali hii ya milima, raslimali nyingine ni upepo ambao unaweza kuvunwa kwa ajili ya kuvuna maji chini ya ardhi. *Water table* ya bonde hili la Wilaya ya Same iko karibu sana hivyo kuwepo kwa mitambo ya kuvuna maji kwa *windpower.* Kuwepo kwa raslimali ya maji katika eneo hili kutamaliza tatizo la ukame na tishio la kuwepo jangwa. Naiomba Wizara ifikirie mpango wa kujenga mabwawa na malambo katika kuvuna maji ya mvua kwenye makorongo mengi yanayopeleka maji Mto Pangani na hatimaye baharini. Naiomba Serikali itupatie majibu ya kupambana na ukame na tishio hili la jangwa katika eneo la Same Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa mwisho unahusu programu ya usafi wa mazingira. Pamoja na mpango mzuri uliopo katika Bajeti, naiomba Serikali ihakikishe kinakuwepo kiwanda cha ku-*recycle* mifuko ya plastiki inayotumika kama *packing material* nchini. Mwaka 2002 Serikai katika Bajeti yake ya Viwanda na Biashara iliahidi kujenga kiwanda cha ku-*recycle* mifuko ya plastiki iliyotumika baada ya *packaging.* Mpaka sasa hatujui hatima ya kiwanda hicho. Badala yake mifuko hiyo inazagaa kila mahali nchini na kuchafua mazingira. Iwapo Serikali imeshindwa kujenga kiwanda hicho, basi ipitishwe Sheria ya kupiga marufuku ya matumizi ya *plastic packaging material* na badala yake itumike mifuko ya karatasi kama ilivyokuwa zamani kwa sababu *packaging* za karatasi zinaweza kuchomwa. Naiomba Serikali ilipatie shauri hili jibu la haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawapongeza Mawaziri wote wawili kwa hotuba zao nzuri na kutamka kuwa naunga hoja mkono kwa asilimia moja kwa matumaini kuwa mapungufu niliyoyataja yatafanyiwa kazi ipasavyo.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kuhusu mazingira na mambo yanayohusu Muungano na Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia kuondoa umaskini kwa pamoja, wakishirikiana na watendaji wao wote wakiwemo Wakurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwa jitihada zake ambazo anaendelea nazo, kwa kuweza kutanzua matatizo ya wananchi kwa kasi na kiasi kikubwa cha utekelezaji na kuizinguka Tanzania nzima bila ya kuchoka.

Wizara ya Makamu wa Rais ni Wizara inayoshughulikia masuala ya Muungano na Muungano hivi sasa tunakaribia kufika miaka 40 ambayo iko njiani na katika muda wote huo tumo katika kutoa ahadi za

kuondoa kero za Muungano. Hata Mheshimiwa Rais wetu alipofungua Bunge hili mwaka 2000, alisema atahakikisha kuwa kero zote za Muungano atazimaliza ndani ya siku 60, lakini hadi hii leo imeshafika miaka mitatu, lakini bado zile kero za mwanzo hazijaondoka na kila siku zikiendelea kero hizi zinakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa yanaongezeka mambo ambayo ni ya kitoto na yasiyo na maana na wala hayaingii akilini kama yanafanywa na watu ambao tunawaita wasomi, ukweli utakaposema gari iliyosajiliwa Zanzibar ni sawa na gari ya kigeni hii ni kweli Mzanzibari ni mgeni katika nchi hii *(Foreigner)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kukatwa kwa umeme uendao Zanzibar ni suala la kishenzi hasa ukizingatia kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini hivi juzi alipokuwa akijibu swali la Mheshimiwa Mwaka, alisema *TANESCO* haijauzwa wala kukodishwa isipokuwa imebadilisha tu *management* kama ni hivyo Mkataba wa umeme uliwekwa na Serikali mbili halali za Tanzania sio *Net Group,* leo hii *Net Group* ana nguvu kuliko Serikali hizi mbili ambazo zilikubaliana katika utekelezaji wa *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache napenda kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu ni moja ya mambo muhimu sana katika kutunza mazingira ya nchi yetu na ni muhimu zaidi kwa sababu kuwepo kwake kungechangia kuwepo kwa mvua ambazo ni muhimu kwa uhai wa binadamu na viumbe wengine wote.

Ili uwepo uhifadhi wa misitu ni vema Idara ya Maendeleo ya Misitu iliyo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii ikaangaliwa upya, ili Idara hii ikakaa mahali ambapo itaonekana na itafanya kazi zake ipasavyo, katika baadhi ya nchi Idara hii ni Wizara kamili ya Maendeleo ya Misitu na Nyuki. Uharibifu wa mazingira unaotokana na uvunaji miti kupita kiasi, umesababisha misitu yote ya Serikali isipokuwa *Sao-Hill* kufungwa, huu ni udhaifu mkubwa sana. Lakini baya zaidi nii ukataji usiodhibitiwa wa miti ya asili, mfano ni milima inayozunguka Mji wa Iringa, ambao miaka 15 tu iliyopita ilikuwa imejaa miti ya asili, leo ni mawe matupu milimani inayofanya madhari ya eneo hilo kuwa si ya kupendeza.

Bila shaka Serikali inaelewa tatizo la mazingira linaloikabili nchi kufuatana na madawa ya sumu yaliyopo *SPM-Mgololo.* Ningependa kuleeza kuwa wazo la kubinafsisha *SPM-Mgololo* ni zuri na linaungwa mkono sana, tahadhari juu ya jambo hili ni kuwa kiwanda hiki asipewe mtu mbabaishaji au asiye na uwezo kifedha kukiendesha. Maana iwapo atakitelekeza madhara yake yatakuwa mabaya sana kwa binadamu na viumbe hai katika nchi yetu. Ieleweke kuwa kukikarabati kiwanda hiki pamoja na mtaji wa awali wa kukiendesha zinahitajika fedha kiasi cha *USD* 30.0 milioni, zipo taarifa kuwa yupo mwekezaji ana mazungumzo na Serikali anataka kukiendesha kwa *USD* 4.0 milioni, kiasi hiki ni kidogo kumuwezesha kukiendesha na kufanya biashara.

Matokeo yake atakitekeleza na matanki ya sumu yaliyopo pale yanayohifadhi tani 400 za madawa yanaweza kuleta madhara makubwa mno kwa binadamu na viumbe hai hadi bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeishauri Serikali ichukue tahadhari kubwa katika kuibinafsisha *SPM* kwani si suala la uchumi tu, bali ni la uhai wa nchi yetu.

**MHE. DR. SULEIMAN JUMA OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kikatiba, zipo Wizara ambazo shughuli zake ni za Muungano. Hivyo, itakuwa ni jambo jema ikiwa Mawaziri wa Wizara hizo kutenga siku maalum, japo chache, wawe wanafanya kazi Zanzibar. Jambo hili litaweza kupunguza baadhi ya matatizo ya Kimuungano.

Pili, Baraza la Mitihani ni asasi ya Muungano. Hata hivyo, wafanyakazi wake takriban wote ni wanaotaka upande mmoja tu. Asasi hii inafaa ikiwa pia inaratibiwa na chombo cha Muungano ingawa inatekelezwa na Wizara ya Elimu (Bara). Yapo malalamiko mengi hasa kwa wanafunzi kule Visiwani na hata hapa Bara kuhusu huduma dhaifu kutoka kwa wafanyakazi wake.

Tatu, Tume ya Mazingira ya Taifa *(NEMC)* inaendelea kufanya kazi nyingi za maendeleo. Hata hivyo, miradi mingi ni ya hali ya juu. Mambo mengi ya mazingira ambayo yanawaathiri wananchi wa

kawaida bado hayajachukuliwa hatua. Taka bado ni nyingi mitaani, maji machafu yamezagaa na inaonesha kuwa nyumba nyingi ama hazina vyoo au unadhifu wa vyoo haupo. Hivyo kuhatarisha hali za wananchi kwa mazingira hayo machafu.

Nne, Ofisi za Makamu wa Rais bado zipo upande mmoja tu. Ofisi ya Makamu kule Zanzibar ni ndogo sana na wafanyakazi wachache tu ambao huwa wanapelekewa tu mambo. Inahitajika katika Ofisi zake kuwe na baadhi ya wafanyakazi japo wachache kutoka pande zote mbili za Muungano. Kwa kweli inahitajika kuwa na watendaji pia kutoka Zanzibar katika Ofisi Kuu zote za Wizara na Asasi za Muungano ili kutekeleza vizuri zaidi masuala ya Muungano .

Tano, ipo haja ya Mawaziri wa Ofisi za Makamu wa Rais kutembelea au kukutana na Wabunge wa Majimbo ya Zanzibar, kubadilishana mawazo na kujua mambo yanayoleta kero au yanayoondoa kero kwa upande wa Zanzibar. Jambo hili litaweza kupunguza malalamiko mengi yaliyopo.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Arcado D. Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar D. Maokola-Majogo, kwa kutupatia hotuba ya kisayansi iliyobeba maeneo yote muhimu yanayojumuisha Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la Muungano ndio kiungo chetu muhimu katika Serikali hizi mbili hivyo ni vyema tukapania na kuazimia kufungua ukurasa mpya wa kuondoa kero za Muungano ambazo ni nyingi mno na inaonekana upande mmoja wa Muungano (Tanzania Bara) unakuwa na kigugumizi katika kuziondoa kero hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mgawo wa asilimia 4.5 kwa SMZ ni ndogo mno kiasi ambacho taswira inaonekana Serikali ya Muungano inajichukulia nafasi na mapato makubwa sana kiasi ambacho haistahili kwa nchi mbili sawa sawa zilizoungana kupishana mgawo wa mapato kiasi kikubwa kikubwa kikubwa kama hiki kama ukitilia maanani sote ni ndugu wa damu wa asili na sio vyema kumkandamiza ndugu yako, hivyo kero hii kwa kiasi kikubwa imechangia kuongezeka kwa kiasi kikubwa umaskini huko Zanzibar (Unguja na Pemba), hii ndio kusema umaskini ulioko Zanzibar unasababishwa na mgawo mdogo wa 4.5 katika Serikali ya Muungano, hivyo Ofisi ya Makamu wa Rais izingatie yafuatayo:-

(i) Mgawo wa asilimia 4.5 kwa Zanzibar uboreshwe na uwezeshwe kufikia asilimia 22.5.

(ii) Kujenga Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar ambapo itakuwa karibu kusimamia na kutatua kero za Muungano, pamoja na kudhibiti kuongezeka kero nyingine, mbali na vyombo vinavyohusika hivi sasa na kuondosha kero za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 6 wa hotuba hii nanukuu: "Serikali zote mbili zilichukuwa hatua ya kutekeleza Muafaka uliofikiwa baina ya vyama vya *CUF* na CCM ili kuleta amani na utulivu nchini kama ilivyopendekezwa na vyama hivyo na kuridhiwa na Serikali zetu".

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Muafaka huo umefanikishwa kwa asilimia mia moja kwa upande wa *CUF*, lakini CCM na Serikali zake mbili yani SMZ na Jamhuri ya Muungano bado kuna mambo mengi yafuatayo hayajatekelezwa kama ifuatavyo:-

(i) Rais wa Zanzibar (Amani Abeid Karume) mpaka leo hajawateua wawakilishi kutoka *CUF* kama inavyoonekana katika Muafaka na hatimaye kuanza kutoa kauli zisizo za kuridhisha zinazoashiria kuwa na nia mbaya ya kutowakubali kuwateua wawakilishi wawili kutoka *CUF.*

(ii) Rais wa Jamhuri ya Muungano (Benjamin William Mkapa) kwa upande wake tangu Tume ya Mheshimiwa Hashim Mbita kuwasilisha mapendekezo kwa Rais, katika Tume ya Kuchunguza matokeo ya tarehe 26 na 27 Januari 2001 mpaka leo hii fidia za waathirika hao hazijawafikia na hazizungumzwi kabisa, zimeachwa bila kupatiwa ufumbuzi, ambapo ni mara chache unapouliza jibu la mambo yanashughulikiwa, ndilo linalotolewa lakini kila jambo lina muda wake, sambamba na hili uhuru wa vyombo vya habari kwa Vyama vya Upinzani bado unakandamizwa na Serikali na hasa Redio na *Television.* Ni matumaini yangu

mambo yaliyobakia kutekelezwa Serikali zote mbili SMZ na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zitaharakisha kukamilisha kero hizi za Muafaka haraka iwezekanavyo chini ya Uongozi wa Rais Benjamin William Mkapa. Ni matumaini yangu mapendekezo nilyoyatoa yatazingatiwa na kufanyiwa utafiti na ufumbuzi kupatikana bila kusahau Serikali ya Jamhuri kuweza kulipa fidia za waathirika haraka iwezekanavyo.

Mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pia napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dr. Shein na Mawaziri wake wawili kwa mipango yao mizuri ya kuendesha Wizara hii pamoja na wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali mchango wangu nauelekeza katika mradi muhimu kwa wananchi yaani *TASAF.* Mradi huu lazima niupongeze kwa sababu umesaidia sana katika mchakato mzima wa kupunguza umaskini, kwa njia tofauti lakini hasa nitaje elimu, afya na miundombinu mbalimbali ikiwemo pia barabara za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachokuja kujitokeza hivi sasa ni wataalam wetu wanapotoa kauli zao kwa wananchi juu ya kuibua mradi, tatizo linakuja kwa viongozi hawa kutofika kwa muda mrefu katika hali ya ukaguzi na maelekezo kwa wananchi, hii inapelekea kuvunjika moyo kwa watu wetu hatimae kuupaka matope mradi mzuri huu na wenye fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa hatuwezi kuzungumzia lolote bila kuacha mazingira, napenda kuishauri Serikali ama iongeze kodi kubwa katika uingizaji mifuko ya rambo ili kuibana biashara hiyo kuingizwa nchini au kufidia ukusanyaji wa taka hizo na kuziangamiza kiutaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini ni moja katika tatizo kubwa linaloikabili nchi yetu, hivyo hatuna budi kutoa kipaumbele kuwaelimisha wananchi juu ya mapambano hayo. Mimi nashauri sera hii iuzwe ndani ya Halmashauri zeti ili nguvu za kueleweka kimipango kwa wananchi wetu nini wafanye, huku ikielekezwa kwa vitendo kuwepo miradi hiyo ya kuzalisha na kuingiza mapato kwa njia nyepesi *(Pilot Project)* na kulinganisha mazingira yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Muungano si suala la kuzungumza kimchezo, hasa ukizingatia jinsi Muungano wetu ulivyokomaa na wananchi wetu wanavyonufaika nao. Mimi nashauri hata hili neno la kero za Muungano libadilishwe kwani Muungano hauna kero labda tungesema marekebisho ndani ya vipengele vya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu ambao tayari una umri wa miaka karibu arobaini tunapaswa tujivunie, kwani ni mfano mzuri wa dunia ikiwemo Afrika, wapo wengi waliojaribu lakini wameshindwa kuuendeleza mfano Senegambia na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu chochote kilichochipuka kutokana na ncha mbili kinapaswa kuangaliwa sana na mara nyingi huwa na matunda mazuri. Mfano *budding* ya mchungwa na mlimao, tunda litokalo hapo hupendeza sana kwa ukubwa na hata ladha, lakini lazima kazi kubwa ipite ya kufanya *prunning,* vinginevyo mmea utaharibika. Hivyo, Waasisi wametuachia neema hii hivyo sisi vijana turekebishe vipengele ili Muungano wetu udumu milele na milele, mwisho, ukishindwa na kulea, utajiri aliokupa Mungu, jaribu kucheza na Ibilisi ili kufikie umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo madogo madogo ya Muungano lazima Waheshimiwa Mawaziri wayamalize bila ya kurudiwa mara kadhaa ndani ya Bunge.

Mfano gari lenye usafili wa nambari za Zanzibar kuhesabiwa kama gari la nje ya nchi hivyo kulipiwa gharama za fedha za kigeni hili limepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuungana na wenzangu kumpongeza Waziri Mheshimiwa Edgar D. Maokola-Majogo, Katibu Mkuu na wote walioshiriki kuandaa hotuba. Hotuba imezingatia mambo mengi yahusuyo mazingira ya nchi yetu hasa wananchi waishio vijijini, jinsi gani ya kuwapelekea elimu hasa katika kujiondoa na hali ngumu yaani umaskini, hivyo pamoja na kuwapongeza nawatakia pia kila la kheri na kazi njema na naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza vile vile Makamu wa Rais kwa jinsi anavyojitahidi kuweka mipango mizuri, yenye mwelekeo wa maendeleo ya wananchi na kwamba aendelee na jitihada ambazo wenye kuona na kuelewa wanaziona na kukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi iendelee inahitaji miundombinu kama barabara, maji, umeme, simu na kadhalika. Hali kadhalika na mikoa na wilaya ni vile vile. Katika Mkoa wa Mtwara wanawake wanajitahidi sana katika kuitekeleza Ilani ya CCM katika kujituma kwa shughuli mbalimbali za kilimo, mazao ya biashara na chakula lakini wanapata tatizo la soko la uhakika na huzingirwa na matatizo makuu niliyoyatoa hapo awali, hivyo kutokana na hayo kuimba wimbo wa kuondoa umaskini bila vitendo, Mkoa huu utakuwa wa kudumu kimatatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusukuma elimu inakuwa ngumu, wazazi wanakosa uwezo, uchumi umeporomoka sasa miaka mitatu na kadhalika na kutokana na matatizo hayo, Halmashauri pia inakosa uwezo hata kama imepitisha taratibu za kuwalipia wanafunzi kwa sasa wanashindwa, hatima yake ni kuongezeka idadi ya watu wasiojua kusoma na kupelekea ule u-kutoelewa. Kwani Serikali yetu inapaswa kutoa maelekezo mbalimbali kwa wananchi yakiwemo ya kuboresha maisha yao na kama elimu hana, hata uelewa unakuwa mgumu na ndio umaskini katika jamii, nashauri Wizara itenge fedha siku zijazo za kuboresha maeneo haya ambayo mimi nayaona ni nyeti sana kwani kama elimu haipo kwa wananchi hata uelewa utakuwa mgumu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mtwara, kwa kipindi hiki unaongoza watoto wa kike kufukuzwa shule kwa ajili ya utoro wa mimba, je, hili Serikali yetu inasema nini? Je, isingekuwa vyema kuweka mikakati ikisaidiana na Serikali Mkoani jinsi ya kudhibiti hali hii inayopelekea wananchi kugandamizwa na wingu la umaskini, zipo sheria za kuwabana wale wanaowapa watoto wa shule mimba, lakini hazina uzito na hakuna anayefuatilia. Je, kuacha watoto wa kike wakose elimu usawa utakuwa upo kwani mtoto wa kike anapokosa shule, mtoto wa kiume anasoma ndio kusema miaka na miaka hata tukifanya sensa mtoto wa kike ataonekana yuko nyuma kielimu na wa kiume anaendelea na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *TASAF* nchini kwetu umeanza vizuri sana tena kwa mafanikio makubwa na ni kitendo cha kujivunia. Napongeza sana kwa wale wote wanaosimamia mipango hii. Nashauri kwa zile Wilaya ambazo bado mpango huu haujaanza, taratibu za haraka zifanywe ili *TASAF* na Wilaya hizo ifike na kuchelewa kuwapelekea ni kuwacheleweshea maendeleo yao kwa mfano Wilaya ya Newala ilikuwa katika mpango kwenye miaka mitatu iliyopita, lakini hadi leo hawajapelekewa, vikao vya Halmashauri kila vikiketi vinakumbushia suala hili. Nashauri wahusika waanzishe Wilaya Newala mara moja.

Mwisho, natoa pongezi na kushukuru Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kuwezesha Semina ya juma moja ya Wanawake wa Mtwara na Lindi, tutasimamia ufuatiliaji wake hatimaye iwe Mikoa ya mfano kwa yote waliyojifunza. Mungu ibariki Tanzania.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kuleta Bungeni hotuba nzuri na yenye mwelekeo. Naunga mkono hoja hiyo.

Nazipongeza juhudi zinazofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kupitia *TASAF*. Dhana ya kupeleka miradi inayosimamiwa na wananchi wenyewe ndiyo itakayotukomboa kuondokana na umaskini.

Ushirikishaji wa wanawake katika utekelezaji ni muhimu na ni vyema uigwe na Wizara na taasisi nyingine nchini.

Hifadhi ya mazingira isiishie tu Siku ya Taifa ya kupanda miti. Zoezi hili liendelezwe hasa vijijini kwa kuwa kuna *NEMC* Kitaifa, chombo kama hiki kiwepo tangu ngazi za vijiji na mkazo uwe hifadhi ya miti na vyanzo vya maji. Maeneo yanayojengwa viwanda vinavyozalisha au kutumia kemikali, yadhibitiwe ili viwanda hivyo visichafue maji na mazingira mengine kama *KTM* Mbagala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kemikali nyingi sana hasa Dar es Salaam, kwenye bohari ambazo zimeisha muda wake. Juhudi za pamoja zifanywe na Wizara ya Kilimo na Chakula, ili kuziteketeza. Kiwanda cha Mbolea cha Tanga kina kemikali hatari sana, utaratibu madhubuti ufanywe kuziondoa ili zisilete athari kwa wakazi jirani.

Kumekuweko na dhana potofu kuwa Muafaka kati ya CCM na *CUF* ni budi uzingatiwe na Serikali zote mbili. Pamoja na kwamba, Serikali zote zinaweza kuwa zinaafiki tendo la Muafaka, sidhani kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalazimika kutekeleza Muafaka kama wengine wanavyodai.

Naipongeza Serikali kwa kuanzisha Tume ya pamoja ya masuala ya fedha. Tume ihakikishe kuwa Serikali zote mbili zinatekeleza wajibu wake kama ilivyoainishwa katika Katiba ili isionekane upande mmoja tu ndiyo unaonufaika zaidi. Imeripotiwa katika vyombo vya habari kuwa baadhi ya wawakilishi waliochaguliwa huko Pemba, waligoma kutamka neno Mapinduzi katika kiapo chao. Kama hayo ni kweli, hivi kiapo chao kilikuwa sahihi na nini lengo lao hasa tunapokuwa tunataka kujenga Taifa linalojivunia Mapinduzi ya mwaka 1964?

Mwisho, naiomba Ofisi ya Makamu wa Rais, kushirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Fedha, Mipango, ili kuhakikisha kuwa Mikoa iliyokithiri kwa umaskini inapata fedha za kutosha ili kuleta maendeleo na kufuta umaskini. Kwa makusudi ielekeze Wahisani na *NGOs* mbalimbali waelekeze nguvu zao kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja hii.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zenu ni nzuri sana hususan Mradi wa *TASAF,* tena zina mvuto na ni za maendeleo. Pamoja na hayo zimetuchonganisha na wananchi wetu. Mnazitangaza na Rais naye katangaza. Kwa hiyo, Wilaya ambazo hazina Mradi wa *TASAF* limekuwa tatizo. Wananchi wanauliza Mbunge ni kwa vipi ameshindwa kuleta Mradi wa *TASAF*? Hili limekuwa tatizo kwani wananchi wanaona kama wamebaguliwa. Vigezo vilivyotumika kupeleka Mradi wa *TASAF* katika maeneo ni vya upendeleo kwani *TASAF* haikupelekwa Wilaya ya Geita. Kama ni umaskini uko huko, watu hawana barabara za vjijijini, hawana maji, vituo vya afya hakuna. Wilaya ya Geita inaongoza kwa kuwa na idadi ya watoto wa shule za msingi lakini hakuna Sekondari. Tafadhali sana naomba nielewe lini Geita itakuwa katika mpango wa *TASAF?* Vinginevyo matangazo mazuri mazuri ya *TASAF* ni sawa na kututambia au kutuongezea matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TASAF* ni tatizo kwa Wabunge wa Geita, kwani wananchi hawaelewi kwa nini wameshindwa kuleta *TASAF* Geita.

**MHE. HERBET J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Napenda kuwapongeza Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mazingira na Muungano, pamoja na Watendaji wa Wizara yake kwa hotuba nzuri na programu zake za kuhifadhi mazingira kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri ufuatao kwa kuboresha mipango ya utekelezaji wa hifadhi ya mazingira hapa nchini. Nashauri Wizara iratibu miradi ya Serikali na wafadhili inayolenga kusaidia kutekeleza mipango ya hifadhi ya mazingira. Pamoja na kuratibu Wizara pia iweze kutoa ushauri

wa karibu kwa Serikali hasa katika kuharakisha ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaotakiwa kuhama ili kutoa nafasi kwa ajili ya hifadhi ya mazingira katika misitu ya asili na vyanzo vya maji. Kwa mfano, Wahisani wa *FINIDA* wamekubali kushirikiana na wananchi kulipa fidia kwa wananchi wa maeneo ya Hifadhi ya Msitu wa Amani, Wilaya ya Muheza, ambao kwa zaidi ya miaka mitatu iliyopita wamekubali kuhama na kusitisha shughuli za kilimo lakini hadi sasa bado hawajalipwa fidia.

Katika hali kama hii wananchi hao wanakosa imani na kupoteza maana ya kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji. Tatizo kubwa ni Serikali kushindwa au kutopanga fungu la kuchangia gharama za fidia kama inavyokubaliwa na Wahisani. Hivyo, ipo haja ya Wizara hii kuchukua jukumu la kuikumbusha Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kulipa fidia katika mipango shirikishi ya hifadhi ya mazingira. Wizara ya Fedha peke yake haitaweza kufahamu mipango yote Mikoani inayohitaji kutengewa fedha kwa utekelezaji hivyo ipo haja ya kuratibu mipango kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uingizaji wa magari chakavu nchini, Wizara hii itoe mchango wa ushauri juu ya uingizaji wa magari chakavu nchini. Nchi zinazotengeneza magari kama Japan zinasheria za viwango vya magari yanayokubalika kutumika nchini mwao. Hivyo, magari yanayovuka muda wa viwango vyao hutolewa na kuuzwa katika nchi maskini ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa sera yao ya kuhifadhi mazingira. Magari hayo yanauzwa kwa bei ndogo sana na Serikali zao hutoa *subsidy* katika gharama za kuyasafirisha magari hayo kutoka nchini mwao. Kwa hali hiyo nchi maskini hugeuzwa *dumping place* ya magari chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima sasa nchi yetu iangalie upya utaratibu wa kuingiza kwa wingi magari chakavu ambayo baada ya kutumika kwa muda mfupi yanageuka kuwa magofu katika maeneo yote ya Miji, Manispaa na miji midogo na kuchafua mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii pia inapaswa kuhamasisha biashara ya uuzaji wa masalio ya vyuma chakavu nje ya nchi ili kupunguza mlundikano uliopo wa uchafu huo. Hivi karibuni kumeanza kuongezeka kwa vikwazo vinavyoweza kukwamisha kuendelea kwa biashara hii. Ni wajibu wa Wizara hii kuendelea kwa biashara ya uuzaji wa masalio ya vyuma chakavu nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia juu ya miti inayokatwa sana kama nishati ya kupikia na kupata moto kwa mahitaji ya nyumbani. Hali hii inafanya ukataji wa miti kuongezeka mwaka hadi mwaka. Nashauri Serikali itafute nishati mbadala ili kuhifadhi misitu yetu. Tukiachia mwenendo huu katika miaka 10 ijayo, Tanzania itakuwa jangwa. Aidha, Serikali kwa pamoja mshirikiane ili nishati ya umeme iwe rahisi na isambazwe nchini kote. Iwapo nishati ya umeme itaendelea kuwa ghali, basi ukataji miti utaendelea na kuathiri mazingira.

Hivi sasa Tanzania ina magari mengi kuliko uwezo wa barabara hasa mijini. Lakini magari mengi haya ni yale yaliyotumika na sisi tunaletewa mabaki. Aidha, magari mengi yanatoa moshi mzito ambao huchafua harufu nzito. Wataalam wanasema moshi ule unaathiri mapafu na kuleta ugonjwa moyo. Je, Serikali haioni kwamba, moshi huu wa magari unachafua mazingira? Serikali lini itatunga sheria ya kupiga marufuku magari yanayotoa moshi mzito? Umefika wakati sasa kwa Serikali kuwa na msimamo ama sivyo nchi yetu itageuka dampo ya magari mabovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia juu ya uondoaji umaskini. Naipongeza Serikali kwa mikakati yake ya kupunguza umaskini nchini. Tanzania ina raslimali kubwa na nyingi katika kila eneo la nchi. Nashauri Serikali ipange kwa mafungu kuwawezesha wananchi jinsi ya kutumia raslimali waliyonayo ili ziwaondolee umaskini. Kwa mfano, Mkoa wa Lindi una minazi mingi na minazi inaweza kutoa aina nyingi ya mazao kwa mfano, madafu kutengeneza kamba, shina linatoa mbao na kadhalika.

Kwa kuwa Mkoa Lindi uko pembezoni na umesahauliwa, jitihada zangu za kutafuta wafadhili wa kuwafundisha wananchi matumizi ya ziada ya mnazi zimegonga ukuta, je, idara ya kuondoa umaskini inaweza kubeba jukumu hilo? Hii ni njia pekee ya kupunguza uzururaji, umaskini na wizi wa nazi, nashauri Serikali iwe na mpango madhubuti wa kusaidia Mkoa wa Lindi.

Mfuko wa *SELF* unalenga kusaidia kuondoa umaskini. Lakini masharti mkopo wa *SELF* ni dhahiri unalenga wenye uwezo na hasa pale riba inapokuwa kubwa na mwombaji awe na biashara. Utaratibu huu unamuweka kando kijana na mwanamke anayetaka kujikwamua kiuchumi, kwa vile anashindwa masharti. Nashauri kuwa Serikali ipitie upya masharti ili kuwasaidia walipaji wadogo wadogo, Serikali iweke mafunzo ya biashara kama sharti muhimu. Mkopaji hata kama ndiyo anaanza biashara, akipata *basic skills* za *enterpreneurship*, ataweza kumudu mkopo. Nashauri pia riba ipunguzwe ili mkopaji aweze kulipa.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi mbili zilizoungana. Siku za karibuni kumekuwa na malalamiko toka kwa watu mbalimbali juu ya kero ya Muungano hasa kwa upande wa Zanzibar. Ni vyema Ofisi ya Makamu wa Rais, ikachukua hatua za dharura katika kukabiliana na tatizo hili, kulipatia ufumbuzi wa kudumu hasa katika sekta zifuatazo: Suala la *TRA*, suala la *BoT*, suala la Mambo ya Nje, gawio la asilimia 4.5 kwa Serikali ya Zanzibar ni dogo mno hivyo iko haja kiwango hiki kikaangaliwa upya na ikibidi kuongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea suala la Muafaka. Nawashukuru wote waliosimamia Muafaka kati ya *CUF* na CCM. Pia natoa shukrani kwa yale mambo yaliyotekelezwa katika Muafaka huo. Hata hivyo, kuna mambo ya msingi ambayo bado hayajatekelezwa. Namshauri Waziri, achukue hatua za dharura kuhakikisha kuwa yale mambo yote ambayo bado hayajatekelezwa yanafanyiwa kazi haraka.

Pia naipongeza Serikali kwa hatua yake ya kutoa mikopo kwa wafanyabiashara ndogo ndogo. Naomba maelezo ni kiasi gani mikopo hii imesaidia wafanyabiashara wa Zanzibar. Je, Serikali inakabiliwa vipi na wimbi la umwagaji taka za viwandani unaofanywa na meli za mataifa makubwa? Tabia ya kumwaga baharini taka zote za makaro ya majumbani na viwandani inachangia kwa kiasi gani uharibifu wa bahari, mito na maziwa nchini mwetu?

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naipongeza hotuba nzuri na maelezo mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri. Hivyo, naunga mkono hotuba hiyo kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo licha ya Wizara kuandaa mipango na programu nyingi za kuboresha mazingira ya nchi yetu hususan maeneo ya Maziwa Tanganyika, Victoria, ipo miradi mikubwa mikubwa ya kuboresha mazingira ya maeneo hayo, tena ikifadhiliwa na Mashirika ya Kimataifa, hakuna juhudi zilizofanywa au zinafanywa au kukusudia kufanywa ili kulinda na kuboresha mazingira ya Ziwa Nyasa.

Je, Serikali ina sababu gani za msingi za kususa au kutelekeza sehemu hii ya nchi? Katika mipango yake ya mazingira angalau Wizara ingefanya utafiti wa kubaini ubora wa maji ya Ziwa Nyasa ambayo yanatumika na wakazi wa huko bila kujua athari zilizopo kwenye maji hayo.

Hata hivyo, naipongeza Wizara kwa kuanza maandalizi ya mradi wa pamoja kuhusu hifadhi ya mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa kwa ushirikiano wa nchi za Malawi na Msumbiji katika hotuba hii ya Bajeti 2003/2004.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii iliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu. Awali ya yote nawapongeza kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (Mazingira na masuala ya Muungano na Kuondoa Umaskini), Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa umakini na umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi zangu kwa jinsi Mfuko wa *TASAF* unavyofanya kazi nzuri kwa kuishirikisha jamii katika kujiletea maendeleo yao kwa njia ya kujitegemea. Natoa ombi maalum wataalam wa Mfuko huu waje Mbinga ili kusaidia juhudi za wananchi wa Mbinga za kuleta maji safi na salama kwa kutumia *gravity.* Wananchi hao wanachohitaji ni kusaidiwa kununua vifaa kama mabomba. Shughuli nyigine zote wanazifanya wenyewe. Mfuko huo ujihadhari na kile kinachoitwa maeneo au Wilaya tajiri na maskini kwa sababu hakuna eneo tajiri hapa Tanzania, wote ni maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mazingira namwomba mtoa hoja alieleze Bunge lako Tukufu hali halisi ya mazingira yetu kwa ujumla kama tunaenda mbele au tunarudi nyuma kuanzia na Mkutano wa *RIO*. Ni kwa lengo la kujipima, katika nyanja mbalimbali. Tathmini ya kina inahitajika ili kujipanga upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa mazinigra unaonekana katika sehemu mbalimbali. Serikali inasema nini kuhusu kemikali iliyoko huko Kiwanda cha Karatasi Mgololo Mkoani Iringa? Hivi nchi inasubiri mpaka janga litokee ndipo ichukue hatua. Kwa nini viwanda vinavyotengeneza Mifuko ya plastiki visifungwe, kwani vinasababisha uchafuzi wa mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za karibuni Serikali ya Kenya ilitangaza azma yake ya kuhusu ujenzi wa bwawa la Ewaso Ngiro *(South),* kwa lengo la kuzalisha *MW 180* za umeme katika Mto Mara, ambao ni muhimu kwa wanyamapori wanaohama kutoka Serengeti, Ngorongoro kwenda Maasai Mara. Nini athari za maamuzi hayo kiikolojia na Serikali yetu inafanya nini kudhibiti tishio hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, suala la nishati ya kuni na mkaa halikupatiwa nishati mbadala, nchi hii na watu wake watajichimbia kaburi la pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namaliza kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ili nichangie hoja ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwanza, nampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa mawasilisho yake mazuri ya hotuba ya Bajeti. Vile vie nampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Umaskini) kwa kazi nzuri ya matayarisho ya Bajeti hiyo. Hali kadhalika nawapongeza kuanzia Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa maandalizi mazuri ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nauelekeza kwenye suala la kuondoa umaskini miongoni mwa wananchi Vijijini kwa kuelewa kuwa ndiyo kero kubwa katika Jimbo langu la Nanyumbu. Labda niseme kuwa Wananchi wa Jimbo la Nanyumbu wanaona kuwa ili kuondokana na umaskini ni lazima kuwepo mabadiliko makubwa kwenye fani za kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara. Fani zote hizo hivi sasa zinatumia teknolojia na zana duni kwa kukosa mtaji wa kutosha ili kubadili hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ili Serikali isaidie Wananchi wa Jimbo langu la Nanyumbu kuondokana na umaskini, kuhakikisha kuwa mikopo nafuu ya mitaji inaelekezwa kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara kupitia mashirika ambayo hayana ukiritimba kama *SIDO* na Mabenki. Ni vizuri mikopo hiyo ikapitia Vyama vya Ushirika vya Msingi kwa kudhaminiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi. Kwa sababu Wilaya ya Masasi ina Majimbo matatu ya Masasi, Lulindi na Nanyumbu, ni vizuri mikopo hiyo ikawekwa kimafungu kwa kila Jimbo ili kuhakikisha kuwa kila Jimbo linafaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezoea kuona mikopo hii ikitolewa katika Miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mtwara, lakini huko Vijijini mikopo hiyo haipo. Kwa wananchi wengi kufika katika Miji hiyo mikubwa kutafuta mikopo ni gharama kubwa hivyo hukata tamaa. Wakati mwingine gharama za kufuatilia mkopo huwa kubwa sana kuliko mkopo unaopatikana hivyo wananchi huona kuwa mikopo hiyo ni usumbufu mkubwa. Kwa hiyo, naomba Serikali ione umuhimu wa kusogeza mikopo hiyo hadi Vijijini waliko walengwa. Kwa kufanya hivyo nina uhakika tutapiga vita umaskini huko Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupata mikopo wananchi wataboresha sana kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara. Wakati mwingine wananchi wataweza hata kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika

mazao yao hivyo wananchi kuongeza thamani ya mazao yao. Kwa kufanya hayo wananchi wengi watapata ajira na kuweza kujiondolea umaskini kwa kupata mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nitamke kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mwisho, nashukuru tena kwa kupata nafasi hii ya kuchangia. Ahsante sana.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi, naomba kushauri mambo matatu kama ifuatavyo:-

Kwanza, inafahamika kuwa kuna tofauti ya umaskini Kimikoa, Kiwilaya na Kikaya. Juhudi za kuondoa umaskini zizingatie tofauti hizi katika Bajeti ya Serikali ya kila mwaka, wale maskini zaidi wasaidiwe zaidi kuliko hali ilivyo sasa hasa kuwapatia elimu ya bure au *subsidized.* Pili, kwa kuwa hivi sasa miradi mingi au programu nyingi zinatekelezwa kwa awamu kama uboreshaji wa Serikali za Mitaa, *PADEP, TASAF* na kadhalika, nashuri pawe na uratibu ili isiwe Wilaya zile zile tu ambazo zinajikuta zikipata miradi na fedha nyingi wakati Wilaya nyingine zinabakia. Pawe na Ofisi ya Uratibu. Tatu, katika awamu ya pili ya *TASAF*, sisi wananchi wa Kongwa, wilaya mpya maskini, tunaomba sana tuingizwe katika mradi huo muhimu na tunaahidi kufanya maajabu kwa uwezeshwaji wa *TASAF* pamoja na nguvu zetu wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Waziri wa Nchi, Mazingira na Muungano, pamoja na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Waziri wa Nchi, Kuondoa Umaskini na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Bwana Raphael Mollel, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, pamoja na viongozi na watumishi wengine katika Ofisi ya Makamu wa Rais na taasisi zake, kwa hotuba nzuri na kazi bora katika utekelezaji na uendelezaji wa majukumu yao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri na maendeleo yenye mafanikio makubwa yanayotokana na jitihada za Ofisi ya Makamu wa Rais, bado kuna nafasi nzuri ya kuboresha maendeleo na mafanikio. Ningependa kuchangia kama ifuatavyo:-

Kuhusu kupambana na umaskini mafanikio makubwa yamepatikana katika jitihada za kupambana na umaskini hasa kwa kupitia mipango shirikishi kupitia *TASAF*, sasa unapanuliwa kwenda kwenye Wilaya zote. Ni matumaini yangu kwamba, kutokana na hatua hii jitihada za kupambana na umaskini zinapata maendeleo makubwa nchini kote. Hata hivyo, wananchi wengi wanapata ugumu wa kuchangia michango yao kwa kiwango cha muda unaostahili kutokana na umaskini uliokithiri. Hivyo, zaidi ya kuwahamasisha wananchi, ipo haja kubwa ya kurahisisha *flexibility,* viwango na muda wa kukamilisha michango. Aidha, nashauri kwamba Mradi wa *SELF* utangazwe na kuenezwa zaidi ili wananchi wengi zaidi waweze kufaidika. Vile vile ipo haja ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kuhakikisha kwamba taasisi zisizo za Serikali *(NGOs),* zinatekeleza madhumuni yao ipasavyo na kuboresha utendaji wao ili jitihada za kupambana na umaskini zipate kasi na mafanikio zaidi.

Kuhusu ulinzi wa mazingira. Inasikitisha kwamba, pamoja na jitihada mbalimbali ukataji miti ovyo, uchomaji moto, uharibifu wa vianzio vya maji, uchafu uliokithiri katika Miji mingi, uchafu wa mazingira kutokana na uchafu wa viwandani, moshi wa magari mabovu na aina nyingine nyingine nyingi za uchafuzi wa mazingira, bado ni kero kubwa dhidi ya jitihada za kulinda na kuboresha mazingira. Ningependa kushauri kwamba, Serikali iwe na mtazamo mkali zaidi na kuchukua hatua thabiti na kali zaidi katika kulinda na kuendeleza mazingira. Ingefaa kuzitazama upya na kuzikazia zaidi sheria, kanuni na taratibu za kulinda mazingira ili wale wanaofanikisha wazawadiwe na wale wanaoharibu wapewe adhabu kali zaidi. Programu maalum za kukuza ufahamu wa wananchi kuwahamasisha na kuwapatia motisha bora zinaweza kuchangia sana katika kulinda na kuendeleza mazingira.

Kuhusu adui rushwa. Hatua thabiti za kupambana na rushwa kwa nguvu zaidi bila shaka zitachangia sana katika kupambana na umaskini na pia kulinda na kuendeleza mazingira. Hivyo basi, vita

dhidi ya rushwa hapana budi viimarishwe zaidi iwapo tunatarajia kupata mafanikio mazuri katika kupambana na umaskini na kulinda mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kwanza kutamka moja kwa moja kwamba naunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri mwenzangu leo asubuhi kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais, hotuba hii tuna ubia mimi na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa. Asubuhi Mheshimiwa Spika aliniandikia ki- *note* na kusema, mbona kwenye jalada kumeandikwa "Waziri wa Nchi, Kuondoa Umaskini na Mashirika Yasiyo ya Serikali" kwamba unaondoa umaskini unaondoa na mashirika yasiyo ya Kiserikali. Nikamwaahidi ya kwamba nitasahihisha tuseme neno sahihi hapa, "ni Uratibu na Uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali", usiunganishe kule kuondoa na yale mashirika ya Kiserikali.

Nami pia napenda kuungana na wasemaji wa awali kwa kumpa pongezi Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya hapa nchini. Mimi na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa ni mashahidi wa kazi anazozifanya za kutembelea maeneo mbalimbali na hata sisi Waheshimiwa Mawaziri kwa njia moja au nyingine tumeshiriki katika ziara zake hususan Zanzibar nimepata nafasi ya kuona kazi kubwa anayoifanya. Kwa hiyo napenda kuungana nao wale wote ambao wamelisemea jambo hili kwa kipindi cha asubuhi na cha jioni hii. *(Makofi)*

Pia ningependa niwashukuru Mheshimiwa Anne S. Makinda ambaye ni Mwenyekiti wa Sekta yetu, kwa mchango wake yeye mwenyewe pamoja na Kamati yake na nilipata nafasi ya kufuatana nao Mikoani na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, busara zao zimetusaidia sana kufika hapa tulipo kwa maana ya kuandaa hotuba hii. Aidha, pia ninapenda kuchukua nafasi hii kurudisha fadhila kwa Mheshimiwa Msemaji wa Upinzani, wasemaji wawili wa sekta yetu, Mheshimiwa Ali Said Juma na Karim Said Othman, kwa jinsi walivyotupongeza kwamba tunashirikiana nao na sisi tumetoa ahadi ya kwamba tutaendelea kushirikiana nao katika nafasi zetu ili kusudi tuweze kuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi waliyoyasema asubuhi yale ambayo yanaendana na sera zetu tutayazingatia na mengine kuyatafakari ili tuweze kuboresha huko tunakokwenda. Napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia mpaka sasa hivi tangu Bajeti hii ianze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda niende kwenye hotuba yetu. Mimi nitajibu hoja zinazohusu eneo ninalolisimamia la kuondoa umaskini na uratibu wa mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini labda niseme kama Mbunge wa muda mrefu, niseme moja tu hili alilolisema Mheshimiwa Charles H. Kagonji. Mimi kama mwanachama wa CCM hili analosema kwamba viongozi wale wanaojihisi kwamba wanaweza kugombea Urais wajitangaze mapema. Nchi nyingi wanafanya namna hiyo kama Marekani na kadhalika. Lakini mimi kwa uzoefu wangu hapa si kwa Urais tu lakini hata kwa Ubunge. Kugombea Ubunge ukianza kujitangaza mapema mapema basi kutakuwa na fisi wengi wanakukimbiza kimbiza, watakuandama wewe, watakufuata chooni, watakusingizia hili, watawatumia watu mbalimbali wakuandike vibaya mwisho hata uongozi wenyewe hautaufikia, hiyo nasemea sura nyingine ya suala hili. Kwa hiyo, wakati mwingine ku-*lay law* na chama kinavyofanya mpaka sasa ni jambo zuri, ukijitangaza mapema watakuuwa mapema. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa atawajumuisha wale waliosema kwa maandishi, waliochangia kwa maandishi pamoja na wale waliochangia kwa kusema. Kwa hiyo, mimi nitajibu hoja zile zilizotolewa na Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge wale wa Upinzani na pia kwa kwenda kwenye zile sekta nilizozisema mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza, tumeambiwa hasa na Mheshimiwa Dr. Bultilda Burian anasema: "Malengo ya Kimataifa ya maendeleo *millenium development goals* yaoanishwe na malengo ya mkakati wa kupunguza umaskini". Ni kweli tunasema kwamba lengo ni kuondoa umaskini uliokithiri ifikapo mwaka 2025 na *percent 50* mwaka 2010. Mkakati wa kupunguza umaskini ni mpango wa utekelezaji wenye malengo ya kupunguza umaskini hatua kwa hatua hadi kufikia lengo hilo. Malengo hayo ya Kimataifa yamejumuishwa katika mkakati wa kupunguza umaskini kama tulivyosema kwenye semina juzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini inafanyika katika mfumo wa ufuatiliaji wa hali ya umaskini nchini na taarifa ya utekelezaji inatolewa kila mwaka. Aidha, pia kumetolewa hoja kwamba kuna umuhimu wa Madiwani na Wabunge washiriki katika mfumo wa ufuatiliaji wa mkakati wa kupunguza umaskini yaani *monitoring unit* inayofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Serikali inatambua umuhimu wa Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kushiriki kikamilifu na tumekubaliana kwenye Kamati ya Sekta kwamba jambo hili linafanyiwa kazi sasa hivi na katika mapitio ya mfumo huu yatakayofanyika mwaka huu wa fedha suala la kushirikishwa Waheshimiwa Wabunge na Madiwani litazingatiwa na litawekwa kwenye mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja pia kwamba kuna haja ya uratibu wa fedha za wafadhili kuelekeza misaada hii katika maeneo muhimu. Suala hili limezungumzwa na Mheshimiwa Bernard Membe na Mheshimiwa Charles H. Kagonji, ameligusia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema ya kwamba tayari Serikali imeandaa mfumo wa ushirikiano na wafadhili yaani Tanzania *Assistance Strategy* ambao unaratibiwa na *secretariat* inayoongozwa na Wizara ya Fedha. Serikali pia inakamilisha mpango wa utekelezaji wa mkakati huu. Makubaliano yamefanyika ili kuwezesha fedha za wafadhili kupitia katika Bajeti ya Serikali. Ndio maana nasema katika suala zima la kuondoa umaskini kwa sababu linagusa sekta mbalimbali hayo yanazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetolewa hoja na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa kwamba ili kuondoa umaskini suala zima la Mradi wa Chumvi Unguja na Pemba *(NIGP)* ambao unasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais lazima uzingatiwe. Mradi wa chumvi Unguja na Pemba ni mojawapo ya miradi iliyotegemewa kukamilishwa kwa fedha zilizotegemewa kutoka Serikali ya Ubelgiji katika mwaka 2002/2003. Tayari Ofisi ya Makamu ya Rais imeshawasiliana na Waziri wa Fedha ili kupanga kikao na Ubalozi wa Ubelgiji ili utekelezaji wa mradi huu na mingineyo iweze kukamilishwa katika mwaka huu wa Bajeti. Katika kitabu chetu cha hotuba tumeonyesha kiwango kisichopungua bilioni mbili katika kipindi cha miaka mitano, wenzetu wa Ubelgiji watatoa fedha katika maeneo mengine. Kwa hiyo, tutafanya nao mazungumzo ili hiyo kesho, kesho aliyosema Mheshimiwa Faida Bakar iondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ameongelea umuhimu wa mradi wa *SELF* ambao kwa sasa hivi unatekelezwa katika Mikoa sita ya Singida, Dodoma, Morogoro, Pwani, Lindi na Mtwara. Serikali inafanya tathmini mafanikio ya mradi wa *SELF.* Hatua ya kueneza mradi kwenye Mikoa mingine zaidi inafanyika kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* ambao ni wafadhili wa mradi huo. Tunategemea kwa mwaka huu wa fedha Mikoa ifuatayo itaingizwa kwenye mradi nayo ni Mbeya, Iringa, Ruvuma, Mwanza, Mara, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro na Tanga. Katika ile Mikoa sita kwa maana ya Tanzania Zanzibar kwa hivi sasa Mikoa yote mradi huo unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu SELF, tumesema hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2003 umetoa kiasi cha shilingi 55 milioni kwa asasi mbili za kifedha ambazo ni *PRIDE Tanzania* na CHANGAMOTO. Aidha, kiasi hiki kimewanufaisha zaidi wafanyabiashara ndogo ndogo 500 na mradi huo uko mbioni kuanza kutoa mikopo huko Pemba kupitia asasi ya *PRIDE Tanzania.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetolewa hoja kwamba hali ya umaskini mijini iangaliwe na itiliwe mkazo katika mkakati wa kupunguza umaskini, limezungumzwa na Mheshimiwa Dr. Mahanga. Tunakubali kwamba umaskini uko sehemu zote mbili vijijini na mijini. Lakini hadi sasa Serikali imeshafanya utafiti kuhusu hali ya umaskini mijini na kubaini kwamba matatizo ambayo yameelezwa katika Ripoti ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ya mwaka 2002 tutayafanyia kazi. Mapitio ya mkakati wa kupunguza

umaskini yatazingatia matokeo ya utafiti huu ili kuchukua hatua za makusudi kupambana na umaskini mijini na hasa kuboresha makazi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumetolewa hoja kwamba tofauti ya umaskini Kimkoa, Kiwilaya na hata Kikaya izingatiwe katika mkakati wa kupunguza umaskini. Tunakiri kwamba suala hili limejitokeza wazi katika Ripoti ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ya mwaka 2002. Katika kufanya mapitio ya mkakati wa kupunguza umaskini suala hili litakuwa na umuhimu ambao tutaufanyia kazi na litazingatiwa, tumechukua ushauri huo. Hata hivyo, ni muhimu kuwa na mikakati ya Kiwilaya kulingana na mazingira ya sehemu hizo na Serikali itawezesha uandaaji wa mikakati hiyo. Lakini niseme kwamba siri kubwa ya mafanikio katika kuondoa umaskini ni kwa wananchi wenyewe kufanya kazi kwa bidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TASAF,* kwanza zimetolewa pongezi kwa utendaji mzuri wa *TASAF* na Mheshimiwa Rais ambaye amebuni na kuelekeza mradi huu utekelezwe. Serikali inazipokea pongezi hizo za Waheshimiwa Wabunge aidha inawapongeza wananchi kwa kazi nzuri wanayofanya katika kutekeleza mradi huu. Pia Waheshimiwa Wabunge wamempongeza Mr. Kamba ambaye ni Mkurugenzi wa *TASAF,* yupo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba mmetambua utendaji wake mzuri wa kazi na Mr. Kamba hii ni sehemu mojawapo ya motisha sio lazima upewe fedha tu kusemwasemwa Bungeni hapa vizuri ni sehemu ya motisha. Kuna wengine hapa wanaundiwa Tume mpaka wanafukuzwa kazi hapa wewe umesifiwa uondoke nyumbani kalale usingizi wako kwa amani na utulivu na iwe changamoto ya kutekeleza miradi hiyo kwa kasi zaidi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa nasisitiza kwa viongozi wote nchini kuhakikisha kwamba miradi ya *TASAF* wananchi wenyewe ndio waamue kwamba tutekeleze mradi gani, unaanzia chini kwenda juu sio kuagiza kutoka juu kwenda chini. Usiwaangilie wananchi kama wameamua basi sisi tutaelekeza fedha huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mwongozo, tunasema kwamba hali ya upelekaji fedha sasa hivi itakuwa umeboreshwa kwa sababu imesemwa kwamba fedha za *TASAF* wakati mwingine zinachelewa, hilo tumeliboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja kwamba kwa nini *TASAF* isiende Wilaya nyingine? Maandishi mengi tuliyopata hapa yanasema *TASAF* inapelekwa kwa upendeleo, lakini tayari Serikali kama alivyosema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi ilishaamua kwamba *TASAF* iende katika Wilaya zote. Utekelezaji wa uamuzi huu utafanyika katika awamu ya pili ya *TASAF* ambayo maandalizi yake tayari yamekwishaanza. Tunategemea mwaka huu wa fedha 2003/2004 *TASAF* itafika katika kila Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *NGOs,* hoja imetolewa kwamba tangu kupitishwa kwa Sheria ya *NGO* uandikishaji wa *NGOs* katika sheria nyingine umekuwa na urasimu. Kwa mfano, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, alizungumzia juu ya *NGO* ya *The Rift Valley Children Fund* ambayo iliomba usajili. Kabidhi Wasii huandikisha mashirika ya udhamini baada ya kuridhika na utekelezaji wa kanuni za kusimamia uandikishaji. Ofisi ya Makamu wa Rais itafuatilia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetolewa hoja kwamba kanuni za uendeshaji shughuli za *NGOs* na utekelezaji wa sheria hiyo zimefikia hatua gani? Kanuni zipo na tayari zimeandaliwa na tumezifikisha kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili azipitie na kuidhinisha kwa taratibu zilizopo. Ofisi ya Makamu wa Rais iliitisha mkutano wa *NGOs* Morogoro tarehe 10-11/6/2003 na kuweka utaratibu wa kupata wajumbe wa Baraza la *NGOs.* Majina ya wajumbe wa Baraza la *NGOs* yatawasilishwa Ofisi ya Makamu wa Rais ifikapo tarehe 31/7/2003. Baada ya hapo Ofisi ya Makamu wa Rais itaitisha kikao cha Baraza la *NGOs* mwezi *August* mwaka huu ili wachague wajumbe wa Bodi ya Kuratibu *NGOs.* Pia imeshauriwa kwamba fedha wanazopata *NGOs* zijulikane zinafanya nini, wapi, sheria ya *NGO* itekelezwe mara moja. Nimesema utekelezaji utaenda sambamba na kanuni ambazo zinafanyiwa kazi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.Kuhusu Sheria ya *NGOs* imeelekeza kwamba *NGOs* zitoe taarifa za fedha wanakozipata

na kazi zao za mwaka na taarifa hizi zitaonyesha kiasi gani cha fedha nani amefadhili na matumizi yake yamekuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba nilisimama hapa kufanya mambo matatu moja, kuunga mkono hoja iliyotolewa asubuhi na Waziri mwenzangu. Pili, kuthibitisha na kuhakikisha kama mmojawapo ninayefanya kazi kwenye Ofisi ya Rais kwamba Makamu wa Rais anafanya kazi nzuri sana kama walivyoeleza Wabunge wengine na tatu, kujibu hoja hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, mimi kama Mbunge wa Nachingwea napenda kusema maneno mawili, matatu. Kwanza kuwashukuru wananchi walioniwezesha kukaa Bungeni kwa vipindi sita kwa kunichagua mfululizo na hakuna maajabu tunayofanya kuchaguliwa mfululizo lakini ni vizuri wakati mwingine hata Mbunge wa zamani anajifunza vitu kwa Mbunge mpya na Mbunge mpya pia anaweza kujifunza mambo kwa Mbunge wa zamani. Lakini nasema kinga yangu kubwa wamekuwa wananchi nathibitisha hapa kwamba nakaa hapa Bungeni na nimefuatilia mambo yote ya kikao hiki isipokuwa safari yangu niliyotumwa na Waziri Mkuu kwenda Geneva kuongoza ujumbe wa Tanzania kwenye Mkutano wa Maendeleo ya Kimataifa, siku zote niko hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kusema jambo moja ambalo ni mafanikio makubwa kwa kipindi chote nilichokaa. Kero namba moja ya Nachingwea ni maji na nilitoa ahadi kwamba Chama cha Mapinduzi kikishinda mwaka 2000 tutapambana na tatizo la maji. Hapa nasimama kumshukuru, wale Waandishi wa Habari mnaonipenda naomba habari hizi zifike Nachingwea, kwamba kwa mara ya kwanza Mheshimiwa Edward N. Lowassa, baada ya kushirikiana na mimi kama Mbunge na Bwana Nicodemas Banduka kama Mkuu wa Mkoa na Mheshimiwa Gama na wazee na wananchi wa Nachingwea kutafuta chanzo cha maji cha uhakika tumekubaliwa kwamba Wilaya ya Masasi na Nachingwea tutaelekeza nguvu zetu sasa kwenye mradi wa chanzo cha maji cha Mwinji na kwa mara ya kwanza ameweka kwenye kasma ya Serikali ili kiwe ndio chanzo cha maji cha muda mrefu. Sio hilo tu, Wilaya ya Nachingwea kama ilivyo ya Masasi, Liwale na Kilwa mwaka huu tumewekwa kwenye miradi ya Benki ya Dunia ili kutekeleza mradi huo. Sasa nikimaliza kazi hiyo nitajua cha kufanya mwaka 2005 lakini namshukuru Mheshimiwa Lowassa kwa kazi hiyo na wananchi mjue jambo hili nimeshughulikia kikamilifu kama mnavyoniamini na naomba muendelee kuniamini. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja iliyotolewa. Nawashukuru wataalam wetu kwa jinsi walivyotusaidia mpaka kutufikisha hapa tulipofika, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA CNHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nijaribu kutoa maelezo na pengine majibu kwa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia humu Bungeni na wale waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kabisa kwamba hoja na michango zilizoibuliwa zinafikia karibu 40. Kwa muda nilionao wa kama dakika 47 sio rahisi kuzizungumzia zote lakini tunaweza kuziweka katika makundi na baadaye kwa sababu hii ni sehemu ya ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kutekeleza katiba, kuishauri na kuisimamia Serikali zitafanyiwa kazi ipasavyo. Kwanza nianze kuwashukuru wale waliopata nafasi ya kuzungumza hapa ndani ya Bunge. Nianze kwa kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Anne Makinda, Makamu Mwenyekiti Hassan Rajab KhatiB, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ambaye namshukuru sana kwa kuunga mkono hoja, Mheshimiwa Ali Said Juma, Mheshimiwa Dr. Batilda Buriani, Mheshimiwa Issa Mohamed Suleiman, Mheshimiwa Zuhura S. Abdallah, Mheshimiwa Yusuf Kombo Juma, Mheshimiwa Abdallah Khamis Feruzi, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Semindu Kisange Pawa, Mheshimiwa Bernard K. Membe, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Kheri Ameir, Mheshimiwa Abdulatif Hussein Esmail, Mheshimiwa Paul Kimiti na kaka yangu Mheshimiwa Edgar Maokola-Majoga. Kama sikukosea ni 16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa njia ya maandishi jumla yao ni 36 na tunawashukuru sana kwa michango yao, nao ni Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Ireneus N. Ngwatura,

Mheshimiwa Mbaruk H. Mwandoro, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Mwadini A. Jecha, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Bahati A. Abeid, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Thecla Boma, Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Shaibu Ameir, Mheshimiwa Zahor Khamis, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe na Mheshimiwa Ruth Msafiri. Nawashukuru sana kwa michango yao na ushauri waliotupatia sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hoja zilizoibuliwa ziko kama 40 sina hakika kama naweza kuzitaja zote lakini kuna *TANESCO, TASAF, BOT,* Chuo cha *Marine, TRA,* Katiba, taka za plastiki, magari chakavu, *EWASONGISU;* Mgololo, Ziwa Jipe na Nyumba ya Mungu, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika, nishati ya kuni na mkaa. *NIGP, SELF,* vyanzo vya maji na uchomaji moto, mazingira ya Pwani, Sheria za Mazingira, Wabunge, Madiwani katika mkakati wa umaskinin, fedha za wafadhili, uharibifu wa mazingira utokanao na uchimbaji madini, uainisho wa mkakati wa *millennium development goals,* watoto yatima, UKIMWI, malaria, akina mama, *maternal tax, child mortality, NEMC,* kodi ya migodi iongezwe, mikataba ipitiwe na Kamati za Bunge, wachimbaji wanunue vitu nchini, wawekezaji wanunue vitu na huduma nchini, urasimu katika usajili wa *NGOs,* ukataji miti, tathmini ya *Reo,* mifugo katika mbuga za Mbeya inaharibu mazingira Chunya, meli kumwaga uchafu Baharini, mashamba ya chumvi, shamba la chumvi Kunduchi, bonde la Bubu Shinyanga, Singida na Arusha, jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais, *registration and harassment* ya magari yenye namba ZNZ, Sheria ya *NGOs* na wavuvi wa Kojani kunyanyaswa. Haya ni baadhi ya yale yaliyosemwa au ni masuala yaliyoibuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye sehemu kuu zile saba lakini zaidi hizi mbili, katika suala la Muungano, masuala ambayo yamejitokeza, kwanza nishukuru katika michango yote hakuna hata Mheshimiwa Mbunge mmoja aliyesema hatuutaki Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilikuwa naangalia mkanda nilivyokuwa katika Jimbo langu la Uchaguzi, nilikuwa nawaeleza wapiga kura wa Jimbo la Muhambwe kwamba nafanya kazi wapi nikawaambia kwamba Muungano ni matunda ya kazi ya wanadamu na hakuna binadamu aliye mkamilifu. Sasa kwa vyovyote vile tunapokuwa na matunda ya mikono na fikra za binadamu lazima mtakuwa na matatizo kwa sababu ninyi wenyewe sio wakamilifu. La msingi kwanza tunakubaliana Muungano tunauhitaji. Kuna Mheshimiwa Mbunge amesema wananchi wananufaika na kuwepo kwa Muungano. Sasa pengine ni vizuri tukaanza kujiuliza hivi tunaposema juu ya kero, tena mwingine amependekeza kwamba wala tusiseme kero tuangalie vipengele katika Muungano ambavyo ndivyo tunavipa jina la kero ili tuweze kutazama kama turekebishe au tufanye nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema na nilipokuwa naiangalia kanda nilipokuwa katika Jimbo la Muhambwe sijui nani alinipiga picha kule za *video* tunachokihitaji na kama walivyosisitiza Waheshimiwa Wabunge wengi ni kulijadili suala hili bila jazba. Ni suala la kuainisha matatizo tunayoyabatiza kero za Muungano. Hivi ni kweli ni kero za Muungano kwa maana ya wenye Muungano wao Watanzania au ni wakati mwingine, ni mawazo yangu na naomba pengine tukubaliane kwamba baadhi yetu viongozi tunaweza kuwa sababu ya kile kinachoitwa kero za Muungano. Sasa kwa sababu sisi tunasema ni viongozi watumishi tujali maslahi ya wenye Muungano wao, maslahi yetu binafsi kiongozi mmoja mmoja tuyaweke pembeni. Kwa kufanya hivyo, nina haki azma ya kutunza, kuudumisha Muungano wetu kwa kile tunachokubaliana kweli Muungano wetu utadumu daima dumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetolewa hoja kwamba mafuta na gesi ambazo zinatamkwa rasmi katika jedwali la masuala ya Muungano kwa mujibu wa Katiba yetu kile kifungu alichokitaja Mheshimiwa Mbunge wa Magomeni, sasa kama tunataka mambo haya yaondoke katika masuala ya Muungano upo utaratibu basi wa kurekebisha Katiba sio kila mtu kukaa mahali pake na kuanza kusema haya mambo

yaondoke kwenye Muungano. Tunao utaratibu katika nchi yetu kwa kufanya mambo kwa mujibu wa utaratibu, sheria na kanuni. Ninachotaka kusisitiza hapa ni suala la kufuata utaratibu wa kujadiliana ili kuondoa tatizo mara linapojitokeza katika jamii yetu ya Watanzania. Katika masuala yanayohusu Muungano nadhani tufuate utaratibu huo huo na mifano tunao. Muafaka ni ushahidi hai wa matatizo yanayoweza kutupata Watanzania lakini tukakaa pamoja sisi wenyewe kwa maslahi ya Taifa yetu na watu wake wote tukatatua matatizo kila yanapojitokeza, katika suala la Muungano tusifanye tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limegusiwa tatizo lilojitokeza juzi la kukatwa umeme kule Zanzibar na hakika mmesoma magazeti yanasemaje. Mimi kwa kuwa tulikuwa hapa muda mwingi sijasoma magazeti lakini nilisikia kwa mbali. Niseme tu kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais kazi yake ni kuratibu shughuli zote zinazofanyika katika Ofisi hii na tunaporatibu tunaainisha maeneo ya kuwasiliana na kushirikiana. Pengine katika suala hili ninukuu kile nilichokisema mwaka jana nilipokuwa nikijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kipindi kama hiki, katika kitabu hiki ni ukurasa wa 160, nilikuwa najibu hoja ya Mheshimiwa Issa Suleiman alipokuwa amechangia na nikampongeza kwamba alikuwa amefanya utafiti mkubwa na mzuri tu, nilisema na nanukuu: “Ushauri wake amesema kwamba Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika wakutane ili washauriane". Mimi hili nalikubali, ndivyo inavyosemeka hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili kwa sababu nimesema kazi yetu ni kuratibu ni kweli na kama Mheshimiwa Spika alivyoelekeza leo asubuhi na Mheshimiwa Mbunge mmoja ametuarifu mchana huu kwamba Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika sisi kazi yetu ni kuratibu lakini wao wanahusika moja kwa moja wamekwishakutana, wameshauriana na tunachokiamini ni kwamba tatizo hili lililojitokeza halitorudiwa tena. Mengine katika eneo hili la Muungano ilikuwa ni ujenzi kwanza Ofisi ya Benki Kuu Tanzania *(BOT)* na Ofisi ya Makamu wa Rais kule Zanzibar. Hili la ujenzi wa Ofisi ya Benki Kuu *(BOT)*, katika suala la uratibu ni kweli kwamba Waziri wa Fedha atakapokuja hapa atalitolea maelezo kwa kina lakini katika suala zima la uratibu hili tumekwishakubaliana kwamba kufanyike ushauri ili tuone la kufanya katika kujenga Ofisi ya Benki Kuu kule Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ujenzi wa *Marine Science Institute,* Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilitoa Kiwanja Na.530 eneo la Buyu na barua iko hapa kumbukumbu yake ni ndefu tu lakini ya tarehe 11/10/2002. Aidha, upimaji ulifanyika baada ya kupata kibali kilichotolewa tarehe 11/10/2002. Tunachosema ni kwamba ujenzi ni pamoja na kuanza taratibu za kujihakikishia umepata kiwanja, michoro ili uweze kujenga jengo linalohusika. Sasa sio la kusema tuko mbioni tunachosema shughuli zimekwishaanza na tunashukuru kwa ushauri tuliopewa kwamba kituo hiki kijengwe.

Kuhusu ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ujumla hatua zinachukuliwa kuijenga Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar na Dar es Salaam. Sehemu ile ya Mwanakwerekwa sio ngeni kule tumepata kiwanja cha kujenga Ofisi ya Makamu wa Rais na wakati mmoja kuna watu walisema naona Makamu wa Rais ameukata keshaanza kuporomosha ghorofa lakini waliposoma vibao vya wale *contractor* na jengo lenyewe wakasema aah kumbe Ofisi ya Makamu Rais maana walifikiri ni nyumba yake binafsi. Pale Dar es Salaam, wale Waheshimiwa Wabunge ambao sisemi mmebahatika kuja Ofisini kwangu lakini mmefika ofisi kwangu mmeona hali ya ofisi sina haja ya kueleza zaidi lakini tumeshapata michoro ya jengo katika Ofisi zilizopo mtaa ule wa Luthuli, michoro hiyo imekamilika kinachofanyika ni uchunguzi wa udongo. Tumeshatangaza zabuni au tenda na ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, haya ndio ningependa niyazungumzie katika yale ya msingi yaliyojitokeza kuhusiana na suala zima la Muungano. Nakiri sikuyaeleza yote na kama nilivyokiri mwanzoni kabisa si rahisi kuyaelezea yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mazingira, niseme la jumla kwamba michango tuliyoipokea ukienda kwa undani inalenga kutukumbusha na kutuhimiza kwamba unapozungumzia suala la mazingira iwe ni hifadhi ya Ziwa Jipe, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa ambalo Mheshimiwa Kolimba huwa analisemea sana na nitamwomba aangalie Kitabu cha Nne, ukurasa wa 27, kuna milioni 105 ambazo zitatumika kuendeleza kile ambacho kimeshaanza katika Maziwa kama Ziwa Victoria na Tanganyika maana huko nyuma ilikuwa inaonekana kama Ziwa Nyasa limeachwa pembeni.

Tunachokizungumzia ni ile hifadhi ya mazingira ya maeneo haya, siku moja niliwaambia kule Bagamoyo hatufanyi matambiko tu, ndani ya ziwa, bahari au mito mikubwa kuna rasilimali

inayowawezesha wananchi kufanya shughuli zao, aidha, kwa mtu mmoja mmoja kujitafutia riziki au vikundi kujitafutia maendeleo. Lakini usipohifadhi mazingira ya ziwa au bahari na pwani rasilimali ile itatoweka na utabakia katika hali ya kuwa maskini wakati ulikuwa na fursa ya kuweza kutumia rasilimali zile kupambana na umaskini ipasavyo. Sasa haya ndiyo tunayoyazungumzia juu ya hifadhi ya mazingira kwa maana ya maeneo kama hayo ninayoyatolea mfano.

Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nina hakika tunazungumzia usafi wa ardhi, usafi wa udongo kwa maana ya ardhi, hewa na maji kwa sababu hewa tunayovuta, Waheshimiwa Wabunge wamechangia, kwa mfano, Kampuni ya *BP* kuleta petrol isiyo na risasi ni moja ya mambo ambayo yakizingatiwa tunapunguza uchafuzi wa hewa na sote tunajua tunavuta hewa ili tuweze kuendelea kuishi. Ukichafua mazingira ya hewa ni kwamba unasababisha mazingira ya kifo. Huo ni uchafuzi wa hewa na namshukuru sana Mheshimiwa Janguo katika mchango wake wa maandishi amesema kwamba, tunapozungumzia juu ya hifadhi ya mazingira yapo mazingira tunayoyaona physical na yapo mazingira mengine hayaonekani kwa mfano, air pollution na kadhalika, yapo mambo mengi sana katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapozungumzia usafi wa maji yawe ni viwandani au maji ya kutumia kwa kunywa na shughuli nyingine za ndani kinacholengwa ni kwamba maji yale yasiwe chanzo cha maradhi ambayo yanaharibu afya za wananchi na mwishoni yasababishe vifo. Ndiyo mambo unayoyajumuisha unapozungumzia juu ya suala la hifadhi ya mazingira kwa ujumla. Ardhi kwa maana ya udongo, sote tunajua tunalima ili tupate chakula na mambo mengine. Hewa, wote tunavuta hewa ili tuendelee kuishi. Nasikia Madaktari, nadhani Mheshimiwa Dr. Mwinyi hapa anaweza akatuambia ubongo ukikosa hewa ya Oksijeni nadhani kwa dakika tatu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Thelathini.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Enhee, dakika thelathini basi wewe binadamu unakuwa kitu kingine, unaitwa aliyekuwa na uhai umetoweka. Kwa hiyo, hewa ni muhimu sana. Maji hivyo hivyo, kwa hiyo kwa msingi na kwa muhtasari nilitaka niseme hivyo kwamba tunapozungumzia haya mambo ya uhifadhi wa mazingira tunalenga huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie maeneo mahsusi. Kulikuwa na kwa mfano taka za plastiki na ni kweli kila utakapokwenda Mijini au Vijijini taka hizi za plastiki zimezagaa. Sasa kinachozungumzwa hapa na ushauri tulioupata ni kwamba ni vizuri itafutwe mifuko mbadala maana sasa hivi tunaweza kusema tupige marufuku ile mifuko ya rambo. Lakini nilipokuwa shule nilijifunza kwamba katika haya mambo yetu ya maendeleo ya kiuchumi na jamii unapotatua tatizo moja sasa hivi unazalisha tatizo lingine. Sasa unaweza ukasema na nawapongeza sana wenzetu katika Serikali ya Mapinduzi wa Zanzibar wao nadhani wamepiga marufuku mifuko ya rambo. Sisi tumeanza kwa kuweka kodi katika mifuko hii ambayo inaingizwa holela holela tu na mingine ukienda dukani unapewa wala huambiwi ulipie. Hizi ni hatua ambazo tumeanza kuzichukua. Kwa mfano, katika kupitisha bajeti ya nchi iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha mifuko hii ya plastiki imewekwa kodi ya asilimia 15. Lengo ni kupunguza hii kasi ya kuingiza mifuko hivi hivi tu kwa sababu mingine tunadhani inaingia bila kutozwa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huo huo cha muhimu ni kuhimiza matumizi mazuri ya mifuko hii ikiwa ni pamoja na kuhimiza kurejereza naambiwa hicho ni Kiswahili kwa neno la *to re-circle* mifuko na matumizi ya mifuko mbadala. Pengine ni vizuri tukaeleza kwamba inawezekana watu wetu katika mambo haya, mengine ni ya siku hizi hizi ingawa tunaweza kusema ni ya siku nyingi, lakini sina hakika kama wananchi wanafahamu mifuko ile ya plastiki pale inapokuwa hairuhusu hewa wala maji kuingia katika udongo na udongo ukikosa hewa na maji vile vijidudu vidogo (bakteria) hufa. Mahali ambapo udongo hauna bakteria kwa kweli udongo ule ni sawa na jangwa hakiwezi kuota kitu wala kustawi. Ndiyo athari ya mifuko hii ya plastiki, lakini sina hakika kama tumetoa elimu ya kutosha kuhusiana na hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kulikuwa na suala la nishati ya kuni na mkaa inasababisha uharibifu wa mazingira. Kabisa nakubaliana nalo na kinachofanyika nadhani Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini katika ule mkakati wa kupeleka umeme hadi Vijijini ni moja ya lengo la kuokoa mazingira yetu kwa maana ya kutokukata miti kwa kiasi hicho. Vile vile kwa wakazi wa Mijini ushuru wa

bidhaa ya gesi ya kupikia umepunguzwa kwa kiasi cha asilimia 50 ili kuwawezesha watu kutumia gesi zaidi kuliko mkaa na kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu lilikuwa Ziwa Nyasa na nimekwishalizungumzia katika utangulizi, sina haja ya kurudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanda cha Mgololo tumepata mchango kutoka kwa Mheshimiwa Benito Malangalila. Ni kweli kabisa ambacho anasema yeye, ushauri wake ni kwamba asipewe mwekezaji mbabaishaji. Ninachokumbuka wakati Menejimenti ya kiwanda hicho walipokuja Ofisi ya Makamu wa Rais kutueleza hatari inayotukabili kama madawa ya sumu yatavuja kwamba tunaweza tukapata tatizo la wananchi wetu karibu milioni moja kupoteza maisha yao na eneo lote la bonde la Rufiji kuharibika mazingira yake na pengine hata pwani ya Dar es Salaam. Kitu ambacho sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais tulikuwa tunajiuliza ni kwamba ukishaona ukubwa wa athari hizi huwezi ukatoa tarakimu ya fedha ambayo nadhani wachumi wanasema *opportunity cost* kwamba hili ukaliacha ukasema tunaweza kuliacha hivyo hivyo bora liende kama unajua unahatarisha maisha ya wananchi wako kiasi cha milioni moja. Kwa hiyo, nakubaliana na *concern* yake kwamba asipewe mwekezaji mbabaishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa mazingira ya Ziwa Jipe na tumepata mchango wa Mheshimiwa Mbunge wa Mwanga Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe. Mimi kwanza nirejee kuishukuru sana Kamati ya Maliasili na Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokwenda kule Ziwa Jipe tarehe 27 Januari, 2003 ilikuwa baada ya Mheshimiwa Mbunge kusema, hivi ninyi Serikali mnajua Ziwa lile linatoweka kwa upande wa Tanzania. Baadaye Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa akasema kitu hicho hicho. Sasa nilipokwenda ingawa nilikuwa nafikiria kabla ya kufika ndiyo nikathibitisha ule usemi wa Kiingereza, *seeing is the living.* Ni kweli kabisa sehemu kubwa ya Ziwa lile upande wetu wa Tanzania unatoweka. Sasa nilipoona ukubwa wa tatizo hili nikasema nimwombe Mwenyezi Mungu pengine Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hii wakikubali twende wakaone kusudi tusibakie peke yetu katika Ofisi ya Makamu wa Rais tuna tatizo kubwa *in our hands,* halafu wenzetu ambao wanatushauri na kutusimamia wasilijue. Nawashukuru sana kwa kukubali kwenda mpaka kule na kwa kweli wametupa ushauri kwamba tusifanye mchezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii yote niseme ni kwa sababu Serikali yetu ya Tanzania inawapenda watu wake. Wapo wakulima wadogo wadogo na wachungaji wa kawaida. Kwingine wangeweza kukwambia hivi mnakwenda huko kufanya nini Waziri mzima na Waheshimiwa Wabunge? Lakini sisi tumesema ni watumishi wa watu, lazima twende tujifunze matatizo yao na tuone kwa pamoja tunatafuta ufumbuzi wake. Kwa hiyo, nampongeza sana sana Mheshimiwa Profesa Maghembe na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kutufikisha mahali tukafika kuona ukubwa wa tatizo lililokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine nadhani tulilopata mchango ni kwamba kuhusiana na ujenzi wa bwawa la umeme Ewasongiro nchini Kenya, nchi jirani na rafiki. Baada ya kutathmini athari za mazingira katika eneo hili suala la mradi huu lilijadiliwa kwa kina chini ya Kamati ya Maliasili na Mazingira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baada ya kuona athari tukafika mahali wenzetu Kenya wakasema tunakubali kusitisha mradi huu. Tunashukuru ushirikiano ndiyo huzaa mambo kama haya ya kuelewana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria mama ya mazingira na hasa suala la Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC),* niseme wengine wamekuwa wanasema jamani *NEMC* ina meno ya bandia au ya plastiki, tunafanyaje ili *NEMC* ipate meno haya yanayong'ata. Niseme tu na nimewahi kumpongeza sana Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais hadharani na ninarudia, ujio wake umetuongezea kasi na *Inshallah* Mwenyezi Mungu akipenda Januari tunaweza kupitisha Muswada wa Sheria mama ya Mazingira hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya mkutano wa *Rio de Janeiro* na ule wa *Johannesburg* yamejumuishwa katika *Millennium Goals* na maeneo mahsusi kama utekelezaji wa programu ya maziwa makubwa ambayo ni Victoria na Tanganyika na utekelezaji wa Mikataba mbalimbali ya Kimataifa kuhusu mazingira. Naomba nirejee kuwashukuru Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa upande wa Upinzani ni kwamba

kitu cha kwanza tarehe 20/6/2003 alichoniomba ni kwamba tunaomba ile Mikataba ili na sisi tusiwe gizani. Ndicho nilichosema mnapokuwa na masuala ya msingi Kitaifa tofauti zenu za kisiasa mnaweka pembeni mnakuwa kitu kimoja. Sasa tunao pia utekelezaji wa miradi midogo midogo ya hifadhi ya mazingira chini ya *UNEP* na *GEF* na uboreshaji wa mazingira ya Chozani, Chwaka Zanzibar na karibu Chozani wameweka (W) nadhani tuiondoe na karibu asilimia 30 ya nchi imetengwa kama maeneo ya hifadhi ya bioanuwai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo maeneo ambayo nilifikiri niyatolee maelezo lakini nirejee kusema kwa yale ambayo hatukutoa maelezo ya moja kwa moja Mheshimiwa Mbunge kachangia vipi kwa kusema hapa Bungeni au kwa maandishi, katika Ofisi ya Makamu wa Rais tunao utaratibu wa kutengeneza karatasi kama hizi.

*(Hapa Mheshimiwa Waziri alionyesha karatasi kwa Waheshimiwa Wabunge)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Kama tulivyosema mwaka jana, safari hii vile vile tutafanya hivyo, tuwapatie Waheshimiwa Wabunge ili iwe ni nyenzo ya kuendelea kwa Waheshimiwa Wabunge kutushauri na kushirikiana na sisi katika kutekeleza azma yetu ya kuwa viongozi watumishi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

**FUNGU 26 - MAKAMU WA RAIS**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... .Shs. 1,423,363,400/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 31 - OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... ... Shs. 2,512,221,012/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... Shs. 60,302,500/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Union Secretariat* ... ... ... ... ... Shs. 10,384,118,390/=

**MHE. ISSA MOHAMED SULEIMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati nilipochangia kuna sehemu moja nilikuwa nimechangia hasa kwa kutaka maelezo baadaye na kwa bahati nzuri suala la ku-*empower Zanzibar* yaani kuiwezesha kiuchumi limezungumzwa pia na Mheshimiwa Kimiti. Mimi kwa maoni yangu ni kwamba lina umuhimu sana kwa wakati tuliokuwa nao na nimezungumza kwamba kuna haja ya Muungano wetu kuelekea kwenye masuala ya kiuchumi yaani uwe Muungano wa kiuchumi. Kwa bahati mbaya Mheshimiwa Waziri alikuwa na mengi ambayo amesema. Kwa hiyo, hilo hakuliona. Ninachokitaka ......

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa katika hiki kifungu kidogo tusaidie basi kifungu gani?

**MHE. ISSA MOHAMED SULEIMAN:** Kwanza ni *programme 20, Union Coordination, Sub vote 2001,* lakini nataka kwenye kale kamshahara ka Mkurugenzi *sub vote 250100* ya Sekretariet ya Muungano. Nataka maelezo madogo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ambayo nataka......

**MWENYEKITI:** Nataka nikuelewe sawasawa Mheshimiwa, umesema kifungu kidogo cha mshahara?

**MHE. ISSA MOHAMED SULEIMAN:** Ni *basic salary* ya *Pensionable Posts.*

**MWENYEKITI:** Sasa hiyo ni *Pensionable Posts.*

**MHE. ISSA MOHAMED SULEIMAN:** Kuna mshahara wa Mkurugenzi hapo.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Waziri tunaomba maelezo.

**MHE. ISSA MOHAMED SULEIMAN:** Sijatoa maelezo yenyewe ninayoyataka.

**MWENYEKITI:** Haya toa maelezo.

**MHE. ISSA MOHAMED SULEIMAN:** *Okay,* maelezo ninayoyataka Mheshimiwa Waziri akubali kwamba ipo haja ya kufanya badiliko sasa kuelekea kwenye Muungano wa kiuchumi kwa sababu ameli-*omit* kabisa kwamba ni suala ambalo halina umuhimu.

**MWENYEKITI:** Nasikitika sana Mheshimiwa katika kifungu hiki hilo halipo.

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilichangia kwa maandishi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba ufafanuzi kwa kuwa haya ninayotaka kuyazungumza yanahusiana na masuala vile vile ya Kimuungano na hii ndiyo sehemu ambayo inaratibu masuala ya Kimuungano. Nilichokuwa nakiombea ufafanuzi kwamba kwa kuwa hii inaratibu masuala ya Kimuungano nataka kuzungumzia katika *point* ya kiuchumi.

Katika zile Wizara ambazo siyo za Kimuungano lakini zinapozungumzia masuala ya kimisaada zinazungumza kwa jina la Tanzania na wanapokuwa hasa nje ya nchi wanai-*represent Tanzania* katika masuala yote iwe ya misaada na mengineyo. Sasa katika mchango wangu nilimwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba haoni haja kwa sasa tunapokuwa nje tukawa na timu ya Tanzania ili haya maslahi ya pande zote mbili tukaweza kuyawasilisha ikiwa ni sehemu mojawapo ya kuondoa haya matatizo yetu ya Kimuungano. Hilo la kwanza.

Pili, nilimwomba Mheshimiwa Waziri pia atusaidie ili kuonyesha ile picha ya Kimuungano, katika hii Wizara yake, utumishi upo vipi Kimuungano?

Hiyo nayo pengine ingetusaidia na pengine tungeweza kumsaidia pengine hata kumshauri kwa suala hilo. Lakini pia naona hilo halikuwa na majibu.

Halafu la mwisho, mara nyingi katika vikao vyetu vya Bunge vya kawaida tumekuwa tunapata matatizo wakati mwingine tunavutana pasipo na ulazima katika ile Miswada ambayo inahusu Jamhuri nzima ya Muungano. Sasa nyuma huko tuliwahi kujibiwa hapa Bungeni kwamba Ofisi hii ndiyo inayohusika au inayopelekewa ile Miswada kwa madhumuni ya kuwasiliana na upande wa pili wa Muungano. Sasa bado naona hilo tatizo lilikuwa linaendelea. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie tatizo nini hapa ili hili suala tuweze kusaidia na kuona mvutano ule unamalizika kabisa kabisa ambao nahisi sio wa lazima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naona tunarukia mambo ilikuwa maelezo ya jumla kama haya yawepo kwenye kifungu kile cha 1001. Haya ya jumla haya ndiyo pale watu wangeogelea wanavyotaka. Sasa huku kumekuwa ni *very specific* ndiyo maana napata shida ni kitu gani hapa kinaulizwa hapa, ikawa ngumu.

Pamoja na hayo kwa sababu sasa nadhani watu hawajaelewa. Mheshimiwa Waziri una maelezo kwa haya mawili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nitoe maelezo kwa kifupi sana kuhusu haya mambo aliyoyazungumzia Mheshimiwa Zahor kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inajumuisha Tanzania Bara na Zanzibar tunapokwenda nje kutafuta mikopo, misaada au wahisani wanapoona nia yenu njema tunapopata misaada hii ni nini kinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika Mheshimiwa Mbunge anakumbuka au amewahi kusikia kile kilichotokana na Tume ya Mheshimiwa Shellukindo kwamba katika kupunguza matatizo haya ambayo yanajitokeza, asilimia 4.5 ya misaada hii ielekezwe Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Sasa ukizungumzia kwamba hivi picha ya Muungano inakuwaje. Katika misaada utaratibu ni huo huo wa asilimia 4.5 na kuna Mheshimiwa Mbunge amechangia kwamba tutumie takwimu, lakini mimi sitaki kwenda huko kwenye takwimu maana itatuvurugia suala hili zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu picha ya Muungano kiutumishi. Tunao watumishi kutoka upande wa pili wa Muungano kwa maana ya Tanzania Zanzibar katika Ofisi hii ya Makamu wa Rais. Niruhusu pia niseme nafasi za utumishi zinapokuwa wazi matangazo hutolewa katika vyombo vya habari kwa maana ya magazeti ili wanaohitaji kuajiriwa na wenye sifa ya kuajiriwa wapeleke maombi kwa Idara yetu ya Utawala. Halafu taratibu za ajira katika utumishi wa umma zifuatwe na tunao katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mvutano katika Miswada, tatizo liko wapi? Miswada kama tunavyojua ikishatangazwa na Katiba inasema kama ni Miswada sheria ya kutumika pande zote za Muungano inakuja hapa Bungeni inatamka kwamba sheria baada ya Mheshimiwa Rais kuridhia Mswada unaopitishwa na Bunge inasema Katiba itamke kama itatumika pande zote za Muungano.

Sasa mvutano unawezekana ukawa siyo wa lazima kama vile kwa mfano katika michango iliyotolewa ni kwamba pengine Muungano hauna matatizo inawezekana ni watendaji wanazusha mambo yao.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - *Poverty Eradication* ... ... ... ... ... .. Shs.1,311,218,436/=
Kif. 4001 - *Non-Government Organizations* ... ... .Shs. 68,630,776/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamatibila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 - *Environment* ... ... ... ... ... ... ... ....Shs. 819,700,686/=

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina matatizo makubwa na hicho kifungu hasa naipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi nzuri wanayofanya.

Kwa niaba ya wananchi wa Kunduchi tunayo malalamiko kuna shamba la chumvi ambalo lipo katikati yetu na huyu mtu anamilikishwa hilo shamba anapewa *right of occupancy* kwa nia ya kukopa. Akishapewa *right of occupancy* maana yake ni kwamba ameshamiliki kabisa, hatuna tena sauti napo na shamba la chumvi lilivyo by nature linaingilia mazingira ya pale na sasa limeshaharibu ile mikoko iliyokuwa ina-surround lile eneo na bahari sasa inatufikia kule tunakoishi.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatupa *commitment* gani juu ya lile tatizo la shamba la chumvi kule Kunduchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lamwai item ipi ili iweze kumsaidia zaidi Mheshimiwa Waziri?

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kifungu chote kinahusiana na environmental protection na ninalalamika juu ya environmental protection effort zinazofanyika kule kwenye ufukwe wa Kunduchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri maelezo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuonyesha kuwa hata Meza kidogo ilikuwa inataka kusema hasa hasa ni item gani. Lakini ni kweli kama nilivyosema ukitaka kukizungumzia kifungu hiki kwa jumla ninachoweza kusema ni kwamba katika shughuli zote za kujitafutia riziki au maendeleo lazima utaathiri mazingira kwa namna moja ama nyingine. Lakini tunachokifanya katika Ofisi ya Makamu wa Rais ni huyo ambaye anataka kufanya shughuli yoyote ile kupewa kile tunachoita *environmental impact assessment* kusudi azingatie masharti nini kifanyike na nini kisifanyike ili asije akaathiri mazingira yenyewe na afya ya binadamu.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *sub vote* hiyo hiyo ya 5001, nataka kuizungumzia Mgololo, sasa sijui nitumie ile ya equipments au ya *fuel* sielewi ila ni kuhusu kemikali zilizokuwa *stored* pale Mgololo.

Tatizo kubwa moja ni kwa hilo la mwekezaji achaguliwe kwa uangalifu hilo amelieleza Waziri, lakini lingine kubwa zaidi ni kuwa kama zile kemikali hazitumiki zitakuja kuharibu matanki yote yaliyopo pale na zitaanza kuvuja na kuingia kwenye mito na ndiyo hiyo itawaua watu hawa milioni moja.

Sasa sijui kama wataweza kutumia hizo kwa kukifungua kile kiwanda, sasa hivi kiwe kinafanya kazi ili tumalize zile kemikali katika matanki ili yawe matupu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo:-

Mwekezaji yeyote atakayechukua kiwanda cha *ASPM* cha Mgololo lazima atumie makemikali yale yote, *process* ya uzalishaji ina hatua kwa hatua. Unapoanza kutoka kwenye kukata magogo yale ili yawe *pulp,* halafu baadaye unayapitisha katika mkondo wa uzalishaji wa karatasi katika sehemu mbalimbali.

Sasa ile *process* ndiyo itakayofanya matumizi ya kemikali ya aina zote katika *reprocess.* Kwa maana hiyo basi utaweza kuzuia uharibifu wa mazingira. Lakini kama ile *process* haifanyiki basi hatari kwa mazingira itakuwa ni kubwa sana. Ndiyo maana juhudi za Serikali ni kukiwezesha kiwanda kile kizalishe mali kwa kiwango kikubwa kama inavyotarajiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais

Kif. 1001 *Administration and General* ... ... ... ... ... 476,699,700/=

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi naomba kupata clarification katika kifungu hiki. Tunao mpango wa muda mrefu wa kuhamishia Makao Mkuu ya nchi yetu katika Mji wa Dodoma na suala hili limekuwa likizuiliwa sana na uhaba wa raslimali tulizokuwa nazo na mimi ninadhani kadri tunavyopata raslimali kidogo za kujenga kitu chochote tungelikijenga Dodoma.

Sasa ujenzi wa Ofisi ya Makamu ya Rais nadhani imezungumzwa hiyo Ofisi itajengwa katika Jiji la Dar es Salaam. Sasa naomba kupata uhakika ni kitu gani hasa kinaendelea. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Emmanuel Kipole kwa kutumia Kanuni barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokiuliza Mheshimiwa Mbunge ni kwamba azma yetu ya kuhamia Dodoma, mbona tunajenga Ofisi katika Jiji la Dar es Salaam! Kabla hatujahamia Dodoma lazima tuwe na mahali pa kufanyia kazi. Niongeze tu katika hili na kweli kabisa Waheshimiwa Wabunge ambao mmefika Ofisini kwangu mtakubaliana na mimi hata kwa kaka yangu Mheshimiwa Edgar Maokola- Majogo kwa kweli tunafanya kazi katika mazingira ambayo hayalingani kiafya, kihadhi kwa kile kinachotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kitu kimoja tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba anatulinda na anawalinda viongozi wetu. Si jambo la kawaida viongozi wa Wakuu wa Taifa letu wawili, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Makamu wake wanakaa katika Ofisi mmoja, kwa maana ya jengo moja. Tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu atulindie viongozi wetu. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, sisi Watanzania tumekuwa watu wa kuvuta subira sana. Kuna mambo mbalimbali huwa tunayazungumza hata hapa Bungeni tunatakiwa kuvuta subira. Sasa mimi nadhani Ofisi ya Makamu ya Rais imekuwepo pale kwa muda mrefu na kwa kweli wamevuta subira katika hiyo hali ngumu. Inakuwaje sasa hiyo Ofisi tusianze kuijenga Dodoma kwa hizi fedha tulizonazo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya nyongeza ukizingatia na yale niliyoyatoa mwanzoni. Ni kweli kabisa kabla hatujahamia Dodoma na tunahamia hatua kwa hatua. Halafu kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema jamani *Rome wasn't built in a day.* Sasa ni kweli tumeanza kuhamia Dodoma hatua kwa hatua. Lakini pia tunahitaji Ofisi kwa ajili ya mahali pa kufanyia kazi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 *Poverty Eradication* ... ... ...Shs. 2,977,800,000/=
Kif. 5001 *Environment* ... ... ... ... . Shs. 6,437,570,500/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2003/2004 Fungu 26 na Fungu 31, Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 81fasili ya 5, naomba kutoa hoja kwamba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka*

*2003/2004 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hakuna shughuli nyingine. Kwa hiyo, naliahirisha Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 1.09 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi
Tarehe 24 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*